# HATARI KUBWA MBELE YETU

Kitabu hiki kimetungwa

kwa kukusanya

maandiko ya

ELLEN G. WHITE

1970

Kimetayarishwa na

Robert W. Olsen

HATARI KUBWA MBELE YETU

Kitabu hiki kimetungwa

kwa kukusanya

maandiko ya

ELLEN G. WHITE

Mfasiri: M. Mwamalumbili

The Crisis Ahead - Kiswahili

## UTANGULIZI

Mkusanyo huu wa maandiko umetayarishwa ili kutumika katika darasa la Karama ya Unabii katika Chuo cha Yunioni ya Pasifiki. Hili sio jaribio la kupanga kwa ukamilifu mfuatano wa matukio ya siku za mbele katika mafundisho yetu ya dini, bali ni mkusanyo tu mahali pamoja, kwa kusudi la kujifunza, semi muhimu sana za E. G. White zinazohusu unabii ule unaongojea kutimizwa kabla ya marejeo yake Kristo. Madondoo haya yamepangwa katika utaratibu ninaouona mimi kuwa una mantiki ndani yake, ila yamepangwa hivyo bila kuleta athari kwa aina nyingine ya mpangilio au maoni yaliyo kinyume na haya kutoka kwa wengine.

Ni vigumu mno kuzipanga sura hizi katika mfululizo ulio mkamilifu kwa vile sura nyingi katika hizo zina mambo yanayoingiliana. Kwa mfano, "Mvua ya asika" na "Sauti Kuu" ni uzoefu unaokwenda sambamba, mmoja ni chanzo na mwingine ni matokeo yake. Sura juu ya "Shetani Kuja kama Kristo" ingeweza kuwekwa karibu na ile ya "Kufungwa kwa Mlango wa Rehema", lakini basi, inaonekana kwamba ni vyema kujifunza somo hilo kwa kulihusisha na lile la "Miujiza ya Shetani."

Bwana alimwagiza Dada White "kuwapa waalimu katika shule zetu jukumu la kuwaandaa wanafunzi wao kwa kile kinachoujia ulimwengu huu." FE 526, 527. Kisha Bwana akampa nabii wa kike yuyo huyo habari ambayo imetolewa katika muhtasari huu wa mafundisho. Ni ombi langu kwamba Mungu apate kumjazi kila mwanafunzi atakayejifunza muhtasari huu.

Robert W. Olson

## UFUNGUO WA VIFUPISHO

AA----- Acts of the Apostles

1BC----- The Seventh-day Adventist Bible Commentary, Gombo1 (2BC, na kadhalika kwa Magombo 2-7).

ChS----- Christian Service

CM----- Colporteur Ministry

COL----- Christ Object Lessons

CSW----- Counsels on Sabbath School Work

CT----- Counsels to Parents, Teachers, and Students

CW----- Counsels to Writers and Editors

DA----- Desire of Ages

Ed----- Education

Ev----- Evangelism

EW----- Early Writings

FE----- Fundamentals of Christian Education

FL----- The Faith I live By

GC----- Great Controversy

GCB----- General Conference Bulletin

GW----- Gospel Workers

KH----- That I May Know Him

LS----- Life Sketches

MB----- Thoughts from the Mount of Blessing

MH----- The Ministry of Healing

ML----- My Life Today

MM----- Medical Ministry

MYP----- Messages to Young People

OHC----- Our High Calling

PK----- Prophets and Kings

PP----- Patriarchs and Prophets

RH----- The Review and Herald

SC----- Steps to Christ

SD----- Sons and Daughters of God

3SG----- Spiritual Gifts, Gombo la 3

SL----- Sanctified Life

SLP----- Sketches from the Life of Paul

1SM----- Selected Messages, Gombo la 1 (2SM kwa Gombola 2).

1SP----- Spirit of Prophecy, Gombo la 1 (4SP kwa Gombo la 4).

SR----- The Story of Redemption

ST----- The Signs of the Times

1T----- Testimonies, Gombo la 1 (2T, n.k. kwa magombo 2-9).

TM----- Testimonies to Ministers

AH----- Adventist Home

Y A L I Y O M O


1. Hatari Kubwa Mbele Yetu
2. Muungano wa Makanisa
3. Sheria ya Jumapili kwa Taifa Zima
4. Sheria ya Jumapili kwa Ulimwengu Mzima
5. Kipindi Kifupi cha Wakati wa Taabu
6. Pepeto Kuu
7. Mbele ya Watawala na Wafalme
8. Miujiza ya Shetani

9. Shetani Katika Umbile la Kristo

10. Roho Mtakatifu

11. Mvua ya Masika

12. Sauti Kuu

13. Nyakati na Majira

14. Muhuri wa Mungu

15. Alama ya Mnyama

16. Kufungwa kwa Mlango wa Rehema

17. Ukamilifu Ndani ya Kristo

18. Amri ya Kifo

19. Wakati wa Taabu ya Yakobo

20. Kipindi Kikuu cha Wakati wa Taabu

21. Nyumbani Hatimaye

Sura ya 1

## HATARI KUBWA MBELE YETU

1. Ni vidokezo gani vimo katika Maandiko vinavyoonyesha kwamba wakati wa taabu wa kuogofya uko mbele yetu? Dan. 12:1.

a. Kwa waovu ----- Ufu.14:9,10; Ufu. 16:1-21.

b. Kwa wenye haki ----- Ufu. 13:15-17.

2. Bibi White anakielezaje kipindi kile cha dhiki kinachoujia ulimwengu wetu?

(1) "Hatari Kubwa ya Kuogofya." "Kazi ambayo kanisa limeshindwa kufanya katika kipindi hiki cha amani na usitawi, litapaswa kuifanya katika kipindi cha hatari kubwa ya kuogofya, chini ya mazingira ya kukatisha tamaa sana, yaani, ya kuogofya sana." Ev.31; 5T 463.

(2) "Hatari Kubwa ya Mwisho."

a. "Katika kipindi hiki cha maovu yanayotapakaa kila mahali tunaweza kujua ya kwamba hatari kubwa ya mwisho imekaribia. Wakati uasi juu ya Sheria ya Mungu utakapokuwa umeenea karibu katika ulimwengu wote, watu wake watakapokuwa wanakandamizwa na kuteswa na wanadamu wenzao hapo ndipo Bwana atakapoingilia kati." COL 178.

b. "Maafa katika nchi kavu na baharini, hali ya kutotulia ya jamii, tetesi za vita, hutuonya juu ya mambo mabaya yatakayotokea mbele. Hubashiri matukio yanayokuja ya kiwango kikubwa mno.

"Mawakala wa uovu wanayaunganisha majeshi yao na kuyaimarisha. Wanajizatiti kwa hatari kubwa ile ya mwisho. Mabadiliko makubwa yatatokea mara moja katika ulimwengu wetu, na mabadiliko yale ya mwisho yatakuwa ya haraka-haraka." 9T 11.

(3) "Pambano la maana sana" la vizazi." "Hatari kubwa inawangojea watu wa Mungu. Hatari inawangojea walimwengu. Pambano la maana sana la vizazi vyote ndio kwanza liko mbele yetu." 5T 711.

(4) "Hatari ya Vizazi Vyote." Tunasimama mlangoni mwa hatari ya vizazi vyote. Kwa mfuatano wa haraka hukumu za Mungu zitakuja moja baada ya nyingine ----- moto, na mafuriko, na tetemeko la nchi, pamoja na vita na umwagaji wa damu. Hatupaswi kushangazwa wakati huu na matukio makuu na ya kukata maneno; maana malaika wa rehema hawezi kuendelea kwa muda mwingi zaidi kuwakinga wale wasiotaka kutubu." PK 278.

(5) Hatari kubwa sana tangu wakati ulipoanza kuwako. "Tunaukaribia wakati ambao, zaidi ya wakati mwingine wo wote uliopita tangu kuwako kwa ulimwengu huu, utataka kujitoa wakf kikamilifu kwa kila mmoja aliyepata kulitaja jina lake Kristo." GW 323.

(6) "Hatari Kubwa Sana." "Wakati huu wa sasa ni wakati wa kusisimua mno kwa wote wenye uhai. Watawala na viongozi wa siasa, watu wanaovikalia vyeo vyenye dhamana na mamlaka, wanaume na wanawake wanaotafakari sana wa tabaka zote, mawazo yao wameyakaza juu ya matukio yanayotokea kutuzunguka. Wanaangalia uhusiano uliopo miongoni mwa mataifa. Wanachunguza nguvu inayoingia katika kila kitu cha asili [ardhi, hewa, moto, maji], nao wanatambua ya kwamba jambo fulani kubwa na la kukata maneno li karibu kutokea, ----- ya kwamba ulimwengu huu umefikia ukingoni mwa hatari kubwa sana." PK 537; Ev 703,704, Ed 179.

(7) "Dhoruba."

a. "Dhoruba inaanza kuja ambayo itaupotosha na kuujaribu msingi wa kiroho wa kila mmoja wetu kufikia upeo wake." 5T 129.

b. "Dhoruba inakuja, ina ghadhabu isiyo na huruma. Je! tumejiweka tayari kukabiliana nayo?" 8T 315.

(8) "Tufani."

a. "Mungu amefunua kile kitakachotokea katika siku zile za mwisho, ili watu wake waweze kujiweka tayari kusimama dhidi ya tufani hiyo ya upinzani na ghadhabu." 5T 452.

b. "Tufani inakuja, nasi yatupasa kuwa tayari kukabiliana na ghadhabu yake kwa njia ya kuwa na toba kwa Mungu na imani kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Bwana tasimama kuitetemesha sana dunia hii. Tutaona dhiki pande zote. Maelfu ya meli yatazamishwa chini ya vilindi vya bahari.

Majeshi ya wanamaji yatazama chini, na maisha ya wanadamu yatatolewa mhanga kwa mamilioni. Mioto itawaka bila kutazamia, wala hakuna juhudi iwayo yote ya kibinadamu itakayoweza kuizima. Majumba ya kifalme ya duniani humu yatafagiliwa mbali katika ukali wa ndimi za mioto hiyo. Ajali katika njia za reli zitazidi kuongezeka mara kwa mara; kiwewe, migongano, na vifo bila hata taarifa ya dakika moja vitatokea katika njia zote kuu za usafiri. Mwisho umekaribia, mlango wa rehema [karibu] unafungwa. Hebu na tumtafute Mungu maadamu anapatikana, tumwite maadamu yu karibu!" MYP 89,90.

(9) "Pambano la Kuogofya Mno ambalo Halijapata Kushuhudiwa." "Pambano ambalo limetufikia sisi litakuwa la kuogofya mno ambalo halijapata kushuhudiwa." 7T 407.

(10) "Pambano la Kutisha." "Shetani anayakusanya majeshi yake; je! sisi kila mmoja peke yake tumejiweka tayari kukabiliana na pambano la kutisha ambalo li mbele yetu sasa? Je! tunawatayarisha watoto wetu kwa hatari hiyo kubwa?" AH 186.

(11) "Jaribio Kuu." "Endapo waumini wa ile kweli hawategemezwi na imani yao katika siku hizi za amani linganifu, ni kitu gani, basi, kitakachowainua juu wakati ule wa jaribio kuu utakapokuja na amri kutangazwa dhidi ya wale wote ambao watakataa kuiabudu sanamu ile ya mnyama, wala kuipokea alama yake juu ya vipaji vya nyuso zao au katika mikono yao? Kipindi hicho cha kutisha hakiko mbali. Badala ya kuwa dhaifu na kusitasita, watu wa Mungu wangekuwa wanakusanya nguvu zao na ujasiri kwa ajili ya wakati huo wa taabu." 4T 251.

(12) "Hofu Kuu." "Uasi karibu sana umefikia kipeo chake. Machafuko yamejaa duniani, na hofu kuu karibu sana itawajia wanadamu. Mwisho umekaribia sana." 8T 28.

3. Je, wakazi wa mbinguni wana habari kuhusu pambano letu linalokuja?

"Malimwengu yote yanaangalia kwa shauku isiyoelezeka kuiona kazi hii ya mwisho ya kufungia pambano kuu kati ya Kristo na Shetani." 5T 526.

4. Je, sehemu kubwa ya wakazi wa dunia hii wana habari juu ya matukio yaliyo karibu kutokea?

a. "Sisi tunaoijua kweli tungekuwa tunajiweka tayari kwa kile kitakachoupata ulimwengu huu hivi karibuni kama mshangao mkubwa mno kwao." 8T 28; 7BC 911.

b. "Wakristo wangekuwa wanajiandaa kwa kile kitakachoupata ulimwengu huu hivi karibuni kama mshangao mkubwa mno kwao, na maandalizi hayo wangeyafanya kwa njia ya kujifunza Neno la Mungu kwa bidii na kujitahidi kuyafanya maisha yao kupatana na amri zake [kumi].... Mungu anataka pawepo na uamsho na matengenezo." PK 626.

5. Je, sisi kama Waadventista Wasabato tunaitambua kweli kweli hatari iliyo mbele yetu?

a. " 'Wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo,' hivi punde utakuja juu yetu; tutahitaji uzoefu ambao hatunao sasa, na ambao wengi ni wavivu mno kuupata. Mara nyingi ndivyo mambo yalivyo ya kwamba taabu inayotarajiwa huonekana kuwa ni kubwa kuliko ilivyo hasa; lakini jambo hilo si

kweli kuhusu hatari kubwa iliyo mbele yetu. Maelezo ya wazi kabisa hayawezi kukifafanua kiwango cha ukubwa wa mateso hayo." GC 622.

b. "Sisi tuko ukingoni kabisa mwa wakati ule wa taabu, na mifadhaiko ambayo haijapata kuingia katika mawazo yetu i mbele yetu." 9T 43.

6. Je, yawezekana kwa Wakristo kutojiweka tayari kwa taabu ile inayokuja, ijapokuwa wao wamepata maonyo ya nyuma? Marko 8:31,32; 9:31; 10:32-34; Mathayo 26:56; Luka 24:6-8.

7. Kwa nini wanafunzi wake walikuwa hawajajiweka tayari kabisa?

a. "Hawakuweza kulistahimili wazo la kwamba yeye ambaye matumaini yao yote yalikuwa yamejengwa juu yake angeweza kuteseka na kufa kifo cha aibu sana. Maneno ambayo walihitaji kuyakumbuka yalikuwa yamefutika katika mawazo yao; na wakati wa kujaribiwa ulipofika, uliwakuta hawajawa tayari. Kifo cha Yesu kikayavunjilia mbali matumaini yao yote kana kwamba alikuwa hajawaonya mapema." GC 594.

b. "Petro hakuwa na hamu ya kuuona msalaba katika kazi yake Kristo." DA 415.

8. Je, Bwana ametupa muhtasari ulio wazi wa matukio yanayoambatana na kufungwa kwa mlango wa rehema?

a. "Matukio yale yanayoambatana na kufungwa kwa mlango wa rehema na kazi ile ya maandalizi kwa ajili ya wakati wa taabu, vimeonyeshwa kwa wazi. Makundi na makundi ya watu hawana ufahamu wo wote [hawajui] kuhusu kweli hizi za maana sawa na vile ambavyo zingekuwa hazijapata kufunuliwa kwao kamwe." GC 594.

b. "Amepewa ramani inayoonyesha kila alama ya njia katika safari yake ya kwenda mbinguni, wala isingempasa kukisia kitu cho chote." GC 598.

c. "Katika historia tunapaswa kuona utimilizo wa unabii,kujifunza mkono wa Mungu unavyofanya kazi katika matapo (movements) makubwa ya matengenezo, na kuelewa maendeleo ya matukio katika kuyakusanya mataifa kwa vita ile ya mwisho katika pambano lile kuu." MH 442; 8T 307.

9. Je, hii ina maana kwamba tunaweza kuelewa kwa undani elezo moja moja la matukio hayo yanayotarajiwa kabla hayajatokea?

a. "Alama ya Mnyama ni sawa kabisa na vile ilivyobainishwa tayari. Si yote kuhusu suala hilo yamefahamika, wala yataweza kufahamika mpaka hapo mbingu zitakapokunjwa kama ukurasa." 6T 17; 8T 159.

b. "Mengi juu ya mambo hayo yameonyeshwa kwangu, lakini mimi naweza kutoa maelezo machache tu kwenu. Enendeni kwa Mungu ninyi wenyewe, ombeni mwelimishwe na mbingu, ili mpate kujua ya kwamba mnaijua hasa kweli ni nini, ili uwezo ule wa Shetani ufanyao miujiza utakapodhihirishwa, kisha yule adui akawajia kama malaika wa nuru, mpate kupambanua kati ya

miujiza ya kweli ya Mungu na miujiza ya bandia [uongo] ya mamlaka zile za giza." RH, 12-24-1889, uk.3.

10. Je, ni muhimu jinsi gani kwetu kujifunza unabii ule unaohusu siku hizi za mwisho?

a. "Tunapokaribia mwisho wa kufungwa kwa historia ya ulimwengu huu, unabii ule unaohusu siku hizi za mwisho unataka hasa tuufanyie utafiti wetu." COL 133.

b. "Wangepaswa kuyajua mambo yale ambayo hayana budi kutokea kabla ya kuifunga historia ya ulimwengu huu. Mambo hayo yanahusika na usitawi wetu wa milele, na waalimu pamoja na wanafunzi wao wangeyaangalia kwa makini zaidi." 6T 129.

c. "Kisha mimi nikamwona malaika yule wa tatu. Malaika aliyeandamana nami akasema, 'Kazi yake ni ya kutisha. Ujumbe wake ni wa kuogofya. Huyo ndiye malaika anayechagua ngano kutoka katika magugu, na kuitia muhuri, au kuifunga, ngano hiyo tayari kwa kuwekwa katika ghala ile ya mbinguni. Mambo hayo yangejaa katika mawazo yetu yote, yaani, yangeyavuta mawazo yetu yote.' " EW 118.

d. "Katika majira ya usiku maneno haya yalinenwa kwangu: 'Waagize waalimu katika shule zetu kuwatayarisha wanafunzi wao kwa kile kinachoujia ulimwengu.' " FE 526,527.

e. "Lakini iko siku aliyoiweka Mungu kwa ajili ya kufungwa kwa historia ya ulimwengu huu: 'Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja.' Unabii huo unatimia haraka sana. Mengi, mengi sana yangeweza kusemwa juu ya masomo haya ya maana sana." FE 335.

f. "Walinzi na wapaze sauti zao na kutoa ujumbe huu ambao ndio ukweli wa leo. Hebu na tuwaonyeshe watu mahali tulipofikia katika historia ya unabii." 5T 516.

g. "Jitihada kubwa zingefanyika kuliweka somo hili mbele ya watu. Ukweli huu wa kutisha unapaswa kuwekwa sio tu mbele ya watu wa ulimwengu huu, bali pia mbele ya makanisa yetu , ya kwamba siku ya Bwana itakuja ghafula, bila kutazamia. Onyo la kutisha la unabii huu ni kwa kila mtu. Asiwepo hata mmoja anayejisikia kuwa yu salama mbali na hatari ile ya kugutushwa. Tafsiri ya unabii ya mtu awaye yote [isiyopatana na Maandiko] isiwanyang'anye uhakika wa kuyajua matukio ambayo yanaonyesha kwamba tukio hilo kuu limekaribia sana." FE 336.

11. Sisi tumeonywa tusifanye kitu gani hasa?

a. "Uko wakati wa taabu unaowajia watu wa Mungu, lakini hatupaswi kuuweka mbele ya watu daima, na kuwafanya [kusababisha] waweze kupata wakati wao wa taabu mapema. Kupepetwa kuko miongoni mwa watu wa Mungu, lakini huo sio ukweli wa leo wa kuyapelekea makanisa yetu." 1SM 180; 2SM 13.

b. "Ziko nyakati za dhoruba mbele yetu, lakini tusitamke neno hata moja liletalo mashaka au kukatisha tamaa [kwa waumini]." ChS 136.

12. Tukiwa tumeizingatia hatari kubwa inayokuja, tungekuwa tunafanya nini hivi sasa?

"Kama Mungu amepata kunena kupitia kwangu, basi, wakati utakuja mtakapopelekwa mbele ya mabaraza, na kila msimamo wa ile kweli mnayoishikilia utakosolewa kwa ukali sana. Muda ambao wengi sana wanauacha kupotea bure ungetumika kulitii agizo ambalo Bwana ametupa la kujiweka tayari kwa hatari kubwa inayokuja." 5T 717.

13. Ni akina nani pekee watakaosimama imara katika Pambano Kuu la mwisho?

a. "Hakuna watakaoweza kusimama katika Pambano lile Kuu la mwisho isipokuwa wale walioiimarisha mioyo yao kwa zile kweli za Biblia." GC 593.

b. "Jifunzeni Biblia zenu kwa namna ambayo hamjapata kamwe kujifunza kwa siku za nyuma. Msipoinuka na kukifikia kiwango kile cha juu cha utakatifu katika maisha yenu ya kidini, hamtakuwa tayari kwa kufunuliwa [kuja] kwake Bwana wetu." 5T 717.

c. "Tunazikaribia nyakati zile za dhoruba.... Kila msimamo wa imani yetu utachunguzwa; na kama sisi si wanafunzi wakamilifu wa Biblia, tulioimarishwa, tuliotiwa nguvu, na kutulia [katika kweli], basi, hekima ya wakuu wa ulimwengu huu itatufanya sisi tupotee." 5T 546.

d. "Ni wale tu ambao wamekuwa wanafunzi wenye bidii wa Maandiko, na ambao wameipenda hiyo kweli [wameishi kulingana na hiyo kweli], watakaolindwa kutokana na madanganyo yenye nguvu yatakayouteka ulimwengu wote." GC 625.

## SURA YA 2

## MUUNGANO WA MAKANISA

1. Je, kila dhehebu la Kiprotestanti katika nchi ya Amerika litaingia katika Muungano wa Makanisa unaokuja?

"Makanisa Makuu ya Marekani, yatakapoungana katika mafundisho yale wanayoshirikiana pamoja, watakapoishawishi serikali yao kuyatia nguvu kisheria maagizo yao na kuzipa ruzuku taasisi zao, hapo ndipo Amerika ya Kiprotestanti itakuwa imeunda sanamu ya utawala wa kidini wa Roma, na adhabu ya serikali haitaweza kuepukwa kutolewa juu ya wale wasioafiki." GC 445.

2. Kwa msingi gani makanisa ya Kiprotestanti hatimaye yataweza kuungana?

"Tofauti kubwa ya imani inayojitokeza katika makanisa ya Kiprotestanti inaangaliwa na wengine kama ni ushahidi wa kutosha kuonyesha kwamba hakuna juhudi yo yote inayoweza kufanywa ili kupata umoja utakaolazimishwa. Lakini kwa miaka mingi, katika makanisa yenye imani ya Kiprotestanti, pamekuwa na maoni yenye nguvu, yanayoendelea kukua ambayo yanapendelea muungano uwepo uliojengwa juu ya mafundisho yale wanayoshirikiana pamoja. Kuupata muungano kama huo, mjadala wa mafundisho yale ambayo wote walikuwa hawaafikiani ----- haidhuru yawe ya maana jinsi gani kutokana na msimamo wa Biblia ----- itabidi utupiliwe mbali." GC 444.

3. Ni mafundisho gani makuu mawili yenye makosa ambayo makanisa hayo yameyashikilia kwa pamoja?

"Kwa njia ya makosa makuu mawili ----- imani kwamba roho haifi, na utakatifu wa Jumapili ----- Shetani atawaleta watu chini ya madanganyo yake. Wakati lile la kwanza linaweka msingi wa imani ya mizimu (spiritualism), lile la pili linaleta mapatano ya kushirikiana na Roma." GC 588.

4. Je, Uprotestanti hatimaye utaweza kuungana na Ukatoliki?

a. "Neno la Mungu linafundisha kwamba matukio hayo [ya kuikandamiza Sabato] yatarudiwa wakati ule Wakatoliki wa Roma na Waprotestanti watakapoungana kwa lengo la kuitukuza Jumapili." GC 578.

b. "Kwa jinsi gani Kanisa la Roma linaweza kujinasua kutokana na shtaka la kuabudu sanamu hatuwezi kuelewa.... Na hiyo ndiyo dini ambayo Waprotestanti wanaanza kuiangalia kwa upendeleo mkubwa sana, na ambayo hatimaye itaungana na Uprotestanti." RH, 6-1-1886, uk.338.

c. "Maadam muda wa majaribio bado ungalipo, itapatikana nafasi kwa mwinjilisti wa vitabu kufanya kazi yake. Madhehebu za dini zitakapoungana na upapa ili kuwatesa watu wa Mungu, basi, mahali pale ambapo uhuru wa dini utakuwapo patafunguliwa kwa uinjilisti wa vitabu." 6T 478.

5. Je, kutakuwa na muungano wa makanisa au muungano katika utendaji wake?

a. "Ulimwengu unaojidai kuwa ni wa Kiprotestanti utaungana kwa mapatano na yule mtu wa dhambi (kuasi), hapo ndipo kanisa na ulimwengu vitakuwa katika mwafaka potovu." 7BC 975.

b. "Uroma katika Ulimwengu ule wa Zamani [Ulaya], na Uprotestanti Asi katika ule Mpya [Marekani], watafuata njia ile ile moja katika kuwashughulikia wale wanaoziheshimu amri zote [kumi] za Mungu." GC 616.

6. Je, Roma itabadilika au Uprotestanti ndio utakaobadilika ili kufanya kuunganika tena kuwezekane?

a. "Muungano huo, kwa hali yo yote, hautafanyika kutokana na badiliko katika Ukatoliki; kwa maana Roma haibadiliki kamwe. Inadai kwamba haiwezi kukosea. Ni Uprotestanti, basi, utakaobadilika. Kupokea mawazo mapana yaliyo huru kwa upande wake [Uprotestanti] kutauleta mahali ambapo utaushika kwa nguvu mkono wa Ukatoliki. 'Biblia, Biblia, ndiyo msingi wa imani yetu,' kilikuwa ndicho kilio cha Waprotestanti katika siku zile za Luther, wakati Wakatoliki walipopaza sauti zao, wakisema, 'Mababa, Desturi, Mapokeo.' Siku hizi Waprotestanti wanaona ni vigumu kuyathibitisha mafundisho yao kutoka katika Biblia, hata hivyo, hawana ujasiri wa kimaadili kuweza kuipokea kweli ambayo inaambatana na msalaba; kwa hiyo, kwa kasi wanaufuata msimamo wa Ukatoliki.... Naam, Waprotestanti wa karne ya kumi na tisa wanakaribia kwa kasi kwa Wakatoliki katika kukosa uaminifu wao kuhusu Maandiko." RH, 6-1-1886, uk.338.

b. "Waprotestanti wa Marekani watakuwa mstari wa mbele katika kuinyosha mikono yao juu ya ghuba ili kuushika mkono ule wa Imani ya Mizimu; kisha watainyosha juu ya shimo kubwa lenye kilindi kirefu [bahari] kushikana mikono na Mamlaka ile ya Roma; hapo ndipo, chini ya uongozi wa muungano huo wa utatu [Uprotestanti, Umizimu, na Ukatoliki], nchi hii [ya Marekani] itafuata katika nyayo za Roma kwa kuikanyaga chini ya miguu yake haki ya mtu ya kuamini kama dhamiri yake inavyotaka." GC 588.

c. "Uprotestanti utakapounyosha mkono wake ng'ambo ya ghuba kuushika mkono wa Mamlaka ya Roma, utakapounyosha juu ya shimo kubwa lenye kilindi kirefu kushikana mikono na Imani ya Mizimu [toka Mashariki ya Mbali - India, China, n.k.], hapo ndipo nchi yetu [Marekani], chini ya uongozi wa muungano huo wa utatu, itakapokuwa imeikataa kila kanuni ya Katiba yake kama Serikali ya Kiprotestanti na ya Jamhuri, na kuiweka sheria inayotangaza uongo na madanganyo ya upapa, ndipo sisi tutaweza kujua ya kwamba wakati umewadia kwa utendaji wa miujiza ya ajabu ya Shetani na ya kwamba mwisho u karibu." 5T 451.

d. "Uprotestanti utaipa mkono wa ushirika Mamlaka ile ya Roma. Ndipo itapitishwa sheria dhidi ya Sabato ya Uumbaji wa Mungu, kisha ndipo Mungu naye atafanya 'kazi yake ya ajabu' katika nchi [ulimwengu]." 7BC 910.

e. "Taifa letu [la Marekani] litakapozikataa kanuni za serikali yake hata kuweza kutunga Amri ya Jumapili, kwa tendo hilo Uprotestanti utakuwa umeshikana mikono na Upapa...." 5T 712.

7. Je, Upapa hatimaye utakuwa na nguvu kiasi gani hapa Amerika?

"Waprotestanti... wanafungua mlango kwa upapa katika Amerika ya Kiprotestanti ili upate kushika tena hatamu zake za utawala ambazo umezipoteza katika Ulimwengu ule wa Zamani [Ulaya - tangu 1798]." GC 573.

8. Ni nani atakayewaongoza watu hao watakapoungana ili kuwapinga wafuasi wa Mungu?

"Tunapoikaribia hatari kubwa ile ya mwisho, ni jambo la maana sana kwetu sisi kwamba amani na umoja viwepo miongoni mwa vyombo vya Bwana. Ulimwengu umejawa na dhoruba na vita na ugomvi. Hata hivyo, chini ya kiongozi mmoja ---- Mamlaka ya Kipapa ----- watu wataungana kumpinga Mungu kwa njia ya mashahidi wake. Muungano huo umeimarishwa kabisa na yule Mwasi Mkuu [Shetani]." 7T 182.

9. Kusema kweli, ni nani hasa anayesimama nyuma ya Papa?

"Mmoja amesondwa kidole katika unabii kuwa ni mtu wa dhambi (kuasi). Yeye ndiye mwakilishi wa Shetani.... Hapa yupo mtu aliye msaidizi mkuu wa Shetani, aliye tayari kutekeleza kazi ile aliyoianzisha Shetani kule mbinguni, ya kujaribu kuirekebisha sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Na ulimwengu huo wa Kikristo umeziunga mkono juhudi zake kwa kumpokea mtoto huyo wa Upapa ----- yaani, amri hiyo ya Jumapili." 7BC 910; RH, 3-9-1886, uk. 146.

10. Je, tungekuwa tukifanya nini sasa, ili kukabiliana kwa ufanisi na upinzani wa jamii hiyo iliyoungana pamoja ya Mataifa hayo ya Kikristo?

"Ulimwengu wote uko kinyume nasi, makanisa yale yanayopendwa sana na watu yako kinyume nasi, sheria za nchi hivi punde zitakuwa kinyume nasi. Kama ulipata kuwako wakati ambapo watu wa Mungu wangeshikamana kwa karibu sana, ni sasa." 5T 236.

## SURA YA 3

## AMRI YA JUMAPILI KWA TAIFA ZIMA

1. Biblia yasemaje juu ya Amerika ya Kiprotestanti itakavyoisujudu Mamlaka ile ya Kikatoliki ya Roma? Ufu.13:11-17.

2. Je, unabii huo utatimizwa lini?

a. "Unabii wa Ufunuo 13 unatangaza kwamba mamlaka ile iliyowakilishwa na mnyama aliye na pembe kama za mwana-kondoo ita"ifanya dunia na wote wakaao ndani yake wausujudu upapa ----- ulioonyeshwa hapo kama mnyama "mfano wa chui."... Unabii huo utatimizwa wakati ule Marekani itakapotunga amri ya kuitunza Jumapili, tendo ambalo Roma inadai kuwa ni kuutambua ukuu wake kwa namna ya pekee." GC 578,579.

b. "Kulazimisha utunzaji wa Jumapili kwa upande wa Uprotestanti ni sawa na kulazimisha ibada ya upapa." GC 448.

3. Shinikizo la kuitungia amri [sheria] Jumapili litatoka wapi?

a. "Viongozi wakuu wa kanisa na serikali wataungana ili kuwahonga, kuwashawishi, au kuwalazimisha watu wa tabaka zote wapate kuiheshimu Jumapili. Kule kukosekana kwa mamlaka ya Mungu [katika Biblia] kutafanya zipate kutungwa amri kali za ukandamizaji. Rushwa katika ngazi za kisiasa inaharibu moyo ule wa kupenda haki na kuijali kweli; hata katika Amerika iliyo huru, watawala na watunga sheria, ili kupata upendeleo wa umma, watakubali madai ya wengi wanaopendelea iwepo amri [sheria] ya kulazimisha utunzaji wa Jumapili." GC 592 (Angalia pia 4SP 410).

b. "Ili kujipatia hali ile ya kupendwa na watu wengi na haki ya kuweza kuteuliwa, watunga sheria watakubaliana na madai ya kuwapo kwa amri ya Jumapili." 5T 451.

c. "Watunga sheria watakubaliana na madai ya kuwapo kwa amri za Jumapili." PK 606.

d. "Waprotestanti wa Marekani watakuwa mstari wa mbele katika kuinyosha mikono yao juu ya ghuba ili kuushika mkono wa Imani ya Mizimu; tena, watainyosha juu ya shimo kubwa lenye kilindi kirefu kushikana mikono na Mamlaka ile ya Roma; hapo ndipo, chini ya uongozi wa muungano huo wa utatu, nchi hii itafuata katika nyayo za Roma kwa kuikanyaga chini ya miguu yake haki ya mtu kuamini kama dhamiri yake inavyotaka." GC 588.

e. "Iwapo watu wanaweza kushawishika kupendelea iwepo amri ya Jumapili, basi, wachungaji na mapadre wanakusudia kutumia nguvu ya mvuto wao wa pamoja katika kujipatia marekebisho ya dini katika Katiba ya nchi, na kulilazimisha Taifa zima [la Marekani] kuitunza Jumapili." RH, Extra 12-24-1889, uk.2.

4. Je! hao wanaoitetea Amri ya Jumapili wanatambua wanalolitenda?

a. "Pana watu wengi, hata miongoni mwa wale walio katika shughuli hiyo ya kutaka itungwe Amri ya Jumapili, ambao wamepofushwa macho yao wasiweze kuona matokeo yatakayofuata baada ya kitendo hicho kutekelezwa. Hawaoni ya kwamba wanaupiga rungu uhuru wa dini moja kwa moja. Wako wengi ambao hawajapata kuyaelewa kamwe madai ya Sabato ya Biblia na msingi wa uongo ambao Amri ya Jumapili inaukalia." 5T 711. b. "Wanafanya kazi hiyo wakiwa vipofu. Hawaoni ya kwamba kama Serikali yao ya Kiprotestanti inaziachilia mbali kanuni zilizowafanya kuwa Taifa huru, linalojitegemea, na kwa njia ya kutunga sheria wanaingiza katika Katiba ya Nchi, kanuni ambazo zitatangaza uongo wa upapa na madanganyo ya upapa, watakuwa wanajitumbukiza katika utawala wa hofu wa Roma wa Zama zile za Giza." RH, Extra 12-11-1888, uk.4.

c. "Kuna nguvu ya Kishetani inayoliendesha tapo [kundi] hilo la Jumapili, ila imejificha. Hata watu wale waliojiingiza katika kazi hiyo, wamepofushwa macho yao wasiweze kuona matokeo yatakayofuata baada ya kazi ya tapo lao kukamilika." RH 1-1-1889, uk.1; 7BC 975.

5. Ni nani hasa aliye mwanzilishi mwamba mkuu wa kuitungia amri Jumapili?

a. "Hakuna hatua yo yote iliyochukuliwa katika kuitukuza Sabato hiyo ya sanamu, na kuileta Jumapili ipate kutunzwa kwa kuitungia amri [sheria], isipokuwa ni yule Shetani aliye nyuma yake, na ndiye amekuwa mtendaji mkuu." 7BC 977.

b. "Bunge litakapotunga sheria ambazo zinaitukuza siku ya kwanza ya juma, na kuiweka mahali pa siku ile ya saba, hapo ndipo hila ya Shetani itakuwa imekamilika." 7BC 976.

c. "Sabato hiyo ya uongo [Jumapili] italazimishwa kwa njia ya kuitungia sheria [amri] ya ukandamizaji. Shetani na malaika zake wako macho sana, nao wanashughulika vibaya sana, wakifanya kazi kwa nguvu na ustahimilivu kupitia kwa wakala wao wa kibinadamu ili kulitimiza kusudi lake la kufutilia mbali katika mioyo ya watu maarifa ya kumjua Mungu." 7BC 985; RH 12-13-1892.

6. Je, Amri hiyo ya Jumapili inaonyesha dharau juu ya nani?

"Juhudi zaidi ya wazi itafanyika kuitukuza sabato hiyo ya uongo, na kumwonyesha dharau Mungu Mwenyewe kwa kuibadili siku ile aliyoibariki na kuitakasa. Sabato hiyo ya uongo [Jumapili] italazimishwa kwa sheria ya ukandamizaji." 7BC 985.

7. Je, tutazamie kuziona sheria za Jumapili katika majimbo yanayojitawala (states) fulani fulani tu au Bunge la Marekani litachukua hatua ya kuitunga sheria hiyo[kwa Taifa zima]?

a. "Nchi yetu [ya Marekani] imeingia hatarini. Wakati unakaribia ambapo watunga sheria [Wabunge] wake watakapozikataa kabisa kanuni zile za Uprotestanti na kuunga mkono uasi wa Kanisa Katoliki. Watu hao ambao Mungu amewatendea maajabu makubwa sana, akiwatia nguvu kulitupilia mbali lile kongwa linaloumiza sana la upapa, kwa njia ya sheria ya taifa zima wataitia nguvu nyingi imani potofu ya Roma, na kwa njia hiyo kuuamsha utawala ule wa mabavu ambao unangojea tu uguswe ili uanze tena ukatili wake na udikteta." 4SP 410 (1884); ST, 7-17-1907, uk.1907, uk.7.

b. "Tunaona ya kwamba juhudi zinafanywa ili kutuwekea vizuizi katika uhuru wetu wa dini. Hoja ya Jumapili sasa inafikia viwango vikubwa. Marekebisho ya Katiba yetu ya nchi yanasisitizwa katika Bunge la Marekani, na mara yatakapopatikana, basi, ni lazima ukandamizaji utafuata." RH, 12-18-1888, uk.786 (Angalia pia 5T 711).

c. "Hivi karibuni kitatokea kipindi cha kusisimua sana kwa wote walio hai. Malumbano ya zamani yataanza tena; malumbano mapya yatazuka. Mandhari [picha] ya mambo yale yatakayotendwa kama maigizo katika dunia yetu bado hata hayajapata kuingia katika mawazo yetu. Shetani yuko kazini kupitia kwa mawakala wake wa kibinadamu. Wale wanaofanya juhudi ya kuibadilisha Katiba ya Nchi na kujipatia nafasi ya kutunga sheria inayolazimisha utunzaji wa Jumapili hawatambui hata kidogo matokeo yake yatakavyokuwa. Hatari kubwa imetukabili hivi sasa." 5T 753.

d. "Taifa letu litakapozikataa kabisa kanuni za Serikali yake hata kutunga sheria ya Jumapili, katika kitendo hicho Uprotestanti utakuwa umeshikana mikono na upapa." 5T 712.

e. "Hatari kubwa inawangojea watu wa Mungu. Karibu sana Taifa letu litajaribu kuwalazimisha wote kuitunza siku ya kwanza ya juma kama siku takatifu. Kwa kufanya hivyo, hawatakuwa na haya [aibu] kuwalazimisha wanadamu kinyume cha sauti ya dhamiri zao wenyewe ili kuitunza siku ambayo Taifa linaitangaza kuwa ndiyo Sabato."

RH, Extra 12-ll-1888, uk. 4.

e. "Sheria ya Mungu itakapobatilishwa, na uasi kuwa dhambi ya Taifa hili, hapo ndipo Bwana atakapotenda kazi kwa ajili ya watu wake." RH, Extra 12-11-1888, uk.3.

g. "Kwa agizo lile linalolazimisha [utunzaji wa] siku ile iliyowekwa na upapa kwa kukiuka sheria ya Mungu, Taifa letu litajitenga kabisa mbali na haki." 5T 451.

8. Je, Marekani litaendelea kuwa Taifa lililopata upendeleo wa Mungu baada ya kuchukua hatua ya kisheria na kuiweka kando Sheria ya Mungu?

a. "Watu wa Marekani ni watu waliopata upendeleo; lakini watakapouwekea vizuizi uhuru wa dini, kuachilia mbali Uprotestanti, na kuunga mkono upapa, hapo ndipo kikombe chao cha maovu kitakuwa kimejaa, na 'uasi wa Taifa' hili utaandikwa katika vitabu vile vya mbinguni." RH, 5-2-1893, uk.274.

b. "...Kwa hiyo, uasi huo na uwe ishara kwetu sisi ya kwamba kikomo cha uvumilivu wa Mungu kimefikiwa, ya kwamba kikombe cha maovu ya Taifa letu kimejaa...." 5T 451.

9. Je, matokeo ya uasi wa Taifa letu hili yatakuwaje?

a. "Wakati unakuja ambapo sheria ya Mungu, kwa maana ya pekee, itabatilishwa katika nchi yetu. Watawala wa Taifa letu, kwa njia ya kutunga sheria Bungeni, wataitia nguvu sheria hiyo ya Jumapili, na kwa njia hiyo watu wa Mungu wataingia katika hatari kubwa sana. Taifa letu, katika vikao vyake vya Bunge, litakapotunga sheria za kuzibana dhamiri za watu kuhusu haki zao za kidini, likilazimisha utunzaji wa Jumapili, na kutumia nguvu ya ukandamizaji dhidi ya wale wanaoitunza Sabato ya Siku ya Saba, hapo ndipo sheria ya Mungu, kwa makusudi na nia kamili, itakuwa imebatilishwa katika nchi yetu; na uasi wa Taifa hili utafuatiwa na maangamizi yaTaifa hili." RH, 12-18-1888, uk. 785; 7BC 977.

b. "Ni katika wakati ule wa uasi wa Taifa hili, wakiwa wanazitekeleza sera za Shetani, watawala wa nchi hii watakapojipanga wenyewe upande wa mtu yule wa dhambi, ----- hapo ndipo, kikombe chao cha maovu kitakuwa kimejaa; uasi wa taifa hili ni ishara ya maangamizi ya Taifa hili." GCB 1891, uk.259.

c. "Matokeo ya uasi huu yatakuwa ni maangamizi ya Taifa hili." RH, 5-2-1893, uk. 274.

d. "Waprotestanti watashughulika sana na watawala wa nchi hii kutunga sheria zitakazourejesha ukuu alioupoteza mtu yule wa dhambi, anayeketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ndiye Mungu. Kanuni za Ukatoliki wa Roma zitahifadhiwa na kulindwa na Serikali hii. Uasi huo wa Taifa hili utafuatiwa kwa haraka sana na maangamizi ya Taifa hili.... Serikali za Kiprotestanti zitaifikia njia ngeni, nyembamba ipitayo katikati ya milima. Wataongolewa na dunia. Pia, katika kujitenga kwao na Mungu, watafanya kazi kuufanya uongo na uasi wao kwa Mungu viwe ndiyo sheria ya Taifa." RH, 6-15-1897, uk.370.

e. "Makanisa ya Kiprotestanti yatakapoungana na mamlaka za kidunia kuiimarisha dini hiyo ya uongo, ambayo kwa kuipinga mababu zao walistahimili mateso makali sana, hapo ndipo sabato ya papa itakapolazimishwa kwa mamlaka iliyoungana ya kanisa na serikali [dola]. Patakuwa na uasi wa Taifa, ambao utaishia tu katika maangamizi ya Taifa hili. Ev 235 (1899).

f. "Makanisa ya Kiprotestanti yatakapotafuta msaada kutoka kwa mamlaka za kidunia, hivyo kuiga mfano wa kanisa lile asi, ambalo kwa kulipinga babu zao walistahimili mateso makali sana, hapo ndipo patakuwa na uasi wa Taifa ambao utaishia tu katika maangamizi ya Taifa hili." 4SP 410 (1884); ST 7-17-1907, uk. 7.

g. "Makanisa ya Kiprotestanti yatakapoungana na mamlaka za kidunia kuiimarisha dini hiyo ya uongo,... dola hii itakapotumia mamlaka yake kulazimisha amri hizo na kutoa ruzuku kwa taasisi za kanisa ----- hapo ndipo Amerika ya Kiprotestanti itakuwa imeunda sanamu ya upapa, na kutakuwa na uasi wa Taifa ambao utaishia tu katika maangamizi ya Taifa hili."

ST, 3-22-1910; 7BC 976.

10. Je, Amerika ya Kiprotestanti itaiundaje sanamu ya mnyama?

a. "Makanisa makuu ya Marekani yatakapoungana katika mafundisho yale wanayoshirikiana pamoja, watakapoishawishi serikali kuyatia nguvu maagizo yao kisheria na kuzipa ruzuku taasisi zao, hapo ndipo Amerika ya Kiprotestanti itakuwa imeunda sanamu ya utawala [wa kidini] wa Roma, na adhabu ya serikali haitaweza kuepukwa kutolewa juu ya wale wasioafiki." GC 445 (Angalia pia 4SP 278).

b. "Katika tendo lile lile la kulazimisha wajibu wa kidini kwa kutumia mamlaka ya kidunia, makanisa yenyewe yangeunda sanamu ya mnyama; kwa hiyo, kulazimisha utunzaji wa Jumapili kule Marekani kungekuwa ndiko kulazimisha ibada ya mnyama na sanamu yake." GC 449.

11. Je, kulazimisha utunzaji wa Jumapili (kuunda sanamu ya mnyama) kule Marekani kutakuja baada au kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema?

a. "Bwana amenionyesha waziwazi ya kwamba sanamu ya mnyama itaundwa kabla ya mlango wa rehema kufungwa; maana hiyo ndiyo itakuwa jaribio kubwa kwa watu wake Mungu.... Hilo ndilo jaribio ambalo watu wa Mungu hawana budi kuwa nalo kabla hawajatiwa muhuri." 7BC 976.

b. "Kwa agizo lile linalolazimisha siku iliyowekwa na upapa, Taifa letu litajitenga kabisa mbali na haki. Uprotestanti utakapounyosha mkono wake ng'ambo ya ghuba kuushika mkono wa Mamlaka ya Roma, utakapounyosha juu ya shimo kubwa lenye kilindi kirefu kushikana mikono na Imani ya Mizimu, nchi yetu, chini ya uongozi wa muungano huo wa utatu, itakapokuwa imeikataa kila kanuni ya Katiba yake kama Serikali ya Kiprotestanti na ya Jamhuri, na kutunga sheria inayotangaza uongo na madanganyo ya upapa, hapo ndipo tunaweza kujua kwamba wakati umewadia kwa utendaji wa miujiza ya ajabu ya Shetani na ya kwamba mwisho u karibu.

Kama vile kukaribia kwa majeshi yale ya Kirumi kulivyokuwa ishara ya maangamizi ya Yerusalemu yaliyokuwa karibu sana kwa wanafunzi wake wale, hivyo ndivyo uasi huo unavyoweza kuwa ishara kwetu kwamba kikomo cha uvumilivu wa Mungu kimefikiwa, na ya kwamba kikombe cha maovu ya Taifa letu kimejaa, na ya kwamba malaika yule wa rehema karibu ataruka kwenda zake, asirudi tena kamwe." 5T 451.

c. "Njozi za Anna zinaweka kuundwa kwa sanamu ya mnyama baada ya kufungwa kwa mlango wa rehema. Hivyo sivyo mambo yalivyo. Unajidai kuziamini shuhuda; hebu na zikuweke sawa katika suala hili. Bwana amenionyesha mimi waziwazi kwamba sanamu ya mnyama itaundwa kabla ya mlango wa rehema kufungwa; maana hiyo ndiyo itakuwa jaribio kuu kwa watu wa Mungu, ambalo kwalo umilele wao utaamuliwa." 2SM 81.

12. Kwa kuzingatia matarajio ya kutungwa kwa Amri ya Jumapili, Waadventista wanaokaa katika miji mikubwa wanasihiwa kufanya nini upesi iwezekanavyo?

a. "Anataka sisi tuishi mahali palipo na nafasi ya kutosha. Watu wake hawapaswi kusongamana katika miji mikubwa. Anawataka kwenda na familia zao nje ya miji mikubwa, ili wapate kujiandaa vizuri kwa uzima ule wa milele. Kitambo kidogo tu watatakiwa kuiacha miji mikubwa.... Tokeni katika miji mikubwa upesi iwezekanavyo...." 2SM 356.

b. "Hatari kubwa inakuja haraka kuhusiana na utunzaji wa Jumapili.... Kama kwa mpango wa Mungu tunaweza kujipatia mahali palipo mbali kutoka katika miji mikubwa, basi, Bwana atatutaka sisi kufanya hivyo. Kuna nyakati za taabu mbele yetu.... Nauona umuhimu upo wa kuharakisha kuyaweka mambo yote tayari kwa hatari hiyo." 2SM 359.

13. Sheria za Jumapili zitatoa onyo gani kwa Waadventista ambao bado wanaendelea kukaa katika miji mikubwa?

"Kama kuzingirwa kwa Yerusalemu na majeshi ya Warumi kulivyokuwa ishara ya kukimbia kwa Wakristo wale wa Yudea, ndivyo kutwaa madaraka kwa upande wa Taifa letu katika kutoa amri iie inayolazimisha sabato ya papa kutakavyokuwa onyo kwetu. Basi huo utakuwa ndio wakati wa kuondoka kwenye miji midogo kwenda kwenye makazi ya upweke mahali pa faragha miongoni mwa milima." 5T 464,465.

14. Je, tutazitumiaje siku za Jumapili baada ya Amri za Jumapili kupitishwa?

a. "Waadventista Wasabato walitakiwa kuonyesha hekima yao kwa kujizuia kufanya kazi zao za kawaida katika siku ile, wakiitumia kwa shughuli za kimishonari.

"Kuzipinga Amri za Jumapili kutawaimarisha tu washupavu wa dini wanaojaribu kuzilazimisha kwao ili kuongeza mateso yao. Msiwape nafasi yo yote kuwaita ninyi kuwa wavunjaji wa sheria hizo.... Mtu hapokei alama ya mnyama kwa sababu anaonyesha kwamba anatambua hekima ya kutunza amani kwa kujizuia kufanya kazi inayoleta uvunjaji wa sheria hizo....

"Wakati wo wote inapowezekana, endesheni huduma za kidini katika siku hiyo ya Jumapili.... Waalimu wetu katika shule zetu waitumie Jumapili kwa shughuli za kimishonari." 9T 232,233.

b. "Msifanye maandamano yo yote siku ya Jumapili kupinga sheria hiyo." 9T 235.

c. "Wakati mmoja wale waliokuwa wasimamizi wa shule yetu ya Avondale waliniuliza mimi wakisema: 'Tufanye nini? Mapolisi wanaoilinda sheria hiyo wameagizwa kuwakamata wale wanaofanya kazi siku ya Jumapili.' Mimi niliwajibu hivi: 'Litakuwa ni jambo rahisi sana kuliepuka tatizo hilo. Itoeni siku ya Jumapili kwa Bwana kama siku ya kufanya kazi ya kimishonari. Nendeni nje na wanafunzi wenu kuendesha mikutano mahali mbalimbali, na kufanya kazi ya uganga. Watawakuta watu majumbani mwao, nao watakuwa na wakati mzuri sana wa kuifundisha ile kweli. Njia hii ya kuitumia Jumapili sikuzote inakubaliwa na Bwana." 9T 238.

d. "Tulipokuwa tunaishi mahali paitwapo Cooranbong, ambapo shule yetu ya Avondale imejengwa,... Hoja ya kufanya kazi Jumapili ilikuja kwetu kwa ajili ya kuitafakari. Ilionekana kana kwamba punde kamba zingetufunga sana kila upande hata tusiweze kufanya kazi yo yote siku ya Jumapili. Shule yetu ilikuwa katikati ya misitu, mbali na kijiji cho chote au kituo cha reli. Hakuna ye yote aliyekuwa anaishi karibu kiasi cha kutosha kutufanya tuingiwe na wasiwasi kwa njia iwayo yote kwa jambo lo lote ambalo tungeweza kulifanya. Hata hivyo, tulikuwa tunachunguzwa. Maofisa wa polisi walishurutishwa kuja kuangalia tulichokuwa tukifanya katika eneo lile la shule; nao walikuja hakika, lakini hawakuweza kuwaona wale waliokuwa wanafanya kazi. Imani yao na heshima yao kwa watu wetu ilikuwa imepatikana kutokana na kazi ile tuliyokuwa tumeifanya kwa wagonjwa katika jumuia ile kiasi kwamba hawakutaka kuingilia kati kazi yetu isiyokuwa na madhara yo yote ambayo sisi tuliifanya katika siku ya Jumapili.

"Wakati mwingine ndugu zetu walipotishiwa kuteswa, tena wakawa wanauliza kile ambacho wangeweza kufanya, niliwapa ushauri uo huo niliokuwa nimeutoa kujibu hoja ya kuitumia Jumapili kwa michezo. Niliwaambia, "Itumieni Jumapili kwa kufanya kazi ya kimishonari kwa ajili yake Mungu. Waalimu, nendeni pamoja na wanafunzi wenu.'...

"Waalimu katika shule zetu na waitumie Jumapili kwa shughuli za kimishionari." CT 459-551.

15. Je, mtazamo wetu leo uweje? Twawezaje kufanya kazi na kuomba?

a. "Hatufanyi mapenzi ya Mungu tunapokaa kimya tu, bila kufanya kitu cho chote kuuhifadhi uhuru wa dhamiri zetu. Maombi ya bidii, yenye kuleta matokeo yangekuwa yakipanda mbinguni ili janga hilo lipate kuahirishwa mpaka hapo tutakapoweza kuimaliza kazi ambayo imeachwa kwa muda mrefu sana. Hebu na pawe na maombi yanayotolewa kwa bidii sana, kisha na tufanye kazi kulingana na maombi yetu. Yaweza kuonekana kwamba Shetani anashinda na ya kwamba kweli imeshindwa na makosa [mafundisho potofu] na uongo;... Lakini Mungu angetutaka sisi kukumbuka alivyowatendea watu wake wa zamani kuwaokoa kutoka kwa maadui wao. Sikuzote amechagua upeo wa matatizo ili kuonyesha uweza wake, yaani, wakati ule ilipoonekana ya kuwa hakuna uwezekano wo wote wa kuokoka kutoka katika utendaji wa Shetani. Shida ya mwanadamu ni nafasi ya Mungu ya kutenda kazi yake." 5T 714.

b. "Tungejifunza kwa bidii Neno la Mungu, na kuomba kwa imani ili Mungu apate kuzizuia nguvu za giza; maana mpaka sasa ujumbe umekwenda karibu kwa watu wachache mno, na ulimwengu huu unapaswa kuangazwa kwa utukufu wake. Ukweli wa leo ----- amri za Mungu [kumi] na Imani ya Yesu ----- bado haujatangazwa kama unavyopaswa kutangazwa.... Yatupasa kuwa na msimamo thabiti ya kwamba sisi hatutaiheshimu siku ya kwanza ya juma kama sabato...." RH, Extra 12-24-1889, uk.2.

c. "Kwa miaka mingi tumekuwa tukiitazamia Amri ya Jumapili kutungwa katika nchi yetu; na sasa kwa vile tapo hilo liko juu yetu, tunauliza hivi, Watu wetu watafanya nini katika suala hili?... Tungemtafuta Mungu hasa ili watu wake wapewe neema na nguvu sasa. Mungu wetu yu hai; wala hatuamini kwamba wakati umefika kabisa ambao angeruhusu uhuru wetu uwekewe vizuizi. Nabii aliwaona malaika wanne wamesimama katika pembe nne za nchi, wakizizuia pepo nne za nchi, upepo usivume juu ya nchi, wala juu ya bahari, wala juu ya mti wo wote. Malaika mwingine akipanda kutoka maawio ya jua, akawapigia kelele, akisema, 'Msiidhuru nchi, wala bahari, wala

miti, hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao.' Hii inaonyesha kazi tunayopaswa kuifanya sasa, ambayo ni kumlilia Mungu wetu ili malaika wale waendelee kuzizuia pepo zile nne mpaka Wamishonari wapate kutumwa sehemu zote za dunia, na mpaka watakapokuwa wamelitangaza lile onyo juu ya wale wanaoivunja Sheria ya Yehova." RH, Extra 12-11-1888, uk.4,5.

d. "Jukumu zito limekabidhiwa kwa wanaume na wanawake wenye maombi katika nchi nzima, kupeleka dua ili Mungu alifagilie nyuma wingu hili la maovu, na kutupatia miaka michache zaidi ya kufanya kazi kwa ajili ya Bwana." RH, Extra 12-11-1888, uk.4.

e. "Twaona ya kwamba wale ambao sasa wanazishika amri zake Mungu wanahitaji kujishughulisha ili waweze kupata msaada maalum ambao ni Mungu peke yake awezaye kuwapa. Wangefanya kazi kwa bidii zaidi ili kuchelewesha kwa muda mrefu iwezekanavyo janga hilo linalotishia. RH 12-18-1888, uk. 785.

f. "Iwapo hawafanyi lo lote kuielimisha mioyo ya watu, na kwa njia ya ujinga wa kutoijua kweli Mabunge yetu yangeweza kuzikataa kanuni za Uprotestanti, na kuunga mkono na kulitia nguvu kosa la Roma, yaani, sabato ya bandia [Jumapili], basi, Mungu atawashikilia watu wake waliopokea nuru kubwa kuwa wanawajibika kwa utovu wao wa juhudi na uaminifu. Lakini kama suala hili la kutunga sheria ya dini linawekwa mbele ya watu kwa busara na kwa akili, nao wanaona ya kwamba kwa njia hiyo ya kuilazimisha Jumapili uasi wa Roma ulitokea, ya kwamba ulimwengu wa Kikristo ungeweza kuigiza tena kitendo kama hicho, na ya kwamba utawala wa mabavu wa vizazi vile vilivyopita ungerudiwa tena, basi, lo lote lijalo na lije, sisi tutakuwa tumefanya wajibu wetu." RH Extra 12-24-1889, uk.3.

g. "Hebu watu wa Mungu wanaozishika amri zake [kumi] wasinyamaze wakati kama huu, kana kwamba tulikuwa tunaikubali hali hii na kuipenda. Kuna matarajio mbele yetu ya kupigana vita ya kudumu, kwa hasara ya kufungwa, kupoteza mali zetu na hata maisha yenyewe katika kuitetea Sheria ya Mungu [Amri Kumi], ambayo inabatilishwa kwa sheria za wanadamu." RH 1-1-1889, uk.1; 7BC 975.

h. "Ni matumaini yangu kuwa tarumbeta itatoa sauti ya hakika kuhusu tapo [kundi] hili linalotaka kuiweka Amri ya Jumapili. Nadhani kwamba ingekuwa bora sana kama katika magazeti yetu somo la umilele wa Sheria ya Mungu [Amri Kumi] lingetolewa kama somo maalum.... Hivi sasa tungekuwa tunafanya kila tuwezalo kuishinda sheria hiyo ya Jumapili." CW 97,98 (1906).

j. "Wale waliokwisha kuonywa juu ya matukio yaliyo mbele yao hawapaswi kukaa wakiwa wanaingojea kimya kimya dhoruba ile inayokuja, wakijifariji wenyewe kwamba Bwana atawalinda wale walio waaminifu katika siku ile ya taabu. Yatupasa sisi kuwa kama watu wanaomngojea Bwana wao, si kwa kukaa bila kazi, bali kwa kufanya kazi kwa juhudi nyingi, kwa imani isiyotikisika. Huu sasa sio wakati wa kuiacha mioyo yetu kujazwa na mambo yale yasiyo na maana... Tapo hilo la Jumapili hivi sasa linasonga mbele gizani. Viongozi wake wanaficha hoja halisi, na wengi wanaojiunga na tapo hilo wao wenyewe hawaoni ni wapi mkondo wake wa chini unakokwenda. Itikadi zake ni laini, na mwonekano wake ni wa Kikristo; lakini litakaponena, litaifunua roho ile ya joka. Ni jukumu letu kufanya yote yaliyo katika uwezo wetu kuiepusha hatari hii inayotishia. Tungejitahidi kuzizima hisia za chuki kwa kujiweka wenyewe katika nuru ile

inayofaa mbele ya watu. Tungeweka mbele yao hoja halisi ya jambo hilo, hivyo kuingilia kati kwa kupinga kunakofaa dhidi ya hatua za kuuwekea kizuizi uhuru wa dhamiri zetu. Yatupasa kuyachunguza Maandiko, na kuweza kutoa sababu kwa imani yetu." RH Extra 12-11-1888, uk. 4.

k. "Vitabu vya 'Patriarchs and Prophets, Daniel and Revelation, na The Great Controversy' vinahitajika sana sasa kuliko vilivyopata kuhitajika huko nyuma. Vingetawanywa kwa wingi sana kwa sababu kweli zile vinazozisisitizia zitayafungua macho mengi yaliyopofuka.... Wengi miongoni mwa watu wetu wamekuwa vipofu kwa umuhimu wa vitabu vile vile hasa vinavyohitajika sana. Kama busara na ustadi vingekuwa vimeonyeshwa kwa wakati ule katika kuviuza vitabu hivyo, basi, tapo hilo la Sheria ya Jumapili lisingefika hapo lilipo leo." CM 123; RH 12-16-1905.

l. "Hatuwezi kufanya kazi ili kuwafurahisha watu wale watakaoutumia mvuto wao kuukandamiza uhuru wa dini, na kuanzisha hatua za ukandamizaji ili kuwaongoza au kuwalazimisha wanadamu wenzao kuitunza Jumapili kama Sabato. Siku ya kwanza ya juma sio siku ya kuiheshimu. Ni sabato ya bandia, na washiriki wa familia yake Bwana hawawezi kushirikiana na watu hao wanaoitukuza siku hiyo, na kuivunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi] kwa kuikanyaga chini ya miguu yao Sabato yake. Watu wa Mungu hawapaswi kupiga kura ili kuwaweka watu kama hao katika ofisi; maana wanapofanya hivyo, wanashiriki pamoja nao dhambi zile watakazozitenda wakiwa ofisini." FE 475; GW 39l,392.

## SURA YA 4

## AMRI YA JUMAPILI KWA ULIMWENGU MZIMA

1. Biblia inasemaje juu ya kuinuka tena ulimwenguni kote kwa uongozi ule wa Roma ya Kikatoliki kabla ya mwisho wa wakati? Ufunuo 13:3,8.

2. Ni Taifa gani lililopata upendeleo litakaloongoza katika kulazimisha utunzaji wa Jumapili?

a. "Kundi lilo hilo lilitoa madai yake ya kwamba kuenea haraka kwa ufisadi kwa sehemu kubwa kulichangiwa na kuinajisi ile wanayoiita 'Sabato ya Kikristo,' na ya kwamba kule kulazimisha utunzaji wa Jumapili kungeyaboresha sana maadili ya jamii. Madai hayo yanasisitizwa hasa katika Amerika, ambako fundisho la Sabato ya Kweli limehubiriwa karibu kwa mapana yake yote." GC 587.

b. "Mataifa ya kigeni yatafuata mfano wa Marekani. Japokuwa Taifa hili linaongoza, hata hivyo hatari iyo hiyo itawajia watu wetu katika sehemu zote za ulimwengu." 6T 395.

3. Ni mataifa mangapi yatakayofuata mfano huo wa Marekani?

a. "Amerika, nchi yenye uhuru wa dini, itakapoungana na upapa katika kuzitenda jeuri dhamiri za watu na kuwalazimisha watu kuiheshimu sabato hiyo ya uongo [Jumapili], hapo ndipo watu wa kila nchi ulimwenguni watakapoongozwa kufuata mfano wake." 6T 18 (Angalia GCB 1-28-1893).

b. " '[A]liwanywesha Mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake [mafundisho yake potofu]' Ufunuo 14:6-8. Hii inakuwaje? Kwa kuwalazimisha watu kuikubali sabato bandia [Jumapili]." 8T 94.

c. "Suala hili la Sabato ndilo litakuwa hoja kuu katika Pambano Kuu la mwisho ambalo kwalo ulimwengu wote utakuwa na sehemu yake ya kufanya." 6T 352.

4. Ni dini gani hasa ya ulimwengu mzima inayohusika na kulazimisha utunzaji huu wa Jumapili?

a. "Kwa vile Sabato imekuwa jambo la pekee la mabishano katika Mataifa ya jamii za Kikristo, na wenye mamlaka ya dini [ya Muungano] na serikali wameungana katika kulazimisha utunzaji wa Jumapili, basi, wale walio wachache sana watakaoendelea kukataa kukubaliana na madai hayo yanayopendwa na wengi watakuwa watu wa kuchukiwa mno ulimwenguni kote." GC 615.

b. "Jamii yote ya Kikristo itagawanyika katika makundi makuu mawili, wale wanaozishika amri [kumi] za Mungu na imani ya Yesu, na wale wanaomsujudu mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa yake." GC 450; 9T 16; 2SM 55.

5. Ni jambo gani litakalowapata Waadventista Wasabato ambao hawawezi kukubaliana na Amri hiyo ya Jumapili?

a. "Amri ile itakayoitia nguvu ibada ya siku hii [ya Jumapili] itatangazwa ulimwenguni kote.... Maonjo na mateso yatawajia wale wote ambao, kwa kulitii Neno la Mungu, watakataa kuisujudu sabato hiyo ya uongo [Jumapili]." 7BC 976.

b. "Ulimwengu wote utachochewa kuwa na uadui dhidi ya Waadventista Wasabato, kwa sababu hawatakubali kumsujudu papa kwa njia ya kuiheshimu Jumapili, siku iliyowekwa na mamlaka hiyo ya Mpinga Kristo. Ni kusudi lake Shetani kusababisha wafutiliwe mbali duniani, ili ukuu wake humu duniani usipate kupingwa." TM 37; RH 8-22-1893.

c. "Mamlaka za ulimwengu huu, zikiwa zimeungana pamoja kuzipiga vita Amri [Kumi] za Mungu, zitatangaza amri kwamba 'wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini na walio huru kwa watumwa' (Ufunuo 13:16), watafuata kwa lazima desturi za kanisa kwa kuitunza sabato hiyo ya uongo [Jumapili]. Wale wote watakaokataa kutii watakabiliwa na adhabu kutokana na sheria za serikali zao, na hatimaye itatangazwa kwamba wanastahili kifo." GC 604.

6. Ni athari gani zitakazoletwa na uamsho huo wa bandia juu ya karibu wote wanaojiita Wakristo kwa jina tu?

"Wakatangaza ya kwamba wao walikuwa na ile kweli; ya kwamba miujiza ilitendeka kati yao; ya kwamba uwezo mkuu na ishara na maajabu yalitendeka miongoni mwao; na ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo ile Milenia [miaka elfu moja] waliyokuwa wanaingojea kwa muda mrefu sana. Ulimwengu wote uliongolewa na kuafikiana na Amri ile ya Jumapili." Letter 6, 1884.

7. Ni alama gani mbili zinazopingana zitapokewa na makundi hayo mawili ya watu katika ulimwengu huu hapo Jumapili itakapotiwa nguvu kwa kuitungia sheria?

a. "Wakati utunzaji wa sabato hiyo ya uongo [Jumapili] kwa kuitii amri ya serikali, kinyume na amri ile ya nne, utakuwa ni kiapo cha utii kwa mamlaka ile inayopingana na Mungu, utunzaji wa Sabato ya Kweli, kwa kuitii Sheria ya Mungu [Amri Kumi], ni ushahidi wa utii kwa Muumbaji. Wakati kundi moja, kwa kuikubali alama ya utii kwa mamlaka za duniani, linapokea Alama (chapa) ya Mnyama, lile jingine, kwa kuichagua ishara ya utii kwa Mamlaka ile ya Mbinguni, litapokea Muhuri wa Mungu." GC 605.

b. "Matokeo ni ya kuogofya ambayo kwayo ulimwengu huu utakabiliwa nayo. Mamlaka za ulimwengu huu, zikiwa zimeungana pamoja kuzipiga vita Amri [Kumi] za Mungu, zitatangaza amri kwamba 'wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa,' (Ufunuo 13:16), watafuata kwa lazima desturi za kanisa kwa kuitunza sabato hiyo ya uongo [Jumapili]. Wale wote watakaokataa kutii watakabiliwa na adhabu kutokana na sheria za serikali zao, na hatimaye itatangazwa kwamba wanastahili kifo. Kwa upande mwingine, Sheria ya Mungu [Amri Kumi] inayoamuru Siku ya Mapumziko iliyowekwa na Muumbaji inataka watu wote waitii na kutishia ghadhabu dhidi ya wote wanaozivunja amri zake [kumi].

"Jambo hilo likiwa limewekwa wazi hivyo mbele yake [kila mtu], hapo ndipo ye yote atakayeikanyaga sheria ya Mungu chini ya miguu yake ili kuitii amri ile iliyotungwa na binadamu atapokea Alama ya Mnyama...." GC 604.

8. Je, Amri hiyo ya Jumapili kwa ulimwengu mzima ina uhusiano gani na kufungwa kwa mlango wa rehema?

a. "Mungu anayapa Mataifa muda fulani wa majaribio." 4BC 1143.

b. "Kwa usahihi usioweza kukosewa Yule wa Milele angali bado anatunza akaunti ya Mataifa yote. Ingawa rehema zake hutolewa, zikiwa na mwito wa kuwataka wanadamu kutubu, akaunti

hiyo itaendelea kubaki wazi; lakini hesabu hizo zitakapofikia kiwango fulani ambacho Mungu amekiweka, utekelezaji wa ghadhabu yake utaanza. Akaunti hiyo itafungwa. Uvumilivu wa Mungu utakoma. Hakuna tena maombezi ya rehema kwa ajili yao." 5T208.

c. "Mungu anatunza kumbukumbu ya Mataifa: hesabu zinajaa dhidi yao katika vitabu vile vya mbinguni; na wakati ule itakapokuwa imepitishwa sheria kwamba uvunjaji wa siku ya kwanza ya juma utakabiliwa na adhabu, hapo ndipo kikombe chao kitakuwa kimejaa."

7BC 910.

d. "Hesabu zinazozidi kuongezeka katika vitabu vile vya kumbukumbu vya mbinguni zitakapoonyesha kiwango cha jumla ya maovu kuwa kimetimia, ndipo ghadhabu itakapokuja, pasipo kuchanganywa na maji, na hapo ndipo itakapojulikana ya kuwa ni jambo kubwa mno jinsi gani kuuchosha uvumilivu wa Mungu. Hatari hiyo kubwa itafikiwa wakati ule mataifa yote yatakapokuwa yameungana kuibatilisha Sheria ya Mungu." 5T 524.

e. "Dunia hii karibu sana imefikia mahali ambapo Mungu atamruhusu yule mharabu [mwangamizaji] kufanya mapenzi yake juu yake. Kule kuziweka sheria za wanadamu mahali pa Sheria ya Mungu, kule kuitukuza Jumapili kwa amri za kibinadamu tu, badala ya Sabato ile ya Biblia, ndilo tendo la mwisho katika mfululizo wa matukio hayo. Tendo hilo la kubadilisha [siku ya ibada] litakapoenea ulimwenguni kote, hapo ndipo Mungu atakapojidhihirisha Mwenyewe. Atasimama katika utukufu wake wa kifalme kuitetemesha sana nchi hii. Atatoka mahali pake kuja kuwaadhibu wakazi wa dunia hii kwa ajili ya maovu yao, na nchi itaifunua damu yake, wala haitawafunika tena hao waliouawa." 7T 141.

f. "Kuweka ile iliyo ya uongo mahali pa ile iliyo ya kweli ndilo tendo la mwisho katika mfululizo wa matukio haya. Tendo hilo la kubadilisha [siku ya ibada] litakapoenea ulimwenguni kote, hapo ndipo Mungu atakapojidhihirisha Mwenyewe. Sheria za wanadamu zinapotukuzwa kuliko sheria za Mungu, mamlaka za dunia hii zinapojaribu kuwalazimisha watu kuitunza siku ya kwanza ya juma, basi, jueni ya kwamba wakati umewadia kwa Mungu kutenda kazi yake. Atasimama katika utukufu wake wa kifalme, na kuitetemesha sana nchi. Atatoka mahali pake kuja kuwaadhibu wakazi wa dunia hii kwa ajili ya maovu yao." 7BC 980.

9. Je, hivi Waadventista Wasabato wote wanaamini kwamba Amri ya Jumapili kwa ulimwengu wote itapitishwa kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema?

La, hawaamini hivyo wote. Baadhi ya wanafunzi wa Biblia na Roho ya Unabii wanatazamia kwamba kutungwa kwa Amri ya Jumapili hakutaenea duniani kote mpaka kipindi fulani kipite baada ya kufungwa kwa mlango wa rehema.

Madondoo yaliyoorodheshwa chini ya Swali la 8 juu yanatafsiriwa kwa njia kama hii. Usemi mwingine wa kuwaunga mkono wanaoutumia ni huu: "Yesu atakapoondoka patakatifu pa patakatifu, Roho wake anayezuia ataondolewa kutoka kwa watawala na watu. Wataachwa katika udhibiti wa malaika waovu. Hapo ndipo sheria kama hizo zitatungwa kwa ushauri na uongozi wake Shetani, kama wakati usingekuwa mfupi sana, hakuna mwenye mwili ambaye angeweza kuokoka." 1T 204.

## SURA YA 5

## KIPINDI KIFUPI CHA WAKATI WA TAABU

(Kabla ya Kufungwa kwa Mlango wa Rehema)

1. Je, mara nyingi ni jambo gani lililowasibu watoto wa Mungu wakati uliopita?

2 Tim. 3:12; Yohana 15:20; 16:2; Dan. 7:25; Ufu.13:7.

2. Je, Shetani amebadilika au bado ni mtesaji yule yule? Ufu.12:13,17.

3. Ni matatizo gani ya pekee atakayowaletea watu wa Mungu katika siku zilizo mbele yetu? Ufu.13:15-17.

4. Taabu hizo zitaanza lini, kuhusiana na kufungwa kwa mlango wa rehema?

a. "Niliona kwamba Mungu anao watoto wake ambao hawaijui wala hawaitunzi Sabato. Hawajaikataa nuru juu ya siku hiyo. Na mwanzo wa wakati wa taabu, tulijazwa na Roho Mtakatifu tulipotoka na kuitangaza Sabato kwa ukamilifu zaidi." EW 33.

b. " 'Mwanzo wa wakati wa taabu,' uliotajwa hapa, hauhusu wakati ule mapigo yatakapoanza kumiminwa, bali ni kipindi kile kifupi muda mfupi tu kabla hayajaanza kumiminwa wakati Kristo akiwa ndani ya patakatifu [kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema]." EW 85.

5. Sababu mojawapo kuu ni ipi ya kipindi hiki [kifupi] cha taabu?

a. "Sabato ya Mungu itakuwa inakanyagwa chini ya miguu yao, na sabato ya uongo [Jumapili] itakuwa inatukuzwa. Katika kuiweka Amri ya Jumapili upo uwezekano wa kutokea mateso makali sana kwa wale wanaoitunza siku ya saba. Utekelezaji wa mipango ya Shetani utasababisha mateso kwa watu wa Mungu. Lakini watumishi waaminifu wa Mungu hawana haja ya kuogopa athari za pambano hilo." 2SM 375.

b. "Kama upapa ama kanuni zake zitatungiwa sheria tena na kutiwa nguvu, basi, mioto ya mateso itawashwa tena dhidi ya wale ambao hawatakubali kwenda kinyume na dhamiri zao na ile kweli ili kuyastahi makosa [mafundisho potofu] yanayopendwa na watu wengi. Uovu huo uko karibu kutimizwa." 5T 712.

6. Je, watu wa Mungu watateswa kwa kutoitunza Jumapili au kwa kuitunza Sabato?

a. "Ulimwengu wa Kiprotestanti leo unamwona Mordekai mlangoni katika kundi lile dogo linalotunza Sabato. Tabia yake na mwenendo wake, vikionyesha kicho alicho nacho kwa Sheria ya Mungu, ni kemeo la daima kwa wale waliotupilia mbali kumcha Mungu na ambao wanaendelea kuikanyaga kwa miguu yao Sabato yake; mdukizi huyo [kundi dogo lishikalo Sabato] ni lazima aondolewe mbali na njia yao kwa kutumia mbinu fulani." 5T 450.

b. "Watu wa Mungu watausikia mkono ule utesao kwa sababu wanaitakasa siku yake ya saba." 7BC 975; 9T 229.

c. "Hebu na pawepo na uamsho wa imani na uwezo wa kanisa lile la kwanza, hapo ndipo roho ya utesaji itakapofufuka tena, na ile mioto ya mateso itawashwa tena." GC 48.

7. Je, chuki ile kwa Waadventista Wasabato itakuwa kali kiasi gani?

a. "Wale wanaoiheshimu Sabato ya Biblia watashutumiwa kuwa ni maadui wa sheria na taratibu za nchi, na wavunjaji wa vizuizi vilivyowekwa ili kuyalinda maadili ya jamii, waleta vurugu na ufisadi, wanaoziita hukumu za Mungu kuanguka juu ya nchi. Aibu yao inayotokana na kuwa waangalifu sana itatangazwa kuwa ni ukaidi, ushupavu, na dharau kwa mamlaka.

Watashtakiwa kuwa wana chuki kwa serikali. Wachungaji wale wanaokana kwamba Sheria ya Mungu haiwafungi watu, watahubiri kutoka katika mimbara zao juu ya wajibu wa kuonyesha utii kwa viongozi wa serikali wenye mamlaka kama jambo lililoamriwa na Mungu. Katika kumbi za Mabunge na mahakama za Sheria, wale wanaozishika amri [kumi] wataelezwa vibaya na kuhukumiwa adhabu. Picha mbaya itawekwa juu ya maneno yao; tafsiri mbaya mno zitatolewa kwa makusudi yao." GC 592 (Angalia pia PK 183,184).

b. "Kabla vita havijaisha na ushindi kupatikana, sisi kama watu wa pekee tutapitia uzoefu unaofanana na ule wa Paulo. Tutakutana na moyo ule ule mgumu, ujasiri ule ule wa kikatili, chuki ile ile isiyokoma.... Mateso yatatokea tena dhidi ya wale walio waaminifu kwa Mungu; makusudi yao yatatiliwa mashaka, juhudi zao bora sana zitatafsiriwa vibaya, majina yao yatatupiliwa mbali kama maovu.... Mungu angependa watu wake wajiandae kwa hatari ile kubwa inayokuja hivi punde. Tuwe tayari ama tusiwe tayari, sisi sote ni lazima tukabiliane nayo." SLP 251,252.

c. "Utakuja wakati ambapo sisi tutatendewa kama wahaini kwa sababu ya kuitetea kweli ile ya Biblia." 6T 394.

d. "Mali, vipaji, elimu, vitaunganishwa pamoja ili kuwafunika [watu wa Mungu] na dharau. Watawala watesaji, wachungaji, na washiriki wa kanisa watakula njama dhidi yao. Kwa sauti na kalamu, kwa majisifu, vitisho, na dhihaka, watajaribu kuipindua imani yao." 5T 450.

8. Ni vyama gani vitakavyofanya mambo yawe magumu sana kwa Waadventista kuendelea kwa muda mrefu na kazi yao katika miji mikubwa?

a. "Vyama vya Wafanya kazi vitakuwa mojawapo ya njia zitakazoleta juu ya dunia hii wakati wa taabu ambao mfano wake haujapata kuwapo kamwe tangu mwanzo wa dunia hii." 2SM 142.

b. "Kwa sababu ya vyama hivyo na miungano ya aina mbalimbali, itakuwa vigumu sana hivi karibuni kwa taasisi zetu kuendesha kazi zake katika miji mikubwa. Onyo langu ni hili: Tokeni mijini. Msijenge hospitali zetu zo zote katika miji mikubwa." 2SM 142.

c. "Watu wachache watajiunga pamoja kunyonya mali yote itakayopatikana katika mikondo fulani ya biashara. Vyama vya wafanya kazi vitaundwa, na wale watakaokataa kujiunga katika vyama hivyo watakuwa ni watu wa kuangaliwa sana [kwa jicho baya]." 2SM 142.

d. "Wakati unaharakisha kuja ambapo Vyama vya Waajiri vitakuwa na uwezo mkubwa wa uongozi wenye ukandamizaji mbaya sana. Tena na tena Bwana ameniagiza kwamba watu wetu wanapaswa kuziondoa familia zao mbali na miji mikubwa, kwenda sehemu za mashambani, ambako wanaweza kuzalisha chakula chao wenyewe; kwa maana siku zijazo tatizo la kununua na kuuza litakuwa kubwa sana." 2SM 141.

9. Ni tangazo gani la amri ya serikali litakalotolewa kuhusu kununua na kuuza kadiri wakati unavyozidi kusonga mbele?

a. "Katika Pambano Kuu la mwisho lihusulo kupambana na Shetani, wale walio waaminifu kwa Mungu wataona msaada wote wa kibinadamu unaondolewa kwao. Kwa kuwa watakataa kuivunja

Sheria yake ili kuzitii mamlaka za kidunia, watapigwa marufuku wasiweze kununua wala kuuza." DA 121,122.

b. "Shetani asema hivi... 'Kwa hofu ya kukosa chakula na nguo, watajiunga na ulimwengu kuivunja Sheria ya Mungu. Dunia yote itakuwa chini ya utawala wangu." PK 183,184 (Angalia pia 5T 152).

c. "Karibu sana mali ile iliyohodhiwa itakuwa haina thamani yo yote. Tangazo litakapotolewa kwamba hakuna atakayeweza kununua wala kuuza isipokuwa yule aliye na alama (chapa) ya mnyama, hapo ndipo mali nyingi sana itakuwa haina faida yo yote. Mungu anatutaka sisi kufanya kila lililo katika uwezo wetu sasa kulipeleka onyo hili kwa ulimwengu mzima."

RH 3-21-1878, uk. 91.

d. "Wakati unakuja tutakapokuwa hatuwezi kuuza kwa bei yo yote ile. Tangazo litatolewa hivi karibuni kuwakataza watu kununua au kuuza kwa mtu ye yote isipokuwa kwa yule aliye na alama ya mnyama. Tulinusurika kuifikia hali hiyo katika mji wa California kipindi kifupi kilichopita; lakini hicho kilikuwa ni kitisho tu cha kuvuma kwa pepo zile nne. Mpaka sasa bado zimeshikiliwa na malaika wale wanne. Sisi hatujawa tayari kabisa. Kuna kazi inayohitaji kufanyika, baada ya hapo malaika hao wataagizwa kuziachilia, ili pepo zile nne zipate kuvuma juu ya nchi. Wakati ule utakuwa ni wakati wa mkataa kwa watoto wa Mungu, wakati wa taabu ambao mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa. Sasa ndiyo nafasi yetu ya kufanya kazi." 5T 152.

10. Ni sheria gani ya ziada itakayotungwa kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema?

"Matukio ya ajabu yataonekana mara moja mbele ya ulimwengu. Mwisho wa mambo yote umekaribia. Wakati wa taabu karibu utawajia watu wa Mungu. Hapo ndipo amri itakapotangazwa ikiwakataza wale wanaoishika Sabato ya Bwana kununua na kuuza, na kutoa tishio kwao la adhabu, na hata kifo, kama hawataitunza siku ya kwanza ya juma kama Sabato.

" 'Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo....' " RH 11-19-1908, uk. 5.

11. Vijana wengine watatendewaje na wazazi wao?

"Utii unaoambatana na maadili kwa Neno la Mungu utahesabiwa kama ni uasi. Akiwa amepofushwa na Shetani, mzazi atatumia ukali na ukatili kwa mtoto wake aaminiye; bwana au bibi atamkandamiza mtumishi wake anayezishika amri. Upendo utaondolewa; watoto watanyang'anywa urithi wao na kufukuzwa mbali na nyumbani kwao." GC 608.

12. Wengine watatendewaje na Mahakama za Sheria?

a. "Wote wanaothibitisha uaminifu wao kwa utii wao kwa sheria yake Yehova wajiandae kukamatwa, kuletwa mbele ya mabaraza ambayo hayana kanuni ya juu na takatifu kama ile ya Mungu." RH 12-26-1899, p. 83; 7BC 977.

b. "Huruma nyingi za uweza huu zitajionyesha katika seli za magereza na katika vifungo vya gereza la chini ya ardhi. Tayari maandalizi yanaendelea mbele, na matapo yanasonga mbele, ambayo mwisho wake yataiunda sanamu ya mnyama." RH 4-23-1889, uk. 257.

c. "Wanaoitetea kweli watakapokataa kuiheshimu Sabato ya Jumapili, baadhi yao watatupwa gerezani, wengine watafukuzwa mbali na kwao, wengine watatendewa kama watumwa. Kwa hekima za kibinadamu, yote haya kwa sasa yanaonekana kuwa hayawezekani kabisa kutokea; lakini Roho wa Mungu azuiaye atakapoondolewa kwa wanadamu, nao watakapokuwa chini ya uongozi wa Shetani, ambaye anazichukia amri [kumi] za Mungu, kutatokea mambo ya ajabu sana. Moyo unaweza kuwa mkatili sana hofu ya Mungu na upendo wake unapoondolewa." GC 608.

13. Je, yawezekana kwamba baadhi yao wataweza kujitoa mhanga kabisa?

a. "Kuna matarajio mbele yetu ya pambano hilo kuendelea, kwa hasara ya kufungwa, kupoteza mali zetu, na hata maisha yenyewe, kwa kuitetea Sheria ya Mungu." 5T 712.

b. "Kama [Shetani] alivyoyaongoza mataifa ya kishenzi kuiangamiza Israeli, ndivyo siku zijazo atakavyozichochea mamlaka za uovu za dunia kuwaangamiza watu wa Mungu. Watu watatakiwa kutoa utii wao kwa amri za wanadamu na kuivunja Sheria ya Mungu.

"Wale walio waaminifu kwa Mungu watatishiwa, watashutumiwa, watapigwa marufuku. Wata'salitiwa na wazazi, na ndugu, na ukoo wao, na marafiki,' hata kufa." PK 587,588.

14. Je, wale watakaokuwa wamehukumiwa adhabu kwa ajili ya imani yao wataogopa kuwekwa katika seli za magereza au kukabiliwa na kifo chenyewe?

a. "Iwapo tutatakiwa kuteswa kwa ajili yake Kristo, basi, tutaweza kwenda gerezani huku tukimtegemea yeye kama vile mtoto mdogo anavyowategemea wazazi wake. Sasa ndio wakati wa kujenga imani yetu kwa Mungu." OHC 357.

b. "Hatuwezi kuwa na ujasiri na ushupavu waliokuwa nao wafia dini wale wa zamani mpaka hapo tutakapoletwa mahali pale walipokuwa wamewekwa wao.... Kama mateso hayo yanaweza kurudi tena, basi, neema itatolewa kuiamsha kila nguvu ya moyo ili upate kuonyesha ushujaa wa kweli kweli." OHC 125.

d. "Muumini anaposimama kizimbani katika mahakama zile zisizo na haki kwa ajili ya ile kweli, Kristo anasimama kando yake.... Mmoja anapofungwa ndani ya kuta za gereza, Kristo anaujaza moyo wake na furaha kwa upendo wake. Mmoja anapouawa kwa ajili yake, Kristo husema, ' (Mimi) ni hai hata milele na milele.... Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu.' Ufu.1:18. Maisha yale yanayotolewa sadaka [mhanga] kwa ajili yangu yanahifadhiwa kwa ajili ya utukufu ule wa milele." DA 669.

15. Ni akina nani watakaokuwa vibaraka wa Shetani wenye mafanikio makubwa sana katika kuwaeleza vibaya na kuwashtaki Waadventista?

"Watu wenye talanta na hotuba tamu, ambao hapo kwanza waliifurahia hiyo kweli, watautumia uwezo wao huo kuwadanganya na kuwapotosha watu. Watakuwa maadui wachungu sana wa ndugu zao wa zamani. Waadventista Wasabato watakapoletwa mbele za mahakama mbalimbali kuitetea imani yao, waasi hao watakuwa vibaraka wa Shetani walio na mafanikio makubwa sana katika kuwaeleza vibaya na kuwashtaki, na kwa taarifa zao za uongo na masingizio watawachochea watawala dhidi yao." GC 608.

l6. Ni makundi gani mawili ya Kikristo yenye nguvu yatakayojiunga pamoja kuwatesa wale wanaoitetea kweli?

a. "Ulimwengu unaojidai kuwa ni wa Kiprotestanti utafanya muungano na mtu yule wa dhambi.... Maandiko yanafundisha kwamba upapa utajipatia tena ukuu wake uliopotea, na ya kwamba mioto ya mateso itawashwa tena...." 7BC 975.

b. "Wengi watadai ya kuwa hakuna matumaini kwamba upapa utafufuka tena. Iwapo utajipatia tena ukuu wake ulioupoteza, basi, itakuwa ni kwa njia ya Uprotestanti kuupa mkono wa kuume wa ushirika. Kama utaingia katika mamlaka yake kisheria kwa kibali cha watu wale walio na kigeugeu, basi, mioto ya mateso itawashwa tena dhidi ya wale wasiotaka kwenda kinyume na dhamiri zao na ile kweli ili kufuata makosa [mafundisho potofu] ya upapa. Mara tu mioyo ya ulimwengu wa Kikristo itakapogeuka na kumpa kisogo Mungu; na kuiacha sheria yake idharauliwe na siku yake takatifu ikanyagwe chini kwa miguu, hapo ndipo watakapokuwa tayari kuchukua hatua yo yote ko kote kule atakakowaongoza Shetani." RH 1-1-1889, uk. 1.

c. "Kanisa litaomba msaada kutoka kwa mkono ule wenye nguvu wa mamlaka ya kiserikali, na, katika kazi hiyo, wafuasi wa Kanisa Katoliki na Waprotestanti wataungana pamoja." GC 607.

d. "Wale wote ambao hawatakubali kutii amri ya mabaraza ya kitaifa na kuzitii sheria za kitaifa za kuitukuza sabato ile iliyowekwa na mtu yule wa dhambi, kwa kutoijali ile siku takatifu ya Mungu, wataona, sio tu mamlaka ya ukandamizaji ya Roma, bali ya ule ulimwengu wa Kiprotestanti, yaani, sanamu ya mnyama." 2SM 380.

e. "Wachungaji wapendwao na watu wengi, kama wale Mafarisayo wa zamani, wakiwa wamejaa hasira nyingi wakati mamlaka yao itakapohojiwa, wataukataa ujumbe huo wakidai kwamba unatoka kwa Shetani na kuwachochea halaiki wapendao dhambi kuwatukana na kuwatesa wale wanaoutangaza [ujumbe huo]. GC 607.

f. "Waprotestanti wanafanya kazi kwa kujificha ili kuileta Jumapili mbele ya watu, kama walivyofanya Waroma. Katika nchi nzima upapa unajenga majengo yake marefu na makubwa sana, katika vyumba vyake vya siri mateso yake ya zamani yatarudiwa tena." 5T 449,450 (Angalia pia GC 581).

17. Je, mateso hayo yatakuwa ya aina moja kila mahali?

"Kadiri ujumbe huu wa rehema unavyoendelea kutolewa kwa ulimwengu, patakuwa na mwito wa kufanya juhudi kwa niaba ya taasisi nyingine na mashirika ya biashara sawa na yale yanayotoa msaada kwa shule zetu. Na kwa kadiri muda wa majaribio unavyoendelea kuwapo, patakuwapo na

nafasi kwa mwinjilisti wa vitabu kufanya kazi yake. Madhehebu za dini zitakapoungana na upapa kuwatesa watu wa Mungu, mahali pale palipo na uhuru wa dini patafunguliwa kwa uinjilisti wa vitabu. Endapo mahali pamoja mateso yatakuwa makali sana, basi, watenda kazi na wafanye kama Kristo alivyoahidi. Lakini watakapowafukuza [watakapowatesa] katika mji huu, kimbilieni mwingine.' Kama mateso yatakuja pale, basi, kimbilieni mahali pengine zaidi. Laiti kama isingalikuwa kwa mateso hayo wasingeweza kutawanyika na kwenda mbali sana kuitangaza kweli." 6T 478.

18. Washiriki wa Kanisa wasiotakaswa wataathiriwaje na dhoruba hiyo ya dhihaka, maonjo na dharau?

"Dhoruba ile itakapokaribia, kundi kubwa la wale walioikiri imani hii ya ujumbe wa malaika wa tatu, watapaacha mahali pao, na kujiunga katika safu za upinzani. Kwa kujiunga na ulimwengu na kushiriki roho yake, watakuja kuyaangalia mambo katika nuru karibu ile ile; na jaribio hilo litakapoletwa kwao, watakuwa tayari kuchagua upande ule ulio rahisi, yaani, unaopendwa na wengi." GC 608.

19. "Kondoo wa kweli" watayapokeaje mateso yatakapokuja?

"Dhoruba ya mateso itakapovuma juu yetu kweli kweli, ndipo kondoo wa kweli watakapoisikia sauti ya Mchungaji yule wa kweli. Juhudi za kujikana nafsi zitafanywa ili kuwaokoa waliopotea, na wengi ambao wametangatanga mbali na zizi lake watarudi na kumfuata Mchungaji huyo Mkuu. Watu wa Mungu watashikamana kwa karibu sana na kumkabili adui yao kwa umoja katika uwanja wa mapambano. Kwa kuzingatia hatari ile kubwa ya aina moja inayowakabili wote, kugombania ukubwa kutakoma; hakutakuwa na mabishano kuhusu nani atakuwa mkubwa kuliko wote." 6T 401.

20. Ni uweza gani mkuu wa Mungu utakaoonekana katika dunia yote baada ya mateso hayo kuanza?

"Upendo wa Kristo, yaani, upendo kwa ndugu zetu, utaushuhudia ulimwengu ya kwamba sisi tumekuwa pamoja na Yesu na tumejifunza kwake. Hapo ndipo ujumbe wa malaika yule wa tatu utakapovuma na kuwa sauti kuu, na nchi yote itaangazwa kwa utukufu wake Bwana." 6T 401.

21. Mtazamo wetu wa sasa na mwenendo wetu ungekuwaje tunapoingojea taabu ile inayokuja mbele yetu?

a. "Tena na tena ujumbe huu nimepewa mimi ya kwamba haitupasi kusema neno moja, kuchapisha sentensi moja, hasa kwa kuwataja watu isipokuwa kama ni lazima sana kufanya hivyo katika kuitetea ile kweli, ambayo itawachochea maadui zetu dhidi yetu na kuamsha hasira zao kiasi cha kuwa moto [kuchemka] sana. Kazi yetu itafungwa hivi karibuni, na karibuni wakati wa taabu, ambao mfano wake haukuwapo, utatujia, ambao habari zake hatuna wazo hata kidogo juu yake." 9T 241.

b. "Hebu kila mmoja na akumbuke ya kwamba kwa vyo vyote vile sisi hatutakiwi kuyakaribisha mateso hayo. Hatutakiwi kutumia maneno makali yanayochoma. Katika kila

makala iliyoandikwa yaondoe, yaondoe katika kila hotuba unayotoa. Acha Neno la Mungu lifanye kazi ya kuchoma, kukemea; wanadamu na wajifiche na kukaa ndani ya Yesu Kristo....

"Patakuwapo na wakati wa taabu mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa."

9T 244.

c. "Wakati umefika mateso yatakapowajia wale wanaoitangaza kweli. Hali ya mambo haipendezi; lakini, japokuwa ni hivyo, hebu sisi na tusiache juhudi zetu za kuwaokoa wale walio tayari kuangamia, ambao fidia yao alilipa Mfalme yule wa Mbinguni kwa kuutoa uhai wake wa thamani. Njia moja ikishindwa, jaribuni nyingine. Juhudi zetu zisiwe kama za wafu, yaani, zisizovutia kwa watu. Kadiri tunavyojaliwa kuwa na uhai wetu, na tufanye kazi kwa ajili ya Mungu wetu." 9T 227.

## SURA YA 6

## PEPETO KUU

1. Je, fundisho la Biblia juu ya somo la subira ya watakatifu linasema kwamba 'ukiokolewa mara moja, basi, utaendelea kubaki katika hali ya kuokolewa daima'? Je, kuna uwezekano kwa Mkristo wa kweli kupoteza upendo wake kwa Mungu? Mt. 24:13; 13:18-23; 1Kor.9:27; 10:12; Ebr. 6:4-6; Eze. 18:24; 2 Petro 2:20,21.

2. Je, Biblia inaeleza habari za uasi wa watu fulani maalum ambao zamani walipata kibali cha Mungu? Eze. 28:15; 2 Petro 2:4; 1 Sam.10:9; 28:15.

3. Je, uasi wa dini ("kupepetwa" kwa washiriki kwenda nje ya Kanisa la Mungu) unakomea tu kwa karne zile zilizopita?

a. "Mtikiso Mkuu umeanza na utaendelea, na wote wasiotaka kuchukua msimamo thabiti, usiotaka kushindwa, katika kuitetea ile kweli, na kujitoa mhanga kwa ajili ya Mungu na kazi yake, watatikiswa. Malaika yule akasema, 'Je, mnadhani kuna mtu ye yote atakayeshurutishwa kujitoa mhanga? La, la. Lazima iwe ni kafara inayotolewa kwa hiari.' " EW 50,51 (1850).

b. "Niliona kwamba hivi sasa tu katika wakati wa mtikiso. Shetani anafanya kazi kwa nguvu zake zote kuzipokonya roho za watu kutoka katika mkono wake Kristo...." 1T 429 (1864).

c. "Mungu sasa anawapepeta watu wake, akiyapima makusudi yao na nia zao. Wengi watakuwa kama makapi tu ----- si ngano, wala thamani yo yote haimo ndani yao." 4T 51 (1876).

d. "Tunaishi katika wakati wa mtikiso, wakati ambapo kila kitu kinachoweza kutikiswa kitatikiswa. Mungu hatawasamehe wale wanaoijua kweli kama hawazitii amri zake kwa neno na kwa matendo." 6T 332 (1900).

e. "Mara tu watu wa Mungu watakapotiwa muhuri katika vipaji vya nyuso zao ----- huo si muhuri wa aina yo yote au alama inayoweza kuonekana kwa macho, bali ni kule kutulia [kujizatiti] katika kweli, kiakili na kiroho, ili wasiweze kuondoshwa ----- Mara tu watu wa Mungu watakapotiwa muhuri na kuwa tayari kwa mtikiso huo, utakuja. Naam, tayari umeanza; hukumu [adhabu] za Mungu zi juu ya nchi hivi sasa, kutupa sisi onyo, ili tupate kujua kile kinachokuja." 4BC 1161 (1902).

f. "Hata katika siku hizi zetu pamekuwa na pataendelea kuwa na familia nzima ambazo zamani zilipata kuifurahia kweli, lakini zikapoteza imani kwa sababu ya kuletewa habari za masingizio na uongo kuhusiana na wale ziliokuwa zinawapenda na ambao zilipeana nao mashauri mazuri sana. Ziliifungua mioyo yao ipate kupandwa magugu; magugu hayo yakaota miongoni mwa ngano; yakapata nguvu; zao la ngano likapungua na kuzidi kupungua; na ile kweli ya thamani ikapoteza nguvu yake kwao." TM 411.

4. Ni uzoefu gani wa siku za mbele zilizo karibu kuja ambao utaongeza sana idadi ya waasi kutoka katika Kanisa la Waadventista Wasabato?

a. "Wakati hauko mbali jaribio hilo litakapomjia kila mtu. Alama ya Mnyama italazimishwa juu yetu. Wale ambao hatua kwa hatua wametii madai ya ulimwengu huu na kufanana na desturi za ulimwengu huu hawataona kuwa ni jambo gumu kuzitii mamlaka zilizopo, kuliko kukabiliana na dhihaka, matusi, kutishiwa kufungwa, na kifo. Pambano lenyewe ni juu ya amri [kumi] za Mungu na amri za wanadamu. Wakati huo ndipo dhahabu itakapotenganishwa mbali na takataka ndani ya kanisa." 5T 81.

b. "Dhoruba inapokaribia, kundi kubwa lililoikiri imani ya ujumbe wa malaika wa tatu, bali halijatakaswa kwa kuitii kweli hiyo, litaondoka mahali pake, na kujiunga katika safu za upinzani." GC 608.

c. "Kazi ambayo kanisa limeshindwa kufanya wakati wa amani na usitawi litapaswa kuifanya wakati ule wa hatari ya kutisha chini ya mazingira ya kukatisha tamaa, yaani, ya kuogofya sana.... Na wakati ule kundi lile lililokuwa na imani ya juu juu tu, ambalo halikupenda mabadiliko, ambalo mvuto wake umeendelea kwa taratibu kurudisha nyuma maendeleo ya kazi hiyo, litaikana imani...." 5T 463.

d. "Maonjo yatakapozidi kuwa mengi kutuzunguka, hapo ndipo mtengano na umoja, vyote viwili, vitaonekana katika safu zetu. Baadhi ya wale walio tayari kuchukua silaha za vita sasa, watajionyesha wazi kuwa hawajajenga juu ya Mwamba ule ulio imara katika nyakati zile za hatari halisi; wataanguka majaribuni. Wale waliopata nuru kuu na upendeleo wa thamani, lakini hawakuitumia vizuri, chini ya kisingizio hiki au kile, watajitenga mbali nasi." 6T 400.

e. "Wakati huu ambapo mateso hayapo wameingia katika safu zetu watu wanaoonekana kuwa ni wakamilifu na Ukristo wao hautiliwi mashaka, lakini ambao, kama mateso yangeweza kutokea, basi, wangeondoka na kutuacha." Ev 360.

5. Zaidi ya hayo mateso, ni sababu gani nyingine zilizopo zitakazoleta "mtikiso" huo wa watu wa Mungu?

a. "Nikauliza maana ya mtikiso niliokuwa nimeuona, nikaonyeshwa kwamba utasababishwa na ule ushuhuda mnyofu unaotokana na shauri la yule Shahidi wa Kweli kwa Walaodikia. Huo utakuwa na athari moyoni mwa mpokeaji, nao utamwongoza kuiinua juu bendera na kuitangaza kweli tupu bila kuipindisha. Wengine hawatastahimili kusikia ushuhuda huo mnyofu. Watasimama na kuupinga, na hilo ndilo litakaloleta mtikiso miongoni mwa watu wa Mungu." EW 270.

b. "Roho wa Mungu ameutia nuru kila ukurasa wa Maandiko Matakatifu, lakini wapo wale ambao kwao yanaleta maono kidogo tu, kwa sababu hayaeleweki kikamilifu. Mtikiso ukija, kwa njia ya kuletwa kwa nadharia potofu, wasomaji hao wa juu juu, wasiotia nanga yao mahali po pote, wanakuwa kama mchanga unaohama-hama. Wanateleza na kuingia mahali po pote panapowafaa kulingana na mwelekeo wa hisia zao zilizojaa uchungu...." TM 112.

c. "Wakiwa hawajaipenda ile kweli, watachukuliwa na madanganyo ya yule adui; watazisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani, nao watajitenga na imani."

6T 401.

6. Ni maneno gani anayotumia Bibi White kuelezea uzoefu huo?

"Katika pepeto kuu ambalo halina budi kutokea upesi tutaweza kuwa katika hali bora ya kuzipima nguvu za Israeli. Dalili zaonyesha kwamba wakati u karibu Bwana atakapoonyesha ya kuwa pepeto lake li mkononi mwake, naye atausafisha sana uwanda wake." 5T 80.

7. Je, ushirika wetu wote wa kanisa umejengwa kutokana na Wakristo waaminifu?

a. "Kutokana na yale niliyoonyeshwa mimi, hawapatikani zaidi ya nusu ya vijana wanaoamini dini na kweli ambao wameongoka kweli kweli." 1T 158; MYP 131 (1857).

b. "Majina yanaandikwa katika vitabu vya kanisa hapa duniani, lakini sio katika kitabu kile cha uzima. Nikaona ya kwamba katika vijana ishirini hakuna hata mmoja ajuaye maisha ya dini yalivyo hasa." 1T 504; MYP 384 (1867).

c. "Katika njozi ile ya mwisho niliyopewa, nilionyeshwa ukweli unaoshangaza sana ya kwamba ni sehemu ndogo tu ya wale wanaokiri kuiamini kweli sasa ambao watatakaswa kwayo na kuokolewa." 1T 608 (1867).

d. "Mimi nimeeleza mbele yao kwamba, kutokana na yale niliyoonyeshwa, ni idadi ndogo tu ya wale ambao sasa wanajidai kuiamini kweli watakaookolewa mwishowe..." 2T 445 (1870).

e. "Nawaambieni, si wachungaji wachache wanaosimama mbele ya watu kufafanua Maandiko walio wachafu. Mioyo yao imejaa ufisadi, mikono yao ni michafu." 5T 78 (1882).

f. "Ni usemi ulio mzito sana ninaoutoa kwa kanisa, kwamba hakuna hata mmoja katika watu ishirini ambao majina yao yameandikwa katika vitabu vya kanisa aliye tayari kuifunga historia yake ya duniani, naye kwa kweli angekuwa hana Mungu wala matumaini duniani kama vile alivyo mwenye dhambi wa kawaida." ChS 41 (1893).

8. Katika siku hizi za raha na mafanikio ambazo sisi tunazifurahia sasa, tunaweza kutazamia kitu gani kutokea katika kanisa letu?

a. "Mafanikio yanaongeza idadi kubwa ya waumini. Dhiki inawasafisha na kuwaondoa kanisani wale walio waovu." 4T 89.

b. "Mafarakano yatatokea ndani ya kanisa. Makundi mawili yatakuzwa. Ngano na magugu vitakua pamoja tayari kwa mavuno." 2SM 114.

9. "Pepeto Kuu" litakapotokea, ni jambo gani litakalowapata washiriki wa kanisa letu ambao hawajajitoa wakf?

a. "Siku ile itakapokuja Sheria ya Mungu itabatilishwa, na kanisa litapepetwa kwa majaribu makali kama moto ambayo yatawajaribu wote wanaoishi hapa duniani, hapo ndipo sehemu kubwa ya wale wanaodhaniwa kuwa ni waaminifu watasikiliza roho zidanganyazo, nao watageuka na kuwa wasaliti na kuzifichua siri za amana zile takatifu walizokabidhiwa. Watakuwa watesaji wabaya kupindukia kwetu sisi." 6BC 1065.

b. "Nyota nyingi ambazo tumezitamani sana kwa mng'ao wake wakati huo zitazimika katika giza." PK 188 (Angalia pia 5T 81).

c. "Makapi kama wingu yatapeperushwa mbali na upepo, hata kutoka mahali pale tunapouona uwanda uliojaa ngano nyingi." 5T 81.

d. "Mtikiso huo wa Mungu unayapeperusha makundi kwa makundi kama majani makavu." 4T 89.

e. "Katika kazi ile nzito ya mwisho ni wakuu wachache mno watakaoshiriki kufanya kazi." 5T 80.

10. Ni asilimia ngapi ya washiriki wote wa kanisa la Waadventista Wasabato itakayoasi?

a. "Hivi punde watu wa Mungu watajaribiwa kwa maonjo yaliyo kama moto, na sehemu kubwa ya wale ambao sasa wanaonekana kuwa wakweli na waaminifu watakuwa kama madini isiyofaa kitu." 5T 136.

b. "Kusimama na kuitetea kweli na haki wakati wengi wanatuacha peke yetu, kupigana vita vile vya Bwana wakati mashujaa ni wachache ----- hilo litakuwa ndilo jaribio letu. Kwa wakati huu yatupasa kukusanya joto kutokana na ubaridi wa wengine, kuwa na ujasiri badala ya woga wao, na kuwa na utii badala ya uasi wao." 5T 136.

c. "Sheria ya Mungu [Amri Kumi] itakapobatilishwa, kanisa litapepetwa kwa majaribu makali kama moto, na sehemu yao kubwa kuliko vile tunavyotarajia sasa, watasikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani." 2SM 368; Ev 361.

11. Je, Waadventista Wasabato wote ambao hawajajitoa wakf watapepetwa na kutoka kanisani katika kipindi hiki cha majaribu kabla ya mlango wa rehema kufungwa?

"Wale wanaojidai kuwa waumini watakaoufikia wakati ule wa taabu pasipo kujiweka tayari, kwa kukata tamaa kwao, wataziungama dhambi zao mbele ya watu wote kwa maneno yaliyojaa uchungu mkali sana unaowaka kama moto, wakati waovu wanashangilia sana juu ya dhiki yao. Kesi ya wote hao haina matumaini. Kristo anaposimama, na kutoka patakatifu pa patakatifu, hapo ndipo unapoanza wakati ule wa taabu, na kesi ya kila mtu itakuwa imekatwa." 3SG 134.

12. Je, watu wetu wangekuwa wanakumbushwa daima kwamba mateso yanakuja na idadi yao kubwa itaasi?

"Uko wakati wa taabu unaowajia watu wa Mungu, lakini haitupasi kuliweka jambo hilo mbele ya watu daima, na kuwahamasisha waweze kupata wakati wao wa taabu mapema. Patakuwapo na mtikiso miongoni mwa watu wa Mungu, lakini huo sio ukweli wa leo wa kuyapelekea makanisa...." 1SM 180; 2SM 13.

13. Je, washiriki wetu wengi watakapoondoka, Kanisa la Waadventista Wasabato litasambaratika?

a. "Kanisa linaweza kuonekana kana kwamba linakaribia kuanguka, lakini halianguki. Linasalia, wakati wenye dhambi walioko Sayuni watakapopepetwa na kutoka nje ----- makapi

yatatenganishwa na ngano. Hilo ni jaribu la kuogofya sana, lakini hata hivyo halina budi kutokea." 2SM 380.

b. "Kanisa ni bohari ya kutunzia mali ya utajiri wa neema yake Kristo, na kwa njia ya kanisa hatimaye utadhihirishwa upendo wa mwisho ulio mwingi sana kwa ulimwengu huu ambao utaangazwa kwa utukufu wake." TM 50.

c. "Ngome za Shetani hazitashinda kamwe. Ushindi utaambatana na ujumbe wa malaika wa tatu. Kama vile yule Amiri [Kamanda] wa Jeshi la Bwana alivyoziangusha chini kuta zile za Yeriko, ndivyo watu wa Bwana wazishikao amri zake [kumi] watakavyopata ushindi mkubwa, na nguvu zote za upinzani zitashindwa." TM 410.

14. "Jaribu hilo la kutisha sana" litayaathirije matarajio na msimamo wa Waadventista watiifu watakaobaki kanisani?

a. "Acha upinzani utokee, acha ushupavu wa dini na kutostahimili maoni ya wengine vishike hatamu ya utawala tena, acha moto wa mateso uwashwe tena, hapo ndipo wale wanaoipokea kweli kwa shingo upande na wanafiki watakapoyumba na kuiacha imani yao; lakini Mkristo wa kweli atasimama imara kama mwamba, imani yake itazidi kuwa na nguvu zaidi, tumaini lake litang'aa kuliko katika siku zile za usitawi wake." GC 602.

b. "Katikati ya vivuli vinavyozidi kuwa vyeusi vya hatari kubwa ya mwisho inayoukabili ulimwengu huu, nuru ya Mungu itang'aa sana, na wimbo wa matumaini na imani utasikika kwa wazi kabisa na kwa sauti za juu kabisa." Ed 166.

c. "Dhoruba ya mateso itakapovuma juu yetu kweli kweli, ndipo kondoo wa kweli wataisikia sauti ya Mchungaji wa kweli. Juhudi za kujikana nafsi zitafanywa ili kuwaokoa waliopotea, na wengi ambao wametangatanga mbali na zizi lake watarudi na kumfuata Mchungaji huyo Mkuu. Watu wa Mungu watashikamana kwa karibu sana na kumkabili adui yao kwa umoja katika uwanja wa mapambano. Kwa kuzingatia hatari yao kubwa ya aina moja inayowakabili wote, kugombania ukubwa kutakoma; hakutakuwa na mabishano kuhusu nani atakuwa mkubwa kuliko wote.... Ndipo ujumbe wa malaika wa tatu utakapozidi kuvuma na kuwa sauti kuu, na nchi yote itaangazwa kwa utukufu wa Bwana." 6T 40l.

15. Wana nini sasa juu ya vipaji vya nyuso zao hao Waadventista wasiotikisika?

"Mara tu watu wa Mungu watakapotiwa muhuri katika vipaji vya nyuso zao ----- huo si muhuri wo wote au alama inayoweza kuonekana kwa macho, bali ni kule kutulia [kujizatiti] katika kweli, kiakili na kiroho, ili wasipate kuondoshwa ----- mara tu watu wa Mungu watakapotiwa muhuri na kuwekwa tayari kwa mtikiso huo, utakuja. Naam, tayari umekwisha kuanza; hukumu [adhabu] za Mungu sasa ziko juu ya nchi, kutupa sisi onyo, ili tupate kujua kile kinachokuja." 4BC 1161.

16. Ujumbe sasa unapoendelea kuvuma sana hata kufikia kiwango cha sauti kuu, matokeo yake yatakuwaje?

a. "Bendera baada ya bendera zikavutwa chini na kuachwa mavumbini wakati kombania baada ya kombania kutoka katika Jeshi la Bwana wanajiunga na yule adui, na kabila baada ya kabila kutoka katika safu za yule adui wakajiunga na watu wa Mungu wazishikao amri zake [kumi]" 8T 41.

b. "Idadi ya kombania hii ilikuwa imepungua sana. Baadhi yao walikuwa wametikiswa na kutupwa nje na kuachwa kando ya njia. Wazembe na wale wasiojali, ambao hawakujiunga na wale waliouthamini sana ushindi na wokovu kiasi cha kuomba kwa bidii na kuteseka sana moyoni mwao kwa ajili yake, hawakuupata, nao waliachwa nyuma katika giza, na mahali pao pakajazwa mara moja na wengine waliokuwa wanaipokea ile kweli na kuingia katika safu zake." EW 271 (Angalia pia 1T 182).

c. "Bwana anao watumishi wake waaminifu, ambao wakati wa mtikiso, yaani, wakati wa kujaribiwa, wataonekana wazi. Kuna wengi walio wa thamani ambao kwa sasa wamefichwa, ambao hawajapata kupiga goti lao kwa Baali. Hawajaipata nuru ile ambayo imekuwa ikiangaza kama ndimi za moto mkali sana juu yenu ninyi. Lakini huenda ikawa ni ndani ya mtu mwenye umbile la nje la ovyo ovyo, asiyevutia, ikaweza kujionyesha tabia hiyo safi, inayong'aa, ya Ukristo ule wa kweli. Wakati wa mchana tunaangalia mbinguni bali hatuzioni nyota. Ziko kule, zimewekwa imara mahali pake katika anga hilo, lakini jicho letu haliwezi kuzipambunua. Wakati wa usiku tunauona mng'aro wao halisi." 5T 80,81.

d. "Bila kuzijali nguvu [mamlaka] zile zilizojiunga pamoja kupigana na ile kweli, idadi yao kubwa wanaamua kusimama upande wa Bwana." GC 612.

SURA YA 7

# MBELE YA WATAWALA NA WAFALME

1. Kwa njia gani wakati mwingine Mungu ameipeleka injili yake kwa wakuu wa nchi? Mt. 10:17-20; Marko 13:9-11; Mdo. 5:21,27; 25:22; Wafilipi 1:12,13.

2. Mbele ya nani watu wa Mungu watapata fursa ya kushuhudia imani yao katika siku za usoni zilizo karibu kuja?

a. "Wale wote wanaoonyesha uaminifu wao kwa kuitii Sheria yake Yehova [Amri Kumi] wajiandae kukamatwa, kuletwa mbele ya mabaraza ambayo hayana kanuni ya juu na takatifu kama ile ya Sheria ya Mungu [Amri Kumi]." 7BC 977.

b. "Wengi watalazimika kusimama katika mahakama za sheria; wengine watalazimika kusimama mbele ya wafalme [na Ma-Rais], na mbele ya wasomi wa dunia hii, kujitetea kwa ajili ya imani yao." OHC 355.

c. "Wakati hauko mbali watu wa Mungu watakapoitwa kutoa ushuhuda wao mbele ya watawala wa dunia hii. Hakuna hata mmoja katika watu ishirini anayetambua ni hatua za haraka jinsi gani tunazokwenda kuelekea kwenye hatari hiyo kubwa katika historia yetu...." OHC 355.

d. "Watakuwa na fursa ya kuipeleka nuru mbele ya wale wanaoitwa wakuu wa dunia hii, na kama ninyi mmejifunza Biblia zenu, kama mko tayari kutoa jibu kwa kila mtu awaulizaye kuhusu tumaini lililo ndani yenu kwa upole na kutetemeka, basi, adui zenu hawataweza kushindana na hekima yenu." OHC 355.

e. "Wengi wataitwa kusema mbele ya mabaraza na mahakama za sheria, pengine, wakiwa wametenganishwa na kila mmoja akiwa peke yake. Uzoefu ule ambao ungewasaidia katika wakati huo wa dharura wamepuuzia kuupata, na [sasa] mioyo yao imelemewa na mzigo mzito wa majuto kwa nafasi zilizopotezwa bure na haki zilizotupiliwa mbali." 5T 463.

3. Je, tutapimwa kama makundi au kama mtu mmoja mmoja?

a. "Washiriki wa kanisa watapimwa mmoja mmoja na kuthibitishwa. Watawekwa katika mazingira ambayo watalazimishwa kutoa ushuhuda wao kwa ajili ya ile kweli." 5T 463.

b. "Hivi sasa haionekani kwetu kama kutakuwa na uwezekano kwa ye yote kulazimika kusimama peke yake; lakini iwapo Mungu amepata kunena kupitia kwangu, basi, wakati unakuja tutakapopelekwa mbele ya mabaraza na mbele ya maelfu kwa ajili ya jina lake, na kila mmoja atalazimika kutoa sababu ya imani yake. Ndipo ukosoaji mkali utakuja kwa kila msimamo uliochukuliwa kwa ajili ya hiyo kweli. Basi, tuna haja ya kujifunza Neno la Mungu, ili tupate kujua kwa nini tunayaamini mafundisho hayo tunayoyatetea." RH 12-18-1888,

uk. 786 (Angalia pia 5T 717 na Ev 69).

4. Je, hiyo inamaanisha kwamba ni wachungaji tu, au kila mshiriki wa kanisa angejiandaa kupimwa hadharani?

"Wengi watalazimika kusimama katika mahakama za kutunga sheria; wengine watalazimika kusimama mbele ya wafalme na mbele ya wasomi wa dunia hii, kuitetea imani yao.... Hebu na asiwepo mtu ye yote anayewaza kwamba hana haja ya kujifunza, ati kwa sababu yeye hahitajiki kuhubiri kibwetani [mimbarani]. Hujui kile ambacho Mungu anaweza kutaka kutoka kwako." OHC 355.

5. Je, sisi sote tu tayari sasa kuhojiwa kwa ajili ya imani yetu?

a. "Nimeonyeshwa kwamba wengi wanaojidai kuujua ukweli wa leo hawajui wanachokiamini. Hawaujui ushahidi wa imani yao. Hawana tathmini sahihi ya kazi ya wakati huu. Wakati wa kushtakiwa kwao utakapokuja, wapo leo wanaume wanaowahubiri wengine ambao, watakapochunguza misimamo waliyo nayo, watajikuta kwamba kuna mambo mengi ambayo hawawezi kutoa sababu ya kuridhisha. Mpaka hapo watakaposhtakiwa watakuwa hawaujui ujinga mkubwa waliokuwa nao. Na wapo wengi ndani ya kanisa ambao wanayachukulia mambo kwa juu juu tu ya kwamba wanajua kile wanachokiamini; lakini, mpaka hapo mabishano yatakapotokea, hawaujui udhaifu wao. Wakitengwa mbali na wale wa imani moja na kulazimishwa kusimama mmoja mmoja, peke yake, kuelezea imani yake, hapo ndipo watakaposhangaa kuona jinsi mawazo yao yalivyochanganyikiwa kuhusu kile walichokipokea kama kweli." 5T 707.

b. "Wale walio na ujuzi wa juu juu tu wa ile kweli hawataweza kuyafafanua Maandiko, na kutoa sababu zilizo dhahiri kwa imani yao. Watachanganyikiwa, wala hawatakuwa watenda kazi wasiokuwa na sababu ya kutahayari." OHC 355.

6. Tungekuwa tukifanya nini kwa sasa ili kuwa tayari tutakapopelekwa kushtakiwa kwa ajili ya imani yetu?

a. "Niliona ya kwamba watakatifu ni lazima wapate ujuzi kamili wa ukweli wa leo, ambao watalazimika kuutetea kutokana na Maandiko hayo." EW 87.

b. "Watumishi wake Kristo hawatakiwi kuandaa hotuba yo yote iliyopangwa vizuri hapo watakapopelekwa kushtakiwa kwa ajili ya kweli waliyo nayo. Maandalizi yao sharti yafanyike siku kwa siku, kwa kuweka mioyoni mwao akiba ya kweli hizo za thamani za Neno la Mungu, kwa kujilisha mafundihso ya Kristo, na kwa njia ya maombi ili kuimarisha imani yao; hapo ndipo,

watakapopelekwa kushtakiwa, Roho Mtakatifu atawakumbusha kweli zile zile ambazo zitaifikia mioyo ya wale watakaokuja kusikiliza. Mungu ataimulika ghafula nuru yake ambayo ilipatikana kwa kuyachunguza Maandiko kwa bidii katika kumbukumbu yao kwa wakati ule ule itakapohitajika." OHC 356; CSW 41.

c. "Watu wetu wanayo haja ya kuyajua maneno aliyosema Mungu; wanahitaji kuwa na ujuzi uliopangwa vizuri wa kanuni za kweli ile iliyokwisha kufunuliwa, ambayo itawatayarisha kwa kile kinachoujia ulimwengu huu, na kuwakinga wasichukuliwe na kila upepo wa elimu [mafundisho ya dini]." 5T 273.

d. "Watu wetu wameangaliwa kama ni watu walio duni mno kuweza kufahamika, lakini mabadiliko yatakuja. Ulimwengu wa Kikristo hivi sasa unaunda matapo ambayo yatafanya uwepo ulazima wa kuwaleta watu wale wanaozishika amri [kumi za Mungu] mahali ambapo wataweza kujulikana sana.... Kila msimamo wa imani yetu utachunguzwa sana; na endapo sisi sio wanafunzi kamili wa Biblia tuliojizatiti, tuliotiwa nguvu, na kutulia, basi, hekima ya wakuu wa dunia hii itatupoteza." 5T 546.

e. "Hakuna ye yote, isipokuwa wale waliojiimarisha mioyo yao kwa zile kweli za Biblia, atakayeweza kusimama katika pambano lile kuu la mwisho." GC 593.

7. Ni jambo gani lililo la maana sana hata kuliko uwezo ule wa kutoa sababu ya imani yetu?

a. "Uwezo wa kutoa sababu ya imani yetu ni jambo zuri kuwa nalo, lakini iwapo ile kweli haiendi chini kuliko hilo, basi, mtu huyo hataokolewa kamwe. Moyo hauna budi kutakaswa na uchafu wote wa kimaadili." OHC 142.

b. "Hivi sasa mnatakiwa kujitayarisha kwa wakati ule wa kujaribiwa. Hivi sasa mnapaswa kujua kama miguu yenu imejikita juu ya Mwamba ule wa Milele. Kila mmoja wenu ni lazima awe na uzoefu [wa maisha ya Kikristo] wake mwenyewe, wala usiwategemee wengine kwa nuru yako. Utakapopelekwa kupimwa, unajuaje kama hutakuwa peke yako, pasipokuwa na rafiki ye yote wa kidunia kando yako? Je, wakati huo utaweza kutambua ya kwamba Kristo ndiye msaada wako?" OHC 356.

8. Kusudi la kushtakiwa huku hadharani ni nini?

"Mungu anakusudia kwamba kweli inayowapima watu itapewa kipaumbele na kuwa somo la uchunguzi na mjadala, hata kama ni kwa njia ya dharau iliyowekwa juu yake. Akili za watu ni lazima ziamshwe. Kila mabishano, kila shutuma, na kila singizio, vitakuwa ndiyo njia ya Mungu ya kuchokoza uchunguzi na kuziamsha akili za watu ambazo vinginevyo zingesinzia." 5T 453; RH Extra 12-11-1888, uk. 4.

## SURA YA 8

## MIUJIZA YA SHETANI

1. Je, imani ya mizimu [uchawi au mapepo] ilikuwa ni tatizo katika siku za Biblia? Kut.22:18; Law. 20:6,27; Kum. 18:9-12; Marko 5: 1-18; 9:14-29; Mdo. 16:16-18.

2. Je, nyakati fulani Shetani alijigeuzaje na kuwa kitu fulani au mtu fulani anayevutia macho kuliko yeye mwenyewe? Mwanzo 3:1-5; 1Sam. 28:6-14.

3. Je, bado anao uwezo huo wa kujigeuza mwenyewe ili apate kufanana na kitu kile anachokitaka? 2 Kor. 11:13-15.

4. Kwa kusudi gani Shetani atafanya miujiza yake katika siku za mwisho kabisa za historia ya ulimwengu huu? Ufu.16:13,14; 13:13,14; 2The. 2:9,10; Mt. 24:4,24.

5. Ni wapi imani ya mizimu ya leo [ya kisasa] ilikoanzia?

a. "Naliona kwamba kule kugonga-gonga kwa ajabu katika mji ule wa New York [Hydesville, N.Y. katika mwaka wa 1848] na mahali pengine zilikuwa ni nguvu za Shetani, na ya kwamba mambo kama hayo yangezidi kuongezeka na kuwa ya kawaida, yakiwa yamevikwa vazi la dini ili kuwalaza usingizi wale waliokwisha kudanganywa ili wajisikie ya kuwa wana usalama zaidi, na, kama ikiwezekana, kuivuta mioyo ya watu wa Mungu wapate kuyaangalia mambo hayo na kuwafanya wapate kuingiwa na mashaka juu ya mafundisho ya uweza wa Roho Mtakatifu." EW 43.

b. "Kule kugonga-gonga kwa ajabu kulikoanzisha imani ya mizimu ya kisasa hakukutokana na hila za kibinadamu wala ujanja wao, bali kulikuwa ni kazi ya moja kwa moja ya malaika wale wabaya...." GC 553.

6. Ni kwa njia ipi imani ya mizimu sasa inabadilisha mfumo wake?

"Imani ya Mizimu sasa inabadilisha mfumo wake, ikificha baadhi ya mambo yake yaliyokuwa yanachukiza, inavaa vazi la Kikristo.... Wakati ambapo zamani ilimkana Kristo na Biblia, sasa inakiri kupokea vyote viwili. GC 557,558.

7. Shetani sasa anafanya maandalizi gani maalum?

a. "Shetani kwa muda mrefu amekuwa akijitayarisha kufanya juhudi yake ya mwisho kuudanganya ulimwengu.... Kidogo kidogo ametayarisha njia kwa madanganyo yake ya kilele kwa kuiendeleza imani hiyo ya mizimu." GC 569.

b. "Roho wa Mungu pole pole anaondoka katika ulimwengu huu. Shetani pia anakusanya majeshi yake ya uovu, akiwaendea 'wafalme wa nchi na wa ulimwengu mzima' kuwakusanya chini ya bendera yake, kuwapa mafunzo kwa ajili ya 'vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi' " 7BC 983.

8. Baada ya tukio gani tunaweza kutazamia maonyesho maalum ya utendaji [wa Shetani] wa miujiza yake ya ajabu?

a. "Kwa njia ya amri ile inayoitia nguvu siku iliyowekwa na upapa na kuivunja Sheria ya Mungu, Taifa letu litajitenga kikamilifu mbali na haki. Uprotestanti utakapounyosha mkono wake juu ya ghuba kuushika kwa nguvu mkono wa mamlaka ile ya Roma, utakaponyosha juu ya shimo kubwa lenye kilindi kirefu kushikana mikono na Imani ya Mizimu, chini ya uongozi wa muungano huo wa utatu, nchi yetu itakapoikataa kila kanuni ya Katiba yake ya nchi kama serikali ya Kiprotestanti na Jamhuri, na kutunga sheria inayotangaza uongo wa upapa na madanganyo yake, basi, hapo ndipo tunaweza kujua kwamba wakati umewadia kwa utendaji wa miujiza ya Shetani na kwamba mwisho u karibu." 5T 451.

9. Je, pepo hao wabaya watatetea utunzaji wa Sabato au wa Jumapili?

"Uwezo wa kufanya miujiza uliodhihirika kupitia katika Imani ya Mizimu utatumia mvuto wake dhidi ya wale wanaochagua kumtii Mungu kuliko wanadamu. Habari kutoka kwa pepo hao

zitatangaza kwamba Mungu amewatuma kuwathibitishia wale wanaoikataa Jumapili kosa lao, wakisisitiza kwamba sheria za nchi zingetiiwa kama Sheria ya Mungu." GC 590,591.

10. Kwa njia zipi hasa Shetani atawadanganya wengi?

a. "Mandhari za kuogofya za viumbe vya ajabu hivi punde zitaonekana mbinguni, kama ishara ya uwezo ufanyao miujiza wa mashetani." GC 624.

b. "Watu watatokea wakijidai kwamba wao ndio Kristo mwenyewe, na kudai cheo na heshima kubwa ambayo ni yake Mkombozi huyo wa ulimwengu. Watafanya miujiza ya ajabu ya uponyaji na kutangaza kwamba wamepewa mafunuo kutoka mbinguni yanayopingana na ushuhuda wa Maandiko." GC 624.

c. "Wagonjwa wataponywa mbele yetu. Miujiza itatendeka mbele ya macho yetu. Je, tuko tayari kwa jaribio hilo linalotungojea wakati ishara hizo za ajabu za uongo za Shetani zitakapoonekana kwa wazi kabisa?" 1T 302.

d. "Kwa aina fulani za madanganyo, Shetani ataweza kufanya maajabu ambayo yataonekana kuwa ni miujiza halisi. Hilo ndilo alilotumainia kulifanya kuwa suala la jaribio kwa Waisraeli wakati wa ukombozi wao kutoka Misri." 2SM 52.

11. Je, [Shetani] anaponya wagonjwa kweli?

a. "Mandhari za ajabu, atakazohusika nazo sana Shetani, zitatokea. Neno la Mungu linatangaza kwamba Shetani atatenda miujiza. Atawafanya watu kuwa wagonjwa, na kisha kwa ghafula ataondoa kwao uwezo wake wa kishetani. Hapo ndipo watafikiriwa kuwa wameponywa. Matendo hayo ya uponyaji unaoonekana yatawatia Waadventista Wasabato katika jaribio." 2 SM 53.

b. "Chini ya uongozi wa pepo hao wabaya, watu watafanya miujiza. Watawafanya watu kuwa wagonjwa kwa kuwatupia tego lao [uchawi wao] juu yao, kisha watalitegua tego hilo, wakiwafanya watu wengine kusema kwamba wale waliokuwa wagonjwa wameponywa kwa mwujiza. Jambo hilo Shetani amelifanya tena na tena." 2SM 53.

c. "Ataitawala miili ya wanadamu, na kuwafanya wanaume na wanawake kuwa wagonjwa. Kisha kwa ghafula ataacha kuutumia uwezo wake huo mbaya, hapo ndipo itatangazwa kwamba mwujiza umefanyika." MM 110.

12. Je, tunaweza kutazamia kukoma kwa ishara hizi na maajabu haya ya uongo mara tu baada ya kuanza?

"Tunaonywa kwamba katika siku zile za mwisho [Shetani] atafanya kazi yake kwa kutumia ishara na maajabu ya uongo. Naye ataendelea na maajabu hayo mpaka mlango wa rehema utakapofungwa, ili apate kuwaonyesha ya kwamba huo ni ushahidi wa kwamba yeye ni malaika wa nuru wala sio wa giza." 2SM 51; 7BC 911; 5BC 1099.

13. Ni mwujiza gani wa aina ile ya Eliya utakaotendwa na baadhi ya wafuasi waaminifu wa Shetani?

a. "Katika Neno imeelezwa kwamba yule adui atafanya kazi yake kupitia kwa mawakala wake waliojitenga na imani, nao wataonekana kana kwamba wanafanya miujiza, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje mbele ya wanadamu." 2SM 54.

b. "Tusiyaamini madai ya wanadamu. Kama Kristo anavyoeleza, wanaweza kudai kwamba wanafanya miujiza ya kuponya wagonjwa. Je! hilo ni la ajabu, wakati nyuma yao wakati uo huo anasimama yule mlaghai mkuu [Shetani], mtenda miujiza ambaye hapo baadaye atafanya moto ushuke kutoka mbinguni uje mbele ya wanadamu?" 2SM 49.

c. "Naliona ya kwamba punde ingefikiriwa kuwa ni kufuru kusema vibaya juu ya kule kugonga-gonga [kwa ajabu], na ya kwamba kungeenea zaidi na zaidi [katika sehemu nyingi], ya kwamba uwezo wa Shetani ungeongezeka, na baadhi ya wafuasi wake waaminifu wangekuwa na uwezo wa kufanya miujiza, na hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje mbele ya wanadamu." EW 59,86,87.

d. "Watumishi wa Mungu, nyuso zao zikiwa zimeangazwa na nuru na kung'aa kwa kujitoa kwao wakf, wataharakisha kwenda kila mahali kutangaza ujumbe ule utokao mbinguni. Kwa maelfu ya sauti, ulimwenguni kote, onyo hilo litatolewa. Miujiza itatendeka, wagonjwa wataponywa, na ishara na maajabu zitafuatana na hao waaminio. Shetani pia atafanya kazi yake kwa ajabu zake za uongo, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje mbele ya wanadamu. Ufunuo 13:13. Kwa njia hiyo wakazi wa dunia hii watafikishwa mahali pa kuwa na msimamo wao." GC 612.

e. "Ni ajabu zile za uongo za Shetani ambazo zitauteka ulimwengu, naye atafanya moto ushuke kutoka mbinguni uje mbele ya wanadamu. Yeye atafanya miujiza; na uwezo huo wa ajabu wa kufanya miujiza utaifagilia dunia yote kwake. 2SM 51.

f. "Yeye anadai kuwa ndiye Kristo, naye ataingia na kujifanya kama ndiye mganga mkuu mmishonari. Atafanya moto ushuke kutoka mbinguni uje mbele ya wanadamu, kuthibitisha kwamba yeye ndiye Mungu." MM 87,88.

14. Je, huo ni moto kweli au una mwonekano tu wa moto?

" 'Anafanya maajabu makuu, hata kufanya moto ushuke kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu, na kuwadanganya wakaao duniani kwa njia ya miujiza ile ambayo anao uwezo wa kuifanya.' Ufunuo 13:13,14. Sio ulaghai mtupu unaotabiriwa hapa. Watu watadanganywa kwa miujiza ambayo mawakala wa Shetani wanao uwezo wa kuifanya, sio ile wanayojifanya kuifanya." GC 553.

15. Maadui wake Kristo watauangaliaje uwezo huo wa kufanya miujiza?

a. "Wafuasi wa papa, wanaojigamba kwa miujiza yao kuwa ndiyo ishara ya hakika ya kanisa la kweli, watadanganyika bila shida yo yote kwa uwezo huo ufanyao maajabu." GC 588.

b. "Maadui wake Kristo, wakiwa wamechochewa na Shetani, watakapowataka [watu wa Mungu] kuwaonyesha mwujiza fulani, wao wangewajibu kwa upole kama vile Mwana wa Mungu alivyomjibu Shetani, akisema, 'Imeandikwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako." Kama hawatashawishwa na ushuhuda huo uliovuviwa, basi, maonyesho ya uweza wa Mungu yasingeweza kuwaletea faida yo yote." 4SG-a 150.

c. "Wale wasioamini watawataka [watu wa Mungu] kutenda mwujiza fulani, kama wao wanasadiki kwamba uwezo wa pekee wa Mungu umo ndani ya kanisa lao, na kwamba wao ni wateule wa Mungu. Wasioamini, wanaoteseka kwa udhaifu mbalimbali wa mwili, watawataka kuwafanyia mwujiza juu yao, kama Mungu yu pamoja nao. Wafuasi wa Kristo wangepaswa kuuiga mfano wa Bwana wao. Yesu, pamoja na uweza wake kama Mungu, hakufanya matendo yo yote makuu kwa ajili ya kumfurahisha Shetani. Wala watumishi wake Kristo hawawezi kufanya hivyo. Wangewaelekeza wale wasioamini kwenye neno lile lililoandikwa, yaani, ushuhuda ule uliovuviwa, kuwa ndio ushahidi unaoonyesha kwamba wao ndio watu wa Mungu watiifu, na warithi wa wokovu." 4SG-a 151.

16. Watu wengi watafikiri ni nani anayefanya maajabu hayo ndani ya makanisa yao?

a. "Kabla ya hukumu za Mungu za mwisho kuja juu ya dunia hii patakuwa na uamsho wa zamani wa kumcha Mungu ambao haujapata kushuhudiwa tangu siku zile za mitume.... Adui yule wa roho zetu anataka kuizuia kazi hiyo; na kabla ya tapo kama hilo kuja, atajaribu kulizuia kwa kuleta uamsho wa bandia. Katika makanisa yale atakayoweza kuyaweka chini ya uwezo wake wa ulaghai, atafanya ionekane kana kwamba mbaraka ule wa pekee wa Mungu [Roho Mtakatifu] umekwisha kumwagwa; patakuwa na mwonekano wa kile kitakachofikiriwa kuwa ni ari kubwa katika mambo ya kidini. Makundi kwa makundi watashangilia sana wakisema kwamba Mungu anafanya maajabu kwa ajili yao, wakati kazi hiyo ni ya roho yule mwingine [mapepo]. Chini ya vazi la dini, Shetani atajaribu kuueneza mvuto wake juu ya ulimwengu wa Kikristo." GC 464.

b. "Kabla ya kutolewa kwa ile sauti kuu ya malaika yule wa tatu, yeye [Shetani] anatumaini kuwadanganya wale walio waaminifu na kuwaongoza kufikiri kwamba Mungu bado anafanya kazi kwa ajili ya makanisa hayo [yaliyoasi]. Lakini nuru itaangaza, na wale wote walio waaminifu watatoka katika makanisa hayo yaliyoanguka na kusimama pamoja na wale wa Masalio [Waadventista Wasabato]." EW 261.

c. "Kwa njia ya Imani ya Mizimu, miujiza itafanyika.... na maajabu mengi yasiyokanushika yatatendwa. Na kwa vile mapepo hayo yatadai kuwa yana imani na Biblia, na kuziheshimu taasisi za kanisa, basi, kazi yao itakubalika kuwa ni maonyesho ya uwezo wa Mungu." GC 588.

17. Je, miujiza itaambatana pia na huduma ya watu wa Mungu wakati wa ile "sauti kuu"?

"Katika njozi za usiku picha zilipita mbele yangu za Tapo Kuu la Matengenezo miongoni mwa watu wa Mungu. Wengi walikuwa wakimsifu Mungu. Wagonjwa waliponywa, na miujiza mingine ilitendeka. Roho ya maombezi ilionekana, kama vile ilivyoonekana kabla ya siku ile kuu ya Pentekoste. Mamia kwa maelfu walionekana wakizitembelea familia, na kufungua mbele yao Neno la Mungu. Mioyo ilichomwa kwa uweza wa Roho Mtakatifu, na roho ya uongofu wa kweli ilionekana. Kila upande milango ya kuitangaza ile kweli ilifunguliwa. Ulimwengu ulionekana kana kwamba umeangazwa na mvuto kutoka mbinguni. Mibaraka mingi ilipokewa na watu wake Mungu waliokuwa wakweli na wanyenyekevu." 9T 126.

18. Tuiangalieje miujiza hiyo? Je, itakuwa jaribio kama ilivyokuwa katika siku za Eliya?

a. "Njia aliyoitumia Kristo kufanya kazi yake ilikuwa ni ile ya kulihubiri Neno, na kupunguza mateso kwa matendo ya miujiza yake ya uponyaji. Walakini, mimi nimeagizwa kwamba sisi hatuwezi kufanya kazi kwa njia hiyo kwa wakati huu, maana Shetani atatumia uwezo wake kwa njia hii ya kufanya miujiza. Watumishi wa Mungu leo wasingeweza kufanya kazi yao kwa njia ya miujiza, kwa sababu miujiza ya uponyaji ya bandia, inayodaiwa kuwa inatoka kwa Mungu, itafanywa." 2SM 54.

b. "Kama hatuipokei ile kweli na kuipenda, basi, tunaweza kujikuta tumo miongoni mwa kundi la wale watakaoiangalia miujiza inayotendwa na Shetani na kuiamini. Mambo mengi ya ajabu yataonekana kana kwamba ni miujiza ya ajabu, ambayo yangeangaliwa kuwa ni madanganyo yaliyobuniwa na baba wa huo uongo [Ibilisi]." 2SM 53.

c. "Shetani, akiwa amezungukwa na malaika zake wabaya, akijidai kwamba yeye ndiye Mungu, atafanya miujiza ya kila namna, kuwadanganya, yamkini, hata walio wateule. Watu wa Mungu hawatauona usalama wao katika kutenda miujiza, maana Shetani, kwa kuigiza miujiza ile watakayoitenda, atafanya miujiza yake ya bandia [uongo]." 9T 16 (Angalia pia 2SM 55).

19. Tutabainishaje kati ya miujiza ile ya kweli na ile ya uongo?

a. "Iwapo wale ambao kupitia kwao miujiza inatendeka, kwa sababu ya maonyesho hayo wanaelekea kutoa udhuru wao kwa kuiacha Sheria ya Mungu [Amri Kumi], tena wanaendelea katika uasi wao, ijapokuwa wanao uwezo [ wa kufanya miujiza] kwa kiwango kikubwa kiwacho chote, haifuati kwamba hao wanao uwezo mkuu wa Mungu. Kinyume chake, huo ni uwezo wa kufanya miujiza wa yule mlaghai mkubwa [Shetani]." 5BC 1099.

b. "Madanganyo makubwa ya mwisho karibu yataonekana mbele yetu. Mpinga Kristo atafanya matendo yake ya ajabu mbele ya macho yetu. Kwa karibu sana [miujiza] ile ya bandia itafanana na ile ya kweli hata itakuwa vigumu sana kuitofautisha isipokuwa kwa njia ya Maandiko Matakatifu. Kwa ushuhuda wa hayo [Maandiko] kila usemi na kila mwujiza ni lazima upimwe." GC 593.

c. "Maonyesho ya miujiza kamwe hayatachukua mahali pa Biblia." 2SM 48.

20. Ni madanganyo gani ya Shetani yanayofanikiwa sana na kuipumbaza akili kwa kuyaangalia?

a. "Shetani anajipenyeza katika mioyo ya maelfu kwa kuja katika umbile la rafiki zao waliokufa.... Kwa njia ya Imani ya Mizimu wengi miongoni mwa wagonjwa, wafiwa, na wadadisi, huongea na pepo hao wabaya. Wale wote wanaothubutu kufanya hivyo wako katika uwanja wa hatari." RH 9-7-1911.

b. "Hayo ni madanganyo yake Shetani yanayofanikiwa sana na kuipumbaza akili kwa kuyaangalia, ----- ambayo yamekusudiwa kuzigusa hisia za huruma zilizomo ndani ya mioyo ya wale waliowazika wapendwa wao kaburini. Malaika hao wabaya wanakuja katika umbile lile lile la wapendwa wale [waliokufa], na kusimulia matukio yanayohusu maisha yao, na kutenda matendo yale yale waliyotenda walipokuwa wangali hai. Kwa njia hii [malaika hao waovu] wanawashawishi watu kuamini kwamba rafiki zao waliokufa ni malaika sasa, wanarukaruka angani juu yao, na kuzungumza nao. Malaika hao waovu, wanaojifanya [wanaojigeuza] kuwa rafiki wale waliokufa, wanaangaliwa kwa namna fulani ya ibada ya sanamu, na kwa wengi neno lao lina uzito kuliko Neno la Mungu." ST, 8-26-1889.

21. Kwa jinsi gani [mwujiza] ule wa bandia unaonekana kuwa ni wa kweli?

a. "[Shetani] anao uwezo wa kuleta mbele ya watu umbile lile lile la rafiki zao waliokufa. [Umbile lile] la bandia halina dosari yo yote; umbile lake ni lile lile la sikuzote, maneno yake, na sauti yake huigizwa kabisa kwa namna ya kushangaza sana." GC 552.

b. "Wapendwa wao wataonekana wakiwa wamevaa mavazi ya nuru [ishara ya mapepo], mwonekano wao utakuwa sawa kabisa na ule uliojulikana wakati walipokuwa hapa duniani." RH 4-1-1875.

22. Je, jambo hilo litakuwa ni uzoefu wa mtu mmoja tu au watu wengi watakutana ana kwa ana na malaika hao wabaya wanaokuja katika umbile la wapendwa wetu waliokufa?

a. "Wengi watakutana ana kwa ana na roho hizo za mashetani [mapepo] zikija katika umbile lile lile la ndugu zao au rafiki zao [waliokufa] na kuwatangazia uzushi [mafundisho ya dini ya uongo] wa hatari kubwa sana. Wageni hao wanaokuja kututembelea wataugusa moyo wa huruma ulio ndani yetu na kufanya miujiza ili kuyatilia nguvu madanganyo yao." GC 560.

b. "Si neno gumu kwa malaika hao wabaya kuja katika umbile la watakatifu na wenye dhambi waliokwisha kufa, na kuigiza maumbile yao ili yaweze kuonekana kwa macho ya kibinadamu. Ishara hizo zitatokea mara kwa mara, na mambo ya kushangaza sana yataonekana kadiri tutakavyokaribia mwisho ule wa wakati." Ev 604.

c. "Naliona ya kwamba watakatifu wanalazimika kuijua kweli kwa ukamilifu, ambayo wataweza kuitetea kutoka katika Maandiko hayo. Yawapasa kujua hali ya wafu ikoje; maana roho zile za mashetani zitawatokea, zikijidai kuwa ni wale marafiki zao wapendwa na ndugu zao [waliokufa], ambao watawatangazia kwamba Sabato imebadilishwa, pamoja na mafundisho mengine pia ambayo hayana msingi katika Biblia. Watafanya kila wawezalo kuamsha hisia za

huruma ndani ya mioyo yao, kisha watafanya miujiza mbele yao kuthibitisha kile wanachowatangazia."  EW 87.

23. Ni akina nani tena ambao roho hizo zidanganyazo [mapepo] zitakuja katika umbile lao?

a. "Mitume, kama roho hizo zidanganyazo zitakavyokuja katika umbile lao, watafanywa wayakanushe maneno yale waliyoyaandika wakiongozwa na Roho Mtakatifu walipokuwa wangali hapa duniani.  Watakana asili ya kimbingu ya Biblia...."  GC 557.

b. "Yule adui [Shetani] anajiandaa kuihadaa dunia yote kwa njia ya uwezo wake wa kufanya miujiza.  Atachukua umbile lile lile la malaika wale wa nuru, atakuja katika umbile lile lile la Yesu Kristo."  2SM 21,96.

## SURA YA 9

## SHETANI KATIKA UMBILE LA KRISTO

1. Kilele cha madanganyo ya Shetani ni nini? Yeye atajigeuza mwenyewe ili kuwa nani?

a. "Pambano litaendelea kuwa kali na kali zaidi. Shetani atachukua uwanja [wa mapambano] na kuja katika umbile lile lile la Kristo. Atakielezea vibaya, atakitumia vibaya, na kupotosha kila kitu kwa kadiri atakavyoweza, ili kuwadanganya, yamkini, hata walio wateule." TM 411.

b. "Nguvu [ya uovu] kutoka chini inafanya kazi yake kuzileta mandhari zile za mwisho katika mfululizo ule wa matukio ----- Shetani atakuja kama Kristo, na kufanya kwa njia ya madanganyo yote ya udhalimu wake ndani ya wale wanaojifungamanisha pamoja katika vyama vile vya siri." 8T 28; 6BC 1106; 7BC 911.

c. "Iwapo watu wanadanganyika kirahisi sasa, watasimamaje wakati ule Shetani atakapokuja katika umbile lile lile la Kristo, na kufanya miujiza? Ni akina nani ambao hawatatekwa kwa maelezo yake potofu wakati ule utakapofika ----- atakapojidai ya kuwa yeye ni Kristo wakati yeye ni Shetani tu ila amechukua [ameigiza] umbile halisi la Kristo, na kuonekana kwa macho kuwa anazitenda kazi zake Kristo? Ni kitu gani kitakachowashika watu wa Mungu wasiweze kutoa utii wao kwa makristo wa uongo? 'Wala msiwafuate' (Luka 17:23)."

2SM 394 (Angalia pia 2SM 58).

2. Kwa jinsi gani Shetani anakaribia sana kufanana na Kristo?

a. "Ilikuwa ni kwa njia ya kuonyesha uwezo wake wa ajabu, kwa kumfanya yule nyoka chombo chake, Shetani alisababisha anguko la Adamu na Hawa kule Edeni. Kabla ya mwisho wa wakati atazidi kufanya miujiza yake mikubwa zaidi. Kwa kadiri ya upeo wa uwezo wake ulivyo, atafanya miujiza halisi.... Lakini kuna mpaka ambao Shetani hawezi kuuvuka; na hapo ndipo anapotumia madanganyo yake ili kumsaidia kwa kuigiza kazi [mwujiza] ile ambayo hana uwezo halisi wa kuifanya. Katika siku hizi za mwisho ataonekana kwa njia ambayo atawafanya wanadamu wapate kuamini ya kwamba yeye ndiye Kristo amekuja mara ya pili duniani. Kwa hakika atajigeuza mwenyewe na kuwa malaika wa nuru. Lakini ijapokuwa atachukua sura kama ile ya Kristo kwa kila hali, kwa kadiri ya mwonekano wa nje utakavyokuwa, hataweza kumdanganya mtu ye yote isipokuwa wale ambao, kama Farao, wanajaribu kuipinga kweli [Yoh.17:17]" 5T 698.

b. "Shetani atafanya kazi yake kwa madanganyo yote ya udhalimu na kuja katika umile lile lile la Kristo; na kama ingaliwezekana, angewadanganya hata walio wateule. Kwa vile [umbile] lile la bandia linafanana sana na lile halisi, je! si jambo la maana ya kuwa mpate kujihadhari, ili mtu awaye yote asipate kuwadanganya ninyi?" 2SM 87.

c. "Shetani hajaruhusiwa kuigiza kuja kwa jinsi ile ile atakavyokuja Yesu mara ya pili."

GC 625.

3. Shetani atafanya nini na kusema nini na watu wataitikiaje?

a. "Kama tendo lake la kilele katika mfululizo mkubwa wa madanganyo yake, Shetani mwenyewe atakuja katika umbile lile lile la Kristo. Kwa muda mrefu kanisa limetangaza kwamba linatazamia marejeo ya Mwokozi kama utimilizo wa matumaini yake. Sasa yule mlaghai mkuu [Shetani] atafanya ionekane kana kwamba Kristo amekwisha kuja. Katika sehemu mbalimbali za dunia, Shetani atajionyesha mwenyewe mbele ya watu kama kiumbe chenye utukufu kinachong'aa kwa mng'ao unaotia macho kiwi, kufanana na maelezo yale yaliyotolewa na Yohana katika kitabu cha Ufunuo kumhusu Mwana wa Mungu. Ufunuo 1:13-15. Utukufu ule unaomzunguka [Shetani] unazidi kiwango cha [utukufu wa] kitu cho chote yalichopata kukiona macho ya kibinadamu. Kelele za shangwe zinasikika hewani: 'Kristo amekuja! Kristo amekuja!' Watu wanaanguka chini mbele yake na kumsujudu, wakati yeye anainua mikono yake juu, na kutamka mibaraka yake juu yao, kama vile Kristo alivyowabariki wanafunzi wake alipokuwa hapa duniani. Sauti yake ni nyororo na tulivu, lakini ni tamu sana kama muziki. Kwa sauti ya upole, iliyojaa huruma anatoa baadhi ya mafundisho ya kweli zile zile nzuri za mbinguni ambazo Kristo alizinena; anaponya

magonjwa ya watu, kisha, akiwa katika umbile lile la kuigiza la Kristo, anadai kwamba ameibadili Sabato [Jumamosi] kuwa Jumapili, naye anawaamuru wote kuitakasa siku hiyo [Jumapili] aliyoibariki yeye. Anawatangazia kwamba wale wanaoendelea kuitakasa siku ya saba wanalikufuru jina lake kwa kukataa kuwasikiliza malaika zake [mapepo] aliowatuma kwao kuwapa nuru ya kweli. Hayo ndiyo madanganyo yake yenye nguvu, ambayo yatawateka karibu watu wote. Kama wale Wasamaria walivyodanganywa na Simoni Mchawi, makundi na makundi ya watu, kuanzia kwa wadogo na kwenda kwa wakubwa, watayasikiliza maneno hayo ya kichawi, wakisema: Huu ndio 'uweza mkuu wa Mungu.' " GC 624,625.

b. "Kwa kadiri kuja kwa Bwana Yesu mara ya pili kunavyozidi kukaribia, ndivyo nguvu za Shetani zinavyozidi kuinuka kutoka chini. Shetani sio tu kwamba ataonekana kama mwanadamu, bali atakuja katika umbile lile lile la Kristo; na ulimwengu huu ulioikataa kweli [Biblia] utampokea kama Bwana wa mabwana na Mfalme wa wafalme." 5BC 1105,1106.

4. Je, ataweza kupokewa hata na wakuu wa serikali?

"Akiwa amejigeuza kama malaika wa nuru, atatembea hapa duniani kama mtenda maajabu; kwa lugha tamu atatoa maoni ya hali ya juu. Maneno mazuri yatasemwa naye na matendo mazuri yatatendwa naye. Kristo atakuwa ameigizwa kabisa kimaumbile, lakini katika jambo moja itakuwapo tofauti kubwa sana. Shetani atawageuza watu wasiitii Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Ukiliondoa jambo hilo, kwa vizuri sana ataiigiza haki, kama ingaliwezekana, angeweza kuwadanganya hata walio wateule. Wafalme waliovikwa taji, Ma-Rais, Watawala katika ngazi za juu, watainamisha vichwa vyao chini na kukubaliana na nadharia zake potofu." FE 471,472.

5. Tutafanyaje tutakapoamriwa kumsujudu [Shetani]?

Shetani alikuja kama malaika wa nuru katika nyika ile ya majaribu ili kumdanganya Yesu; naye haji kwa mwanadamu katika umbile la kutisha, kama picha yake inavyoonyeshwa wakati mwingine, bali kama malaika wa nuru. Atakuja katika umbile lile lile la Kristo, akifanya miujiza mikubwa; na watu watajitupa chini na kumwabudu kama Yesu Kristo. Tutaamriwa kumwabudu kiumbe huyo, ambaye ulimwengu utamtukuza kama Kristo. Tutafanyaje, basi? Waambieni ya kwamba Kristo ametuonya sisi dhidi ya adui kama huyo [Mt.24:23-28], ambaye ni adui mbaya mno wa mwanadamu, lakini ambaye anajidai kwamba yeye ndiye Mungu; tena kwamba Kristo atakapoonekana, atakuja kwa nguvu na utukufu mwingi, akiandamana na malaika kumi elfu mara kumi elfu na maelfu mara maelfu; na ya kwamba atakapokuja sisi tutaijua sauti yake." 6BC 1105,1106; RH 12-18-1888, uk. 787.

6. Kwa upeo gani makanisa yale yaliyoasi yatamtukuza Shetani hatimaye?

"Katika kizazi hiki Mpinga Kristo ataonekana kuwa ndiye Kristo hasa, na hapo ndipo Sheria ya Mungu [Amri Kumi] itakapobatilishwa kabisa na mataifa yote ya dunia yetu. Uasi huo dhidi ya Sheria takatifu ya Mungu utakuwa umekomaa kabisa. Lakini Kiongozi halisi wa uasi huo wote ni Shetani aliyejivika mavazi kama malaika wa nuru. Watu watadanganyika, nao watamtukuza yeye na kumweka mahali pa Mungu, na kumfanya kuwa Mungu. Lakini Mungu mwenye uwezo wote ataingilia kati, na kwa yale makanisa yaliyoasi yatakayoungana katika kumtukuza Shetani, hukumu itatamkwa hivi: 'Kwa sababu hiyo mapigo yake yatakuja katika siku moja, mauti, na huzuni, na

njaa, naye atateketezwa kabisa kwa moto. Kwa maana Bwana Mungu aliyemhukumu ni mwenye nguvu.' " TM 62.

7. Kumwagwa kwa ghadhabu ya Mungu (mapigo saba ya mwisho) kutatokea lini kuhusiana na kuja kwa Shetani katika umbile hilo la Kristo?

a. "Kidogo kidogo ametayarisha njia kwa madanganyo yake ya kilele kwa kuanzisha Imani ya Mizimu. Bado hajafikia ufanikishaji kamili wa hila zake; lakini utafikiwa katika sehemu ile itakayosalia ya mwisho wa wakati. Nabii anasema: 'Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura,... Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi.' Ufunuo 16:13,14. Ukiacha wale wanaolindwa kwa nguvu ya Mungu, kwa njia ya imani katika neno lake, ulimwengu wote utafagiwa na kuingia katika safu za madanganyo hayo. Kwa haraka sana watu wanalazwa usingizi katika usalama wa kufisha, kuja kuamshwa tu na kule kumwagwa kwa ghadhabu ya Mungu." GC 561,562.

b. "Baada ya kumpa kisogo Yesu, watayavuta mawazo ya ulimwengu yawaelekee wao na miujiza yao pamoja na maajabu yao ya uongo, ambayo wanadai yanayazidi sana matendo [miujiza] yale ya Kristo. Kwa njia hiyo ulimwengu wote utanaswa katika mtego, na kulazwa usingizi wakidhani wako salama, wasiweze kugundua udanganyifu wao mkuu mpaka pale mapigo yale saba ya mwisho yatakapomiminwa." EW 266.

c. "Lakini watu wa Mungu hawatapotoshwa. Mafundisho ya Kristo huyo wa uongo hayapatani na Maandiko. Baraka yake inatamkwa juu ya wale wanaomsujudu mnyama na sanamu yake, yaani, kundi lile lile hasa ambalo juu yao Biblia inatangaza kwamba ghadhabu ya Mungu isiyochanganywa na maji itamiminwa." GC 625.

8. Kwa muda gani Shetani ataendelea kubaki hapa duniani katika umbile lake linalofanana na lile la Kristo?

Hakuna maelezo yo yote juu ya hoja hii. Ni wazi hataweza kuonekana wakati ule wa pigo la saba, ama sivyo, watu wangemgeukia kwa hasira, kwa maana imeandikwa hivi: "Lakini wote wanaungana na kuwatupia shutuma zao kali sana wachungaji [wao waliowadanganya]."

GC 655.

9. Tutajiandaaje kwa madanganyo hayo ya Shetani ili tupate kuupinga uwezo wake wa ajabu wa kufanya miujiza?

a. "Nendeni kwa Mungu ninyi wenyewe, ombeni kwamba mpate kuelimishwa na mbingu, ili mpate kujua ya kwamba mnaijua ile kweli, ili uwezo ule wa Shetani ufanyao miujiza ya ajabu utakapojidhihirisha, na adui yule kuja kama malaika wa nuru, mpate kubainisha miujiza ya kweli ya Mungu na miujiza ya bandia ya mamlaka ile ya giza." RH 12-24-1889, uk.3.

b. "Wengi walioupokea ujumbe [wa malaika] wa tatu hawakuwa wameupata uzoefu katika ujumbe ule wa kwanza wa aina mbili. Shetani alilijua jambo hilo, na jicho lake baya lilikuwa juu

yao apate kuwaangusha; lakini malaika yule wa tatu alikuwa anawaelekeza macho yao kuangalia patakatifu pa patakatifu, na wale waliokuwa wameupata uzoefu huo katika ujumbe uliopita walikuwa wanawaonyesha njia ya patakatifu pale pa mbinguni. Ujumbe huo [wa aina tatu] ulionyeshwa kwangu kama ndiyo nanga kwa watu wa Mungu. Wale wanaouelewa na kuupokea watalindwa wasiweze kufagiliwa mbali na madanganyo mengi ya Shetani." EW 256.

10. Je, Waadventista Wasabato wote wanakubaliana kwamba Shetani atakuja katika umbile lile lile la Kristo kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema?

La, hawakubaliani. Wanafunzi wengi wa Biblia na Roho ya Unabii walio na uwezo [wa kuyajua Maandiko] wanaweka kuja kwa Shetani katika umbile la Kristo wakati ule wa pigo la sita. Madondoo makuu mawili ya E.G. White wanayotoa kuwaunga mkono katika mtazamo huo ni haya:

a. "Kidogo kidogo ametayarisha njia kwa madanganyo yake ya kilele kwa kuanzisha Imani ya Mizimu. Bado hajafikia ufanikishaji kamili wa hila zake; lakini utafikiwa katika sehemu itakayosalia ya wakati ule wa mwisho. Nabii anasema: Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura;... Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi."

GC 561,562.

b. "Mandhari za kuogofya za viumbe vya ajabu hivi punde zitaonekana mbinguni, zikiwa ni ishara ya uwezo ule wa mashetani ufanyao miujiza. Roho za mashetani zitawaendea wafalme wa nchi na wa ulimwengu wote, kuwafunga katika madanganyo hayo, na kuwahamasisha wajiunge na Shetani katika pambano lake la mwisho dhidi ya serikali ile ya mbinguni. Kwa njia ya wajumbe hao [roho za mashetani], watawala na raia watadanganyika kwa njia ile ile moja. Watu watatokea wakijidai kuwa wao ndio Kristo Mwenyewe, na kudai cheo chake na heshima kubwa ambayo ni yake Mkombozi huyo wa ulimwengu. Watafanya miujiza ya ajabu ya uponyaji na kutangaza kwamba wamepewa mafunuo kutoka mbinguni yanayopingana na ushuhuda wa Maandiko.

"Kama tendo lake la kilele katika mfululizo wa matukio ya madanganyo yake, Shetani mwenyewe atakuja katika umbile lile lile la Kristo." GC 624.

Matumizi ya Dada White ya kifungu cha maneno kisemacho "sehemu iliyosalia ya wakati ule wa mwisho" na matumizi ya lugha ya pigo lile la sita kuelezea kuja kwa mwisho kwa Shetani katika umbile lile la Kristo huonekana kuwa ni hoja nzito zinazopendekeza madanganyo hayo kutokea katika kipindi kile cha pigo la sita.

Walakini, njia hiyo ya kufikiri si lazima kwamba itufikishe kwenye hitimisho hilo. Kifungu cha maneno kisemacho "sehemu iliyosalia ya wakati ule wa mwisho" hakielekezi mawazo kwa siku zile za mbele tu. Dada White anasema kwamba sisi tumo katika wakati huo hivi sasa: "Shetani kama jenerali mwenye nguvu ameutwaa uwanja wa mapambano, na katika sehemu iliyosalia ya wakati ule wa mwisho anafanya kazi kwa kutumia njia zote zinazoweza kufikirika ili kufunga mlango dhidi ya nuru ile ambayo Mungu angetaka iwafikie watu wake." RH Extra 12-24-1889, uk. 3. "Sisi tunaishi katika sehemu iliyosalia ya wakati ule wa mwisho." Ev 217 (1903).

Zaidi ya hayo, matumizi yake ya lugha hiyo ya pigo la sita hayajawekewa mipaka kwa kipindi fulani cha mbele. Ni kweli kwamba mashetani yanauendea ulimwengu wote katika kipindi kile cha pigo la sita, lakini hivyo ndivyo hasa Shetani anavyofanya leo. "Roho wa Mungu anaondolewa taratibu kutoka ulimwenguni humu. Pia Shetani anayakusanya [sasa] majeshi yake ya uovu, akiwaendea 'wafalme wa nchi na wa ulimwengu wote,' kuwakusanya chini ya bendera yake, kuwapa mafunzo kwa ajili ya "vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi.' " 7BC 983 (1890).

Katika nuru ya madondoo hayo mawili ya E.G. White tunaweza kuhitimisha kwamba ni sababu ya maana kabisa ya kutumia maneno haya "sehemu iliyosalia ya wakati ule wa mwisho" na Shetani kwenda kwa "wafalme wa nchi..." kuhusu kipindi fulani kitakachokuja kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema. Hivyo kilele cha madanganyo yake, yaani, kuja kwake katika umbile lile la Kristo, kunaweza kuwekwa pia kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema.

## SURA YA 10

## ROHO MTAKATIFU

1. Ni somo gani ambalo Kristo alipenda sana kuongea juu yake?

"Kristo, Mwalimu Mkuu, alikuwa na masomo mbalimbali mengi sana ya kuchagua [kuongea juu yake], lakini lile aliloongelea sana juu yake lilikuwa ni juu ya kipawa kile cha Roho Mtakatifu." 1SM 156.

2. Katika mpango wa Mungu kwa ajili ya ukombozi wetu, kipawa hiki cha Roho kina umuhimu gani kwetu?

a. "Katika kipawa hicho cha Roho, Yesu alimpa mwanadamu wema mwingi sana ambao mbingu iliweza kutoa." OHC 150.

b. "Kabla hajajitoa mhanga yeye mwenyewe kuwa dhabihu yetu, Kristo alitafuta kipawa cha maana sana, kilicho kamili, ili kuwapa wafuasi wake, kipawa ambacho kingeleta karibu sana nao nguvu zile za neema yake zisizokuwa na kikomo. 'Nami nitamwomba Baba,' alisema, 'naye atawapa Msaidizi Mwingine [Mfariji].' " DA 668,669.

c. "Roho Mtakatifu alikuwa ndiye kipawa cha juu kuliko vyote ambacho [Kristo] aliweza kumwomba Baba yake kwa ajili ya kuwatukuza watu wake. Roho huyo ilikuwa atolewe kama njia ya kuwazaa mara ya pili, na pasipo huyo kafara ya Kristo [msalabani] isingekuwa na faida yo yote kwetu." DA 671.

3. Je, hivi sisi tunakithamini ipasavyo kipawa hiki kilichoahidiwa kwetu?

"Muda mfupi tu kabla ya kuwaacha wanafunzi wake na kwenda kwenye majumba yale ya kifalme mbinguni, Yesu aliwatia moyo kwa kuwapa ahadi hiyo ya Roho. Ahadi hiyo ni yetu sisi kama vile ilivyokuwa yao, lakini ni mara chache jinsi gani imewekwa mbele ya watu wetu, na kule kupokewa kwake kuongelewa juu yake katika kanisa. Kama matokeo ya kimya hicho juu ya somo hili kuu la maana sana, ni ahadi gani tunayojua habari zake kidogo kuhusu kutimizwa kwake kabisa kuliko ahadi hiyo ya thamani ya kipawa hicho cha Roho Mtakatifu, ambacho kwacho ufanisi

utatolewa kwa kazi yetu yote ya kiroho? Ahadi ya Roho Mtakatifu kwa nadra inatajwa katika hotuba zetu [mahubiri yetu], yaani, inagusiwa kwa nasibu, na hayo ndiyo yote [kuhusu ahadi hiyo]. Unabii umehubiriwa sana, mafundisho ya Biblia yamefafanuliwa; lakini kile ambacho ni cha muhimu kwa kanisa ili wapate kukua katika nguvu za kiroho na ufanisi, ili mahubiri yaweze kuchoma mioyo ya watu, na roho zipate kuongolewa kwa Mungu, kwa sehemu kubwa kimeachwa katika mahubiri ya wachungaji wetu." TM 174 (Angalia pia 8T 21).

4. Je, tunapaswa kuziondolea mbali dhambi zetu zote kabla hatujampokea Roho Mtakatifu, au Roho Mtakatifu ndiye anayetusaidia sisi kuziondolea mbali dhambi zetu? Yohana 16:7-9.

a. "Pasipo utendaji wa Mungu, mwanadamu asingeweza kufanya jema lo lote. Mungu anamtaka kila mtu apate kuifikilia toba, lakini mtu hawezi hata kutubu isipokuwa kama Roho Mtakatifu anafanya kazi moyoni mwake." 8T 64.

b. "Ni Roho anayetuhakikishia dhambi zetu, naye, kwa kibali cha mwanadamu huyo, anaziondoa dhambi toka moyoni mwake." OHC 152.

c. "Bwana Yesu anatenda kazi yake kwa njia ya Roho Mtakatifu, maana huyo ndiye mwakilishi wake [hapa duniani]. Kwa njia ya huyo anaingiza maisha ya kiroho ndani ya moyo wa mtu huyo, akiziamsha nguvu zake ili zipate kutenda mema, akiusafisha uchafu wa tabia yake, na kuifanya ipate kufaa kwa ufalme wake." OHC 152.

5. Mwujiza huo wa kuzaliwa mara ya pili unatokeaje? Yohana 3:5; l Kor. 6:11.

a. "Kuna kuifia nafsi na dhambi, na kutokea maisha mapya kabisa. Badiliko hilo linaweza kuletwa tu kwa utendaji ule wenye kuleta matokeo wa Roho Mtakatifu." DA 172.

b. "Kazi ya Roho Mtakatifu moyoni... haiwezi kuelezeka kama vile ulivyo mwendo wa upepo. Mtu anaweza kushindwa kueleza wakati halisi au mahali, au kuyafuatilia mambo yote yaliyoleta uongofu wake; lakini hilo halithibitishi kwamba yeye hajaongoka. Kwa njia ile isiyoonekana kama vile upepo, Kristo anafanya kazi yake daima ndani ya moyo huo. Kidogo kidogo, pengine pasipo yule mpokeaji kutambua, mivuto inafanywa moyoni inayoelekea kumvuta mtu huyo kwa Kristo. Mivuto hiyo inaweza kupokewa kwa njia ya kumtafakari yeye, kwa njia ya kusoma Maandiko, au kwa njia ya neno litokalo kwa mhubiri yule aliye hai. Roho anapotoa mwito wake wa moja kwa moja, kwa ghafula mtu huyo anajisalimisha mwenyewe kwa Yesu kwa furaha. Kwa wengi tendo hilo huitwa kuongoka kwa ghafula; lakini ni matokeo ya muda mrefu ya ubembelezi wa roho wa Mungu kwake, ----- Ni hatua ya ustahimilivu, ya muda mrefu." DA 172.

c. "Roho wa Mungu anapoudhibiti moyo wa mtu, anayabadilisha maisha yake.... Mbaraka huo unakuja wakati ule mtu huyo anapojisalimisha mwenyewe kwa Mungu kwa njia ya imani. Hapo ndipo uweza ule ambao hakuna jicho la kibinadamu liwezalo kuuona huumba kiumbe kipya katika sura yake Mungu." DA 173.

d. "Ni kwa njia yake Roho Kristo anakaa ndani yetu; na Roho huyo wa Mungu, akipokewa moyoni kwa imani anakuwa mwanzo wa uzima ule wa milele [kwa mtu huyo]." DA 388.

6. Ni mara ngapi tunahitaji kuongoka kwa njia ya Roho Mtakatifu?

"Kumfuata Yesu kunataka kuongoka kabisa mwanzoni, na marudio ya kuongoka huko kila siku." SD 207.

7. Sisi kama Wakristo, tunawezaje tu kuyapinga majaribu yanayotukabili kila siku? Rum.8:1,4,9,13,14.

a. "Dhambi ingeweza kupingwa na kushindwa tu kwa njia ya uweza ule mkuu wa Nafsi ile ya Tatu ya Uungu [Roho Mtakatifu]...." DA 671.

b. "Alikuja kuzivunja kazi za Ibilisi, naye amefanya mpango kwamba Roho Mtakatifu apate kutolewa kwa kila mtu atubuye, ili kumlinda asiendelee kutenda dhambi." DA 311.

c. "Kristo amemtoa Roho wake kuwa uweza wa kimbingu wa kushindia mielekeo yetu yote ya dhambi tuliyorithi na ile tuliyojizoeza wenyewe, na kuipiga chapa tabia yake juu ya Kanisa lake." DA 671.

8. Ni nani hasa anayekaa pamoja nasi, kwa njia ya kuwako kwake huyo Roho?

a. "Kwa njia ya Roho wake, Kristo alipaswa kukaa daima mioyoni mwa watoto wake. Muungano wao naye ulikuwa wa karibu sana kuliko pale alipokuwa pamoja nao kimwili."

SC 75.

b. "Roho Mtakatifu ni Msaidizi [Mfariji] wetu, yeye ni kama kuwapo kwake Kristo mwenyewe moyoni mwetu." RH 11-29-1892.

c. "Siku ile ya Pentekoste Msaidizi huyo aliyeahidiwa kwetu alishuka chini, nguvu kutoka juu ikatolewa, na mioyo ya waumini wale ikasisimka kwa kutambua kuwako kwake Bwana wao aliyekuwa amepaa juu." GC 351.

9. Roho Mtakatifu anapofanya kuwako kwake Yesu kuwe kwa hakika kwetu, jambo hilo litaziathirije tabia zetu? 2 Kor.3:18; Gal.5:22,23; 1 Petro 1:2; 2 The.2:13.

a. "Kule kutugawia Roho wake ni sawa na kutugawia maisha yake Kristo. [Roho] anamjaza mpokeaji na sifa za tabia yake Kristo." DA 805.

b. "Moyo wa kibinadamu kamwe hautaijua furaha mpaka hapo utakapojitoa ili upate kufinyangwa na Roho wa Mungu. Roho anaufanya moyo wake uliofinyangwa upya upate kufanana na Kielelezo kile, yaani, na Yesu Kristo. Kwa uongozi wake [Roho], uadui dhidi ya Mungu unageuzwa na kuwa imani na upendo, na kiburi kinakuwa unyenyekevu. Mtu huyo anatambua uzuri wa ile kweli, na Kristo anaheshimiwa kwa njia ya tabia nzuri na kamilifu [ya mtu huyo]." OHC 152.

c. "Roho alipaswa kumtukuza Kristo kwa kuufunua utajiri wa neema yake [Kristo] kwa ulimwengu huu. Sura kamili ya Mungu inatakiwa kurudishwa ndani ya wanadamu. Heshima ya Mungu, heshima ya Kristo inahusika katika tendo hilo la kuikamilisha tabia ya watu wake." OHC 154.

d. "Kwa njia ya imani Roho Mtakatifu anafanya kazi yake moyoni mwa mtu kuumba utakatifu ndani yake; lakini hilo haliwezi kufanyika mpaka mjumbe huyo wa kibinadamu afanye kazi yake pamoja na Kristo. Tunaweza kutayarishwa kwa ajili ya mbingu kwa njia ya Roho Mtakatifu peke yake, akifanya kazi yake moyoni mwetu.... Ni kazi yake Roho Mtakatifu kuudhibiti uchu wetu wa chakula, kuutakasa moyo, na kumfanya mtu mzima awe mwungwana." RH 11-1-1892.

## SURA YA 11

## MVUA YA MASIKA

1. Je, tangu dhambi iingie [duniani humu] umepata kuwapo wakati wo wote ambapo Mungu hajafanya kazi yake kwa njia ya Roho wake Mtakatifu? Mwanzo 6:3; Isa.63:10,11.

a. "Tangu mwanzo, Mungu amekuwa akifanya kazi yake kwa njia ya Roho wake Mtakatifu...." AA 53.

b. "Ni kazi yake Roho Mtakatifu tangu kizazi hata kizazi kugawa upendo wake katika mioyo ya kibinadamu, kwa maana upendo ni kanuni iliyo hai ya undugu." 8T 139.

c. "Katika kipindi kile cha wazee, uongozi wa Roho Mtakatifu mara nyingi ulikuwa umedhihirishwa kwa njia inayoonekana wazi, lakini si katika utimilifu wake." AA 37.

2. Ni utendaji gani wa asili anaoutumia Bwana kuielezea kazi ya Roho Mtakatifu?

Zek. 10:1; Hosea 6:3; Yoeli 2:28.

" 'Naye huwanyeshea mvua, mvua ya masika, na mvua ya vuli.'... Mungu anatumia utendaji kazi huo wa asili kuiwakilisha kazi ya Roho Mtakatifu." TM 506.

3. Mvua ya kwanza (ambayo, katika nchi ya Palestina, inakuja mwishoni mwa mwezi wa Oktoba au katika mwezi wa Novemba) inafanya kazi gani?

"Katika nchi za Mashariki mvua hunyesha katika majira yale ya kupanda mbegu. Ni ya muhimu ili mbegu zipate kuota. Chini ya manyunyu ya mvua yaliyo na uwezo wa kuotesha mbegu, jani jororo huchipua." TM 506.

4. Mvua ya masika (inayonyesha katika mwezi wa Machi au mapema katika mwezi wa Aprili) inafanya kazi gani?

"Mvua ya masika, inayonyesha karibu na mwisho wa msimu, inaikomaza nafaka na kuitayarisha kwa mavuno." TM 506.

5. Kwa jinsi gani mvua ile ya kwanza inaiwakilisha kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya moyo wa mtu mmoja mmoja?

a. "Kama vile umande na mvua inavyotolewa kwanza ili kuzifanya mbegu zipate kuota, na hatimaye kuyakomaza mavuno, ndivyo Roho Mtakatifu anavyotolewa kuiendeleza mbele, toka hatua moja kwenda hatua nyingine, kazi ile ya ukuaji wa kiroho." TM 506.

b. "Mahali po pote katika maisha yetu hatuwezi kuendelea bila msaada wa yule anayetuwezesha kuanza mara ya kwanza. Mibaraka ile inayopokewa chini ya mvua ya vuli [mvua ya kwanza] inahitajika kwetu mpaka mwisho." TM 507.

6. Kwa jinsi gani mvua ya masika inaiwakilisha kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya mtu mmoja mmoja?

a. "Kukomaa kwa nafaka kunawakilisha ukamilisho wa kazi ya neema ya Mungu ndani ya moyo. Kwa uweza wa Roho Mtakatifu sura ya Mungu kimaadili inatakiwa kukamilishwa katika tabia yetu. Sisi tunapaswa kubadilishwa kabisa ili tupate kufanana na Kristo." TM 506.

b. "Roho Mtakatifu anataka kukaa ndani ya kila moyo. Akikaribishwa kama mgeni wa heshima, basi, wale wanaompokea watafanywa kuwa watimilifu ndani yake Kristo. Kazi ile njema iliyoanzwa itakamilishwa; mawazo matakatifu, na matendo kama yale ya Kristo yatachukua mahali pa mawazo machafu, hisia potovu za moyoni, na matendo ya uasi." CH 561.

c. "Tunapomwomba sana Mungu ili atupatie Roho wake Mtakatifu, basi, (Roho huyo) hufanya kazi yake ndani yetu kutupatia upole, unyenyekevu wa moyo, kutambua haja yetu ya kumtegemea Mungu kwa mvua ile ya masika inayotukamilisha [tabia zetu]." TM 509.

7. Ni katika baadhi ya matukio gani Bwana anamtuma Roho wake kwa watu wake?

"Makusanyiko ya kanisa, kama yale ya makambi, makusanyiko ya kanisa la nyumbani, na matukio yote ambayo juhudi ya kuongoa roho inafanyika, hizo ndizo nafasi alizoziteua Mungu kwa ajili ya kutoa mvua ya kwanza [mvua ya vuli] na mvua ya masika." TM 508.

8. Je, watu wanaoishi katika hali ya upweke wanaweza kupokea mvua ya masika ya Roho Mtakatifu katika maisha yao wenyewe hata kama sehemu kubwa ya majirani zao hawaupokei mbaraka huo? Mwanzo 5:24.

a. "Tabia ya utauwa ya nabii huyo (Henoko) huwakilisha hali ya utakatifu inayopaswa kufikiwa na wale wote watakao"nunuliwa katika nchi" wakati ule atakapokuja Kristo mara ya pili." PP 88,89.

b. "Na katika siku hizi zetu tunao akina Henoko." COL 332.

9. Kwa jinsi gani mvua ile ya kwanza inaiwakilisha kazi ya Roho kwa kanisa zima kwa jumla?

a. "Kumwagwa kwa Roho katika siku zile za Mitume ulikuwa ndio mwanzo wa mvua ya kwanza, au mvua ya vuli, na matokeo yake yalikuwa mazuri mno. Mpaka mwisho wa wakati Roho atakaa ndani ya kanisa la kweli." AA 54,55.

b. "Maovu yalikuwa yakilundikana kwa karne nyingi na yangeweza tu kuzuiwa na kupingwa kwa uweza mkuu wa Roho Mtakatifu, Nafsi ya Tatu ya Uungu, ambaye angekuja si katika nguvu iliyopunguzwa, bali katika utimilifu wa uweza wa Mungu." TM 392.

10. Ni matayarisho gani ya moyo na maisha walikuwa wamefanya wanafunzi wale yaliyofanya mvua ile ya kwanza iwezekane kumwagwa kwa kanisa lile la kwanza?

a. "Hawakungoja kivivu. Kumbukumbu inasema kwamba walikuwa 'daima ndani ya hekalu, wakimsifu Mungu.' Luka 24:53." AA 35.

b. "Walijinyenyekeza mioyo yao kwa toba ya kweli na kuungama [dhambi ya] kutokuamini kwao." AA 37.

c. "Mitume waliomba kwa bidii kubwa ili waweze kufaa kuonana na watu na katika maongezi yao ya kila siku kusema maneno yatakayowaleta wenye dhambi kwa Yesu." AA 37.

d. "Wakaweka mbali tofauti zao zote, na tamaa yao yote ya ukubwa, kisha wakakaribiana sana katika ushirikiano wao wa Kikristo." AA 37.

e. "Ilikuwa ni baada ya wanafunzi wale kuwa na umoja kamili, walipokuwa hawagombanii kuwa nani atakuwa wa kwanza, ndipo Roho alipomwagwa juu yao." 8T 20.

f. "Walikuwa wamebeba mzigo mzito sana wa wokovu wa roho za watu." AA 37.

11. Kwa jinsi gani mvua ile ya kwanza iliweza kuathiri hali ya kiroho ya washiriki wale wa kanisa?

a. "Chini ya uongozi wa Roho, maneno ya toba na maungamo yalichanganyika na nyimbo za sifa kwa ajili ya dhambi zao zilizosamehewa." AA 38.

b. "Wale ambao wakati ule wa Pentekoste walikuwa wamejazwa na nguvu kutoka juu, kwa tendo hilo hawakuwa huru kutokana kukabiliwa na majaribu na maonjo zaidi.... Walilazimika kujitahidi kwa kutumia nguvu zao zote walizopewa na Mungu ili kuweza kufika kwenye cheo cha wanaume na wanawake cha kimo cha utimilifu ndani ya Kristo Yesu." AA 49.

c. "Kila siku waliomba kupewa nguvu mpya ya neema yake, ili wapate kufika juu zaidi na hata juu zaidi kuelekea kwenye utimilifu huo." AA 49.

d. "Chini ya utendaji wa Roho hata wale waliokuwa dhaifu kuliko wote, kwa kuiweka imani yao katika Mungu, walijifunza kuzikuza nguvu zao walizopewa kama amana na kutakaswa, kusafishwa, na kuwa waungwana. Kwa unyenyekevu walipojiweka chini ya uwezo huo wa Roho Mtakatifu unaowaumba upya, walipokea utimilifu wote wa Mungu, nao waliumbika kwa sura yake Mungu." AA 49,50.

12. Kwa jinsi gani mvua ile ya kwanza iliweza kuathiri uwezo wao wa kuwashuhudia wengine?

a. "Nini kilichofuata? Upanga wa Roho, ulionolewa upya kwa nguvu ile na kuoshwa katika radi zile zilizotoka mbinguni, ukakata-kata na kupenya katika hali ile iliyokuwapo ya kutokuamini. Maelfu wakaongolewa kwa siku moja." AA 38.

b. "Roho Mtakatifu... aliwawezesha kunena kwa ufasaha lugha ambazo kabla ya hapo walikuwa hawazijui." AA 39.

c. "Mioyo yao ilijazwa na mzigo wa ukarimu uliokuwa mkamilifu mno, wenye kina mno, na mpana mno, hata ukawasukuma kwenda kwenye miisho ya nchi, wakishuhudia uweza wake Kristo." AA 46.

d. "Kuonekana kwa ndimi zile za moto kuliashiria juhudi kubwa ambayo kwayo wale mitume wangeweza kufanya kazi yao, na uweza ambao ungeweza kuambatana nao katika kazi yao." AA 39.

e. "Matokeo ya kumwagwa kwa Roho siku ile ya Pentekoste yalikuwaje? Habari njema za Bwana wao aliyefufuka zikapelekwa mpaka kwenye ncha za mwisho za ulimwengu huu unaokaliwa na watu." AA 48.

f. "Kanisa liliona mmiminiko wa waongofu ukiingia ndani yake kutoka pande zote. Wale waliokuwa wamerudi nyuma wakaongolewa upya." AA 48.

g. "Shauku ya waumini ilikuwa ni kuidhihirisha tabia inayofanana na ile ya Kristo na kufanya kazi kwa ajili ya kupanua [mipaka ya] ufalme wake." AA 48.

13. Je, Bwana alimwondoa Roho wake baada ya Pentekoste?

"Bwana hakuifungia hazina ile ya mbinguni baada ya kuwamwagia Roho wake wanafunzi wale wa kwanza.... Kama sisi hatupati uweza wake, ni kwa sababu ya usingizi wa kiroho, hali yetu ya kutojali, na uvivu wetu. Hebu na tuondokane na hali hiyo ya kufuata desturi na kuwa kama wafu." 6BC 1055.

14. Kwa jinsi gani mvua ya masika inaiwakilisha kazi ya Roho Mtakatifu kwa kanisa zima la Kikristo kwa jumla?

a. "Katika kipindi kile cha mwisho, kazi ya Mungu duniani itakapokuwa inaendelea kufungwa, juhudi za dhati zitakazotolewa na waumini wale waliojitoa wakf chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu zitaandamana na ishara maalum za fadhili za Mungu." AA 54.

b. "Kazi kuu ya injili haitafungwa kwa maonyesho pungufu ya uweza wa Mungu kuliko yale yaliyoonekana wazi mwanzo wake. Unabii uliokuwa umetimizwa katika kumwagwa kwa mvua ile ya vuli mwanzoni mwa kazi ya injili utatimizwa tena katika mvua ya masika wakati wa kufungwa kwake. Hapa ndipo zilipo zile 'nyakati za kuburudishwa' ambazo mtume Petro alikuwa akizitazamia kuja aliposema: "Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana; apate kumtuma Kristo Yesu.'... Kazi ile itafanana na ile iliyofanyika siku ile ya Pentekoste." GC 611,612.

c. "Kumwagwa kwa Roho Mtakatifu katika siku zile za Mitume ilikuwa ndiyo mvua ya kwanza, na matokeo yake yalikuwa mazuri sana. Lakini, mvua ya masika itakuwa na matokeo makubwa zaidi." 8T 21.

d. "Kile ambacho Bwana aliwafanyia watu wake wakati ule, ni jambo la maana vile vile, na zaidi sana, kwamba awafanyie watu wake leo. Yale yote waliyofanya mitume, kila mshiriki wa kanisa leo anapaswa kufanya. Nasi tunatakiwa kufanya kazi kwa juhudi zaidi ya ile, kuambatana na Roho Mtakatifu kwa kiwango kikubwa zaidi ya kile, kama ongezeko la maovu linavyohitaji mwito dhahiri zaidi utolewe kuwataka watu watubu." 7T 33.

15. Mvua ya masika itaathirije hali yao ya kiroho na ukuzaji wa tabia wa washiriki wa kanisa?

a. "Mvua ya masika, ikiyakomaza mavuno ya nchi, inaiwakilisha neema ya kiroho inayoliandaa kanisa kwa marejeo ya Mwana wa Adamu. Lakini mvua ya vuli isipoanguka, basi, hapatakuwa na uhai; jani la kijani kibichi halitachipua. Manyunyu ya mvua ile ya kwanza yasipoikamilisha kazi yake, basi, mvua ya masika haiwezi kuikamilisha mbegu yo yote."

TM 506.

b. "Karibu na mwisho wa kufungwa kwa kazi ya mavuno ya nchi, imeahidiwa kutolewa neema ya kiroho ya pekee ili kulitayarisha kanisa kwa ajili ya Mwana wa Adamu anayekuja. Kumwagwa huko kwa Roho kunalinganishwa na kunyesha kwa mvua ile ya masika...." AA 55.

c. "Ni mvua ile ya masika inayowahuisha [watu wa Mungu] na kuwatia nguvu ili wapate kupita katika wakati ule wa taabu." 1T 353; 7BC 984.

d. "Watapokea mvua ya masika, na kwa njia hiyo watatayarishwa kwa ajili ya kunyakuliwa kwenda mbinguni." 1T 187.

e. "Wamekwisha kupokea 'mvua ya masika,' yaani, 'kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana,' nao wako tayari kwa saa ile ya kujaribiwa iliyo mbele yao." GC 613.

f. "Wakati ule 'mvua ya masika,' au kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana, itakuja kuipa nguvu sauti kuu ya malaika yule wa tatu, na kuwatayarisha watakatifu kuweza kusimama katika kipindi kile wakati mapigo yale saba yatakapokuwa yanamiminwa." EW 86.

g. "Kabla ya kuja kwa hukumu zile za Mungu za mwisho juu ya nchi, patakuwa na uamsho wa utauwa ule wa kwanza miongoni mwa watu wa Bwana ambao haujapata kushuhudiwa tangu nyakati zile za mitume. Watoto wake watamwagiwa Roho na uweza wake juu yao." GC 464.

16. Kwa jinsi gani mvua ile ya masika itaweza kuathiri uwezo wa kanisa wa kushuhudia?

a. "Chini ya manyunyu ya mvua ya masika mavumbuzi ya mwanadamu, na taratibu za kibinadamu, wakati mwingine zitafagiliwa mbali, mipaka ya mamlaka ya mwanadamu itakuwa kama matete yaliyovunjika, na Roho Mtakatifu atanena kupitia kwa mjumbe hai wa kibinadamu kwa uweza utakaowaondolea watu mashaka. Wakati huo hatakuwapo mtu atakayeangalia kama sentensi zimetungwa vizuri, yaani, kama hakuna kosa lo lote la sarufi. Maji ya uhai yatabubujika katika mifereji yake Bwana [aliyoichagua mwenyewe]." 2SM 58,59.

b. "Wataitangaza kweli kwa nguvu ya uweza wa Roho Mtakatifu. Watu wengi wataipokea imani hii na kujiunga na majeshi ya Bwana." Ev 700.

c. "Wakati ule wa sauti kuu, kanisa, likiwa linasaidiwa na kule kuingilia kati kwa Bwana wake aliyetukuzwa kwa wakati unaofaa, litayaeneza maarifa ya wokovu kwa wingi mno hata nuru hiyo itaweza kufika katika kila jiji na mji. Nchi itajazwa na maarifa ya wokovu." Ev 694.

d. "Watumishi wa Mungu, nyuso zao zikiwa na nuru na zikiwa zinang'aa kwa kujitoa wakf kwao, wataharakisha toka mahali kwenda mahali pengine kutangaza ujumbe ule uliotoka mbinguni. Kwa maelfu ya sauti, ulimwenguni kote, onyo hilo litatolewa. Miujiza itafanyika, wagonjwa wataponywa, na ishara na maajabu vitafuatana na hao waaminio." GC 612.

17. Je, mvua ya masika itakuja baada ya watu wa Mungu kutiwa muhuri au kabla ya kumalizika kazi ile ya kuwatia muhuri?

"Kabla kazi hiyo haijafungwa na kabla ya kumalizika kazi ile ya kuwatia muhuri watu wa Mungu, tutamwagiwa Roho wa Mungu kwa wingi." 1SM 111.

18. Je, mvua ya masika itakuja kabla au baada ya kufungwa kwa mlango wa rehema?

" 'Mwanzo wa wakati wa taabu,' uliotajwa hapa, hauhusiani na wakati ule mapigo yatakapoanza kumiminwa, bali unahusiana na kipindi kile kifupi kabla tu hayajamiminwa, yaani, wakati Kristo yumo ndani ya patakatifu. Wakati ule, yaani, wakati kazi ya wokovu [injili], inakaribia kufungwa, taabu itakuwa inakuja duniani, na mataifa yatakasirika, lakini bado yatazuiwa yasije yakaizuia kazi ile ya malaika wa tatu. Wakati ule 'mvua ya masika' au kuburudishwa kwa kuwapo kwake Bwana, itakuja kuipa nguvu sauti kuu ya malaika yule wa tatu, na kuwatayarisha watakatifu kusimama katika kipindi kile wakati mapigo yale saba ya mwisho yatakapokuwa yakimiminwa." EW 85,86.

19. Je, washiriki wetu wote wa kanisa watapokea nguvu hiyo ya Roho Mtakatifu?

a. "Kuna watu ndani ya kanisa ambao hawajaongoka, ambao hawatajiunga katika maombi ya dhati na ya kudumu. Kazi hiyo tunapaswa kuingia ndani yake kila mtu peke yake. Yatupasa kuomba sana, na kuzungumza kidogo." 1SM 122.

b. "Wale wasiofanya juhudi yo yote inayoonekana, bali wanangojea tu kulazimishwa na Roho Mtakatifu kutenda kazi, wataangamia gizani. Haiwapasi kukaa kimya bila kufanya kitu katika kazi yake Mungu." ChS 228.

c. "Ni wale tu wanaoishi kulingana na nuru waliyo nayo watakaopewa nuru kubwa zaidi. Tusipoweza kusonga mbele kila siku na kuzidhihirisha tabia zetu njema za Kikristo kwa matendo, hatutaweza kutambua Roho Mtakatifu atakapojitokeza katika mvua ile ya masika. Huenda ikawa inanyesha mioyoni mwa wale wanaotuzunguka kila upande, lakini sisi hatutaweza kuitambua wala kuipokea." TM 507.

d. "Nikaona kwamba wengi walikuwa wanapuuzia kufanya matayarisho yanayohitajika sana, nao walikuwa wanatazama mbele kwenye wakati ule wa 'kuburudishwa' na 'mvua ya masika' ili kuwatayarisha kusimama katika siku ile ya Bwana, na kuishi mbele ya macho yake. Lo, ni wengi jinsi gani niliwaona katika wakati ule wa taabu wakiwa hawana kinga! Walikuwa wamepuuzia kufanya matayarisho yaliyohitajika, kwa hiyo hawakuweza kupokea kule kuburudishwa ambako wote ni lazima wapate ili kuwafanya wafae kuishi mbele ya macho ya Mungu aliye Mtakatifu." EW 71.

20. Ni maandalizi gani ya moyo na maisha sisi tunapaswa kufanya ili tuwe tayari kwa kumwagwa kwa wingi kwa Roho wa Mungu kwa njia ile ya pekee?

(1) Bidii katika maombi.

a. "Tungeomba kwa bidii kwa ajili ya kushuka kwa Roho Mtakatifu kama vile wanafunzi wake walivyoomba siku ile ya Pentekoste. Iwapo wao walimhitaji wakati ule, basi, sisi tunamhitaji zaidi leo.... Pasipo kuwa na msaada wa Roho, juhudi zetu za kuihubiri ile kweli zitakuwa ni kazi bure kabisa." RH 8-25-1896, uk. 533.

b. "Uamsho wa utauwa wa kweli miongoni mwetu ndiyo haja yetu kuu kuliko zote na ya muhimu sana katika haja tulizo nazo. Kuutafuta huo ingekuwa ndiyo kazi yetu ya kwanza. Ni lazima pawepo na juhudi ya dhati kuipata baraka hiyo ya Bwana, si kwa sababu Mungu hataki kutupa sisi Roho wake Mtakatifu, bali kwa sababu sisi hatujawa tayari kumpokea. Baba yetu wa

mbinguni yuko tayari kuwapa Roho wake Mtakatifu wale wamwombao, kuliko wazazi wa duniani walivyo tayari kuwapa vipawa vyema watoto wao. Lakini ni kazi yetu, kwa maungamo, kujinyenyekeza, kutubu, na kuwa na bidii katika maombi, kutekeleza masharti yale aliyotuahidi Mungu ili kutupa mbaraka wake huo [Roho Mtakatifu]. Uamsho unaweza kutazamiwa tu kama jibu kwa maombi yetu." 1SM 121.

c. "Huenda tukawa na kiasi fulani cha Roho wa Mungu, lakini kwa njia ya maombi na imani tunapaswa kutafuta daima ili tupate kupewa Roho kwa wingi zaidi. Haitafaa kitu kabisa kuacha juhudi zetu hizo. Tusiposonga mbele, yaani, kama sisi hatujiweki katika hali ile tunayoweza kupokea mvua ile ya kwanza na mvua ya masika, zote mbili, basi, sisi tutazipoteza [tutaziangamiza] nafsi zetu, na uwajibikaji utakuwa mlangoni petu." TM 508.

d. "Kipimo cha Roho Mtakatifu tunachopokea kitalingana na kipimo cha shauku tuliyo nayo na imani yetu itumikayo kukipata, na jinsi tutakavyotumia nuru na maarifa yale tutakayopewa. Tutapewa amana ya Roho Mtakatifu kulingana na uwezo wetu wa kupokea na uwezo wetu wa kugawa [nuru hiyo] kwa wengine." RH 5-5-1896, uk. 273.

(2) Ulitakase hekalu la mwili wako kutokana na uchafu wa kila namna.

a. "Bwana na awasaidie watu wake kulitakasa hekalu la mwili wao kutokana na uchafu wa kila namna, na kuuhifadhi uhusiano wa karibu sana naye ili wapate kuwa washirika wa mvua ile ya masika wakati ule itakapomwagwa." 6BC 1055; RH 7-20-1886.

b. "Hakuna hata mmoja miongoni mwetu atakayetiwa muhuri wa Mungu wakati tabia zetu zina doa moja au waa moja juu yake. Kazi hiyo tumeachiwa sisi ili kuweza kuzisahihisha kasoro zote tulizo nazo katika tabia zetu, yaani, kulitakasa hekalu la mwili wetu kutokana na uchafu wa kila namna. Mvua ya masika itanyesha juu yetu kama vile mvua ya kwanza [mvua ya vuli] ilivyonyesha juu ya wanafunzi wake siku ile ya Pentekoste." 5T 214.

c. "Mvua ya masika itakuja, na mbaraka ule wa Mungu [Roho Mtakatifu] utamjaza kila mtu aliyetakaswa kutokana na uchafu wa kila namna. Ni jukumu letu leo kuisalimisha mioyo yetu kwa Kristo, ili tuweze kutayarishwa kwa wakati ule wa kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana ----- yaani, kutayarishwa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu...." Ev 702; 1SM 191.

d. "Nalionyeshwa ya kwamba kama watu wa Mungu hawafanyi juhudi yo yote kwa upande wao, bali wanangojea tu kuburudishwa kule kuje juu yao na kuyaondoa maovu yao pamoja na kuyasahihisha makosa yao; kama wanalitegemea tukio hilo kuwatakasa kutokana na uchafu wao wa mwili na roho, na kuwafanya wafae na kujihusisha na ile sauti kuu ya malaika yule wa tatu, basi, wataonekana kuwa wamepunguka [wana kasoro]. Kuburudishwa au uweza wa Mungu utakuja juu ya wale tu waliokwisha kujiweka tayari kwa ajili ya uwezo huo kwa njia ya kufanya kazi ile aliyowaagiza Mungu kufanya, kama vile, kujitakasa nafsi zao kutokana na uchafu wote wa mwili na roho, huku wakiutimiza utakatifu wao kwa kumcha Mungu." 1T 619.

e. "Bwana na awasaidie watu wake kulitakasa hekalu la mwili wao kutokana na uchafu wa kila namna, na kuuhifadhi uhusiano wa karibu sana naye ili wapate kuwa washirika wa mvua ile ya masika wakati ule itakapomwagwa." 6BC 1055.

f. "Hakuna kitu cho chote anachokiogopa sana Shetani kama kuona watu wa Mungu wanasafisha njia yao kwa kuondoa kila kipingamizi, ili Bwana apate kumwaga Roho wake juu ya kanisa lake linalodhoofika sana.... Kila jaribu, kila mvuto unaopinga, uwe wa wazi au wa siri, unaweza kupingwa kwa ufanisi, 'si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho yangu, asema BWANA wa majeshi.' Zekaria 4:6." 1SM 124.

g. "Wale wanaolipitia kila jambo, na kustahimili kila jaribio, na kushinda, haidhuru gharama yake iweje, wamelitii shauri la yule Shahidi wa Kweli [Kristo], nao watapokea mvua ya masika, na kwa njia hiyo kutayarishwa kwa kunyakuliwa." 1T 187.

(3) Wekeni mbali mafarakano yote.

a. "Wakristo na wayaweke mbali nao mafarakano yao yote, kwa kujitoa wenyewe kwa Mungu kwa ajili ya kazi ya kuwaokoa wale waliopotea. Hebu na waombe kwa imani mbaraka ule ulioahidiwa [Roho Mtakatifu], nao utakuja. Kumwagwa kwa Roho katika siku zile za mitume ilikuwa ndiyo mvua ya kwanza,' na matokeo yake yalikuwa mazuri sana. Lakini mvua ya masika italeta matokeo makubwa zaidi." 8T 21 (Angalia pia Ev 698).

b. "Mioyo yetu itakapopatana na Kristo, na maisha yetu kuafikiana na kazi yake, hapo ndipo Roho yule aliyemwagwa siku ile ya Pentekoste atamwagwa juu yetu." 8T 246.

(4) Ushindi juu ya kila neno baya na kila tendo baya.

a. "Naliona ya kwamba hakuna mtu ye yote ambaye angeweza kushiriki 'kuburudishwa' [mvua ya masika], isipokuwa kama amepata ushindi juu ya kila dhambi inayomsumbua daima, juu ya kiburi, uchoyo [kujipenda nafsi], juu ya kuupenda ulimwengu huu, na juu ya kila neno baya na kila tendo baya. Kwa hiyo, tungekuwa tunamkaribia Bwana karibu zaidi na zaidi, na kutafuta kwa bidii maandalizi yale yaliyo ya muhimu kutuwezesha sisi kushinda katika vita ile ya siku ya Bwana." EW 71.

(5) Jifunzeni Neno la Mungu.

"Sisi kama watu [wa pekee] tutakapokielewa kitabu hicho [cha Ufunuo] kina maana gani kwetu, basi, miongoni mwetu utaonekana uamsho mkubwa." TM 113.

(6) Iweni watenda kazi wenye bidii katika kazi yake Kristo.

a. "Kumwagwa kwa wingi kwa Roho wa Mungu, anayeiangaza nchi yote kwa utukufu wake [Mvua ya Masika], hakutakuja mpaka hapo tutakapokuwa na watu wetu walioelimishwa, ambao kwa uzoefu wao wanajua maana ya kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Tutakapojitoa wakf kabisa, yaani, kwa moyo wote katika kazi yake Kristo, hapo ndipo Mungu atakapoliona jambo hilo

na kutumwagia kwa wingi Roho wake bila kipimo; lakini jambo hilo halitatokea wakati sehemu kubwa sana ya kanisa sio watenda kazi pamoja na Mungu." ChS 253;

RH 7-21-1896 (Angalia pia Ev 699).

b. "Makanisa yatakapokuwa makanisa hai, yaani, yanayofanya kazi, hapo ndipo Roho atatolewa kama jibu kwa maombi yao ya dhati.... Ndipo madirisha ya mbinguni yatakapofunguka na kutumwagia manyunyu ya mvua ile ya masika." RH 2-25-1890, uk. 113.

c. "Wakati shutuma za uzembe na ulegevu zitakapokuwa zimefutiliwa mbali kutoka kanisani, hapo ndipo Roho wa Bwana atakapodhihirishwa kwa wingi sana. Uweza wa Mungu utadhihirika. Kanisa litaona utendaji unaofaa sana wa yule Bwana wa majeshi. Nuru ya ile kweli itaangaza kwa mionzi yenye nguvu inayoonekana wazi, na, kama nyakati zile za mitume, watu wengi watayaacha mafundisho potofu [ya uongo] na kuipokea ile kweli. Nchi itaangazwa kwa utukufu wake Bwana." 9T 46.

21. Sisi tutakapofanya sehemu yetu, Mungu atafanya nini?

a. "Njia itakapotayarishwa kwa ajili ya Roho wa Mungu, hapo ndipo mbaraka huo utakuja. Shetani hawezi kuyazuia manyunyu ya mbaraka huo [Roho Mtakatifu] kushuka juu ya watu wa Mungu kama vile asivyoweza kuyafunga madirisha ya mbinguni ili mvua isinyeshe juu ya nchi." 1SM 124.

b. "Jibu linaweza kuja ghafula, kwa kasi, pamoja na uweza unaotushinda nguvu; au linaweza kucheleweshwa kwa siku nyingi na majuma mengi, na imani yetu ikaweza kujaribiwa. Lakini Mungu anajua kwa jinsi gani na lini atajibu maombi yetu. Ni sehemu yetu ya kazi kujiweka sisi wenyewe katika hali ile itakayotuunganisha na njia hiyo ya Mungu. Mungu anawajibika kwa sehemu yake ya kazi hiyo. Yeye ni mwaminifu aliyetuahidi. Jambo kubwa na la maana kwetu sisi ni kuwa na moyo mmoja na nia moja, tukiweka kando wivu wetu wote pamoja na ubaya wetu wote, na, kama waombaji wanyenyekevu, kukesha na kungoja. Yesu, Mwakilishi wetu na Kichwa [Mkuu] chetu, yu tayari kutufanyia sisi kile alichowafanyia wale waliokuwa wanaomba na kukesha siku ile ya Pentekoste." Dondoo hili linatoka katika kitabu kiitwacho 'Our Firm Foundation, Gombo la II, uk. 683.

## SURA YA 12

## SAUTI KUU

1. Ni ujumbe gani wa Mungu wenye onyo la mwisho unaotakiwa kutolewa ulimwenguni?

Ufunuo 18:1-5.

a. "Maandiko hayo yanatuelekeza mbele kwenye wakati ule tangazo la anguko la Babeli litakaporudiwa kutolewa tena, kama vile lilivyotolewa na malaika yule wa pili wa Ufunuo Sura ya 14 (fungu la 8), likiwa linataja nyongeza ya maovu yaliyoendelea kuingia ndani ya mashirika ya dini mbalimbali ambayo kwa pamoja yanaunda Babeli, tangu ujumbe huo ulipotolewa kwa mara ya kwanza katika majira yale ya kiangazi ya mwaka wa 1844."

GC 603 (Angalia pia EW 277).

b. "Kama ilivyotabiriwa katika sura ile ya kumi na nane ya Ufunuo, ujumbe wa malaika yule wa tatu utatangazwa kwa uweza mkuu na wale wanaotoa onyo la mwisho dhidi ya mnyama na sanamu yake...." 8T 118.

c. "Ufunuo Sura ya kumi na nane inatupeleka kwenye wakati ule ambao, kama matokeo ya kuukataa ujumbe ule wa onyo wa aina tatu wa Ufunuo 14:6-12, kanisa [la Babeli] litakuwa limefikia kabisa hali ile iliyotabiriwa na malaika yule wa pili, na watu wa Mungu ambao bado wako Babeli wataitwa ili wajitenge na ushirika wake. Ujumbe huu ndio wa mwisho ambao utapata kutolewa kwa ulimwengu huu...." GC 390.

d. "Matangazo hayo, yanayounganishwa na ujumbe wa malaika wa tatu, yanakuwa sehemu ya onyo la mwisho litakalotolewa kwa wakazi wa dunia hii." GC 604.

2. Je, huo ni ujumbe ule ule ambao tumekuwa tukiuhubiri tangu mwaka 1844 au ni mwito fulani wa pekee?

"Yesu alipoanza kazi yake miongoni mwa watu, alilitakasa Hekalu kutokana na matumizi yake mabaya yaliyolinajisi. Miongoni mwa matendo yake ya mwisho ya kazi yake ilikuwa ni kulitakasa Hekalu kwa mara ya pili. Kwa hiyo katika kazi ya mwisho ya kuuonya ulimwengu huu, miito dhahiri ya aina mbili inatolewa kwa makanisa. Ujumbe wa malaika yule wa pili ni huu, "Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake." Ufunuo 14:8. Na kwa sauti kuu ujumbe huo wa malaika wa tatu sauti inasikika kutoka mbinguni ikisema, '...Tokeni kwake, enyi watu wangu, msishiriki dhambi zake [Babeli], wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake.' Ufunuo 18:4,5." 2SM 118; 7BC 985. (Angalia pia EW 277).

3. Kitovu cha ujumbe wa malaika hao watatu ni nini hasa? Ufunuo 14:6.

a. "Watu kadhaa wameniandikia, wakiuliza iwapo ujumbe wa kuhesabiwa haki kwa njia ya imani ndio ujumbe hasa wa malaika yule wa tatu, mimi nimewajibu hivi, 'Huo ndio ujumbe wa malaika yule wa tatu kweli kweli." Ev 190; 1SM 372.

b. "Ujumbe wa haki yake Kristo unatakiwa kutangazwa kutoka katika ncha moja ya dunia kwenda kwenye ncha nyingine ili kutayarisha njia kwa ajili ya Bwana. Huo ndio utukufu wake Bwana, ambao unaifunga kazi ya malaika yule wa tatu." 6T 19.

c. "Kwa rehema zake nyingi, Bwana alituma ujumbe wake wa thamani kubwa sana kwa watu wake kwa njia ya Wazee Waggoner na Jones. Ujumbe huo ulikusudiwa kuleta kwa wazi zaidi mbele ya ulimwengu Mwokozi yule aliyeinuliwa juu, kafara kwa dhambi za ulimwengu mzima. Ulifundisha kuhesabiwa haki kwa njia ya imani katika yule aliye Mdhamini wetu; uliwaalika watu kuipokea haki yake Kristo, ambayo inadhihirishwa kwa utii kwa amri zote [kumi] za Mungu. Wengi walikuwa wamempoteza Yesu. Walihitaji macho yao yaelekezwe kwa Uungu wake, wema wake, na upendo wake usiobadilika kwa familia ya kibinadamu. Mamlaka yote amepewa yeye

mkononi mwake, ili apate kuwagawia wanadamu vipawa vingi na kuwapa kipawa cha thamani kisichokadirika cha haki yake mwenyewe kwa mjumbe huyo wa kibinadamu. Huo ndio ujumbe alioagiza Mungu ili uhubiriwe ulimwenguni kote. Huo ndio ujumbe wa malaika wa tatu, ambao unapaswa kutangazwa kwa sauti kuu, na kuandamana na kumwagwa kwa Roho wake kwa kiwango kikubwa." TM 91,92.

d. "Ujumbe wa mwisho wa rehema unaotakiwa kutangazwa ulimwenguni ni ufunuo wa tabia yake ya upendo. Watoto wa Mungu wanatakiwa kuudhihirisha utukufu wake. Katika maisha yao na tabia zao wanatakiwa kuonyesha kile ambacho neema ya Mungu imewatendea."

COL 415,416.

4. Kwa nini ujumbe huo unasemekana kuwa unatolewa kwa "sauti yenye nguvu" au "sauti kuu" (Ufunuo 18:2)?

"Unaonyeshwa ya kwamba unatolewa kwa sauti kuu; yaani, kwa uweza wa Roho Mtakatifu." 7BC 980.

5. Ni kitu gani kinachofanya sauti kuu iwezekane? Uweza wake unaobidisha unatoka wapi? Zekaria 4:6.

a. " 'Mvua ya masika,' au kuburudiswa kwa kuwako kwake Bwana, itakuja kuitia nguvu sauti kuu ya malaika yule wa tatu na kuwatayarisha watakatifu kustahimili katika kipindi kile yatakapomiminwa mapigo yale saba ya mwisho." EW 86.

b. "Nikawasikia wale waliovikwa silaha wakiitangaza kweli kwa nguvu kubwa. Ilileta matokeo... Nikauliza ni kitu gani kilicholeta mabadiliko hayo. Malaika akajibu, 'Ni ile mvua ya masika , yaani, kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana, sauti kuu ya malaika yule wa tatu.' " EW 271.

6. Sauti hiyo kuu inaelekezwa kwa nani hasa?

a. "Katika Sura ile ya kumi na nane ya Ufunuo, watu wa Mungu wanaitwa watoke Babeli. Kulingana na Maandiko hayo, watu wengi wa Mungu hawana budi kuwa bado wamo Babeli. Ni katika mashirika gani makuu ya dini sehemu kubwa ya wafuasi wake Kristo inapatikana hivi sasa? Bila shaka lo lote, ni katika makanisa mbalimbali yanayokiri imani ya Kiprotestanti." GC 383.

b. "Ni kweli kwamba kuna Wakristo wa kweli katika jumuia ya Wakatoliki wa Roma. Maelfu waliomo ndani ya kanisa hilo wanamtumikia Mungu kulingana na nuru bora waliyo nayo.... Hata hivyo wengi watasimama upande wa watu wa Mungu." GC 565.

c. "Bila kujali giza la kiroho na mkengeuko mbali na Mungu uliomo ndani ya makanisa yale yanayounda Babeli, sehemu kubwa ya wafuasi wa kweli wa Kristo bado wanaweza kupatikana katika jumuia yao." GC 390 (Angalia pia GC 449; 605).

7. Shetani ataingiza nini katika makanisa hayo yapendwayo na watu wengi kabla ya kutimizwa Ufunuo 18:1?

a. "Adui yule wa roho za watu anataka kuizuia kazi hii; na kabla ya wakati wa mabadiliko hayo kuja, atajitahidi kuyazuia kwa kuleta ya bandia. Katika makanisa ambayo anaweza kuyaleta chini ya uwezo wake wa madanganyo atafanya ionekane kana kwamba mbaraka huo wa pekee wa Mungu [Roho Mtakatifu] umemwagwa; pataonekana kile kinachodhaniwa kuwa ni mwamko mkubwa katika mambo ya kidini. Makundi kwa makundi ya watu watashangilia wakisema kwamba Mungu anatenda maajabu kwa ajili yao, wakati kazi hiyo ni ya roho yule mwingine [mapepo]. Akiwa amejificha chini ya vazi la dini, Shetani atajaribu kuueneza mvuto wake huo katika ulimwengu wote wa Kikristo." GC 464.

b. "Shetani atakapoendelea kufanya kazi yake kwa kufanya maajabu yake ya uongo, wakati uliotajwa katika Ufunuo utatimizwa, na yule malaika mwenye uwezo mkuu atakayeiangaza nchi yote kwa utukufu wake atatangaza anguko la Babeli, na kuwaita watu wa Mungu kuachana naye." 7BC 985.

7. Tunawezaje kubainisha uamsho wa bandia wa Shetani na sauti ile kuu?

a. "Kuna msisimko kihisia, kuichanganya kweli na uongo, ambavyo vimekusudiwa kuwapotosha watu. Hata hivyo, hakuna haja kwa ye yote kudanganyika. Katika nuru ya neno la Mungu si vigumu kubainisha hali ya matapo [makundi] hayo. Po pote pale ambapo watu wanadharau ushuhuda wa Biblia, wakigeuka na kuziacha kweli zile zilizo wazi ambazo zinaupima moyo wa mtu na ambazo zinataka kujikana nafsi na kuukataa kabisa ulimwengu, hapo ndipo sisi tunaweza kuwa na hakika ya kwamba mbaraka ule wa Mungu [Roho Mtakatifu] haujatolewa. Na kwa kanuni ile aliyoitoa Kristo Mwenyewe, akisema, 'Mtawatambua kwa matunda [matendo] yao' (Mathayo 7:16), ni dhahiri kwamba matapo hayo hayatokani na kazi ya Roho yule wa Mungu." GC 464, 465.

9. Je, tunajua ni wakati gani hasa itakapomwagwa mvua ile ya masika na yule malaika wa Ufunuo 18 atakaposhuka chini kutoka mbinguni?

"Sina wakati maalum ambao naweza kuzungumza habari zake kuhusu kutakapotokea kumwagwa kwa Roho Mtakatifu ----- malaika yule mwenye mamlaka kuu atakaposhuka kutoka mbinguni, na kuungana na malaika yule wa tatu katika kuifunga kazi ile kwa ulimwengu huu; ujumbe wangu ni kwamba usalama wetu pekee ni kujiweka tayari kwa kuburudishwa huko kutakakotoka mbinguni...." 7BC 984.

10. Je, anguko la Babeli (Ufunuo 18:2) lilikuwa limefikia utimilifu wake wakati ule Bibi White alipokiandika kitabu cha The Great Controversy [Pambano Kuu]?

"Walakini, bado haiwezi kusemwa kwamba 'Umeanguka Babeli.... kwa kuwa mataifa yote wamekunywa [aliwafanya mataifa yote kunywa - KJV] mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake.' Bado hajayafanya mataifa yote kufanya hivyo." GC 359.

11. Ni lini ambapo anguko la Babeli litakuwa limetimilika hata Ufunuo 18:2 iweze kuhubiriwa kama unabii uliotimia kabisa?

a. " '[A]liwanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake.' Ufunuo 14:6-8. Jambo hilo linafanyikaje? Kwa kuwalazimisha watu kuikubali sabato hiyo ya uongo [Jumapili]." 8T 94.

b. "Mpaka hapo hali hiyo itakapofikiwa, na muungano wa kanisa na ulimwengu utakapokamilika kabisa katika mataifa yote ya Kikristo, hapo ndipo itakaposemwa ya kwamba anguko la Babeli, limekamilika. Badiliko hilo linakwenda hatua kwa hatua, na utimilifu kamili wa Ufunuo 14:8 bado uko mbele." GC 390.

12. Kutolewa kwa Amri ya Jumapili na mateso yatakayoambatana nayo kutaathirije mahubiri ya ujumbe wa malaika yule wa tatu?

a. "Dhoruba ya mateso itakapotuangukia kweli kweli,.... hapo ndipo ujumbe wa malaika yule wa tatu utakapovuma sana na kuwa sauti kuu, na nchi yote itaangazwa kwa utukufu wa Bwana." 6T 401.

b. "Mwanzoni mwa wakati wa taabu, tulijazwa na Roho Mtakatifu tulipotoka na kwenda kuitangaza Sabato kwa ukamilifu zaidi." EW 33 (Angalia pia EW 85).

c. "Sabato hiyo ya uongo [Jumapili] italazimishwa kwa sheria ya ukandamizaji. Shetani na malaika zake wako macho sana, tena wanashughulika kwa nguvu sana.... Lakini wakati ambapo Shetani anafanya kazi yake kwa kufanya maajabu yake ya uongo, hapo ndipo utakapotimizwa wakati ule uliotabiriwa katika Ufunuo, na malaika yule mwenye mamlaka kuu atakayeiangaza nchi [dunia yote] kwa utukufu wake, atatangaza anguko la Babeli, na kuwaita watu wa Mungu [walioko Babeli] kuachana naye." 7BC 985; RH 12-13-1892, uk. 769.

13. Uzoefu huo wa ajabu utawaathirije watu wa Mungu?

a. "Kadiri washiriki wa mwili wa Kristo [Kanisa la Kristo] wanavyozidi kukikaribia kipindi kile cha pambano lao la mwisho, yaani 'wakati wa taabu ya Yakobo,' ndivyo watakavyokua [kitabia] na kufanana naye Kristo, nao watashiriki kwa wingi Roho wake. Kadiri ujumbe ule wa tatu utakavyozidi kuvuma sana na kuwa sauti kuu, na kama vile mamlaka (uweza) kuu na utukufu vitakavyoambatana na kazi ile ya kufungia [injili], ndipo watu waaminifu wa Mungu watakaposhiriki utukufu ule. Ni mvua ya masika iwezayo kuwahuisha na kuwatia nguvu ili waweze kustahimili kukipitia kipindi kile cha wakati wa taabu. Nyuso zao zitang'aa kwa utukufu wa nuru ile inayoambatana na malaika yule wa tatu." 7BC 984; 1T 353.

b. "Ujumbe wa malaika wa tatu utakapozidi kuvuma sana na kuwa sauti kuu, hapo ndipo uweza mkuu wa utukufu utakapoambatana na kazi ile ya kuutangaza. Nyuso za watu wa Mungu zitang'aa kwa nuru ile iliyotoka mbinguni." 7T 17.

c. "Kadiri mwisho unavyozidi kukaribia, ndivyo shuhuda za watumishi wa Mungu zitakavyozidi kuwa dhahiri zaidi na zenye nguvu zaidi." RH 12-13-1892, uk. 769.

14. Je, [sauti ile kuu] itaweza kulinganishwa kwa njia yo yote ile na "kilio kile cha usiku wa manane" cha mwaka ule wa 1844?

a. "Malaika yule anayejiunga katika kazi ya kuutangaza ujumbe wa malaika yule wa tatu ataiangaza dunia yote kwa utukufu wake. Kazi itakayoenea ulimwenguni kote na yenye uwezo usiokuwa wa kawaida inatabiriwa hapo. Tapo la Waadventista la mwaka 1840-44 lilikuwa ni udhihirisho wa uweza wake Mungu uliojaa utukufu; ujumbe ule wa malaika wa kwanza ulipelekwa kwa kila kituo cha kimishonari ulimwenguni kote, na katika nchi nyingine palitokea mwamko mkubwa katika mambo ya dini ambao haujapata kuonekana katika nchi yo yote tangu wakati ule wa Matengenezo ya Kanisa ya karne ile ya kumi na sita; lakini hayo yatapitwa na tapo hilo lenye mamlaka kuu chini ya onyo hilo la mwisho la malaika yule wa tatu." GC 611.

b. "Nikaona ya kwamba ujumbe huu utafungwa kwa uwezo mkuu na nguvu inayoipita sana ile ya kilio cha usiku wa manane." EW 278.

c. "Uweza ule uliowachochea watu kwa nguvu kuu katika tapo lile la mwaka 1844 utadhihirishwa tena. Ujumbe wa malaika wa tatu utatangazwa, sio kwa sauti za kunong'ona, bali kwa sauti kuu." 5T 252; Ev 693.

15. "Kilio kile cha usiku wa manane" kilikuwa kama nini?

"Kama wimbi wakati wa maji kupwa na kujaa tapo lile lilipita juu ya nchi yote.... Palikuwa na furaha kidogo tu, lakini zaidi palikuwa na kujichunguza sana moyo, kuungama dhambi, na kuachana na ulimwengu. Maandalizi ya kukutana na Bwana yalikuwa ndiyo mzigo mzito wa watu wale waliokuwa wanajitesa. Palikuwa na maombi ya kudumu na kujitoa wakf kwa Mungu bila kuacha kitu....

"Katika matapo [makundi] yote makubwa ya dini tangu siku zile za mitume, hakuna lililokuwa halina upungufu wa kibinadamu wala hila za Shetani kama lilivyokuwa lile la majira yale ya kupukutisha ya mwaka 1844....

"Walijifunza Neno la Mungu kwa hamu kubwa sana ambayo kabla ya hapo ilikuwa haijulikani.... Wakati ule palikuwa na imani iliyoleta majibu kwa maombi.... Uthibitisho wa kukubaliwa na Mwokozi ulikuwa ni wa muhimu zaidi kwao kuliko chakula chao cha kila siku...." GC 400-403.

16. Sauti kuu italinganishwaje na Pentekoste?

a. "Kazi ile itafanana na ile ya siku ya Pentekoste. Kama vile 'mvua ya vuli' ilivyotolewa kwa kumwagwa Roho Mtakatifu mwanzo wa injili na kusababisha kuchipua kwa mbegu zile za thamani, hivyo ndivyo 'mvua ya masika' itakavyotolewa mwisho wake [injili hiyo] ili kuyakomaza mavuno." GC 611.

b. "Kabla ya hukumu za Mungu kuja hapa duniani patakuwapo miongoni mwa watu wa Mungu uamsho wa utauwa ule wa zamani ambao haujapata kushuhudiwa tangu siku zile za mitume." GC 464.

c. "Kumwagwa kwa Roho katika siku zile za mitume ilikuwa ndiyo mvua ya vuli, na matokeo yake yalikuwa mazuri sana. Lakini mvua ya masika matokeo yake yatakuwa makubwa zaidi." Ev 701.

d. "Wakati unakuja watakapoongolewa kwa siku moja kama wale walioongolewa siku ile ya Pentekoste, baada ya wanafunzi wale kupokea Roho Mtakatifu." Ev 692.

17. Je, miujiza itafanyika kama siku ile ya Pentekoste na mara tu baada ya wakati ule?

a. "Kazi ile itafanana na ile ya siku ya Pentekoste.... Kazi kuu ya injili haitafungwa kwa maonyesho ya uweza wa Mungu yaliyo pungufu kuliko yale yaliyoonyeshwa kwa dhahiri wakati ule wa kufunguliwa kwake [kazi ile ya injili]. Unabii uliotimizwa wakati wa kumwagwa kwa mvua ile ya vuli ilipofunguliwa kazi ya injili utatimizwa tena katika mvua ile ya masika wakati wa kufungwa kwake [kazi ya injili]. Hizo ndizo 'nyakati za kuburudishwa' ambazo mtume Petro alizitazamia aliposema: 'Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana; apate kumtuma Kristo Yesu.' Matendo ya Mitume 3:19,20.

"Watumishi wa Mungu, nyuso zao zikiwa zina nuru na zinang'aa kwa kujitoa wakf kwao, wataharakisha toka mahali kwenda mahali pengine kuutangaza ujumbe ule uliotoka mbinguni. Kwa maelfu ya sauti, ulimwenguni kote, onyo hilo litatolewa. Miujiza itafanyika, wagonjwa wataponywa, na ishara na maajabu yatafuatana na waaminio. Shetani naye atafanya kazi yake kwa maajabu ya uongo hata kushusha moto kutoka mbinguni uje mbele ya wanadamu. Ufunuo 13:13. Hivyo ndivyo wakazi wote wa dunia hii watakavyofikishwa mahali pa kuchagua upande wa kusimama." GC 611,612.

b. "Miujiza mikubwa ikatendeka, wagonjwa wakaponywa, na ishara na maajabu vikafuatana na hao waaminio." EW 278.

18. Mungu ana mtazamo gani kwa wale wanaokana kuwa hatafanya miujiza tena?

"Hapa tunaona kwamba kanisa ----- maskani ya Bwana ----- lilikuwa la kwanza kupata pigo la ghadhabu ya Mungu. Watu wale wa zamani, wale ambao Mungu alikuwa amewapa nuru kubwa na waliokuwa wamesimama kama walinzi wa mambo ya kiroho ya watu, walikuwa wameisaliti amana yao [waliyokabidhiwa]. Walikuwa wamechukua msimamo kwamba haitupasi kutazamia miujiza na mafunuo dhahiri ya uweza wa Mungu kama ilivyokuwa katika siku zile za zamani." 5T 211.

19. Je, kuna uwezekano kwamba karama ile ya lugha inaweza pia kurudiwa?

"Ni kwa shauku kubwa ya moyo wangu mimi natarajia kuona wakati ule ujao ambapo matukio ya siku ile ya Pentekoste yatarudiwa kwa uwezo mkubwa kuliko wa wakati ule uliopita. Yohana asema, 'Naliona ... nchi ikaangazwa kwa utukufu wake.' Hapo ndipo, kama majira yale ya

Pentekoste, watu wataisikia kweli ikinenwa kwao, kila mtu kwa lugha yake mwenyewe." 6BC 1055; RH 7-20-1886.

20. Watoto wa Mungu ambao bado wako Babeli wataitikiaje mwito wa ile sauti kuu?

a. "Watu wengi wataipokea imani hii na kujiunga katika majeshi ya Bwana." Ev 700.

b. "Watu waliokuwa wametawanyika katika mashirika yote ya kidini waliitikia mwito ule, na wale waliokuwa wa thamani [waaminifu] waliharakishwa kutoka katika makanisa hayo yaliyoandikiwa kuangamizwa, kama vile Lutu alivyoharakishwa kutoka Sodoma kabla ya maangamizi yake." EW 279.

c. "Kilele kile cha hatari ile kubwa kitakapokuja, wengi watakuwa tayari kufanya maamuzi yao sahihi hata mbele ya matatizo ya kuogofya mno ambayo yataletwa kupitia kwa ile miujiza idanganyayo ya yule Shetani. Japokuwa hao wataikiri imani na kufanya kazi katika saa ile ya kumi na moja [saa ya mwisho], watapokea ujira ule ule pamoja na wale waliofanya kazi mchana kutwa. Kutakuwa na jeshi la waumini wenye msimamo thabiti watakaosimama kama mwamba katika jaribio lile la mwisho." RH 12-24-1889, uk. 3.

d. "Kwa nini Kristo alitoka kwenda kando ya bahari, na kwenda milimani? Alilazimika kuwapa watu Neno lile la uzima. Wao hawakuliona hivyo kwa dakika ile tu. Wengi sana hawalioni hivyo sasa, hata waweze kuchukua nafasi yao, lakini mambo hayo yanayaongoza maisha yao; na ujumbe huo utakapotolewa kwa sauti kuu, watakuwa tayari kuupokea. Hawatasitasita kwa muda mrefu; watatoka na kuchukua nafasi yao." Ev 300,301.

e. "Ujumbe huo utapelekwa si kwa mjadala zaidi bali kwa kuchomwa moyo sana na Roho Mtakatifu. Sababu zimekwisha kutolewa. Mbegu imekwisha kupandwa, na sasa itaota na kukua na kuzaa matunda. Vitabu vilivyotawanywa na watenda kazi wamishonari vimeushinikiza mvuto wake, lakini bado wengi ambao mioyo yao ilikuwa imeguswa wamezuiwa wasiweze kuielewa kweli kwa utimilifu wake wote au kutoa utii wao. Sasa mionzi ya nuru inapenya kila mahali, kweli inaonekana katika uwazi wake, na watoto waaminifu wa Mungu wanazikata kamba zilizokuwa zimewafunga. Uhusiano wa kifamilia, uhusiano wa kikanisa, sasa hauna uwezo wo wote wa kuwazuia. Kweli ni ya thamani kuliko mengine yote. Bila kujali nguvu [mamlaka] zile zilizoungana dhidi ya ile kweli, idadi kubwa wanachukua msimamo wao upande wa Bwana." GC 612.

f. "Nikawasikia wale waliokuwa wamevaa silaha wakiitangaza kweli kwa nguvu nyingi. Ilikuwa na matokeo mazuri. Wengi walikuwa wamefungwa; baadhi ya wake walifungwa na waume zao, na baadhi ya watoto walifungwa na wazazi wao. Wale walio waaminifu waliokuwa wamezuiwa kuisikia kweli sasa kwa shauku kubwa wakaipokea. Hofu yote ya kuwaogopa ndugu zao ilikuwa imetoweka, na ile kweli peke yake ndiyo waliyoitukuza. Walikuwa na njaa na kiu ya ile kweli; kwao ilikuwa inapendeza sana na ya thamani sana kuliko uhai wao. Nikauliza ni kitu gani kilicholeta badiliko hilo kubwa. Malaika akajibu, 'Ni hiyo mvua ya masika, yaani, kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana, sauti kuu ya malaika yule wa tatu.' " EW 271.

21. Je, Waadventista wo wote waliorudi nyuma watautii ujumbe huo?

"Wengi [miongoni mwa wale] waliotangatanga mbali na zizi lake watarudi na kumfuata Mchungaji wao Mkuu." 6T 401.

22. Ni kitabu gani cha Roho ya Unabii kitakuwa njia ya kuwaongoza wengi kuchukua msimamo wao pamoja na watu wa Mungu wazishikao Amri zake [Kumi]?

"Kitabu hiki cha The Great Controversy [Pambano Kuu], nakithamini mno kuliko fedha au dhahabu, nami natamani sana kwamba kiweze kuwafikia watu.... Matokeo ya kukitawanya kitabu hicho yasikadiriwe kwa kile kinachoonekana kwa macho sasa. Kwa kukisoma, watu wengine wataweza kuamshwa, nao watakuwa na ujasiri wa kujiunga mara moja na wale wanaozishika Amri [Kumi] za Mungu. Lakini idadi kubwa sana ya wale wanaokisoma hawatazijaza nafasi zao [katika kundi la watu wa Mungu] mpaka hapo watakapoyaona matukio yale yale yaliyotabiriwa katika kitabu hicho yakitokea. Kutimizwa kwa baadhi ya mambo yale yaliyotabiriwa humo kutaitia nguvu imani yao ili wapate kuamini ya kwamba yale mengine nayo yatatokea, na wakati ule nchi itakapoangazwa kwa utukufu wa Bwana, wakati kazi [ya injili] inakaribia kufungwa, watu wengi watachukua msimamo wao kwa kuzishika Amri [Kumi] za Mungu kama matokeo ya njia hii [ya kukisoma kitabu hiki]." CM 128,129.

23. Waadventista Wasabato ambao hawajaongoka watalichukuliaje jambo hilo?

a. "Ujumbe huo wa malaika wa tatu hautaeleweka kwao, nuru ile itakayoiangaza nchi kwa utukufu wake itaitwa nuru ya uongo na wale wanaokataa kwenda katika nuru yake ya utukufu inayozidi kuongezeka." RH 5-27-1890, uk. 321.

b. "Wale wanaoweza kusaidia katika _______ wasipoamshwa ili wapate kuutambua wajibu wao, hawataweza kuitambua kazi ya Mungu wakati ule sauti kuu ya malaika yule wa tatu itakaposikika." TM 300.

c. "Ndani ya makanisa [yetu] patakuwa na mafunuo ya ajabu ya uweza wake Mungu, lakini [uweza huo] hautawagusa wale wasiojinyenyekeza wenyewe mbele zake Bwana, na kuifungua mioyo yao kwa maungamo na toba. Katika mafunuo ya uweza huo unaoiangaza nchi kwa utukufu wake, wao wataona tu kuwa ni kitu fulani ambacho katika upofu wao watakifikiria kuwa ni cha hatari kwao, yaani, kitu fulani kitakachoziamsha hofu zao, nao watajifunga kibwebwe [watajikaza] kuupinga [uweza huo]. Kwa kuwa Bwana hafanyi kazi yake kulingana na matarajio na mawazo yao, basi, wataipinga kazi hiyo. 'Kwa nini' wao watasema, 'sisi tusiweze kumjua Roho wa Mungu, wakati tumekuwa kazini kwa miaka mingi sana?" RH 11-7-1918.

d. "Dhoruba ile itakapokuwa inakaribia, kundi kubwa la wale waliokiri imani yao katika ujumbe huo wa malaika wa tatu, bali ambao hawajatakaswa kwa kuitii ile kweli, wataziacha nafasi zao na kujiunga katika safu za wapinzani." GC 608.

24. Wachungaji wale wanaopendwa sana na watu wengi [walio katika makanisa mengine] pamoja na watu wengi waipendao dhambi watalionaje jambo hilo?

a. "Lakini kwa kuwa wengi watakataa kuridhishwa na mamlaka tu ya wanadamu na kutaka wapewe neno lililo wazi, lisemalo, 'Hivi ndivyo asemavyo Bwana,' hapo ndipo wachungaji wale wapendwao sana na watu wengi, kama vile walivyokuwa wale Mafarisayo wa zamani, watajazwa na hasira kali wakati ule mamlaka yao itakapohojiwa, wataukana hadharani ujumbe huo kuwa unatoka kwa Shetani, kisha watawachochea makundi ya watu wengi wanaoipenda dhambi ili wawalaani na kuwatesa wale wanaoutangaza [ujumbe huo].

"Pambano hilo litakapozidi kusonga mbele kwenda katika maeneo mapya na akili za watu zitakapoelekezwa kuiangalia Sheria ya Mungu [Amri Kumi] iliyokanyagwa chini, Shetani atachachamaa. Uwezo utakaoambatana na ujumbe ule utazidi tu kuwakasirisha mno wale wanaoupinga. Wachungaji watatumia juhudi yao inayozidi uwezo wao wa kibinadamu ili kuifungia mbali nuru hiyo isije ikaangaza juu ya makundi yao [waumini wao]. Kwa kila njia iliyo katika uwezo wao watajaribu kuunyamazisha mjadala wo wote juu ya masuala hayo ya maana sana. Kanisa litaomba mkono wa serikali wenye nguvu ulisaidie, na katika kazi hiyo, wafuasi wa papa na Waprotestanti wataungana pamoja. Kadiri tapo [kundi] hilo linalotaka itungwe Amri ya Jumapili litakapozidi kuwa na ujasiri mwingi na kudhamiria zaidi, ndipo sheria itatolewa dhidi ya wale wanaozishika Amri [Kumi za Mungu]. Watatishiwa ya kwamba watatozwa faini na kufungwa, na wengine watapewa vyeo vikubwa vya uongozi, na zawadi nyingine pamoja na marupurupu, kama vivutio kwao ili waikane imani yao." GC 607.

b. "Onyo kuu la mwisho lilikuwa limetangazwa kwa nguvu kila mahali, nalo lilikuwa limewachokonoa na kuwakasirisha sana wakazi wa dunia hii ambao hawakutaka kuupokea ujumbe huo." EW 279.

25. Maarifa hayo ya wokovu yataenea kwa mapana gani?

a. "Wakati ule wa sauti kuu, kanisa likisaidiwa na uingiliaji kati [kwa wakati unaofaa] wa Bwana wake yule aliyetukuzwa, litayaeneza maarifa ya wokovu kwa wingi mno hata nuru hiyo itaweza kupelekwa kwa kila mji mkubwa na mji mdogo. Nchi itajazwa na maarifa ya wokovu. Roho wa Mungu anayeumba upya atakuwa ameifanikisha mno juhudi ya wajumbe wake wote wenye bidii kubwa, kiasi kwamba nuru ya ukweli wa leo itaonekana ikimulika kila mahali."

Ev 694.

b. "Hatari kubwa i juu yetu. Sasa yatupasa kuzitangaza zile kweli kuu kwa siku hizi za mwisho kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Hautapita muda mrefu kabla kila mmoja amelisikia onyo hilo na kukata shauri. Hapo ndipo ule mwisho utakapokuja." Ev 703.

26. Je, watu wa Mungu wanatarajiwa kujiondoa kutoka katika kanisa la Waadiventista Wasabato na kujiunga na kundi fulani lililo safi zaidi na takatifu zaidi wakati ule wa sauti kuu?

a. "Imekuwaje ya kwamba vijitabu hivyo vinavyolitangaza Kanisa la Waadventista Wasabato kama Babeli vimetawanywa kila mahali, kwa wakati uo huo ambao Kanisa hili limekuwa

likimwagiwa Roho wa Mungu? Imekuwa-kuwaje ya kwamba watu wanaweza kudanganyika mno hivyo hata kuweza kufikiri ya kwamba sauti kuu inahusu kuwaita watu wa Mungu kutoka katika ushirika wa Kanisa lile linalofurahia kipindi cha kuburudishwa [Roho Mtakatifu]?"

TM 23.

b. "Utachukua vifungu vya maneno kutoka katika Shuhuda (Testimonies) zangu vinavyozungumzia juu ya kufungwa kwa mlango wa rehema, na juu ya mtikiso ule miongoni mwa watu wa Mungu, nawe utazungumzia juu ya watu walio safi zaidi na watakatifu zaidi kuwa watatoka kutoka miongoni mwa [watajitenga na] watu hawa [Waadventista Wasabato]. Basi, mambo yote hayo yanamfurahisha yule adui.... Wengi wakiyakubali maoni yako unayotoa, na kuongelea juu yake na kuyatendea kazi, basi, tungeweza kuona msisimko mmojawapo mkubwa sana kuliko yote wa washupavu wa dini wasiotumia akili zao ambao umepata kushuhudiwa miongoni mwa Waadventista Wasabato. Hivyo ndivyo Shetani anavyotaka hasa." 1SM 179.

c. "Hivi sasa sisi hatuwezi kuingia katika shirika [dhehebu] jipya lo lote; maana kitendo hicho kitamaanisha uasi kutoka katika ile kweli." 2SM 390.

27. Je, ile sauti kuu itakuja kutokana na mpango wo wote wa kibinadamu?

a. "Hebu niwaambie ninyi ya kwamba katika kazi hiyo ya mwisho Bwana atafanya kazi yake kwa njia ambayo ni tofauti sana na mpangilio wa mambo wa kawaida, na kwa njia itakayokuwa kinyume na mpango wo wote wa kibinadamu. Miongoni mwetu watakuwamo wale watakaotaka kuiongoza kazi ya Mungu, kulazimisha hata mambo gani yatapaswa kufanywa wakati kazi itakapokuwa inasonga mbele chini ya uongozi wa malaika yule anayejiunga na malaika yule wa tatu katika ujumbe ule unaopaswa kutolewa kwa ulimwengu wote. Mungu atatumia njia na mbinu ambazo kwazo itaonekana ya kwamba ameshika hatamu [za kazi hiyo] mikononi mwake yeye Mwenyewe. Watenda kazi watashangaa kuziona njia rahisi atakazozitumia yeye Mwenyewe ili kuitimiza na kuikamilisha kazi yake ya haki." TM 300.

b. "Watenda kazi watawezeshwa kwa nguvu ile ya unenaji itokayo kwa Roho Mtakatifu kuliko kwa kupewa mafunzo yo yote katika taasisi zetu za Maandiko [Vyuo vya Uchungaji]. Watu wenye imani na maombi watabidishwa kusonga mbele wakiwa wamejazwa na juhudi ile takatifu, wakiyatangaza maneno yale atakayowapa Mungu." GC 606 (Angalia pia Ev 700).

c. "Wengi, hata miongoni mwa wale wasiokuwa na elimu, hivi sasa wanatangaza maneno yake Bwana. Watoto wanasukumwa na Roho kutoka na kwenda kutangaza ujumbe huo unaotoka mbinguni. Roho atamwagwa juu ya wote watakaonyenyekea chini ya msukumo wake, nao, wakizitupilia mbali taratibu zote zilizowekwa na wanadamu, kanuni zake zinazowafunga [wasiweze kuwa huru kufanya kazi hiyo] pamoja na mbinu zake za kujihadhari, wataitangaza kweli kwa nguvu ya uweza wa Roho." Ev 700.

d. "Kwa watu wale wanaoitafuta nuru kwa bidii na kwa wale wanaopokea kwa furaha kila mwonzi wa mafunuo hayo ya mbinguni kutoka katika Neno lake takatifu, kwa hao peke yao nuru ile itatolewa. Ni kwa njia ya watu hao Mungu ataifunua nuru na nguvu ile itakayoiangaza nchi yote kwa utukufu wake." 5T 729.

e. "Uweza wa Mungu utakapounganishwa pamoja na juhudi ya kibinadamu, hapo ndipo kazi hii itakapoenea kama moto katika nyasi kavu zilizokatwa. Mungu atatumia wajumbe ambao asili yao mwanadamu hataweza kuifahamu [malaika]; malaika watafanya kazi ile ambayo wanadamu wangeweza kuwa na mbaraka wa kuitimiza, kama wasingalikuwa wamepuuzia kuitikia [kutekeleza] madai yake Mungu." RH 12-15-1885, uk. 769.

## SURA YA 13

## NYAKATI NA MAJIRA

1. Je, hivi tunaujua wakati hasa itakapomwagwa ile mvua ya masika?

a. "Hatupaswi kujua wakati halisi aidha wa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu au wa marejeo yake Kristo." Ev 221; 1SM 188; 6BC 1052; RH 3-22-1892.

b. "Sina [sijapewa] muda maalum wa kuutaja kuhusu wakati ule Roho Mtakatifu atakapomwagwa ----- yaani, malaika yule mwenye mamlaka kuu atakaposhuka kutoka mbinguni, na kujiunga na malaika yule wa tatu katika kuifunga kazi [ya injili] kwa ulimwengu huu; ujumbe wangu kwenu ni kwamba usalama wetu peke yake ni kujiweka tayari kwa kuburudishwa huko kutakakotoka mbinguni, taa zetu zikiwa zimetengenezwa na zinawaka." 1SM 192; 7BC 984.

2. Yesu alisema nini juu ya tarehe ya kurudi kwake? Mathayo 24:36; Yohana 21:22,23; Matendo ya Mitume 1:6,7.

3. Kwa nini maarifa ya kuujua wakati wa kurudi kwake Kristo yamezuiwa kwetu?

"Kwa nini Mungu hajatupa sisi maarifa hayo? ----- Kwa sababu sisi tusingeweza kuyatumia vizuri kama angetupa. Hali ya mambo ingetokea kwa kuyajua maarifa hayo ambayo ingeichelewesha sana kazi ya Mungu ya kuwatayarisha watu ili wapate kusimama katika siku ile kuu inayokuja. Hatupaswi kujishughulisha sana na kukisia nyakati na majira ambayo Mungu hajatufunulia." Ev 221; RH 3-22-1892.

4. Ni dalili gani ambazo zipo zinazoonyesha kwamba Yesu alikuwa tayari kurudi duniani kipindi fulani mara tu baada ya mwaka ule wa 1844, wakati unabii wa mwisho unaotaja wakati ulipofikia mwisho wake?

a. "Nikaona ya kwamba wale walioipokea kweli katika siku hizi za mwisho wangepaswa kujua maana ya kuteswa kwa ajili ya Kristo, ya kwamba wangepitia katika maonjo ambayo yangekuwa makali sana na ya kuumiza ili wapate kutakaswa na kuwekwa katika hali ya kufaa kwa njia ya mateso ili wapate kuupokea muhuri ule wa Mungu aliye hai, wapate kupita katika kipindi kile cha wakati wa taabu, wapate kumwona Mfalme katika uzuri wake, na kukaa mbele zake Mungu na mbele ya malaika wale walio safi na watakatifu....

"Lakini sasa wakati huo karibu sana umekwisha, na kile sisi tulichokuwa tukijifunza kwa miaka mingi, wao watajifunza kwa miezi michache tu." EW 67 (1850).

b. "Nikaonyeshwa kundi lile la watu waliokuwapo katika mkutano ule mkuu [Konferensi]. Akasema yule malaika, 'Wengine ni chakula cha mabuu, wengine watakuwa watu wa kupigwa na mapigo saba ya mwisho, wengine wataendelea kuwa hai na kubaki juu ya nchi kungojea kunyakuliwa atakapokuja Yesu.' " 1T 131,132 (1856).

5. Ujumbe wa Laodikia ulioanza kuhubiriwa mwaka 1856 miongoni mwa Waadventista wanaoitunza Sabato ulikuwa na kusudi gani?

"Nikaona ya kwamba ujumbe huo usingeweza kufanikiwa kumaliza kazi yake katika miezi michache mifupi. Umekusudiwa kuwaamsha watu wa Mungu, kuwafunulia kurudi nyuma kwao, na kuwaongoza wawe na tabia ya kutubu, ili waweze kupata upendeleo wa kuwako kwake Yesu, na kutayarishwa kwa ajili ya sauti kuu ya malaika yule wa tatu. 1T 186 (1859).

6. Je, ujumbe huo ulifanikiwa kulifikia kusudi lake?

"Watu wa Mungu hawako tayari kwa sauti kuu ya malaika wa tatu." 1T 486 (1867).

7. Kwa nini Yesu hakurudi mara moja? (Yona 3:4-10; Yeremia 18:7-10).

"Usiku ule mrefu wa giza unachosha sana, lakini asubuhi inacheleweshwa kwa ajili ya rehema zake, kwa sababu kama Bwana angekuja, basi, wengi sana angewakuta hawajawa tayari." Ev 694; 2T 194 (1868).

8. Hata hivyo, je! Dada White aliamini kwamba kuja kwa Bwana kulikuwa kumekaribia sana?

"Kwa sababu muda ni mfupi, tungefanya kazi yote kwa bidii nyingi na kutumia nguvu zetu maradufu. Watoto wetu huenda wasiweze kuingia katika Chuo Kikuu." 3T 159 (1872).

9. Kwa nini Yesu hakurudi katika miaka ile kabla ya 1883?

a. "Kama Waadventista, baada ya kukatishwa tamaa sana mwaka ule wa 1844, wangekuwa wameishikilia imani yao na kwa kuungana pamoja wangezifuata njia zile alizokuwa amezifungua Mungu, na kuupokea ujumbe ule wa malaika wa tatu na kwa uweza wa Roho Mtakatifu kuutangaza kwa ulimwengu, wangekuwa wameuona wokovu wa Mungu, Bwana angekuwa ametenda kazi yake kwa uweza wake mkuu pamoja na juhudi zao, kazi ingekuwa imemalizika, na Kristo angekuwa amekuja kabla ya wakati huu ili kuwachukua watu wake kwenda nao kwake kuwapa thawabu yao.... Hayakuwa mapenzi ya Mungu kwamba kuja kwake Kristo kungecheleweshwa kiasi hicho.... Kwa miaka arobaini hali ile ya kutokuamini, ya kunung'unika, na maasi, iliwafungia Waisraeli wale wa zamani nje ya nchi ile ya Kanaani. Dhambi zile zile zimewachelewesha kuingia katika Kanaani ile ya mbinguni Israeli ya leo. Katika matukio yote mawili ahadi za Mungu hazikuwa na dosari yo yote. Ni kule kutokuamini, hali ile ya kuupenda ulimwengu, kutojitoa wakf, na migongano miongoni mwa wale wanaojidai kuwa ni watu wake Bwana, kulikotuweka katika dunia hii ya dhambi na huzuni kwa miaka mingi sana." Ev 695,696 (1883).

b. "Kama wote waliokuwa wamefanya kazi pamoja kwa mshikamano katika kazi ile ya mwaka 1844, wangekuwa wameupokea ujumbe wa malaika wa tatu na wangekuwa wameutangaza kwa uweza wa Roho Mtakatifu, Bwana angekuwa ametenda kazi kwa uweza wake mkuu kupitia katika juhudi zao. Gharika ya nuru ingekuwa imemwagwa juu ya dunia hii. Miaka mingi iliyopita wakazi wa dunia hii wangekuwa wameonywa, kazi ya kumalizia ingekuwa imetimilika, na Kristo angekuwa amekuja kwa ajili ya ukombozi wa watu wake." 4SP 291 (1884); GC 458; 8T 116.

10. Licha ya kucheleweshwa huko mpaka wakati huo, nabii huyo bado alikuwa na matarajio gani?

a. "Sauti ya Mtoa-Uzima bado haijawaita watakatifu waliolala kutoka katika magereza yao yenye giza [makaburi], lakini hatujapoteza imani yetu, kwa sababu saa iliyotabiriwa bado haijafika.... Saa hiyo itakuja; haiko mbali sana, na baadhi yetu ambao sasa tunaamini tutakuwa hai juu ya uso wa dunia hii, na tutaona utabiri huo ukithibitika, na kuisikia sauti ile ya Malaika Mkuu [Kristo], na parapanda ya Mungu ikitoa mwangwi wake mlimani, na katika nchi tambarare na baharini, mpaka sehemu za mwisho kabisa za dunia hii. Viumbe vyote vitaisikia sauti hiyo, na wale waliokuwa wameishi na kufa katika Yesu, wataitikia mwito huo wa Mkuu wa Uzima." RH 7-31-1888, uk. 482.

b. "Katika kizazi hiki cha ulimwengu, wakati mandhari za historia ya ulimwengu huu karibu sana zitakoma na sisi tumekaribia sana kuingia katika kipindi kile cha wakati wa taabu ambayo haikupata kuwako, itakuwa heri kwa wote, wanaume na wanawake, kama ndoa chache mno zikifungwa." 5T 366 (1885).

11. Ni ujumbe gani, uliohubiriwa kwa nguvu katika miaka mitatu iliyofuata baada ya Mkutano Mkuu wa Konferensi Kuu (General Conference), ambao ulikuwa ndio "mwanzo" wa sauti kuu?

"Saa ile ya kujaribiwa i juu yetu, kwa maana sauti kuu ya malaika yule wa tatu tayari imeanza kusikika katika ufunuo wa haki yake Kristo, Mkombozi yule anayesamehe dhambi. Huo ndio mwanzo wa nuru ya malaika yule ambaye utukufu wake utaijaza dunia yote." 1SM 363;

7BC 984; RH 11-22-1892, uk. 722.

12. Je, mvua ya masika ilikuwa inamwagwa juu ya watu wa Mungu mwaka ule wa 1872 au tukio hilo lilikuwa ni "kuvuma sana" tu kwa ujumbe ule ambao hatimaye utageuka na kuwa sauti kuu?

"Hatupaswi kuujua wakati halisi aidha wa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu au ule wa kuja kwake Kristo.... Ujumbe wa malaika yule wa tatu unavuma sana na kuwa sauti kuu.... Leo unapaswa kukiweka safi chombo chako ili kiwe tayari kuupokea umande ule wa mbinguni, kiwe tayari kuyapokea manyunyu yale ya mvua ya masika; kwa maana mvua ya masika itakuja, na mbaraka huo wa Mungu [Roho Mtakatifu] utamjaza kila mtu aliyetakaswa kutokana na uchafu wa kila namna. Ni jukumu letu leo kuitoa mioyo yetu kwa Kristo, ili tuweze kutayarishwa kwa wakati wa kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana ----- tuweze kutayarishwa kwa ubatizo wa Roho

Mtakatifu." RH 3-22-1892, uk. 178 (Hotuba [yake] iliyotolewa pale Lansing, Michigan, Sept.5, 1891).

13. Mtazamo wa Dada White katika mwaka ule wa 1891 ulikuwa ni upi kuhusu kukaribia sana kwa marejeo yake Kristo?

"Hamtaweza kusema kwamba atakuja katika muda wa mwaka mmoja, miwili, au miaka mitano, wala msiahirishe kuja kwake kwa kusema kwamba huenda hakutatokea katika kipindi cha miaka kumi au ishirini hivi." RH 3-22-1892, uk.178 (Hotuba [yake] iliyotolewa pale Lansing, Michigan, Sept. 5, 1891); Ev. 221.

14. Kwa nini Yesu alizidi kuchelewesha zaidi kuja kwake mara ya pili?

a. "Endapo Kanisa lake Kristo lingekuwa limefanya kazi yake liliyopewa kama Bwana alivyoliagiza, basi, ulimwengu wote kabla ya wakati huu ungekuwa umeonywa, na Bwana Yesu angekuwa amekuja katika dunia yetu kwa nguvu na utukufu mwingi." DA 633, 634 (1898).

b. "Kama kusudi la Mungu lingekuwa limetekelezwa na watu wake katika kuutangazia ulimwengu huu ujumbe huo wa rehema, basi, kabla ya wakati huu, Kristo angekuwa amekwisha kuja duniani, na watakatifu wangekuwa wamekwisha karibishwa katika mji ule wa Mungu."

6T 450 (1900).

c. "Fundisho la kumbukumbu hii ni kwa ajili yetu. Mungu alikuwa ameitayarisha njia mbele ya watu wake. Walikuwa karibu sana na nchi ile ya ahadi. Kitambo kidogo tu wangekuwa wamekwisha ingia Kanaani. Wao wenyewe walichelewesha kuingia kwao. Wangekuwa wameliweka tumaini lao kwa Mungu, wangekuwa wameingia moja kwa moja. Mungu angekuwa ametangulia mbele yao.... Ndugu na dada, kutokana na nuru niliyopewa najua kwamba kama watu wa Mungu wangekuwa wametunza uhusiano ulio hai naye, kama wangekuwa wamelitii neno lake, basi, hivi leo wangekuwa katika Kanaani ile ya mbinguni." GCB 3-30-1903 (Angalia pia Ev 694).

15. Ni kosa la nani kwamba sisi bado tumo katika dunia hii yenye dhambi, na Yesu bado hajarudi mpaka sasa?

"Tunaweza kuendelea kubaki katika dunia hii kwa sababu ya maasi yetu [kutotii kwetu] kwa miaka mingi zaidi, kama walivyofanya Wana wa Israeli; lakini kwa ajili yake Kristo watu wake wasingekuwa wanaongeza dhambi juu ya dhambi kwa kumshtaki Mungu kwa matokeo ya njia yao mbaya ya utendaji." Ev 696 (1901).

16. Kristo anangojea nini?

"Tabia yake Kristo itakapoonekana kwa ukamilifu ndani ya watu wake, hapo ndipo atakapokuja kuwataka kwa halali kuwa wao ni watu wake mwenyewe. Ni haki ya kila Mkristo, sio tu kutazamia, bali kuharakisha kuja kwa Bwana wetu Yesu Kristo." COL 69.

17. Matarajio ya Bibi White ya kurudi kwake Kristo yalilinganaje na yale ya manabii wa Biblia? Ufu.22:6,7,12,20; 1Kor. 7:29; Rum. 13:11,12.

"Malaika wa Mungu katika ujumbe wao kwa wanadamu wanaonyesha kwamba muda ni mfupi sana. Hivyo ndivyo ilivyoonyeshwa kwangu. Ni kweli kwamba wakati umeendelea kwa muda mrefu zaidi kuliko tulivyotarajia katika siku zile za mwanzo za ujumbe huu. Mwokozi wetu hakutokea upesi kama tulivyotumainia. Lakini, je! hivi neno la Bwana limekosea? Hasha! Yapaswa ikumbukwe ya kwamba ahadi na vitisho vya Mungu kwa namna ile ile moja hutolewa kwa masharti." Manuscript 4, 1883, yamedondolewa na F.M. Wilcox katika kitabu chake cha The Testimony of Jesus, uk. 98-105). Angalia pia katika 7BC 729.

18. Mtazamo wetu leo ungekuwaje?

"Badala ya kuzichosha mno nguvu za akili zetu kwa kukisia-kisia tu nyakati na majira, mambo ambayo Bwana ameyaweka katika uwezo wake, na kuyaficha kwa wanadamu, yatupasa sisi kujitoa nafsi zetu ili tupate kutawaliwa na Roho Mtakatifu, tuweze kutekeleza majukumu yale yanayotukabili hivi sasa, yaani, kuugawa ule mkate wa uzima [Neno la Mungu], ambao haujaghoshiwa [haujachanganywa] na maoni ya kibinadamu, kwa watu wale wanaoangamia kwa kuikosa kweli hiyo." Ev 702; 6BC 1052; RH 3-22-1892.

## SURA YA 14

## MUHURI WA MUNGU

1. Ni tukio gani la pekee linaloelezwa kwamba litatokea muda mfupi tu kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema? Ufu. 7:1-4; Eze. 9:1-6.

"Yohana anaona vitu vya asili ----- tetemeko, tufani, na machafuko ya kisiasa ----- vikionyeshwa kwake kama vimeshikiliwa na malaika wale wanne. Pepo hizo zimedhibitiwa mpaka hapo Mungu atakaposema neno la kuziachilia. Hapo ndipo upo usalama wa Kanisa la Mungu. Malaika wa Bwana wanafanya kama anavyowaagiza, wanazizuia pepo za nchi zisivume juu ya nchi, wala juu ya bahari, wala juu ya mti wo wote mpaka hapo watumwa [watumishi] wa Mungu watakapotiwa muhuri juu ya vipaji vya nyuso zao.... Kazi ya kuwatia muhuri watumwa wa Mungu ni ile ile moja iliyoonyeshwa kwa Ezekieli katika maono yake." TM 444,445.

2. Hivi muhuri wa Mungu aliye hai ni kitu gani? Kutoka 20:8-11; 31:12-17.

a. "Wakiwa wamechelewa mno ndipo wanaiona Sabato ya amri ya nne kuwa ndio muhuri wa Mungu aliye hai." GC 640.

b. "Utunzaji sahihi wa Sabato ndiyo ishara ya utii wetu kwa Mungu." 7BC 981.

c. "Wale ambao wangetaka kuwa na muhuri wa Mungu juu ya vipaji vya nyuso zao ni lazima waitunze Sabato ya amri ya nne." 7BC 970.

d. "Patakuwa na alama itakayowekwa juu ya watu wa Mungu, na alama hiyo ni utunzaji wa Sabato yake takatifu." 7BC 981.

e. "Kwetu kama ilivyokuwa kwa Israeli Sabato hiyo imetolewa kuwa 'agano la milele.' Kwa wale wanaoiheshimu sana siku yake hiyo takatifu, Sabato ni ishara inayoonyesha kwamba Mungu anawatambua wao kuwa ndio watu wake wateule. Ni ahadi yake kwamba atawatimizia agano lake. Kila mtu anayeipokea alama hiyo ya serikali ya Mungu anajiweka mwenyewe chini ya agano hilo la milele la Mungu. Anajifungamanisha mwenyewe kwenye mnyororo ule wa dhahabu wa utii, kila pete [kiungo] ya mnyororo huo ni ahadi yake.

"Amri ile ya nne ndiyo peke yake katika zile kumi iliyo na muhuri wa yule Mtoa-Sheria Mkuu, Muumba wa mbingu na nchi." 6T 350 (Angalia pia PP 307).

3. Hali ya kiroho inatakiwa iweje kwa wale wote wanaoupokea muhuri huo wa kibali chake Mungu?

a. Tabia zao zitakuwa kamilifu.

"Je, tunautafuta utimilifu wake wote, tukizidi kusonga mbele kuelekea kwenye kiwango kile kilichowekwa mbele yetu ----- yaani, utimilifu wa tabia yake? Watu wa Mungu watakapokifikia kiwango hicho, ndipo watakapotiwa muhuri katika vipaji vya nyuso zao. Wakiwa wamejazwa na Roho, watakuwa wametimilika ndani yake Kristo, na malaika yule anayetia alama ile [muhuri ule] atatangaza akisema, 'Imekwisha.' " 6BC 1118.

b. Hakuna kitakachowaondoa katika kweli hiyo.

"Mara tu watu wa Mungu watakapokuwa wametiwa muhuri katika vipaji vya nyuso zao ----- si muhuri wa aina yo yote ile au alama inayoweza kuonekana kwa macho, bali ni kule kutulia [kujizatiti] katika kweli, kiakili na kiroho, ili wasiweze kuondoshwa ----- mara tu watu wa Mungu watakapokuwa wametiwa muhuri na kutayarishwa kukabiliana na ule mtikiso, utakuja. Naam, tayari umekwisha kuanza; hukumu za Mungu hivi sasa ziko juu ya nchi, kutupa sisi onyo, ili tupate kujua kile kinachokuja." 4BC 1161.

c. Wanafanana na Kristo.

"Muhuri wa Mungu aliye hai utawekwa juu ya wale tu wanaofanana na Kristo kitabia." 7BC 970.

d. Ni Washindi.

"Wale wanaoushinda ulimwengu, [tamaa ya] mwili, na yule mwovu, watakuwa ndio hao watakaopendelewa kupokea muhuri huo wa Mungu aliye hai." TM 445.

e. Wao ni Safi wala Hawana Waa.

"Sasa ndio wakati wa kujiweka tayari. Muhuri wa Mungu kamwe hautawekwa juu ya kipaji cha uso cha mwanaume au mwanamke mwasherati. Kamwe hautawekwa juu ya kipaji cha uso cha mwanaume au mwanamke mtaka makuu wala yule mpenda ulimwengu. Kamwe hautawekwa juu ya vipaji vya nyuso za wanaume au wanawake wambea [waongo] au wenye mioyo iliyojaa udanganyifu [hila]. Wote wanaoupokea muhuri huo ni lazima waonekane bila waa mbele zake Mungu ----- yaani, wateule wanaofaa kwenda mbinguni." 5T 216.

f. Huomboleza juu ya dhambi zao wenyewe na juu ya dhambi zilizomo kanisani na katika dunia nzima.

"Wakati ule hatari na mfadhaiko kwa kanisa vitakapofikia kiwango cha juu sana, kundi dogo la wale watakaosimama katika nuru watakuwa wanaugua [wanapiga kite] na kulia kwa sababu ya machukizo yanayofanyika katika nchi. Lakini hasa hasa maombi yao yatakuwa yanapanda juu kwa ajili ya kanisa kwa sababu washiriki wake wanafanya kama wafanyavyo watu wa ulimwengu huu.... Wataomboleza na kujitesa nafsi zao kwa sababu kiburi, uroho wa kuchuma mali, uchoyo [kujipenda nafsi], na udanganyifu karibu wa kila namna umo ndani ya kanisa.... Kundi la wale wasioona haja ya kusikitika kwa ajili ya hali yao ya kiroho iliyoshuka chini sana, wala kuomboleza juu ya dhambi za wengine, wataachwa pasipo [kutiwa] muhuri wa Mungu.... Muhuri wa Mungu utawekwa juu ya vipaji vya nyuso za wale tu wanaougua na kulia kwa sababu ya machukizo yanayofanyika katika nchi." 5T 209-212.

"Ni wale tu ambao, katika msimamo wao mbele za Mungu, wanaijaza nafasi ya wale wanaotubu na kuungama dhambi zao katika siku ile kuu ya upatanisho halisi [asilia], watakaotambuliwa na kutiwa alama [muhuri] kama watu wanaostahili kupewa ulinzi wake Mungu." TM 445.

4. Je, tuko katika kipindi kile cha kutiwa muhuri hivi sasa" Kama ndivyo, kilianza lini?

a. "Naliona kwamba jaribio [kupimwa] la sasa juu ya Sabato lisingeweza kuja mpaka kazi ile ya Yesu ya upatanishi ndani ya mahali pale patakatifu itakapokwisha na atakapokuwa ameingia ndani ya pazia lile la pili [patakatifu pa patakatifu]; kwa hiyo, Wakristo waliolala kabla mlango haujafunguliwa wa kuingilia katika patakatifu pa patakatifu, wakati ule kilio cha manane kilipokwisha katika mwezi ule wa saba wa 1844, na ambao walikuwa hawajaitunza Sabato ya kweli, hivi sasa wanapumzika [makaburini mwao] wakiwa na matumaini; maana wao hawakuipata nuru hiyo wala jaribio hilo juu ya Sabato ambalo sisi tunalo sasa tangu mlango ule ulipofunguliwa. Naliona ya kwamba Shetani alikuwa akiwajaribu baadhi ya watu wa Mungu juu ya jambo hilo. Kwa kuwa Wakristo wengi wema wamekwisha lala usingizi [wa mauti] katika ushindi wa imani wakiwa hawajaitunza Sabato, walikuwa wanaona mashaka kwamba hiyo [Sabato] inaweza kuwa kipimo kwetu hivi sasa.... Shetani hivi sasa anatumia kila hila katika kipindi hiki cha kutiwa muhuri ili kuizuia mioyo ya watu wa Mungu isiweze kuupokea ukweli huu wa leo na kuwafanya wawe wanasitasita." EW 42,43.

b. "Kipindi cha kutiwa muhuri ni kifupi sana, nacho kitakwisha mara moja. Sasa ndio wakati wa kufanya imara kuitwa kwetu na uteule wetu, wakati wale malaika wanne wanaendelea kuzishikilia pepo zile nne." EW 58.

5. Je, tunawajua watu wo wote ambao tayari wamekwisha tiwa muhuri huo?

a. "Nikaona ya kwamba yeye [Bibi Hastings] alikuwa ametiwa muhuri, naye angetoka [kaburini mwake] wakati ule wa sauti ya Mungu [Ufu.16:17] na kusimama juu ya nchi akiwa pamoja na wale 144,000. Nikaona ya kwamba hatuna haja ya kuomboleza juu yake; yeye angepumzika katika kipindi kile cha wakati wa taabu." 2SM 263.

b. "Wapo watu wanaoishi hapa duniani ambao umri wao ni zaidi ya miaka tisini. Matokeo ya kawaida ya uzee yanaonekana katika udhaifu wao wa mwili. Lakini wanamwamini Mungu, na Mungu anawapenda. Muhuri wa Mungu u juu yao, nao watakuwa miongoni mwa idadi ile ambayo Bwana amesema, 'Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa [l844].' " 7BC 982.

6. Je, kuna uwezekano kwamba wapo wanaume na wanawake walio hai hivi leo ambao tayari wameupokea muhuri huo wa Mungu?

"Toleo jingine linasomeka kama ifuatavyo: 'Naam, Bwana asifiwe, ndugu na dada zangu, huu ni mkutano wa ziada kwa wale walio na muhuri wa Mungu aliye hai.' Hakuna jambo lo lote katika maneno hayo ambalo sisi hatulishikilii. Kumbukumbu za kazi zetu zilizochapishwa zitaonyesha imani yetu kwamba wenye haki walio hai watapokea muhuri wa Mungu kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema; na pia kwamba hao watapata heshima ya pekee katika ufalme ule wa Mungu." 1SM 66.

7. Kabla ya kumalizika kazi hiyo ya kuwatia muhuri watu wa Mungu, ni tukio gani tukufu litatokea?

a. "Kabla ya kazi hiyo [ya injili] kufungwa kabisa na kabla ya kazi hiyo ya kuwatia muhuri watu wa Mungu kumalizika, tutapokea kumwagwa kwa Roho wa Mungu [Mvua ya masika]." 1SM 111.

b. "Hakuna hata mmoja wetu atakayepokea muhuri wa Mungu wakati tabia zetu zina doa moja au waa moja juu yake. Imebaki kwetu sisi [ni jukumu letu] kuzirekebisha kasoro hizo katika tabia zetu, kulisafisha hekalu letu kutokana na uchafu wa kila namna. Hapo ndipo mvua ya masika itakapotuangukia juu yetu kama mvua ile ya kwanza [ya vuli] ilivyowaangukia juu yao wale wanafunzi wake siku ile ya Pentekoste." 5T 214.

8. Ni kitu gani kitakachowapata wale ambao hawajatulia [hawajajizatiti] "katika ile kweli... ili wasiweze kuondoshwa"?

"Mara tu watu wa Mungu watakapotiwa muhuri juu ya vipaji vya nyuso zao ----- si muhuri wa aina yo yote ile au alama inayoweza kuonekana kwa macho, bali ni kule kutulia katika ile kweli, kiakili na kiroho, ili wasiweze kuondoshwa ----- mara tu watu wa Mungu watakapotiwa muhuri na

kutayarishwa kwa ule mtikiso, utakuja. Naam, umekwisha anza tayari; hukumu za Mungu hivi sasa ziko juu ya nchi, kutupa sisi onyo, ili tuweze kujua kile kinachokuja."

4BC 1161.

9. Ni amri gani ya ulimwengu mzima itakayopitishwa kabla watu wa Mungu wote hawajatiwa muhuri huo?

a. "Mamlaka za dunia, zikiungana pamoja kupigana vita na wale wazishikao amri [kumi] za Mungu, zitatangaza kwamba 'wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa' (Ufunuo13:16), watafuata desturi za kanisa kwa lazima kwa kuitunza sabato ya uongo [Jumapili].... Kwa upande mwingine, Sheria ya Mungu inayoamuru utunzaji wa siku ile ya mapumziko [Sabato - Jumamosi] iliyowekwa na Muumbaji itawataka watu wote waitii, na kutishia ghadhabu juu ya wote wanaozivunja amri zake [kumi]. Jambo hilo litakapokuwa limewekwa wazi mbele yao, hapo ndipo mtu ye yote yule atakayeikanyaga Sheria ya Mungu chini ya miguu yake kwa kuitii amri iliyotungwa na wanadamu, atapokea alama (chapa) ya Mnyama." GC 604.

b. "Wakati kundi moja, kwa kuikubali alama ile ya utii [Jumapili] kwa mamlaka za kidunia, wanapokea Alama ya Mnyama, kundi lile jingine likiwa limeichagua ishara ile ya utii [Sabato] kwa mamlaka ile ya Mungu, watapokea muhuri wa Mungu." GC 605.

c. "Utakapoitii amri ile inayokuamuru wewe kuacha kufanya kazi siku ya Jumapili... utakuwa unakubali kupokea alama ya mnyama, na kuukataa muhuri wa Mungu. Kama sisi tutaweza kuipokea alama hiyo juu ya vipaji vya nyuso zetu au mikononi mwetu, basi, hukumu zile zilizotamkwa juu ya wale wasiotii [amri zake] bila shaka zitatuangukia sisi [Ufu.16:1-21]. Muhuri ule wa Mungu aliye hai utawekwa juu ya wale wanaoitunza kwa uangalifu sana Sabato ya Bwana." RH 7-13-1897; 7BC 980.

d. "Bwana amenionyesha mimi waziwazi kwamba sanamu ya mnyama itaundwa kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema; kwa maana hiyo ndiyo itakuwa jaribio [mtihani] kubwa kwa watu wa Mungu, ambayo kwayo uzima wao wa milele utaamuliwa.... [Ufunuo 13:11-17, imenukuliwa hapa]....

"Hilo ndilo jaribio ambalo watu wa Mungu ni lazima walipate kabla hawajatiwa ule muhuri. Wale wote watakaouonyesha utii wao kwa Mungu kwa kuishika Sheria yake [Amri Kumi] na kukataa kuipokea sabato ile ya bandia [Jumapili] watajipanga chini ya bendera yake Bwana Mungu Yehova, nao watapokea muhuri wa Mungu aliye hai. Wale watakaoiacha ile kweli yenye asili ya mbinguni na kuipokea sabato ile ya Jumapili, watapokea alama ya Mnyama." 7BC 976.

10. "Hesabu yao waliotiwa muhuri" ni wangapi? Ufunuo 7:14.

11. Je, tunajua kama hesabu hiyo ni hesabu halisi au ni hesabu ya mfano?

"Si mapenzi yake kwamba wao waweze kubishana juu ya hoja zile ambazo hazitawasaidia kiroho, kama vile, Ni nani atakuwamo katika wale mia na arobaini na nne elfu? Jambo hilo wale walio wateule wake Mungu watalijua bila maswali katika muda mfupi ujao." 1SM 174.

12. Yule malaika anayetia alama [muhuri] atakapomaliza kazi yake, Yesu atafanya nini?

a. "Malaika atakayerudi [mbinguni] toka duniani atatangaza kwamba kazi yake imekwisha; jaribio [mtihani] la mwisho limeletwa juu ya ulimwengu, na wale wote waliojionyesha kuwa waaminifu kwa Sheria ya Mungu [Amri Kumi] wamekwisha kupokea 'muhuri wa Mungu aliye hai.' Hapo ndipo Yesu atakapoacha maombezi yake katika patakatifu pale pa mbinguni."

GC 613.

b. "Nikawaona malaika wale wakiharakisha kwenda huku na huku kule mbinguni. Malaika yule mwenye kidau cha wino cha mwandishi kiunoni mwake alirudi kutoka duniani na kutoa taarifa yake kwa Yesu ya kwamba kazi yake alikuwa amemaliza kuifanya, na ya kwamba watakatifu walikuwa wamehesabiwa na kutiwa muhuri. Ndipo nikamwona Yesu, ambaye alikuwa akihudumu mbele ya lile sanduku la agano ambalo ndani yake zilikuwamo zile Amri Kumi, akitupa chetezo chake chini. Akainua mikono yake juu, na kwa sauti kuu akasema, 'Imekwisha.' Na majeshi yote ya malaika wakazivua taji zao na kuziweka kando wakati Yesu alipotoa tangazo hili la kutisha, akisema, 'Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa.' " EW 279,280.

13. Baada ya jambo hilo wale malaika wanne watafanya nini?

"Kabla tu sisi hatujaingia [katika kipindi kile cha wakati wa taabu], sote tulipokea muhuri wa Mungu aliye hai. Ndipo nikawaona wale malaika wanne wakiacha kuzishikilia zile pepo nne. Nikaona njaa kubwa, tauni na upanga [mauaji], taifa likainuka juu ya taifa jingine, na ulimwengu wote ulikuwa katika machafuko." 7BC 968.

14. Ni akina nani peke yao watakaolindwa katika kipindi kile cha wakati wa taabu?

"Wale wanaoupokea muhuri wa Mungu na kulindwa katika kipindi kile cha wakati wa taabu yawapasa kuiakisi sura [kuwa na tabia] ya Yesu kikamilifu." EW 71.

15. Je, muhuri wa Mungu utawekwa juu yetu?

a. "Katika kitambo kidogo kijacho kila mmoja ambaye ni mtoto wa Mungu atakuwa ametiwa muhuri wake [Mungu] juu yake. Laiti kama ungaliweza kutiwa juu ya vipaji vya nyuso zetu! Nani atakayestahimili wazo lile la kupitwa milele na yule malaika anayetoka na kwenda kuwatia muhuri [alama] watumwa wa Mungu katika vipaji vya nyuso zao?" RH 5-28-1889.

b. "Njia yetu tuliyoichagua wenyewe katika kutenda mambo yetu [mwenendo wetu] itaamua iwapo tutaupokea muhuri ule wa Mungu aliye hai, ama tutakatiliwa mbali [tutauawa] kwa silaha zile za maangamizi [mapigo yale saba]. Tayari matone machache ya ghadhabu ya Mungu

yamedondoka juu ya nchi; lakini wakati ule yatakapomiminwa mapigo yale saba pasipo kuchanganywa na maji katika kikombe kile cha hasira yake, ndipo watakuwa wamechelewa mno kuweza kutubu na kupata kinga [ulinzi] yake. Hakuna damu yo yote ya upatanisho itakayoweza kuwaosha mawaa yao ya dhambi.

" 'Wakati huo Mikaeli atasimama.'... Kila kesi itakuwa imekatwa; muda wa majaribio [kupimwa] utakuwa haupo tena, rehema kwa wale wasiokuwa na toba itakuwa haipo tena. Muhuri wa Mungu aliye hai utakuwa juu ya watu wake." 5T 212,213.

## SURA YA 15

## ALAMA YA MNYAMA

1. Yohana, mwandishi wa kitabu cha Ufunuo, anatuonyaje sisi dhidi ya kuipokea Alama ya Mnyama? Ufu.14:9,10; 16:2.

2. Shetani atawatishiaje wale wanaoikataa Alama ya Mnyama? Ufu.13:11,15-17.

3. Alama ya Mnyama ni kitu gani?

a. "Yohana aliitwa ili apate kuwaangalia watu waliokuwa tofauti kabisa na wale wanaomsujudu Mnyama au Sanamu yake kwa kuitunza siku ya kwanza ya juma [Jumapili]. Utunzaji wa siku hiyo ndiyo Alama ya Mnyama." TM 133.

b. "Ishara, au muhuri wa Mungu huonekana katika utunzaji wa Sabato ya siku ya saba [Jumamosi], kumbukumbu yake Bwana ya Uumbaji.... Alama ya Mnyama ni kinyume chake [siku hiyo] ----- yaani, utunzaji wa siku ya kwanza ya juma [Jumapili]." 8T 117.

c. "Alama ya Mnyama ni sabato ya papa...." Ev 234.

d. "Jaribio [mtihani] lile litakapokuja, itadhihirika wazi kwamba alama hiyo ya mnyama ni kitu gani hasa. Ni ule utunzaji wa [siku ya] Jumapili." 7BC 977 (1899).

e. "Utunzaji wa Jumapili bado haujawa Alama ya Mnyama, wala hautakuwa hivyo mpaka hapo itakapotangazwa amri itakayowafanya wanadamu wote kuisujudia hiyo sabato ya sanamu [Jumapili]. Wakati utakuja ambapo siku hiyo itakuwa jaribio lile, lakini wakati ule bado haujafika." 7BC 977 (1899).

4. Bibi White alisema ni watu wangapi waliokuwa na Alama ya Mnyama?

"Hakuna ye yote mpaka sasa aliyeipokea alama hiyo ya mnyama." Ev 234 (1899).

5. Ni lini alama hiyo ya mnyama itakapopokewa? Je, jambo hilo litatokea kabla au baada ya kufungwa mlango wa rehema? Je, patakuwa na uwezekano wo wote kwa mtu ye yote kuteleza na

kuupita mlango wa rehema utakapofungwa bila kupokea ama muhuri wa Mungu, ama alama ya mnyama?

a. "Wakati wa kujaribiwa bado haujaja. Kuna Wakristo wa kweli katika kila kanisa [dhehebu], bila kuiacha jumuia ya Roma ya Kikatoliki. Hakuna wanaohukumiwa mpaka wamepata nuru na kuona uwajibikaji wao kwa amri ile ya nne. Lakini Sheria itakapotangazwa itakayowalazimisha watu wote kuitunza sabato hiyo ya uongo [Jumapili], na ile sauti kuu ya malaika yule wa tatu itakapowaonya watu dhidi ya kumsujudu yule mnyama na sanamu yake, hapo ndipo mstari utakapochorwa waziwazi kati ya [sabato] ile ya uongo na ile ya kweli. Ndipo wale watakaoendelea kuivunja amri hiyo watakapopokea alama ya mnyama." Ev 234,235.

b. "Kama nuru ya ile kweli imetolewa kwako, ikikuonyesha Sabato ile ya amri ya nne, na kukuonyesha wewe kwamba hakuna msingi wo wote katika Neno la Mungu wa kuitunza siku ya Jumapili, kisha wewe ukawa bado unaendelea kuing'ang'ania sabato hiyo ya uongo [Jumapili], na kukataa kuitunza ile Sabato [Jumamosi] ambayo Mungu anaiita 'Siku ya utakatifu wangu,' basi, wewe utapokea Alama ya Mnyama. Jambo hilo litatokea lini? Utakapoitii amri ile itakayokuamuru wewe kuacha kufanya kazi siku ya Jumapili na [kukuamuru] kumwabudu Mungu [siku hiyo] wakati wewe unajua fika kuwa hakuna Neno hata moja katika Biblia linaloionyesha Jumapili kuwa si siku nyingine ila ni siku ya kawaida ya kufanya kazi, basi, wewe utakuwa unakubali kuipokea alama ile ya Mnyama, na kukataa kuupokea muhuri wa Mungu.

"Endapo tutaipokea alama hiyo juu ya vipaji vya nyuso zetu au katika mikono yetu, basi, hukumu zile zilizotangazwa juu ya waasi [wavunjaji wa Sheria] zitatuangukia juu yetu. Lakini muhuri ule wa Mungu aliye hai utawekwa juu ya wale wanaoitunza Sabato ya Bwana kwa uangalifu sana." RH 7-13-1897; 7BC 980 (Angalia pia Ev 235).

c. "Utunzaji wa Jumapili utakapolazimishwa kwa sheria [ile itakayotungwa], na ulimwengu wote utakapokuwa umeelimishwa juu ya uwajibikaji wao kwa Sabato ile ya kweli, ndipo mtu awaye yote atakayeivunja amri hiyo ya Mungu, ili kuitii amri ambayo haina mamlaka ya juu kuliko ile ya Roma, atakuwa anauheshimu upapa na kuuinua juu ya Mungu. Atakuwa anamsujudu Roma pamoja na mamlaka ile [Marekani] inayoitungia sheria siku hiyo iliyoamriwa na Roma. Atakuwa anamwabudu Mnyama na Sanamu yake. Wakati huo wanadamu watakapoikataa siku ile iliyotangazwa na Mungu kuwa ndiyo ishara ya mamlaka yake, na badala yake kuiheshimu ile iliyochaguliwa na Roma kama alama (ishara) ya utii kwa Roma ----- yaani, ile 'Alama [Chapa] ya Mnyama' [Jumapili]. Na jambo hilo halitakuwa hivyo mpaka hapo litakapokuwa limewekwa wazi mbele ya watu wote, nao watafikishwa mahali pa kuchagua kati ya Amri [Kumi] za Mungu na amri za wanadamu, kiasi kwamba wale watakaoendelea kuivunja [Sheria ya Mungu] watapokea 'Alama ya Mnyama.' " GC 449.

d. "Mamlaka za duniani humu, zikiungana kuipiga vita Sheria ya Mungu [Amri Kumi], zitatangaza amri kwamba 'wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, walio huru na watumwa' (Ufunuo 13:16), watafuata desturi za kanisa kwa lazima na kuitunza sabato ile ya uongo [Jumapili].... Kwa upande mwingine, Sheria ya Mungu [Amri Kumi] inayoamuru siku ya mapumziko [Sabato] ya yule Muumbaji wetu inataka utii na kutishia ghadhabu dhidi ya wale wote watakaoendelea kuzivunja Amri zake [Kumi].

"Jambo hilo litakapokuwa limewekwa wazi mbele yake [kila mtu], hapo ndipo mtu awaye yote atakayeikanyaga chini ya miguu yake Sheria ya Mungu [Amri Kumi] ili kuitii amri [ya Jumapili] iliyotungwa na wanadamu ataipokea hiyo Alama ya Mnyama...." GC 604.

e. "Wakati kundi moja, kwa kuikubali ishara ya utii [Jumapili] kwa mamlaka zile za kidunia, wanapokea Alama ya Mnyama, [kundi] jingine likiwa limechagua kuitii ishara [Sabato] ya mamlaka ile ya Mbinguni watapokea Muhuri wa Mungu." GC 605.

SURA YA 16

# KUFUNGWA KWA MLANGO WA REHEMA

1. Je, kuna baadhi ya watu walio hai leo waliokwisha kufunga mlango wao wa rehema, kiasi kwamba Roho Mtakatifu hawezi tena kuwafikia?

a. "Kila siku mlango wa rehema kwa baadhi ya watu unafungwa. Kila saa wengine wanakwenda mbali sana mahali ambako hawawezi kufikiwa na rehema." PP 140.

b. "Kila siku tumekuwa tukishirikiana na wanaume pamoja na wanawake ambao wanaelekea hukumuni. Kila siku huenda imekuwa ndio mstari wa kumgawa mtu fulani mmoja; mtu fulani huenda amekata shauri ambalo baadaye litaamua hatima ya uzima wake wa milele. Je! mvuto wetu ukoje juu ya wasafiri hao wenzetu? Ni juhudi gani tumefanya kuwaleta kwa Kristo?" 5T 466.

2. Je, hivi sisi wenyewe tunajua ni lini muda wetu wa majaribio unaweza kufungwa?

a. "Hatujui ni upesi jinsi gani mlango wa rehema [kutubu] unaweza kufungwa. Kwa urefu wake, tunacho kipindi kifupi tu cha kuishi hapa, wala hatujui ni upesi jinsi gani mshale ule wa mauti unaweza kuipiga mioyo yetu. Hatujui ni upesi jinsi gani tunaweza kuitwa kuiacha dunia hii na mambo yake yote yanayopendeza." MH 454.

3. Ni katika matukio gani manne, kwa uchache, ya wakati uliopita pamekuwapo na kufungwa kwa jumla kwa mlango huo wa rehema kwa sehemu kubwa ya watu?

a. "Palikuwa na mlango uliofungwa katika siku zile za Nuhu. Wakati ule palikuwa na kuondolewa kwa Roho wa Mungu kutoka kwa taifa lile lenye dhambi ambalo liliangamia katika maji yale ya Gharika.... (Mwanzo 6:3)." 1SM 63.

b. "Palikuwa na mlango uliofungwa siku zile za Ibrahimu. Rehema iliacha kuwaombea wakazi wale wa Sodoma...." 1SM 63.

c. "Palikuwa na mlango uliofungwa siku zile za Kristo. Mwana wa Mungu aliwatangazia maneno haya Wayahudi wa kizazi kile waliokuwa hawaamini, akasema, 'Nyumba yenu [Hekalu] mmeachiwa hali ya ukiwa (Mathayo 23:38).' " 1SM 63.

d. "Palikuwa na mlango uliofungwa mwaka ule wa 1844. Wale wote walioiona nuru ya [waliouelewa] ujumbe wa malaika wa kwanza na malaika wa pili na kuikataa nuru ile, waliachwa gizani. Na wale walioipokea na kumpokea Roho Mtakatifu aliyeambatana na tangazo la ujumbe ule uliotoka mbinguni, na ambao baadaye waliikana imani yao na kutangaza kwamba uzoefu wao

waliokuwa wameupitia ulikuwa ni udanganyifu [mtupu], kwa njia hiyo walimkataa Roho wa Mungu, naye hakuendelea tena kuwasihi."  1SM 63.

4. Ni amri gani kutoka mbinguni itakifunga kipindi hicho cha majaribio kwa familia yote ya kibinadamu?  Ufunuo 22:11,12.

5. Ni tendo gani la Kristo litaashiria kwamba maombezi yake kwa ajili ya wenye dhambi yamekoma milele?  Dan.12:1;  Ufu. 15:8.

6. Hivi sisi tunajua ni lini itakapokuja saa hiyo iliyotabiriwa na Mungu?

a. "Mungu hajatufunulia sisi ujumbe huu [tunaouhubiri] utafungwa lini, au muda wa majaribio utakapokwisha.  Mambo yale yaliyofunuliwa tutayapokea kwa ajili yetu sisi wenyewe na kwa ajili ya watoto wetu;  walakini tusijaribu kutaka kujua kile ambacho kimetunzwa kama siri katika mabaraza yake Mungu Mwenyezi [Kum. 29:29]...."  1SM 191;  7BC 989.

b. "Barua zimenijia zikiniuliza mimi iwapo ninayo nuru ya pekee kuhusu wakati ambapo mlango wa rehema utafungwa;  mimi nawajibu kwamba ninao ujumbe huu tu wa kuupeleka, kwamba sasa ndio wakati wa kufanya kazi [ya Mungu] wakati siku hii bado ingalipo, kwa maana usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi."  1SM 191;  7BC 989.

c. "Hakuna amri iliyotolewa kwa mtu ye yote kuyachunguza Maandiko ili, kama inawezekana, kuhakikisha ni lini mlango wa rehema utakapofungwa.  Mungu hana ujumbe kama huo utakaotolewa kwa kinywa cha mwanadamu ye yote anayekufa.  Asingependa ulimi wo wote wa mwanadamu anayekufa utangaze kile ambacho yeye amekificha katika mabaraza [vikao] yake ya siri."  1SM 192;  7BC 990.

7. Je, kuna unabii wo wote unaohusu wakati ambao hauna budi kutimizwa kabla ya kufungwa kwa mlango huo wa rehema?

"Wanadamu hawatapewa ujumbe mwingine unaotaja wakati halisi....  Kipindi kirefu kuliko vyote kilichopata kufanyiwa mahesabu ni kile kinachofika mpaka kwenye majira yale ya kupukutisha [Septemba - Novemba] ya mwaka ule wa 1844."  7BC 971.

8. Ni utabiri gani wa hakika umetolewa kuhusu kulazimisha kisheria utunzaji wa siku ya Jumapili kabla ya kufungwa kwa mlango ule wa rehema?

a. "Bwana amenionyesha waziwazi kwamba Sanamu ya Mnyama itaundwa kabla ya kufungwa kwa mlango ule wa rehema;  kwa maana hiyo ndiyo itakayokuwa jaribio kubwa kwa watu wa Mungu, ambayo kwayo uzima wao wa milele utaamuliwa....  Hilo ndilo jaribio [mtihani] ambalo watu wa Mungu watalazimika kulipata kabla hawajatiwa muhuri."  7BC 976.

b. "Jaribio hilo kuu la mwisho litakuja wakati unakaribia kufungwa mlango ule wa rehema, wakati mtu atakapokuwa amechelewa mno kukidhi mahitaji yake ya kiroho."  COL 412.

9. Pana uhusiano gani kati ya Amri ya Jumapili kwa ulimwengu mzima na kufungwa kwa mlango wa rehema kwa mataifa yote ya dunia hii? (Tazama maelezo chini ya Swali la 8 la Sura ya 4 nyuma ----- AMRI YA JUMAPILI KWA ULIMWENGU MZIMA).

10. Ni majukumu gani matatu yanayotimilika karibu kwa wakati ule ule mmoja wakati wa kufungwa kwa mlango huo wa rehema?

a. "Watu wa Mungu watakuwa wamemaliza kufanya kazi yao.... Malaika yule atakayerudi [mbinguni] toka duniani atatangaza kwamba kazi yake imekwisha.... Hapo ndipo Yesu atakapokoma [atakapoacha] kufanya maombezi yake katika patakatifu pale pa mbinguni. Atainua juu mikono yake na kwa sauti kuu, atasema, 'Imekwisha.' " GC 613.

b. "Marejeo ya kazi zetu [vitabu] zilizochapishwa yataonyesha imani yetu kwamba wenye haki walio hai watapokea muhuri wa Mungu kabla ya kufungwa kwa mlango ule wa rehema; pia kwamba hao watafaidi heshima ya pekee katika ufalme ule wa Mungu." 1SM 66.

c. "Kazi ile ya [hukumu ya] upelelezi itakapokwisha, kesi za wale wote waliokiri ya kuwa ni wafuasi wake Kristo katika vizazi vyote zitakapokuwa zimechunguzwa na kukatwa, ndipo, na sio kabla ya wakati huo, muda wa majaribio utakapofungwa, na mlango wa rehema utakapofungwa." GC 428.

11. Maisha yatakuwaje ulimwenguni humu siku ile mlango wa rehema utakapofungwa? Je, kuna mtu ye yote atakayetambua kwamba saa ya kukata maneno imefika?

a. "Kabla ya ile Gharika, baada ya Nuhu kuingia ndani ya safina, Mungu akamfungia ndani ya safina, yaani, Mungu akamfungia ndani na kuwafungia nje wale wasiomcha Mungu; lakini kwa siku saba watu wale, bila kujua kuwa mwisho wao ulikuwa umewekwa tayari, waliendelea na maisha yao ya kutojali, kupenda anasa na kuyadhihaki maonyo ya hukumu yao iliyokuwa imekaribia sana. 'Ndivyo,' asema Mwokozi, 'kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.' Mathayo 24:39. Kimya kimya, bila kuonekana kama mwivi wa usiku wa manane, itakuja saa ile ya kukata maneno itakayoamua mwisho wa maisha ya kila mtu, kuondolewa kwa mara ya mwisho kwa toleo la rehema kwa wanadamu wenye dhambi." GC 491.

b. "Wakati mtu yule wa biashara amezama [mawazo yake yote yako] katika kutafuta faida yake, wakati mpenda anasa yule anatafuta kujifurahisha nafsi yake, wakati binti yule wa mitindo ya kisasa anayapanga mapambo yake ----- huenda ni katika saa ile Hakimu yule wa dunia yote atakapotamka maneno haya: 'Umepimwa katika mizani nawe umeonekana kuwa umepunguka.' " GC 491.

c. "Hatari kubwa inanyemelea polepole kuja juu yetu. Jua linaangaza huko mbinguni, linapita katika njia yake kama kawaida, na mbingu zingali bado zinatangaza utukufu wake Mungu. Watu wangali bado wanakula na kunywa, wakipanda na kujenga, wakioa na kuolewa. Wafanya biashara bado wanaendelea kununua na kuuza. Watu wanapigana vikumbo, wakigombania nafasi [cheo] ile ya juu sana. Wapenda anasa bado wanajaa kwenye majumba ya michezo, kuangalia mbio za farasi, kwenye kumbi za michezo ya kamari [au bahati nasibu]. Misisimko mikubwa sana iko kila mahali, lakini saa ya kufungwa kwa mlango wa rehema inakaribia sana kufungwa, na kila kesi [ya mwenye

dhambi] karibu itakatwa milele. Shetani anaona kwamba wakati wake ni mchache. Amewaweka mawakala wake wote kazini ili watu wapate kudanganywa, kughilibiwa akili zao, kushughulishwa, na kufurahishana mpaka siku ile ya majaribio itakapofikia mwisho wake, na mlango ule wa rehema utakapofungwa milele."

ChS 51 (Angalia pia FE 335).

12. Maisha yataendelea kuwaje mpaka dakika ile ya kuangamizwa kwa waovu?

a. "Kama vile ambavyo watu wale wa siku za Nuhu hawakutambua, hata Gharika ikaja, ikawachukua wote; ndivyo, kwa maneno yake Mwokozi, 'kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.' Mathayo 24:39. Wale wanaojidai kuwa ni watu wa Mungu watakapojiunga na ulimwengu, na kuishi kama wanavyoishi [walimwengu hao], na kujiunga nao katika anasa zile zilizokatazwa; wakati anasa ya ulimwengu itakapokuwa ndiyo anasa ya kanisa; kengele za ndoa zitakapokuwa zikilia, na wote wakitarajia kuwa na miaka mingi ya usitawi [mafanikio] katika ulimwengu huu ----- ndipo, kwa ghafula kama vile umeme unavyomulika mbinguni, utakuja mwisho wa maono yao mazuri ya mambo yale ya mbele pamoja na matumaini yao ya uongo." GC 338,339.

b. "Sababu za kifalsafa zinafukuzilia mbali hofu ya hukumu za Mungu; waalimu wa kidini wanapoyaelekeza macho ya watu wao kwa vizazi vile virefu vya amani na usitawi vinavyokuja, na walimwengu wanapozama katika shughuli zao za biashara na anasa, wakiwa wanapanda na kujenga, wakila karamu na kujifurahisha, wakiyakataa maonyo ya Mungu na kuwadhihaki wajumbe wake, ----- ndipo maangamizi ya ghafula yatakapowajia, wala hawataokoka." PP 104.

c. "Na ije wakati ule itakapoweza kuja, siku hiyo ya Mungu itakuja kwa waovu bila wao kujua. Maisha yatakapokuwa yakiendelea kama kawaida; watu watakapozama katika anasa zao, katika biashara zao, katika usafiri (wa anga, nchi kavu, na majini), katika kuchuma fedha; viongozi wa dini watakapokuwa wanayatukuza maendeleo na hekima ya ulimwengu huu, na watu watakapokuwa wamelazwa katika hali ya usalama wa uongo ----- kama vile mwivi yule wa usiku wa manane anavyoiba katika makao yale yasiyolindwa, hivyo ndivyo maangamizi ya ghafula yatakavyowajia wale wasiojali na waovu, 'wala hakika hawataokolewa' " GC 38.

d. "Ibada za dini zitaendelezwa na watu wale ambao Roho wa Mungu atakuwa ameondoka kwao kwa mara ya mwisho; na juhudi ya kishetani ambayo mkuu yule wa giza atawachochea kuweza kutekeleza mipango yake miovu sana, itafanana na juhudi ile inayofanyika kwa ajili ya [kumtumikia] Mungu." GC 615.

13. Je, Waadventista Wasabato watatarajia kwamba kufungwa kwa mlango wa rehema kutatokea kwa wakati wake ule ule?

a. "Ukweli huu wa kutisha unapaswa kuwekwa si mbele ya watu wa ulimwengu huu tu, bali pia mbele ya makanisa yetu wenyewe, ya kwamba siku ya Bwana itakuja kwa ghafula, yaani, pasipo kuitarajia." FE 336.

b. "Rehema itakapokoma, itakuwa kwa ghafula, yaani, pasipo kutarajiwa ----- yaani, wakati ule ambapo sisi tutakuwa hatutarajii hata kidogo. Walakini, sisi twaweza kuwa na kumbukumbu yetu safi kule mbinguni leo hii, na kujua kwamba Mungu anatukubali...." 7BC 989.

14. Wenye haki watakuwa wanaishi wapi na watakuwa wakifanya kazi gani mpaka hapo mlango wa rehema utakapofungwa?

"Ngano na magugu huachwa 'vyote vikue hata wakati wa mavuno.' Katika kutekeleza majukumu yao ya maisha wenye haki mpaka mwisho watagusana na waovu. Wana wa nuru wametawanyika miongoni mwa wana wa giza, ili tofauti ipate kuonekana wazi na wote."

5T 100.

15. Je, patakuwa na ishara yo yote ya ajabu hapa duniani kuonyesha kwamba Kristo amemaliza kazi yake ya maombezi kule mbinguni?

Mzee G. A. Irwin aliandika maneno haya katika Nyongeza ya gazeti la Review and Herald la tarehe 21 Juni, 1898, uk. 1, "Giza litawafunika wakazi wa dunia hii Yesu atakapotoka katika patakatifu pa mbinguni, kama lile lililoifunika dunia wakati wa kusulibiwa kwake." Lakini ifahamike wazi kwamba usemi huo hauungwi mkono na Roho ya Unabii. Bibi White asema hivi, "Atakapotoka patakatifu giza litawafunika wakazi wa dunia hii.' GC 614. Giza hilo bila shaka ni la kiroho, yaani, 'giza la makosa [mafundisho potofu] na madanganyo...." EW 104.

16. Je, wenye haki watakuwa na njia nyingine yo yote ya kujua iwapo mlango huo wa rehema utakuwa umefungwa?

a. "Hukumu isiyoweza kubadilika ya patakatifu itakapokuwa imetangazwa na mwisho wa ulimwengu huu utakapokuwa umekazwa kwa milele, wakazi wa ulimwengu huu hawatajua." GC 615.

17. Hivi Shetani atajua kwamba mlango wa rehema umefungwa?

a. "Katika kipindi kile cha wakati wa taabu, Shetani atawachochea waovu, nao watawazingira watu wa Mungu ili kuwaangamiza. Walakini yeye atakuwa hajui kwamba 'msamaha' umeandikwa upande wa pili wa majina yao katika vitabu vile vya mbinguni."

RH 11-19-1908, uk. 5.

b. "Anaona kwamba malaika wale watakatifu wanawalinda, naye anahisi kwamba dhambi zao zimesamehewa; ila hajui kwamba kesi zao zimekatwa katika patakatifu pale pa mbinguni." GC 618.

18. Biblia yasema ni jambo gani litafuata mlango wa rehema utakapokuwa umefungwa? Ufu. 15:8; 16:1; 19:11-15.

a. "Nikaona ya kwamba wale malaika wanne wangeweza kuendelea kuzizuia pepo zile nne mpaka hapo kazi ya Yesu itakapokuwa imekwisha katika patakatifu pale pa mbinguni, hapo ndipo mapigo yale saba ya mwisho yatakapokuja." EW 36.

b. "Kazi ya hukumu ya upelelezi itakapofungwa, mwisho wa watu wote utakuwa umeamuliwa ama kwa uzima [wa milele], ama kwa mauti [ya milele]. Muda wa majaribio utakwisha muda mfupi kabla ya kuja kwa Bwana na mawingu ya mbinguni." GC 490.

# SURA YA 17

# UKAMILIFU NDANI YA KRISTO

1. Je, sisi tuna utakatifu, au haki, kiasi gani wakati wa kuzaliwa kwetu? Ayubu 14:4; Zaburi 51:5; Warumi 3:10,19.

"Adamu aliumbwa akiwa mtu mkamilifu, asiye na dhambi, asiyekuwa na waa hata moja la dhambi juu yake; alikuwa katika sura ya Mungu. Angeweza kuanguka, naye alianguka kwa kuvunja sheria. Kwa sababu ya dhambi yake uzao wake ulizaliwa na mielekeo mibaya ya uasi ya kurithi. 5BC 1128.

2. Ni wangapi wameshindwa na mielekeo yao mibaya ya asili ya kutenda dhambi? Warumi 3:23.

3. Tunapaswa kuwa wakamilifu, au watakatifu, kiasi gani kama tunataka kuokolewa katika ufalme wake Mungu?

"Yule anayeingia mbinguni hana budi kuwa na tabia ile isiyokuwa na waa, wala kunyanzi, wala lo lote kama hayo. Hakuna cho chote kilicho najisi (kinyonge) kinachoweza kuingia kule. Katika jeshi lote la wale waliokombolewa haitaonekana dosari hata moja." MYP 144.

4. Ni maandalizi gani aliyofanya Bwana ili kuliziba pengo lililopo kati ya matakwa yake makamilifu na maisha yetu yasiyo na ukamilifu wo wote? Rum.5:17-19; 1 Petro 2:24.

"Kristo alitendewa tunavyostahili sisi kutendewa, ili sisi tupate kuhesabiwa haki yake, ambayo sisi hatukuishiriki. Alikufa kifo kilichokuwa chetu sisi, ili tupate kuupokea uzima uliokuwa wake. 'Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.' " DA 25.

5. Mwenye dhambi anawezaje kujipatia kipawa hicho cha mbinguni? Rum. 3:24-28.

"Njia pekee ambayo kwayo [mwenye dhambi] anaweza kupata haki ni kwa njia ya imani. Kwa imani anaweza kuleta kwa Mungu wema wa Kristo, na Bwana anaweka utii wa Mwanawe katika akaunti ya mwenye dhambi huyo.." 1SM 367.

6. Baada ya Kristo kutusamehe dhambi zetu na kutufunika kwa vazi lake la haki, sisi, je! tunakuwa wakamilifu au watakatifu kwa kiwango gani mbele zake Mungu? Rum.4:5-7.

a. "Kwa njia ya haki yake Kristo sisi tutasimama mbele zake Mungu tukiwa tumesamehewa, kana kwamba tulikuwa hatujapata kutenda dhambi kamwe." 5BC 1142.

b. "Kwa kafara yake Kristo yenye kuleta matokeo mema, tunaweza kusimama mbele zake Mungu tukiwa safi na bila mawaa, dhambi zetu zikiwa zimelipiwa fidia yake na kusamehewa.... Mwenye dhambi aliyekombolewa, akiwa amevikwa mavazi ya haki yake Kristo, anaweza kusimama mbele za Mungu anayeichukia sana dhambi, akiwa ametimilika kwa wema wake Mwokozi." ST 3-15-1905, uk. 9.

c. "Yesu anaendelea kusema hivi: Kadiri mnavyonikiri Mimi mbele ya watu, ndivyo nami nitakavyowakiri mbele za Mungu na mbele ya malaika zake. Ninyi mnapaswa kuwa mashahidi wangu ulimwenguni, kuwa mifereji ambayo kwayo neema yangu inaweza kutiririka kwa uponyaji wa ulimwengu huu. Kwa hiyo, Mimi nitakuwa mwakilishi wenu mbinguni. Baba yangu haiangalii tabia yenu yenye makosa, bali anawaangalia ninyi kuona kama mmevikwa na ukamilifu wangu." DA 357.

7. Hata kama sisi, kwa maana moja tunaweza kufikiriwa kuwa tumekuwa wakamilifu kuanzia wakati ule wa kuongoka kwetu, ni sehemu gani inayofuatia katika mpango wa Mungu kwa ajili yetu? l The. 4:3.

a. "Kuirejesha ndani ya mwanadamu sura ile ya Muumbaji wake, kumrejesha katika ukamilifu ule alioumbiwa nao, kukuza usitawi wa mwili, nafsi na roho yake ili kusudi lile la Mungu katika uumbaji wake lipate kutimizwa ----- hiyo ndiyo kazi ya ukombozi Hilo ndilo lengo la elimu, yaani, lengo kuu la maisha." Ed 15,16.

b. "Wazo bora la Mungu alilo nalo kwa ajili ya watoto wake ni la juu sana kuliko upeo unaoweza kufikiwa na fikira za juu kabisa za kibinadamu. 'Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.' Amri hii ni ahadi. Mpango wa ukombozi unazingatia kuokolewa kwetu kabisa kutoka katika uwezo wa Shetani. Sikuzote Kristo humtenga mtu yule aliyetubu mbali na dhambi." DA 311.

c. "Watu wanapoongolewa, wokovu wao unakuwa bado haujakamilika. Hapo ndipo wanapopaswa kupiga mbio; pambano linalohitaji nguvu nyingi li mbele yao ili wapate kupiga vita vile vizuri vya imani.'... Vita hiyo ni ya maisha yote ya mtu, na lazima iendelezwe kwa nguvu thabiti kulingana na thamani ya kitu kile unachokitafuta, ambacho ni uzima wa milele...." OHC 163.

d. "Kazi ya utakaso haina budi kuendelea mbele, si kwa kufuata msisimko wa ghafula, bali kwa kusonga mbele kwa uthabiti, na siha, yaani, kusonga mbele kuelekea kwenye ukamilifu ule." RH 3-5-1895.

e. "Haki ile ambayo kwayo sisi tunahesabiwa haki huwa tunawekewa kwenye akaunti yetu; haki ile ambayo kwayo tunatakaswa huwa tunapewa kuwa sehemu yetu kabisa kwa kushirikishwa [kuiweka katika matendo yetu]. Ya kwanza ni haki yetu ya kuingilia mbinguni, ya pili ni stahili yetu ya kuishi mbinguni." MYP 35.

8. Wakati wa uzoefu wetu wa maisha kama Wakristo, je, Bwana anatuangalia sisi kama tumekuwa wakamilifu au wasio wakamilifu ----- au yote mawili?

A. Kama Wakamilifu.

(1) Mkristo aliyezaliwa mara ya pili ni mkamilifu kama vile mtoto mchanga aliyezaliwa hivi karibuni alivyo mkamilifu. Yesu ametusamehe dhambi zetu. Tunahesabiwa haki kwa njia ya haki yake Kristo ile tunayowekewa kwenye akaunti yetu. Mwivi yule msalabani, kutokana na msimamo huu, alikuwa mkamilifu. Angalia madondoo chini ya swali la 6 (nyuma).

(2) Bwana anamwangalia Mkristo yule anayekua kuwa ni mkamilifu iwapo anaridhika na ukuaji wake huo. Huenda tukawa Wakristo kwa kipindi kifupi tu, huenda ufahamu wetu wa mambo ya kiroho ukawa ni kwa sehemu tu, na imani yetu ikawa dhaifu, lakini Mungu bado atatuangalia sisi kuwa tu wakamilifu iwapo tutaendelea kukua kwa taratibu kwa njia ya haki yake Kristo tunayopewa kuwa sehemu yetu kabisa kwa kushirikishwa [kuiweka katika matendo yetu]. "Kwa kila hatua ya kukua kwetu maisha yetu yanaweza kuwa makamilifu; hata hivyo kama kusudi lake Mungu kwa ajili yetu limetimilika, basi, kutakuwa na ukuaji unaoendelea daima." COL 65. Bila kujali makosa yao Biblia inawaita akina Nuhu, Hezekia, na Asa kuwa walikuwa wakamilifu (Mwanzo 6:9; Isa.38:3; 1 Wafalme 15:14). Paulo anazungumza habari za wale walioishi katika siku zake ambao walikuwa wakamilifu (Wafilipi 3:15), lakini kwa pumzi ile ile anasema kwamba huo haukuwa ukamilifu wa kiwango cha juu kabisa kinachoweza kufikiwa (Wafilipi 3:12; angalia swali la 9, dondoo la a na b).

(3) Mkristo anafikiriwa pia kuwa ni mkamilifu, wakati ule anapoifikia hali ile asiyoweza kutenda dhambi, hata kwa wazo moja tu, kwa njia ya haki ya Kristo iliyofanywa kuwa sehemu ya maisha yake (ya kila siku). Mtu kama huyo, kwa njia ya uweza wa Mungu aliopewa, amekifikia kiwango cha juu kabisa cha lengo lile la ukamilifu linaloweza kufikiwa katika maisha haya (tuliyo nayo). Wakati wa kufungwa kwa mlango ule wa rehema kila mmoja wa watakatifu walio hai, atakuwa amelifikia lengo hilo la kiroho kwa neema yake Mungu. Angalia madondoo chini ya swali la 27.

B. Kama Wasio Wakamilifu.

(1) Mwivi yule msalabani na waongofu wote wapya wanaweza kufikiriwa kuwa hawajawa wakamilifu kwa kuwa hawajapata nafasi ya kuzikuza tabia zao. Kuna maendeleo yatakayochukua maisha yote ya mtu katika kuikuza tabia yake [ya Kikristo].

(2) Mkristo aliye na uzoefu [wa maisha ya Kikristo] kwa miaka mingi, kusema kweli, si mkamilifu kwa kadiri anavyoendelea kutenda dhambi, hata kwa mara chache tu. Daudi alikuwa mtu mmoja aliyependwa sana na Mungu, lakini pia alikuwa si mkamilifu kabisa. "Sisi bado hatujawa wakamilifu, lakini ni haki yetu kuvikatilia mbali vifungo vya nafsi na dhambi zetu vinavyotufunga, na kusonga mbele kwenda kwenye ukamilifu ule." AA 565.

(3) Mkristo anayekoma kutenda dhambi, hata kwa wazo moja tu, si mkamilifu kwa maana ile ya kwamba bado kuna mengi anayoweza kujifunza juu ya Mungu. "Hata Mkristo yule aliye mkamilifu sana anaweza kuongezeka daima kukua zaidi na zaidi katika kumjua na kumpenda Mungu." 1T 340. "Kwa kukua kila siku katika maisha ya utakatifu, hataweza kuwa mtu mkamilifu hata kuweza kukifikia cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo [Waefeso 4:13] mpaka hapo muda wake wa majaribio utakapokwisha." 4T 367.

(4) Mkristo asiyetenda dhambi, hata kwa wazo moja tu, bado anakabiliwa na majaribu ya tamaa za mwili wake. Bado anayo vita ya kupigana, naye anapaswa kufanya hivyo mpaka hapo Kristo atakaporudi mara ya pili. Yeye si mkamilifu na ataendelea kuwa hivyo mpaka Kristo atakapompa mwili mpya utakaokuwa umeondolewa mielekeo yote ya dhambi tuliyorithi. "Sisi hatuwezi kusema Mimi sina dhambi mpaka hapo mwili wetu huu wa unyonge (mwovu) [Wafilipi 3:21] utakapobadilishwa na kufanana na mwili wake wa utukufu." ST 3-23-1888. Angalia madondoo chini ya swali la 30 na 31.

(5) Mkristo ambaye anakoma kutenda dhambi, hata kwa wazo moja tu, bado yeye ni binadamu tu, mwenye uwezo wa kufanya makosa bila kukusudia. Anaweza kutumia sarufi mbaya na hata kuweza kuwa na tabia fulani zisizopendeza au mazoea mabaya ya afya yake ya kimwili. Tabia yake huenda ikawa ni kamilifu, lakini yeye kama mwana wa Adamu aliye na dhambi, si mkamilifu. "Kila kitu cha kibinadamu si kikamilifu." 1SM 20. "Kwetu sisi kuwatupa mbali wakosaji, kuwatendea kwa ubaridi, kusingekuwa ndiko kutenda kama vile Kristo alivyotutendea sisi. Sisi tunaweza kukosa. Tunahitaji kuhurumiana sisi kwa sisi na kufikiriana na kusameheana. Hatuwezi kupata ukamilifu mahali ko kote, wala tusiutarajie kuupata. Kwa uvumilivu tunapaswa kuchukuliana na upotovu wa wanadamu, na kujaribu kuwafundisha." Letter B-16-1885.

9. Yesu aliposema, "Basi ninyi mtakuwa wakamilifu," alikuwa na maana gani?

a. "Kristo anaweka mbele yetu ukamilifu wa hali ya juu kabisa wa tabia yetu ya Kikristo, ambao kwa maisha yetu yote tungelenga [tungekusudia] kuufikia. 'Basi ninyi mtakuwa wakamilifu,' asema yeye, 'kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.' Kuhusu ukamilifu huo, Paulo anaandika hivi: 'Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu, la! bali nakaza mwendo....' " MS 148, 1902.

b. "Mtume mwenyewe alikuwa anajitahidi kukifikia kipimo kile kile cha utakatifu ambacho alikuwa amekiweka mbele ya ndugu zake." SL 86.

c. "Kwa uwezo wetu ulio na kikomo chake tunapaswa kuwa watakatifu katika mazingira yetu kama vile Mungu alivyo mtakatifu katika mazingira yake." SD 155; RH 11-1-1892.

d. "Kazi yetu ni kujitahidi katika mazingira yetu ya matendo kuufikia ukamilifu ule ambao Kristo katika maisha yake hapa duniani aliufikia katika kila sura ya tabia yake." SD 154;

MM 253.

e. "Yeye ni Kiolezo chetu.... Hatuwezi kuwa sawa na Kiolezo hicho, lakini hatutapata kibali chake Mungu kama hatukiigi na, kwa kadiri ya uwezo ule ambao Mungu ametupatia, kujitahidi kufanana nacho." 2T 549.

10. Je, lengo hilo ----- ukamilifu katika mazingira yetu ya matendo ----- ni wazo lisilowezekana au ni lengo hasa linaloweza kufikiwa?

a. "Wale tu ambao kwa njia ya imani katika Kristo wanazitii amri zote [kumi] za Mungu ndio watakaoifikia hali ile ya kutotenda dhambi ambayo alikuwa nayo Adamu kabla ya uasi wake. Wanatoa ushuhuda wa upendo wao kwa Kristo kwa kuzitii amri zake zote [kumi]." 6BC 1118.

b. "Mfano huu umetolewa kwetu ili sisi tupate kujua uwezekano mwingi uliopo, yaani, kimo tunachoweza kukifikia ndani na kwa njia ya Kristo. Kipimo anachotuonyesha ni ukamilifu [tukiwa] ndani yake, na kwa njia ya wema wake tunaweza kukifikia. Tunashindwa kulifikia lengo hilo kwa sababu tunaridhika kuyaangalia mambo ya ulimwengu huu kuliko yale ya mbinguni." KH 117.

c. "Yesu hakudhihirisha sifa zo zote za tabia, wala kutumia uwezo wo wote, ambao wanadamu hawawezi kuwa nao kwa njia ya imani katika yeye. Ubinadamu wake mkamilifu ni ubinadamu ule ule ambao wafuasi wake wote wanaweza kuwa nao, iwapo watamtii Mungu kama vile yeye alivyomtii." DA 664.

d. "Amefanya iwezekane kwao kukamilisha tabia yao ya Kikristo kwa njia ya jina lake, na kushinda wao wenyewe kama yeye alivyoshinda kwa ajili yao." 3T 365.

e. "Mungu anatutaka sisi kukifikia kipimo kile cha ukamilifu, naye anaweka mbele yetu kielelezo cha tabia yake Kristo. Katika ubinadamu wake, uliokamilishwa kwa kuyapinga daima maovu yaliyomkabili, Mwokozi alionyesha ya kwamba kwa njia ya kushirikiana na Mungu, wanadamu wanaweza kuufikia ukamilifu wa tabia katika maisha haya. Hiyo ni ahadi ya Mungu kwetu ya kwamba sisi pia tunaweza kupata ushindi kamili." AA 531.

11. Hivi Bwana anakusudia kwamba, kwa neema yake, sisi tunaweza kuishi maisha yetu hapa na wakati huu wa sasa ambayo hayana dhambi kabisa? Yuda 1:24; Wafilipi 4:3l 2 Petro 2:9; 1 Kor. 10:13; 2 Kor.10:5.

a. "Tunaweza kushinda. Naam; kikamilifu, yaani, kabisa. Yesu alikufa ili kutupatia njia ya kutokea, ili sisi tupate kuishinda hasira ya kila namna, kila jaribu, na hatimaye kuketi pamoja naye." 1T 144.

b. "Kristo alikufa ili kufanya iwezekane kwako wewe kukoma kutenda dhambi."

RH 8-28-1894.

c. "Iwapo utasimama chini ya bendera yenye alama za damu ya Mfalme Imanueli, na kufanya kazi yake kwa uaminifu, basi, huna haja kamwe ya kuanguka chini ya majaribu; maana yuko Mungu anayesimama kando yako ambaye ana uwezo wa kukulinda usianguke." OHC 19.

d. "Hakuna udhuru wa kutenda dhambi kwa wote. Tabia takatifu, maisha kama yale ya Kristo, hupatikana kwa kila mtoto wa Mungu anayetubu na kuamini." DA 311.

e. "Maisha yake yanashuhudia kwamba inawezekana kwetu pia kumtii Mungu." DA 24.

f. "Shetani... daima anajaribu kuwadanganya wafuasi wake Kristo kwa maneno yake ya hila kwamba haiwezekani kwao kushinda.... Basi, hebu na asiwepo hata mmoja anayeziangalia kasoro zake kuwa haziwezi kuponywa. Mungu atawapa imani na neema ili wapate kuzishinda." GC 489.

g. "Kristo alikuja ili kutufanya sisi kuwa washirika wa tabia ya uungu, na maisha yake yanatangaza kwamba ubinadamu ukiunganika na uungu, hauwezi kutenda dhambi." MH 180.

h. "Kwa kuishi maisha yale yasiyo na dhambi alishuhudia kwamba kila mwana na binti ya Adamu anaweza kuyapinga majaribu ya yule aliyeileta dhambi katika ulimwengu huu hapo mwanzo." 1SM 226.

i. "Jaribu lenye nguvu kushinda yote halimpi mtu udhuru wo wote wa kutenda dhambi. Haidhuru shinikizo lile linalowekwa juu ya mtu liwe kubwa kiasi gani, dhambi ni tendo letu wenyewe. Haimo katika uwezo wa dunia hii wala wa jehanum kumlazimisha mtu ye yote kutenda dhambi. Nia ya mtu ni lazima ikubali, moyo wake ni lazima ukubali kutii, au tamaa ya mwili wake haiwezi kuishinda akili yake, wala uovu kuishinda haki." ST 4-15-1913.

j. "Hata kwa wazo moja tu hakuweza kuanguka chini ya jaribu lo lote. Hivyo ndivyo inavyoweza kuwa kwetu sisi." DA 123.

12. Je, hilo humaanisha kwamba kila mwelekeo mbaya wa dhambi ulio ndani yetu unaweza kudhibitiwa kabisa?

a. "Iwapo sisi tutakubali, basi, yeye mwenyewe atajifungamanisha kabisa na mawazo na makusudi yetu, ataibadilisha mioyo yetu na akili zetu ili zipate kufanana na mapenzi yake, kiasi kwamba sisi tutakapomtii yeye tutakuwa tunatimiza tu shauku iliyomo mioyoni mwetu."

DA 668.

b. "Kristo alikuja ulimwenguni humu na kuishi sawasawa na sheria ya Mungu [Amri Kumi], ili mwanadamu aweze kupata ushindi kamili juu ya mielekeo yote mibaya ya asili ya moyo wake mpotovu.... Mwanadamu anaweza kusimama akiwa mshindi juu ya nafsi yake mwenyewe, yaani, mshindi juu ya mielekeo yake mibaya." MH 130,131.

c. "Yatupasa kujifunza juu ya Kristo. Yatupasa kujua jinsi yeye alivyo kwa wale aliowakomboa. Yatupasa kutambua ya kwamba kwa njia ya imani katika yeye tunayo haki ya kuwa washirika wa tabia ile ya uungu, na hivyo kuokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa. Hapo ndipo tunapotakaswa na dhambi zote, na kasoro zote za tabia. Hatuna haja ya kubaki na mwelekeo wa dhambi hata mmoja." 7BC 943.

d. "Bila kufanyika hatua ile ya kutubadilisha ambayo yaweza kuja tu kwa njia ya uweza wa Mungu, mielekeo yetu ya dhambi ile ya asili hubaki moyoni katika nguvu zake zote, kutengeneza minyororo mipya, kutuweka katika hali ya utumwa ambayo haiwezi kamwe kuvunjwa kwa nguvu zo zote za kibinadamu." Ev 192.

e. "Mielekeo yetu mibaya inayoutawala moyo ule wa asili ni lazima idhibitiwe kabisa kwa neema yake Kristo, kabla mwanadamu aliyeanguka hajaweza kutayarishwa ili apate kufaa kuingia mbinguni." AA 273.

13. Je, Mkristo yule "asiyebaki na mwelekeo wa dhambi hata mmoja" ameokolewa asiweze kupambana kila siku na mielekeo hiyo mibaya? Je, inakoma kumletea usumbufu?

"Utakaso wa Paulo ulikuwa ni mapambano ya kudumu na nafsi yake. Yeye alisema, 'Ninakufa kila siku.' 1 Kor. 15:31. Nia yake na mapenzi yake kila siku vilipingana na wajibu wake na mapenzi ya Mungu. Badala ya kufuata mwelekeo wake, yeye alifanya mapenzi ya Mungu, haidhuru kama kwa kiasi gani yalikuwa hayapendezi kwake na kwa jinsi gani yalikuwa yakiisulibisha nafsi yake." LS 237.

14. Je, watu wengine hawana mambo mengi ya kuyashinda kuliko wengine, kutokana na hali zile walizorithi kwa wazazi wao pamoja na mazingira yao?

"Wakati baadhi ya watu wanasumbuliwa, wanateswa, na kupata taabu kutokana na tabia zao za kusikitisha, wakilazimika kupigana na maadui wa ndani na uovu unaotokana na hali yao ya asili, wengine hawapati hata nusu ya mambo hayo kupigana nayo." 2T 74,75.

15. Je, Mungu anaziruhusu tofauti hizo kuwako miongoni mwetu? Je, anawatazamia watoto wake wote kuwa na uzoefu unaofanana kabisa wa maisha yao ya Kikristo?

"Waongoze watu kumtazama Yesu kama ndiye pekee tumaini lao na msaidizi wao; mwachie Bwana nafasi ya kufanya kazi yake juu ya moyo wako, kuzungumza na nafsi yako, na kuongoza ufahamu wako. Si muhimu kwako kujua na kuweza kuwaeleza wengine sababu zote za kwa nini kuhusu kile kinachoufanya moyo wako kuwa mpya, au hali ile wanayoweza na wanayopaswa kuifikia ili wasipate kutenda dhambi tena. Wewe hujapewa kazi kama hiyo ya kufanya. Wote hawajaumbwa kwa namna ile ile moja. Kuongoka kwao kote si kwa aina moja...." 1SM 177.

16. Je, wale walio na majaribu yenye nguvu kushinda yote wanaweza pia kupata ushindi kamili juu ya dhambi zao?

a. "Asiwepo hata mmoja wa kusema, Mimi siwezi kuzirekebisha kasoro za tabia yangu. Endapo utafikia msimamo kama huo, basi, utashindwa kuupata ule uzima wa milele. Ugumu u ndani ya nia [mapenzi] yako mwenyewe." COL 331.

b. "Kwa njia ya mpango ule wa ukombozi, Mungu ametoa msaada wa kuweza kuidhibiti kila tabia ya dhambi, na kulipinga kila jaribu, haidhuru liwe na nguvu kiasi gani." 1SM 82.

17. Je, kumepata kuwako na watu siku zile zilizopita ambao, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, wamejifunza kuishi bila [kutenda] dhambi?

a. "Tabia ya utauwa ya nabii huyo (Henoko) inawakilisha hali ya utakatifu ambayo inapaswa kufikiwa na wale watakao'nunuliwa kutoka katika nchi' [Ufu.14:1,4,5] wakati ule wa marejeo yake Kristo." PP 88,89 (Angalia pia RH 7-31-1888).

b. "Hata kwa wazo moja tu Mwokozi wetu hakuweza kuletwa mahali ambapo angeweza kuanguka chini ya uwezo wa jaribu lo lote lile.... Hiyo ndiyo hali ambayo watakutwa nayo wale watakaostahimili katika wakati ule wa taabu." GC 623.

c. "Suala la Danieli liliwekwa mbele yangu. Japokuwa alikuwa mtu wa tabia moja kama sisi, kalamu ya uvuvio humweleza yeye kama mtu aliye na tabia isiyo na waa lo lote. Maisha yake yanatolewa kama kielelezo kizuri kwetu cha vile mwanadamu anavyoweza kuwa hata katika maisha haya tuliyo nayo kama atamfanya Mungu kuwa nguvu zake na kutumia kwa busara nafasi nzuri anazopewa pamoja na haki zilizo katika uwezo wake kuzifikia." 4T 569.

d. "Simama kama Danieli, kiongozi yule wa Serikali, mtu ambaye hakuna jaribu lo lote lililoweza kumchafua." COL 332 (Angalia pia GC 470; OHC 249).

18. Je, siku hizi kuna watu wanaoishi bila kufanya dhambi?

"Katika kila sura ya ujenzi wa tabia yako unapaswa kumpendeza Mungu. Jambo hilo unaweza kufanya; kwa maana Henoko alimpendeza, japokuwa alikuwa akiishi katika kizazi kile kipotovu. Na katika siku hizi zetu wako akina Henoko." COL 332.

19. Je, Wakristo wale wanaoishi karibu sana na Kristo wanatambua jinsi walivyo watakatifu?

a. "Kadiri unavyozidi kumkaribia Yesu, ndivyo kadiri unavyozidi kujiona kuwa una makosa mengi; kwa vile kuona kwako kutakuwa safi zaidi, na mapungufu yako yataonekana kwa tofauti iliyo pana na wazi ukilinganisha na tabia yake kamilifu. Huo ni ushahidi kwamba madanganyo ya Shetani yamepoteza nguvu zake; na ya kwamba mvuto ule unaohuisha wa Roho wa Mungu unakuamsha wewe." SC 64,65.

b. "Kadiri tunavyozidi kuitafakari tabia ya Kristo, na kadiri tunavyouonja uweza wake uokoao, ndivyo kadiri tutakavyoutambua sana udhaifu wetu tulio nao pamoja na upungufu wetu, na kwa juhudi zaidi tutamtazama yeye kama ndiye nguvu zetu na Mkombozi wetu." SC 83.

c. "Kadiri tunavyosogea karibu zaidi kwa Yesu, ndivyo kadiri tunavyozidi kuutambua utakatifu wa tabia yake, na kwa wazi zaidi tunauona ubaya mkuu wa dhambi ulivyo, na hivyo ndivyo hali yetu ya kujisikia kama tunaweza kujitukuza wenyewe itakavyozidi kupungua. Daima moyo utaelekea nje kumtafuta Mungu, yaani, kuwa na ungamo la dhambi linaloendelea, linalotolewa kwa bidii, linalomfanya mtu huyo ahuzunike sana na kuunyenyekeza moyo wake mbele zake [Mungu]. Kwa kila hatua ya kusonga mbele katika maisha yetu haya ya Kikristo, toba yetu itazidi kuwa na kina zaidi na zaidi." AA 561.

d. "Wale wanaouonja utakaso wa Biblia wataonyesha roho ya unyenyekevu. Kama Musa, wameuona utukufu wa kutisha wa Mungu aliye mtakatifu, nao wanajiona ya kuwa hawafai kitu wakijilinganisha na utakatifu na ukamilifu huo uliojaa utukufu wa Mungu yule wa milele."

GC 470.

e. "Wale ambao wanatafuta kweli kweli tabia ile kamilifu ya Kikristo hawatalikaribisha kamwe wazo la kwamba wao hawana dhambi." SL 7.

f. "Kadiri umbali unavyozidi kuongezeka kati yao [wale wanaojisifu] na Mwokozi wao, ndivyo wanavyojiona wenyewe kuwa ni watakatifu zaidi." SL 8.

g. "Hakuna ye yote anayedai kwamba yeye ni mtakatifu ambaye ni mtakatifu kweli. Wale walioandikwa kama watakatifu katika vitabu vile vya mbinguni hawajijui kuwa wako hivyo na hao wanakuwa wa mwisho kujisifu juu ya wema wao wenyewe." ST 2-26-1885, uk. 128.

20. Mtazamo wa Kristo ukoje kwa wale wanaotenda dhambi wakati kwa uaminifu wanajitahidi kuwa Wakristo?

a. "Mara kwa mara tutalazimika kuinama chini na kulia miguuni pake Yesu kwa sababu ya kasoro zetu na makosa yetu; lakini tusikatishwe tamaa. Hata kama tumeshindwa na adui, hatutupwi mbali, hatuachwi wala kukataliwa na Mungu." SC 64.

b. "Yesu anawapenda watoto wake, hata wanapokosa.... Wanapofanya kila wanaloweza, wakimwita Mungu kuwapa msaada wake, uwe na hakika kuwa utumishi huo utakubalika ingawa si mkamilifu. Yesu ni mkamilifu. Haki ya Kristo huwekwa katika akaunti zao, naye atasema, Mvueni nguo hizi zenye uchafu na kumvika mavazi mengine. Yesu anaufidia upungufu wetu usioweza kuepukika." Letter 17a, 1891. Imedondolewa na N. F. Pease katika kitabu chake cha By Faith Alone, uk. 241.

c. "Nia ikiwamo moyoni kumtii Mungu, juhudi zinapofanyika kulifikia kusudi hilo, hapo ndipo Yesu anapoikubali hali hiyo ya moyo pamoja na juhudi yote kama ndiyo huduma bora ya mwanadamu, naye anafidia upungufu uliopo kwa wema wake ule wa uungu." 1SM 382;

ML 250.

d. "Kama mtu yule anayezungumza na Mungu kila siku anapotea katika njia yake, kama kwa dakika moja anageuka asiweze kumtazama Yesu kwa unyofu, si kwa sababu anatenda dhambi kwa

makusudi; maana anapoliona kosa lake, anageuka tena, na kukaza macho yake juu ya Yesu, na ukweli ule wa kwamba amekosa, haumfanyi apendwe kidogo katika moyo wake Mungu." RH 5-12-1896.

e. "Iwapo kwa njia ya majaribu mengi sisi tunaghafilika au kudanganywa na kutenda dhambi, yeye huwa hageuki na kutupa kisogo chake na kutuacha tuangamie. La, la, hivyo sivyo alivyo Mwokozi wetu.... Imani yetu inamtazama yeye, inamshikilia yeye kama ndiye yule mmoja awezaye kuokoa kabisa, na harufu nzuri ya kafara yake itoshayo hukubaliwa na Baba yake." OHC 49.

f. "Mwanadamu, kwa njia ya imani yake katika Yesu Kristo, anapofanya kwa kadiri ya uwezo wake wote, na kuitunza njia ya Bwana kwa utii wake kwa amri zake zile kumi, basi, ukamilifu wake Kristo unahesabiwa juu yake na kuifunika dhambi ya mtu huyo aliyetubu na mtiifu." FE 135.

21. Mwelekeo wa Mkristo anapoanguka katika dhambi uweje?

a. "Kama wewe unashindwa na kudanganywa kiasi cha kuingia dhambini, wakati huo usijisikie kuwa huwezi kuomba... bali umtafute Bwana kwa bidii zaidi." OHC 49.

b. "Tunapovikwa haki ya Kristo, hatutakuwa na hamu ya kutenda dhambi; maana Kristo atakuwa anatenda kazi pamoja nasi. Tunaweza kufanya makosa, lakini tutaichukia dhambi ile iliyosababisha mateso ya Mwana wa Mungu." 1SM 360; MYP 338.

c. "Fanya yote yaliyo katika uwezo wako kujipatia ukamilifu huo; walakini usifikiri kwamba kwa sababu unafanya makosa, basi, wewe umetengwa katika utumishi wake Mungu." MYP 226.

d. "Shetani anapokuambia kwamba Bwana hatakuangalia kwa upendeleo kwa sababu umetenda dhambi, mwambie hivi, 'Yesu alitoa nafsi yake kwa ajili yangu. Alipatwa na kifo cha kikatili sana ili apate kuniwezesha mimi kuyapinga majaribu. Najua kwamba ananipenda mimi, licha ya mapungufu yangu haya. Mimi nakaa katika pendo lake. Yeye ndiye haki yangu na mimi nategemea wema wake." ST 8-13-1902, uk. 2.

22. Je, kalamu ya uvuvio inatuambia habari za watu wengine wanaomcha Mungu ambao nyakati nyingine walishindwa pia na majaribu?

"Kalamu ya uvuvio, ikiwa nyofu katika kazi yake, hutuambia juu ya dhambi zile zilizomshinda Nuhu, Lutu, Musa, Ibrahimu, Daudi, na Sulemani, na ya kwamba hata moyo wa Eliya wenye nguvu ulizama chini ya majaribu wakati wa maonjo yake ya kutisha. Uasi wa Yona na ibada ya sanamu ya Israeli vimeandikwa kwa uaminifu. Kumkana Kristo kwa Petro, ugomvi mkali kati ya Paulo na Barnaba, kushindwa pamoja na udhaifu wa manabii na mitume, vyote vimewekwa wazi na Roho Mtakatifu, ambaye analiinua pazia kutoka katika moyo wa kibinadamu. Hapa mbele yetu yapo maisha ya waumini, pamoja na makosa yao yote na upumbavu wao, ambavyo vimekusudiwa kuwa fundisho kwa vizazi vyote vinavyofuata baada yao. Endapo wasingekuwa na kasoro zo zote katika tabia zao, basi, wangekuwa si binadamu, na asili zetu hizi za dhambi zingetukatisha tamaa ya kuweza kukifikia kiwango kile cha juu cha tabia bora. Lakini tukiwa tunaona mahali pale

walipojitahidi na kushindwa, mahali pale walipojipa moyo na kushinda kwa neema yake Mungu, basi, sisi tunatiwa moyo na kuvutwa kusonga mbele kuvipita vipingamizi ambavyo asili yetu ya dhambi imeviweka njiani mwetu."  4T 12.

23. Pana tofauti gani kati ya Mkristo ambaye wakati mwingine anaingia katika dhambi na yule anayeipenda dunia hii ambaye anatenda dhambi zizo hizo?

a. "Wakati wafuasi wake Kristo wanapotenda dhambi, wanakuwa hawajajisalimisha wenyewe ili wapate kutawaliwa na uovu huo."  5T 474.

b. "Kuingia katika dhambi pasipo kujua ----- yaani, pasipokuwa na nia ya kutenda dhambi, lakini kutenda dhambi kwa kukosa kukesha na maombi, bila kuyatambua majaribu ya Shetani, na kwa njia hiyo kuanguka katika mtego wake ----- ni tofauti kabisa na mtu yule anayefanya mipango na kwa makusudi kabisa anajiingiza mwenyewe katika majaribu hayo na kufanya mpango wa njia ya kuitenda dhambi hiyo."  OHC 177.

c. "Tabia inadhihirika si kwa matendo mema wala kwa matendo mabaya ya mara kwa mara, bali kwa mwelekeo wa maneno na matendo unaotokana na mazoea ya mtu huyo."  SC 57,58.

24. Je, ipo tofauti yo yote kati ya yule anayejiita Mkristo ambaye ni mtumwa wa tabia moja mbaya, na yule anayeipenda dunia hii?

a. "Tamaa ya dhambi moja ikitunzwa moyoni, hatimaye itaibatilisha [itaiondoa] nguvu yote ya injili."  5T 53.

b. "Dhambi moja ya siri ikitendwa, itaonyesha katika tabia kile ambacho ubao ule uliotobolewa na funza utakavyofanya kwa meli ----- yaani, maafa na maangamizi kamili."

4T 90.

c. "Kasoro moja katika tabia, ikikuzwa badala ya kuishinda, humfanya mtu huyo asiwe mkamilifu, na kumfungia mlango wa Mji ule Mtakatifu."  MYP 144.

25. Ni mbaraka gani mkuu wa mbinguni utakaomwagwa hivi karibuni juu ya wale waliopata ushindi juu ya kila dhambi inayowazinga, yaani, wale ambao hawatawaliwi na uovu?

a. Soma maelezo ya kipengele cha pili chini ya swali la 20 la Sura ya 11 - MVUA YA MASIKA.

b. "Wale ambao wangeona afadhali kufa kuliko kutenda tendo lo lote baya, hao ndio peke yao watakaoonekana kuwa waaminifu."  5T 53 (Angalia pia  SC 38).

26. Kusudi la Mvua ya Masika ni nini?

a. "Mvua ya Masika, ikinyesha karibu na mwisho wa majira, huikomaza nafaka, na kuitayarisha kwa kuvunwa na mundu.  Bwana anatumia utendaji huo wa kawaida kuwakilisha kazi ya Roho

Mtakatifu.... Kukomaa kwa nafaka huwakilisha ukamilishaji wa kazi ya neema ya Mungu moyoni mwetu. Kwa uweza wa Roho Mtakatifu sura ya Mungu ya tabia yake inapaswa kukamilishwa katika tabia yetu. Tunapaswa kubadilishwa kabisa ili tupate kufanana na Kristo [katika tabia yetu]. Mvua ya Masika, inapoyakomaza mavuno ya nchi, huiwakilisha neema ile ya kiroho inayoliandaa kanisa kwa ajili ya marejeo ya Mwana wa Adamu." TM 506.

b. "Tunapomtafuta Mungu kwa ajili ya Roho Mtakatifu, atafanya kazi yake ndani yetu kutupatia roho ile ya upole na unyenyekevu, na kutufanya sisi tupate kutambua haja yetu ya kumtegemea Mungu kwa kutupa sisi mvua ile ya masika itukamilishayo." TM 509.

27. Chini ya uwezo ule ukamilishao wa mvua ile ya masika, ni hali gani ya kiroho watakayoifikia watu wa Mungu ----- yaani, wale 144,000 ----- wakati mlango wa rehema utakapokuwa unafungwa? Ufu.14:1,5.

a. "Hata kwa wazo moja tu Mwokozi wetu hakuweza kuanguka chini ya nguvu ya majaribu.... Hiyo ndiyo hali ambayo watakuwa nayo wale watakaosimama katika wakati ule wa taabu." GC 623 (Angalia pia 5T 475).

b. "Je, tunatafuta utimilifu wake, tukisonga mbele daima kwenye kiwango kile kilichowekwa mbele yetu ----- yaani, ukamilifu wa tabia yetu? Watu wa Mungu watakapokifikia kiwango hicho, watatiwa muhuri juu ya vipaji vya nyuso zao. Wakiwa wamejazwa na Roho, watatimilika ndani ya Kristo, na malaika yule anayetia alama [muhuri] atatangaza, akisema, 'Imekwisha.' " OHC 150.

28. Je, ni lazima kiwepo kipindi kirefu cha miaka mingi ili kuweza kuikamilisha tabia hii ya Kikristo?

a. "Tunapokaribia mwisho wa historia ya dunia hii, ama tunaharakisha kuendelea kukua katika Ukristo wetu, ama tunaharakisha kurudi nyuma kwenda kwa [tabia ile ya] walimwengu." RH 12-13-1892, uk. 770.

b. "Yale tuliyoendelea kujifunza kwa miaka mingi, [waongofu wapya] watalazimika kujifunza katika miezi michache tu." EW 67.

29. Kwa nini ni muhimu kabisa kwa wale 144,000 kutotenda dhambi hata kwa wazo moja tu baada ya kufungwa kwa mlango wa rehema?

"Wamepita katika wakati wa taabu ambao mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa;... nao wamesimama bila kuwa na Mwombezi katika kipindi chote cha mwisho cha kumwagwa kwa hukumu zake Mungu." GC 649.

30. Je, bado watasikia vishawishi vya dhambi ndani yao na kujaribiwa baada ya mlango wa rehema kufungwa?

a. "Kadiri Shetani anavyozidi kutawala, tutapaswa kuidhibiti nafsi yetu, yaani, kuzishinda dhambi zile zinazotuzinga; kadiri uhai wetu utakavyoendelea, hapatakuwa na mahali po pote pa kusimama, yaani, hapatakuwa na kiwango cho chote tutakachoweza kukifikia na kusema,

Nimekwisha kufika kabisa. Utakaso ni matokeo ya utii unaoendelea katika maisha yote ya mtu." AA 560,561 (Angalia pia 1T 341).

b. "Kwa wale waliojitahidi sana kwa njia ya imani kukipata kile kiitwacho mwili mtakatifu, ningewaambia hivi, Hamwezi kuupata [mwili kama] huo. Hakuna hata mmoja wenu mpaka sasa aliye na mwili mtakatifu. Hakuna mwanadamu ye yote duniani aliye na mwili mtakatifu.... Twaweza kuwa na ukamilifu wa Kikristo wa nafsi zetu. Kwa njia ya kafara ile iliyotolewa kwa ajili yetu, dhambi zinaweza kusamehewa kabisa.... Mungu na ashukuriwe ya kwamba sisi hatushughuliki na mambo yale yasiyowezekana. Twaweza kudai utakaso." 2SM 32.

c. "Tunaweza kuumba mioyoni mwetu ulimwengu usiokuwa ulimwengu halisi [wa kufikirika tu] na kupiga picha ya kanisa kamilifu, ambalo ndani yake majaribu ya Shetani hayawachochei watu kutenda dhambi; lakini ukamilifu huo umo tu katika mawazo yetu [si katika hali halisi ya mambo yalivyo]." RH 8-8-1893.

31. Majaribu yote yatakoma lini?

a. "Wanadamu watakapopokea mwili mtakatifu, hawatabaki hapa duniani, bali watachukuliwa kwenda mbinguni. Ingawa dhambi inasemehewa katika maisha haya tuliyo nayo, athari zake hazijaondolewa kabisa kwa sasa. Ni katika wakati ule wa kuja kwake, ndipo Kristo atakapo'ubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu' [Wafilipi 3:21; 1 Kor. 15:50-54]" 2SM 33.

b. "Hatuwezi kusema Mimi sina dhambi mpaka hapo mwili wetu huu wa unyonge [mwovu] utakapobadilishwa na kufanana na mwili wake wa utukufu." ST 3-23-1888.

c. "Nikasikia sauti za ushindi kutoka kwa malaika na kwa wale watakatifu zilizovuma kama ala za muziki elfu kumi, kwa sababu wasingesumbuliwa na kujaribiwa tena na Shetani na kwa sababu wakazi wa dunia zile nyingine walikuwa wameokolewa kutokana na kuwako kwake [Shetani] pamoja na majaribu yake." SR 416.

d. "Kuna mielekeo ya dhambi tuliyorithi na ile tuliyojizoeza wenyewe ambayo ni lazima tuishinde. Uchu mbaya wa chakula pamoja na tamaa mbaya za mwili ni lazima vidhibitiwe na Roho Mtakatifu. Hakuna mwisho wa mapambano hayo upande wetu huu wa umilele ule."

CT 20.

SURA YA 18

# AMRI YA KIFO

1. Kusudi la mwisho la Shetani kwa watu wa Mungu ni nini?

a. "Ulimwengu mzima utachochewa kuwa na uadui na Waadventista Wasabato, kwa sababu hawatakubali kuusujudu upapa, kwa kuiheshimu Jumapili, siku iliyowekwa na mamlaka hiyo ya Mpinga Kristo. Ni kusudi la Shetani kuwafanya wote wafutiliwe mbali [wauawe] na uso wa dunia hii, ili ukuu wake juu ya dunia hii usiweze kupingwa." RH 8-22-1893.

b. "Kanisa la Masalio [Waadventista Wasabato] litaingizwa katika maonjo makubwa na dhiki kubwa. Wale wanaozishika amri [kumi] za Mungu na imani ya Yesu watakabiliana na adhabu itakayotolewa kwao na joka na majeshi yake. Shetani anawahesabu watu wote wa dunia hii kama raia zake, ameyadhibiti makanisa yaliyoasi; lakini basi, hapa pana kundi dogo linalopinga ukuu wake. Endapo angeweza kuwafutilia mbali na uso wa dunia hii, basi, ushindi wake ungekuwa umekamilika. Kama vile alivyoyachochea mataifa ya kishenzi [kipagani] ili kuwaangamiza Waisraeli, ndivyo katika siku za usoni zilizo karibu sana atakavyozichochea mamlaka za uovu duniani ili kuwaangamiza watu wa Mungu." 9T 231.

2. Kwa jinsi gani Shetani atalikamilisha kusudi lake hilo?

"Asema yule Mlaghai Mkuu [Shetani]: ... Shughuli yetu kuu ni kulinyamazisha dhehebu hili la Wasabato. Yatupasa kuchochea hasira kali dhidi yao. Kwa upande wetu tutapata msaada kutoka kwa Wakuu na Wenye Hekima wa dunia hii, na kuwashawishi Wenye Mamlaka kutekeleza makusudi yetu. Hapo ndipo sabato yangu [Jumapili] niliyoiweka mimi [kwa kulitumia Kanisa la Roma] itakapotungiwa sheria kali mno, za kuwakandamiza watu. Wale watakaozipuuzia watafukuzwa kwenda nje ya miji na vijiji, na kuteswa kwa njaa na umaskini. Tutakapokuwa tumepata mamlaka hayo, ndipo tutakapoonyesha kile tunachoweza kufanya kwa wale ambao hawatayumba katika utii wao kwa Mungu. Tuliliongoza Kanisa la Roma [katika Zama zile za Giza] kuwaadhibu kwa kuwafunga, kuwatesa, na kuwaua wale waliokataa kutii amri zake [Kanisa la Roma]; na kwa vile sasa tunayaunganisha makanisa ya Kiprotestanti na ulimwengu na mkono huu wa kulia wa uwezo wetu [Kanisa la Roma], basi, hatimaye tutakuwa na sheria ya kuwaua wote ambao hawatatii mamlaka yetu. Kifo kitakapowekwa kuwa ndiyo adhabu ya kuivunja sabato yetu [Jumapili], ndipo wengi walio katika safu za hao wazishikao amri [kumi za Mungu] watakapokuja upande wetu." TM 472,473.

3. Je, mwanzoni adhabu ya kifo itakuwa ni kipengele kimojawapo cha kuivunja ile Amri ya Jumapili kwa ulimwengu mzima?

"Mamlaka za ulimwengu, zikiungana kupigana vita juu ya Amri [Kumi] za Mungu, zitatoa amri kwamba wote 'wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa' (Ufunuo 13:16) watafuata desturi za kanisa kwa lazima kwa kuitunza sabato hiyo ya uongo [Jumapili]. Wale wote watakaokataa kutii wataadhibiwa kisheria, na mwishowe itatangazwa kwamba wanastahili kuuawa." GC 604.

4. Kuhusiana na kufungwa kwa mlango wa rehema, ni wakati gani hasa ambapo adhabu ya kifo itakuwa ndiyo adhabu ya kuivunja Amri ile ya Jumapili?

a. "Matukio ya ajabu [ya kushangaza] yataonekana duniani hivi karibuni. Mwisho wa mambo yote umekaribia. Wakati wa taabu karibu utawajia watu wa Mungu. Wakati huo [wa taabu] ndipo amri itatolewa ikiwakataza wale wanaoishika Sabato ya Bwana wasinunue wala wasiuze, na kuwatiishia ya kwamba wataadhibiwa, na hata kuuawa, kama hawataitunza siku ya kwanza ya juma [Jumapili] kama sabato. 'Wakati huo Mikaeli [Kristo] atasimama, Jemadari Mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo.' " RH 11-19-1908, uk.5.

b. " 'Wakati huo Mikaeli atasimama, Jemadari Mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo; na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile [cha uzima].' Wakati huo wa taabu utakapokuja, kila kesi itakuwa imekatwa [kule mbinguni]; hakutakuwa na muda tena wa majaribio [kupimwa], hakutakuwa na rehema tena kwa wale wasiotubu. Muhuri wa Mungu aliye hai utakuwa juu ya watu wake. Kundi hilo dogo la Waliosalia [Wamasalio], lisilokuwa na uwezo wo wote wa kujihami lenyewe katika pambano hilo la kufisha dhidi ya mamlaka za ulimwengu huu ambazo zitakuwa zimekusanywa pamoja na jeshi lile la Joka [malaika zake Shetani], litamfanya Mungu kuwa ngome yake. Amri itakuwa imepitishwa na mamlaka ile ya dunia ya juu sana [Marekani] kwamba watalazimika kumsujudu Mnyama na kupokea Alama yake chini ya tishio [shinikizo] la mateso na kuuawa. Basi, Mungu na awasaidie watu wake, maana wanaweza kufanya nini katika pambano hilo kali bila msaada wake.' " 5T 212,213.

5. Watakapotishiwa kifungo na kuuawa, je! Waadventista wengine wataiacha imani yao?

"Wakati hauko mbali ambapo jaribio hilo litakuja kwa kila mtu. Alama ya Mnyama italazimishwa juu yetu. Wale ambao hatua kwa hatua wametii matakwa ya ulimwengu huu hawataona kuwa ni jambo gumu kuzitii mamlaka zile zitakazokuwapo kuliko kujiweka wenyewe katika hali ile watakayodhihakiwa, kutukanwa, kutishiwa kufungwa na kuuawa. Pambano ni kati ya Amri [Kumi] za Mungu na amri za wanadamu. Katika wakati huo dhahabu itatenganishwa na takataka (mavi ya dhahabu) ndani ya kanisa." 5T 81.

6. Je, kutakuwa na mauaji ya mashahidi wa Yesu?

a. "Kama vile alivyoyaongoza mataifa yale ya kishenzi [kipagani] kuwaangamiza Waisraeli, ndivyo atakavyozichochea mamlaka za uovu za ulimwengu kuwaangamiza watu wa Mungu. Watu watatakiwa kutoa utii wao kwa amri za kibinadamu na kuivunja Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Wale walio waaminifu kwa Mungu wao watatishwa, watashutumiwa na kupigwa marufuku

[wasiweze kununua wala kuuza]. Wata"salitiwa na wazazi w[ao], nao watawafisha [watawaua] baadhi y[ao]." PK 587,588.

b. "Mbele yetu kuna matarajio ya pambano linaloendelea, kwa hasara ya kufungwa, kupoteza mali zetu na hata uhai wetu , katika kuitetea Sheria ya Mungu [Amri Kumi]." 5T 712.

7. Katika saa hii ya uasi mkuu mno, je! kutakuwa na Waadventista katika kila nchi watakaokuwa waaminifu?

"Katika Afrika ya kishenzi (kipagani), katika nchi za Kikatoliki za Ulaya na za Amerika Kusini, katika nchi ya China, katika nchi ya India, katika visiwa vilivyo baharini, na katika kona zote za giza za dunia. Mungu anayo akiba ya mianga ya wateule wake watakaong'aa katikati ya giza, wakiufunulia wazi ulimwengu ulioasi uwezo ule unaobadilisha tabia wa utii kwa Sheria yake. Hata sasa wanaonekana katika kila taifa, miongoni mwa kila lugha na watu; na katika saa ile ya uasi mkuu mno, juhudi nyingi mno za Shetani zitakapotumika kuwafanya 'wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa,' kupokea kwa tishio la adhabu ya kuuawa, alama ile ya utii kwa siku ya uongo ya mapumziko [Jumapili], hao walio waaminifu, yaani, 'wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na ila, ndipo watakapong'aa 'kama mianga katika ulimwengu.' " PK 189.

8. Mlango wa rehema utakapofungwa na mapigo kuanza kuanguka chini, ni nani watakaolaumiwa kuwa ndio chanzo cha hukumu hizo?

"Mapigo hayo yaliwafanya waovu wawakasirikie sana wenye haki; walidhani kwamba ni sisi tuliowaletea hukumu hizo za Mungu juu yao, na kwamba kama wengeweza kutufutilia mbali juu ya uso wa dunia hii, basi, mapigo yale yangezuiwa." EW 36.

9. Matokeo ya mawazo kama hayo yatakuwa nini?

a. "Amri ikatolewa ili kuwaua watakatifu, ambayo iliwafanya kulia mchana na usiku ili wapate kuokolewa." EW 36,37.

b. "Itasisitizwa kwamba wale wachache wanaosimama kupinga siku iliyowekwa na kanisa na sheria ya nchi, wasivumiliwe; ya kwamba ni heri kwao kuteseka kuliko mataifa mazima kutupwa katika machafuko ya uasi. Hoja iyo hiyo miaka 1800 iliyopita ililetwa dhidi ya Kristo na 'wakuu wa watu.' Hoja hiyo itaonekana kuwa ni ya mkataa na hatimaye itatolewa dhidi ya wale wanaoitakasa Sabato ile ya amri ya nne, wakiwashutumu kuwa wanastahili adhabu kali sana, na kuwapa watu uhuru wa kuwaua baada ya kupita muda fulani uliowekwa." GC 615.

c. "Nikaona viongozi wakuu wa nchi wakishauriana pamoja, na Shetani na malaika zake walishughulika kuwazunguka. Nikaona maandiko, nakala zake zitakawanywa katika sehemu mbalimbali za nchi, zikitoa amri kwamba watakatifu wasipoiacha imani yao ya ajabu, yaani, kuiacha Sabato, na kuitunza siku ya kwanza ya juma, basi, watu watakuwa huru kuwaua baada ya muda fulani uliowekwa kupita." EW 282,283; SR 406.

d. "Yesu atakapoondoka patakatifu pa patakatifu, Roho wake anayezuia ataondolewa kutoka kwa watawala na watu. Wataachwa kutawaliwa na malaika wale waovu. Hapo ndipo sheria hizo zitatungwa kwa ushauri na uongozi wa Shetani, kiasi kwamba kama wakati usingekuwa mfupi sana, hakuna mwenye mwili ambaye angeweza kuokolewa." 1T 204.

e. "Ghadhabu ya mwanadamu itaamshwa juu ya wale hasa wanaoitakasa Sabato ya amri ya nne; na mwishowe amri ya ulimwengu mzima itawashutumu hao kuwa wanastahili kuuawa." PK 512.

10. Ni wakati gani wa taabu ya kutisha kwa wenye haki utafuatia baada ya kutoa sheria ya ulimwengu mzima ya kuwaua?

a. "Amri ikatolewa kuwaua watakatifu, ambayo iliwafanya kulia mchana na usiku ili wapate kuokolewa. Huo ulikuwa ndio wakati wa taabu ya Yakobo." EW 36,37.

b. Angalia madondoo mengine chini ya swali la 4 na 5, Sura ya 19 mbele.

11. Je, itakuwako tarehe maalum iliyowekwa na amri hiyo ambayo baada ya hiyo Waadventista Wasabato wataweza kuuawa?

a. "Ingawa amri ile ya kawaida itakuwa imeweka muda maalum watakapouawa wale wanaozishika amri [kumi za Mungu], adui zao katika matukio mengine wataitangulia amri hiyo, na kabla ya wakati ule uliotajwa watajaribu kuwaua." GC 631.

b. "Wakati uliowekwa katika amri hiyo utakapokaribia, watu watakula njama kuking'oa kabisa kikundi hicho [dhehebu] kinachochukiwa." GC 635.

12. Ni amri gani ya zamani ambayo ilikuwa na tarehe iliyowekwa kwa ajili ya kuwaangamiza watu wa Mungu?

"Amri ambayo itatolewa dhidi ya watu wa Mungu itafanana kabisa na ile iliyotolewa na Ahasuero dhidi ya Wayahudi katika wakati ule wa Esta." 5T 450; PK 605 (Angalia

Esta 3:12,13).

13. Ni pigo gani litakuja baada ya kutolewa amri hiyo ya kifo ya ulimwengu mzima?

"Na 'mito na chemchemi za maji; zikawa damu.' Japokuwa mateso hayo ni ya kutisha kama vile yalivyo hasa, haki ya Mungu itasimama ikiwa imethibitishwa kabisa. Malaika wa Mungu atatangaza, akisema, 'Wewe u mwenye haki,... kwa kuwa umehukumu hivi; kwa kuwa walimwaga damu ya watakatifu na ya manabii, nawe umewapa damu wainywe; nao wamestahili.' Kule

kuwahukumu watu wa Mungu kuuawa wamepata hatia ya hakika ya damu yao kana kwamba walikuwa wameimwaga kwa mikono yao." GC 628.

14. Watakapokuwa wanangojea kuuawa, watu wa Mungu hao watakuwa wapi?

a. "Amri itakapotolewa na watawala mbalimbali wa ulimwengu wote wa Kikristo dhidi ya wale wazishikao amri [kumi za Mungu] na kuondoa kwao ulinzi wa serikali zao, na kuwaacha mikononi mwa wale wanaotaka kuwaangamiza, ndipo watu wa Mungu watapokimbia kutoka mijini na vijijini na kushirikiana pamoja katika vikundi vikundi, wakikaa katika mahali pa ukiwa na upweke mno. Wengi watapata kimbilio lao katika ngome imara za milima.... Lakini wengi kutoka katika mataifa yote, na wa tabaka zote, wa vyeo vya juu na wa vyeo vya chini, matajiri kwa maskini, weusi kwa weupe, watatupwa katika kifungo kisichokuwa cha haki kabisa na cha kikatili mno. Wapenzi wa Mungu watapitisha siku zao za kuchosha humo, wakiwa wamefungwa kwa minyororo, wakiwa wamefungiwa magerezani kwa komeo, wakiwa wamehukumiwa kuuawa, wengine kwa dhahiri wakiwa wameachwa kufa kwa njaa katika magereza yenye giza na yanayochukuza yaliyo chini ya ardhi." GC 626.

b. "Watu wa Mungu ----- wengine wakiwa katika seli za magereza, wengine wakiwa wamejificha mahali pa salama pa upweke misituni na milimani ----- bado watakuwa wakilia wakiomba ulinzi wa Mungu, wakati kila upande kombania za watu wenye silaha, wakichochewa na majeshi yale ya malaika waovu, watakuwa wanajiandaa kwa kazi yao ya mauaji." GC 635.

c. "Wakati huo watu wa Mungu wote hawatakuwa mahali pamoja. Watakuwa katika vikundi mbalimbali, na katika sehemu zote za dunia; nao watahukumiwa kila mmoja peke yake, sio katika makundi. Kila mmoja peke yake sharti akabiliane na jaribio [mtihani] hilo." 4BC 1143.

15. Waovu watajaribu kuwafanyia nini wenye haki waliobaki mijini na vijijini?

a. "Watakatifu walipoiacha miji na vijiji, walifukuzwa na waovu, ambao walitaka kuwaua. Walakini mapanga yaliyoinuliwa juu yao ili kuwaua watu hao wa Mungu yalikatika na kuanguka chini yakiwa hayana nguvu yo yote kama vile mabua makavu. Malaika wa Mungu waliwalinda watakatifu hao." EW 284,285.

b. "Ingawa amri ya jumla itakuwa imeweka muda maalum ambapo wale wazishikao amri [kumi za Mungu] wataweza kuuawa, katika matukio fulani fulani adui zao wataitangulia amri hiyo, na kabla ya muda uliowekwa watajaribu kuwaua. Lakini hakuna ye yote awezaye kuwapita walinzi wale hodari [malaika watakatifu] ambao wamefanya kituo kumzunguka kila mtu [aliye mtakatifu]. Wengine katika kukimbia kwao kutoka mijini na vijijini watashambuliwa; lakini mapanga yale yaliyoinuliwa juu yao yatakatika na kuanguka chini yakiwa hayana nguvu yo yote kama vile majani makavu. Wengine watalindwa na malaika katika umbile la wanadamu wanaopigana vita [wanajeshi]." GC 631.

c. "Wakati ule wa taabu sisi sote tulikimbia kutoka mijini na vijijini, lakini tuliandamwa na waovu, ambao waliingia katika nyumba za watakatifu wakiwa na upanga. Waliinua juu upanga wao ili kutuua, lakini ulikatika na kuanguka chini ukiwa hauna nguvu yo yote kama vile bua kavu." EW 34.

16. Siku ya mwisho iliyowekwa katika amri ile ya kuwaua itakapokaribia, baadhi ya watakatifu wataogopa kitu gani?

a. "Baadhi ya watakatifu wakaanza kuogopa kwamba Mungu hatimaye alikuwa amewaacha kuangamia mikononi mwa waovu." EW 283.

b. "Walakini kwa macho ya kibinadamu itaonekana kana kwamba watautia muhuri ushuhuda wao kwa damu yao, kama walivyofanya wafia dini kabla yao. Wao wenyewe wataanza kuogopa kwamba Bwana amewaacha kuuawa kwa mkono wa maadui zao. Ni wakati wa maumivu makali sana ya kutisha. Usiku na mchana watamlilia Mungu ili awaokoe. Waovu watashangilia, na katika kelele zao za kejeli itasikika sauti isemayo, 'Imani yenu iko wapi, basi? Mbona Mungu hawaokoi mikononi mwetu kama ninyi kweli ni watu wa Mungu?' Lakini wale wanaomngojea watakumbuka jinsi Yesu alivyokuwa anakufa juu ya msalaba ule wa Kalvari, na wakuu wa makuhami na watawala kwa dhihaka zao, walisema, 'aliokoa wengine, hawezi kujiokoa mwenyewe. [Kama] Yeye ni Mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini.' Kama Yakobo, wote watapigana mieleka na Mungu. Nyuso zao zitaonyesha pambano lililo ndani yao. Kupauka uso kutaonekana juu ya kila uso. Walakini, hawataacha kutoa dua zao za dhati." GC 630.

c. "Jicho la Mungu likiangalia katika vizazi vyote kufikia siku zetu, lilikazwa juu ya hatari ile kubwa ambayo watu wake wangekabiliana nayo, wakati mamlaka za dunia zitakapojipanga dhidi yao. Kama mkimbizi aliyekamatwa mateka, watakuwa katika hali ya hofu ya kufa kwa njaa au kwa kuuawa kikatili." GC 634.

17. Ni viumbe gani vya aina tatu vinatakavyowazunguka watakatifu kwa wakati huo?

"Lakini kama macho yao yangefumbuliwa, wangejiona wenyewe kuwa wamezungukwa na malaika wa Mungu. Nyuma yao likija kundi la waovu, na nyuma ya hilo wakija malaika wengi waovu, wakiwaharakisha waovu kuwaua watakatifu. Lakini kabla hawajawakabili watu wa Mungu, waovu hao hawana budi kwanza kulipenya kundi hilo la malaika watakatifu, wenye nguvu nyingi. Jambo hilo litakuwa haliwezekani kabisa." EW 283 (Angalia pia 9T 17).

18. Waovu watafanya mpango gani wa kuwaangamiza watu wa Mungu?

"Ulinzi unaotokana na sheria za kibinadamu utakapoondolewa kwa wale wanaoiheshimu sheria ya Mungu [Amri Kumi], patakuwa na tapo [kundi] la kuwaangamiza hao [watu wa Mungu] litakalotokea katika nchi mbalimbali kwa wakati ule ule mmoja. Muda uliowekwa katika amri utakapokaribia, watu watakula njama kuking'oa kabisa kikundi hicho kinachochukiwa. Watadhamiria kuwapa kipigo cha mwaka kwa usiku mmoja, ambacho kitainyamazisha kabisa sauti yao inayowapinga na kuwakaripia." GC 635.

19. Kwa jinsi gani Mungu atawaokoa watoto wake waaminifu?

a. "Kwa kelele za ushindi, kuzomea, na kulaani, makundi ya waovu yatakuwa tayari kuwarukia mateka wao, wakati, tazama, utusitusi mzito, mnene kuliko ule wa usiku, unaanguka juu ya uso wa dunia.... Ni usiku wa manane Mungu anapoudhihirisha uweza wake wa kuwaokoa watu wake.... Miji ya dunia yenye kiburi kushinda yote itaanguka chini. Majumba ya kifalme, ambayo wakuu wa ulimwengu huu wametumia mali yao nyingi sana kuyajenga ili kujitukuza wenyewe, yatabomoka na kuwa magofu mbele ya macho yao. Kuta za magereza zitapasuka vipande vipande, na watu wa Mungu waliofungwa humo kwa ajili ya imani yao, watawekwa huru." GC 635-637.

b. "Naliona ya kwamba kwa njia ya ajabu Mungu atawalinda watu wake katika kipindi kile chote cha wakati wa taabu. Kama vile Kristo alivyougua rohoni mwake kwa uchungu mkubwa kule bustanini, nao watalia kwa dhati na kupata maumivu makali mchana na usiku ili wapate kuokolewa. Amri itatolewa kwamba wasiiheshimu Sabato ya amri ya nne, [bali] waiheshimu siku ya kwanza, la sivyo, watapoteza maisha yao; lakini wao hawatakubali kuikanyaga chini ya miguu yao Sabato ya Bwana, wala kuiheshimu siku iliyowekwa na upapa. Jeshi la Shetani na waovu watawazingira, na kushangilia juu yao, kwa sababu hapatakuwa na njia kwao ya kuweza kuokolewa. Lakini katikati ya makelele na vifijo vyao hivyo pamoja na kushangilia kwao, ngurumo baada ya ngurumo ya radi itasikika kwa sauti kubwa mno. Mbingu zitakuwa nyeusi, na zitaangazwa tu kwa nuru inayowaka yenye utukufu wa kuogofya mno kutoka mbinguni, hapo Mungu atakaposema kwa sauti yake kutoka katika makazi yake matakatifu [Ufu.16:17-19].

"Misingi ya nchi itatikisika kwa kishindo cha kuogofya mno. Bahari itachemka kama chungu, na nchi yote itasukwasukwa huku na huko kwa namna ya kutisha sana. Kutekwa kwa wenye haki kutageuka, na kwa sauti tamu na minong'ono ya polepole wataambiana wao kwa wao, wakisema, 'Tumeokombolewa. Hiyo ni sauti ya Mungu wetu' " 1T 353,354.

c. "Saa ya giza kabisa ya pambano la Kanisa dhidi ya mamlaka zile za uovu, ni ile inayotangulia muda mfupi tu kabla ya siku ya ukombozi wake wa mwisho." PK 725.

20. Ni watakatifu wangapi watakaouawa chini ya amri hiyo ya kuwaua [itakayotolewa baada ya kufungwa kwa mlango wa rehema]?

a. "Mungu asingewaruhusu waovu kuwaangamiza wale waliokuwa wanatarajia kunyakuliwa kwenda mbinguni, na ambao wasingekubali kupiga magoti yao kwa amri ile ya Mnyama wala kupokea Alama yake. Naliona ya kwamba kama waovu wangeruhusiwa kuwaua watakatifu, basi, Shetani na jeshi lake lote ovu, pamoja na wale wote wanaomchukia Mungu, wangefurahishwa sana. Lo! ingekuwa shangwe ilioje kwa mfalme Shetani kuwa na uwezo katika pambano la mwisho juu ya wale waliokuwa wamemngojea kwa muda mrefu ili kumwona kwa macho yao yule waliyempenda. Wale waliolidhihaki wazo la watakatifu kwenda juu watashuhudia jinsi Mungu anavyowajali watu wake, na kuuona ukombozi wao wa utukufu." EW 284.

b. "Iwapo damu ya Mashahidi wa Kristo Waaminifu ingemwagwa kwa wakati kama huo, basi, isingekuwa mbegu, kama ile ya wafia dini, iliyopandwa ili kuleta mavuno mengi kwa Mungu.... Utakuwa na utukufu ukombozi wa wale waliongojea kuja kwake kwa uvumilivu, ambao majina yao yameandikwa katika kitabu kile cha uzima." GC 634.

21. Ni tukio gani litakalokuwa la kilele cha historia hiyo yote?

"Mara hiyo wingu dogo jeusi likaonekana mashariki, takriban nusu ya kiganja cha mkono wa mtu.... Mfalme wa wafalme atashuka juu ya wingu hilo [malaika wote wa mbinguni], akizungukwa na moto unaowaka pande zote." GC 640,641.

## SURA YA 19

## WAKATI WA TAABU YA YAKOBO

1. Bwana alikielezaje kipindi kile cha kutisha cha uchungu mkali wa moyo ambacho mfalme yule wa Babeli angekileta juu ya Yuda? Yeremia 30:5-7.

2. Muda mfupi tu baada ya malaika yule wa rehema kuruka na kwenda zake [mbinguni], Shetani na majeshi yake atawaletea nini Israeli wa leo?

"Kama vile kukaribia kwa majeshi ya Kirumi kulivyokuwa ishara kwa wanafunzi wake juu ya maangamizi ya Yerusalemu yaliyokuwa karibu sana kutokea, ndivyo uasi huo [wa kuweka Amri ya Jumapili] unavyoweza kuwa ishara kwetu kwamba uvumilivu wake Mungu umefikia kipeo chake,

kwamba kikombe cha uovu wa Taifa letu [Marekani] kimejaa, na ya kwamba yule malaika wa rehema yu karibu sana kuruka na kwenda zake, asiweze kurudi tena. Hapo ndipo watu wa Mungu watakapotupwa katika mandhari zile za mateso na dhiki ambazo manabii wamezielezea kuwa ndio wakati wa taabu ya Yakobo." 5T 451.

3. Ni juu ya jambo gani Shetani atauchochea ulimwengu wote dhidi ya Waadventista Wasabato?

"Kama vile Sabato ilivyo jambo maalum la mabishano katika ulimwengu wote wa Kikristo, na wale wenye mamlaka ya dini na Serikali wameungana pamoja ili kulazimisha utunzaji wa Jumapili, basi, kule kuendelea kukataa kwa kikundi kidogo kutii matakwa yanayopendwa na watu wengi, kutawafanya wawe lengo la kuchukiwa mno na ulimwengu mzima." GC 615.

4. Ni kitu gani kitakuwa chanzo cha moja kwa moja cha kipindi hiki cha dhiki ya kutisha?

a. "Naliona ya kwamba malaika wale wanne wangeendelea kuzizuia pepo zile nne mpaka hapo kazi ya Yesu itakapokwisha katika patakatifu, na baada ya hapo yatakuja yale mapigo saba ya mwisho. Mapigo hayo yaliwafanya waovu wawakasirikie sana wale wenye haki; wao walidhani kwamba ni sisi [Waadventista Wasabato] tuliowaletea hukumu hizo za Mungu juu yao, na ya kwamba kama wangeweza kutufutilia mbali juu ya uso wa nchi, basi, mapigo hayo yangeweza kuzuiwa. Amri [ya kifo] ikatolewa kuwaua watakatifu wote, ambayo iliwafanya kulia mchana na usiku ili wapate kuokolewa. Huo ulikuwa ni Wakati wa Taabu ya Yakobo." EW 36,37.

b. "Amri itatolewa hatimaye dhidi ya wale wanaoitakasa Sabato ya amri ya nne ikiwashutumu kuwa wanastahili adhabu kali sana, na kuwapa watu uhuru wa kuwaua baada ya muda fulani uliowekwa kupita. Ukatoliki wa Roma katika Ulimwengu wa Zamani na Uprotestanti Asi katika Ule Mpya, watafuata njia inayofanana dhidi ya wale wanaoziheshimu amri zote [kumi] za Mungu.

"Hapo ndipo watu wa Mungu watakapotupwa katika mandhari zile za mateso na dhiki zilizoelezwa na nabii yule kama Wakati wa Taabu ya Yakobo." GC 615,616.

5. Kwa nini hatari hiyo kubwa inaitwa "Wakati wa Taabu ya Yakobo"? Mwa.32:24-28.

"Yakobo na Esau wanayawakilisha makundi mawili: Yakobo, anawawakilisha wenye haki, na Esau, waovu. Dhiki ya Yakobo alipojua kwamba Esau alikuwa anamjia na watu [wapiganaji] mia nne, inaiwakilisha taabu ile ya wenye haki wakati ule amri ya kuwaua itakapotolewa muda mfupi tu kabla ya kuja kwake Bwana. Waovu watakapowazingira [wale wenye haki], watajawa na uchungu mwingi wa moyo, kwa maana, kama vile Yakobo, hawawezi kuona njia yo yote ya kuyaokoa maisha yao. Malaika yule alisimama mbele ya Yakobo, naye akamkamata yule malaika na kumshikilia na kupigana naye mieleka usiku kucha. Hivyo ndivyo wenye haki watakavyopigana mieleka na Mungu kwa njia ya maombi katika wakati wao wa taabu na uchungu mwingi, kama vile Yakobo alivyopigana mieleka na malaika yule [Kristo]. Katika dhiki yake Yakobo aliomba usiku kucha ili apate kuokolewa kutoka katika mkono wa Esau. Katika maumivu yao makali kiakili wenye haki watamlilia Mungu mchana na usiku ili wapate kuokolewa kutoka katika mikono ya waovu ambao watakuwa wamewazingira." SR 97; 3SG 131,132.

"Uzoefu alioupata Yakobo usiku ule wa kupigana mieleka na uchungu wake wa moyo unawakilisha maonjo watakayoyapitia watu wa Mungu muda mfupi tu kabla ya Kristo kuja mara yake ya pili. Nabii Yeremia, katika maono yake matakatifu, akiangalia mpaka wakati wetu huu, alisema, '... Ole! maana siku ile ni kuu, hata hapana inayofanana nayo, maana ni wakati wa taabu yake Yakobo; lakini ataokolewa nayo.'

"Yesu atakapoacha kazi yake kama Mwombezi kwa ajili ya mwanadamu, ndipo wakati huo wa taabu utakapoanza. Hadi wakati huo kesi ya kila mtu itakuwa imekatwa, wala hapatakuwa na damu ya upatanisho tena ya kuziosha dhambi [za watu waliochelewa kutubu]. Yesu atakapokuwa anaondoka mahali pake [Patakatifu pa Patakatifu] kama Mwombezi wa mwanadamu mbele zake Mungu, ndipo tangazo hili la kutisha litakapotolewa, "Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu;...' Kisha Roho wa Mungu azuiaye ataondolewa kutoka duniani. Kama vile Yakobo alivyotishiwa kuuawa na ndugu yake mwenye hasira, ndivyo watu wa Mungu watakavyokuwa hatarini kutokana na waovu wanaotafuta kuwaangamiza. Na kama vile yule mzee [Yakobo] alivyopigana mieleka usiku kucha ili apate kuokolewa kutoka katika mkono wa Esau, hivyo ndivyo wenye haki watakavyomlilia Mungu mchana na usiku ili wapate kukombolewa kutoka kwa adui zao wale wanaowazingira." PP 201.

6. Je, Waadventista Wasabato wote wanakubaliana ya kwamba "Wakati wa Taabu ya Yakobo" utaanza mara tu itakapotolewa amri ya ulimwengu mzima ya kuwaua baada ya kufungwa kwa mlango wa rehema?

La, hawakubaliani. Kuna baadhi wanaoamini kwamba Wakati wa Taabu ya Yakobo utaanza wakati ule itakapotolewa Amri ya Jumapili kwa Taifa zima [la Marekani], kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema. Hitimisho lao limejengwa juu ya usemi ufuatao:

"Kujipatia hali ya kupendwa na watu wengi na ile mamlaka ya kuteua watu, wabunge (watunga sheria) watayakubali madai [ya watu] ya kupitisha Amri ya Jumapili.... Kama vile kukaribia kwa majeshi yale ya Kirumi kulivyokuwa ishara kwa wanafunzi wake juu ya maangamizi ya Yerusalemu yaliyokuwa karibu sana kutokea, ndivyo uasi huo [wa Marekani] unavyoweza kuwa ishara kwetu kwamba uvumilivu wake Mungu umefikia kipeo chake, kwamba kikombe cha uovu wa Taifa letu [la Marekani] kimejaa, na ya kwamba yule malaika wa rehema yu karibu kuruka na kwenda zake, asiweze kurudi tena. Hapo ndipo watu wa Mungu watakapotupwa katika mandhari zile za mateso na dhiki ambazo manabii wamezielezea kuwa ndio Wakati wa Taabu ya Yakobo." 5T 451.

7. Je, tunaweza kupata picha kamili ya mateso hayo makali kutoka katika Roho ya Unabii?

"Wakati wa Taabu, mfano wake haukuwapo' karibu utakuja juu yetu; nasi tutahitaji uzoefu [wa maisha ya Kikristo] ambao hatunao hivi sana na ambao wengi wetu tu wavivu mno kuupata. Mara nyingi ndivyo ilivyo ya kwamba taabu inayotarajiwa ni kubwa mno [kimawazo] kuliko ilivyo hasa; lakini hilo si kweli kuhusu hatari hiyo kubwa iliyo mbele yetu. Kuielezea kwa wazi kabisa hakuwezi kufikia kiwango cha mateso yale makali kitakavyokuwa. Katika wakati ule wa maonjo, kila mtu atapaswa kusimama peke yake mbele za Mungu." GC 622.

8. Je, Wakati wa Taabu ya Yakobo utakuwa ni jaribio [mtihani] kali mno hata kwa Wakristo wale wa kweli? 1 Kor. 10:13.

a. "Si salama sikuzote kuomba uponyaji usiokuwa na masharti.... Yeye anajua kama wale ambao dua zinatolewa kwa ajili yao wangeweza kustahimili maonjo na majaribio yale ambayo yangewajia iwapo wangeendelea kuishi au la. Yeye anajua mwisho tangu mwanzo wake. Wengi watalazwa na kulala [makaburini mwao] kabla ya mateso yale makali kama moto ya Wakati ule wa Taabu kuujia ulimwengu wetu." CH 375.

b. "Bwana ameniagiza mara nyingi kwamba watoto wengi wadogo watalazwa [makaburini mwao] kabla ya kuja Wakati ule wa Taabu. Tutawaona tena watoto wetu. Tutakutana nao na kuwajua katika majumba yale ya kifalme kule mbinguni." 2SM 259.

9. Watu wa Mungu watakuwa wapi wakati huo [wa Taabu ya Yakobo]?

Angalia madondoo chini ya swali la 4 la Sura ya 18 nyuma.

10. Je, ni jambo linalofaa kwetu kufanya mpango wa kujiwekea sasa akiba ya mahitaji yetu ya kimwili kwa ajili ya Wakati ule wa Taabu?

a. "Bwana amenionyesha mimi tena na tena ya kwamba ni kinyume na Biblia kufanya maandalizi yo yote ya mahitaji yetu ya kimwili kwa ajili ya Wakati ule wa Taabu. Nikaona ya kwamba iwapo watakatifu walikuwa wamejiwekea akiba ya chakula nyumbani mwao, au mashambani mwao kwa ajili ya Wakati ule wa Taabu, wakati upanga, njaa, na tauni vitakapokuwa juu ya nchi, basi, kingeporwa kutoka kwao na mikono yenye nguvu, na wageni wangeyavuna mashamba yao." EW 56.

b. "Nyumba na mashamba havitakuwa na faida yo yote kwa watakatifu Wakati ule wa Taabu, maana wakati ule itawapasa kukimbia mbele ya makundi yenye ghadhabu kubwa."

EW 56.

11. Ni nani basi, atakayetulisha?

a. "Hapo ndipo utakuwa ndio wakati wa sisi kumtegemea Mungu kabisa, naye atatulisha." EW 56. [Isa.33:16; 41:17,18; 1 Fal. 17:2-9.]

b. "Mungu yule aliyemtunza Eliya, hatampita kando mmoja wa watoto wake wanaojitolea mhanga. Yeye anayezihesabu nywele za vichwa vyao atawatunza, na wakati ule wa njaa watashibishwa. Wakati waovu wanaendelea kufa kwa njaa na tauni, malaika watawalinda wenye haki, na kuwapa mahitaji yao. Kwake yeye 'aendaye kwa haki' imetolewa ahadi hii, 'atapewa chakula chake; maji yake hayatakoma.' " GC 629.

12. Chakula kingi kiasi gani watapewa watakatifu hao?

a. "Wakati wa Taabu karibu sana uko mbele yetu; na hapo ndipo shida kubwa itawafanya watu wa Mungu kujikana nafsi zao, na kula kiasi cha kutosha tu kuendeleza uhai; lakini Mungu atatutayarisha kwa wakati ule. Katika saa ile ya kutisha shida yetu itakuwa ndiyo nafasi ya Mungu ya kuwapa watu wake nguvu yake ya kuwaimarisha, na kuwapa chakula." 1T 206; CD 202.

b. "Chakula [Mkate] na maji ndiyo yote aliyoahidi kwa Wamasalio [Waadventista Wasabato] kwa kipindi kile cha Wakati wa Taabu." 3SG 252; SR 129.

c. "Watu wa Mungu hawataepukana na mateso; lakini wakati wakiwa wanateswa na kuona dhiki, wakati wanastahimili umaskini na kuteseka kwa kukosa chakula, hawataachwa kuangamia." GC 629.

d. "Malaika wakawapa chakula [mkate] na maji wakati waovu walipokuwa wakiendelea kuteseka kwa njaa na kiu." EW 282.

e. "Nikaona ya kwamba chakula chetu [mkate] na maji tutapewa kwa hakika wakati ule, na ya kwamba hatutapungukiwa wala kuteseka kwa njaa; kwa maana Mungu anaweza kuandaa meza kwa ajili yetu jangwani. Ikibidi anaweza kuwatuma kunguru wale kutulisha, kama vile alivyofanya kumlisha Eliya, au kudondosha mana kutoka mbinguni, kama alivyofanya kwa Waisraeli." EW 56.

f. "Maangamizi ya hakika yanawatishia, nao kama Yakobo hawataruhusu imani yao kufifia, kwa sababu ya maombi yao kutojibiwa upesi. Ingawa watakuwa wanateseka kwa maumivu ya njaa, hawatakoma kutoa dua zao kwake." 3SG 135.

13. Ni msaada kiasi gani wa kuungwa mkono kimawazo tunaweza kutegemea kupata kutoka kwa marafiki zetu wakati ule wa maonjo makali sana?

"Imani ya mshiriki mmoja mmoja wa Kanisa itajaribiwa kana kwamba hakuwako mtu mwingine ye yote duniani." 7BC 983.

14. Je, Bwana atajibu mara moja maombi ya watu wake watakapomwita ili awaokoe?

a. "Kule kuchelewa kwenyewe, japo ni kuchungu sana kwao, ndilo jibu bora kupita yote kwa dua zao walizotoa. Wanapojitahidi kungoja kwa matumaini kwamba Bwana atatenda kazi yake, hapo ndipo wanapoongozwa kutumia imani yao, tumaini lao, na saburi yao, mambo ambayo wameyatumia kidogo mno katika uzoefu wao wote wa kidini [uliopita]." GC 631.

b. "Kipindi kile cha dhiki na uchungu mwingi wa moyo kilicho mbele yetu kitahitaji imani inayoweza kustahimili uchovu, uchelewevu, na njaa, ----- yaani, imani ambayo haitazimia, japokuwa inajaribiwa vikali sana." GC 621.

15. Baadhi ya watakatifu wataanza kuogopa kitu gani hasa?

Angalia madondoo chini ya swali la 16, Sura ya 18.

16. Licha ya mateso na njaa, kitakachosababisha uchungu sana mioyoni mwao ni kitu gani hasa?

"Ingawa watu wa Mungu watakuwa wamezingirwa na maadui zao walionuia kuwaangamiza, hata hivyo uchungu wa moyoni utakaowatesa sana si hofu ya kule kuteswa kwa ajili ya ile kweli; wao wataogopa kwamba kwa njia ya kosa lao fulani lililojificha ndani yao watashindwa kutambua kutimizwa kwa ahadi ile ya Mwokozi, aliyosema: Mimi nami 'nitakulinda, utoke katika saa ya kujaribiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote.' Ufunuo 3:10. Laiti kama wangalikuwa wanao uhakika wa msamaha wao, hapo ndipo wasingeweza kuogopa yale mateso ya mwili wala kifo; walakini endapo wangeonekana kuwa hawastahili, na kupoteza maisha yao kwa sababu ya kasoro walizo nazo katika tabia zao, basi, hapo ndipo jina la Mungu lingetukanwa." GC 619.

17. Hivi wao wenyewe watajionaje?

"Wenye haki, katika dhiki yao, watakuwa na hisia kubwa ya kutostahili kwao, na kwa machozi mengi watakiri kutokufaa kwao kabisa, na kama Yakobo watadai ahadi za Mungu kwa njia ya Kristo, ambazo zimetolewa kwa watu kama hao, yaani, wenye dhambi wasioweza kujitegemea wenyewe, wasiokuwa na uwezo wo wote, na wanaotubia dhambi zao." 3SG 132; SR 97; 1SP 121, 122.

18. Je, wenye haki kwa nafsi zao wenyewe, wataweza kuzikumbuka dhambi zao halisi walizozitenda?

a. "Hawawezi kuzikumbuka dhambi zao zenyewe hasa [walizozitenda], lakini katika maisha yao yote wanaweza kuona wema kidogo tu. Dhambi zao zilitangulia kwenda hukumuni

[1 Tim. 5:24], na msamaha ulikuwa umeandikwa kule. Dhambi zao zilikuwa zimechukuliwa na kupelekwa katika nchi ya usahaulifu, hawakuweza kuzikumbuka." 3SG 134,135;

1SP 123,124.

b. "Lakini japokuwa wanazo hisia nzito za kutofaa kwao, hawana maovu waliyoyaficha ambayo wanapaswa kuyadhihirisha. Dhambi zao zimekwisha tangulia hukumuni, nazo zimefutwa; hawawezi kuzikumbuka." GC 620.

19. Walakini, hao wenye haki watakapokumbushwa dhambi zao zilizopita, wataingia katika hali gani iliyo karibu sana na kukata tamaa?

a. "Yakobo akamshika sana yule malaika katika dhiki yake, wala hakutaka kumwachilia aende zake. Alipotoa dua zake kwa machozi, yule malaika akamkumbusha makosa yake yaliyopita, kisha akajitahidi kumponyoka Yakobo, ili kumpima na kumthibitisha. Hivyo ndivyo wale wenye haki, katika siku ya utungu wao, watakavyopimwa, watakavyothibitishwa, na kujaribiwa, ili kuidhihirisha nguvu ya imani yao, uvumilivu wao na tumaini lao lisilotikisika katika uwezo wa Mungu kuwaokoa.

"Yakobo hakuweza kugeuziwa mbali, alijua kwamba Mungu ni mwenye rehema nyingi, naye aliomba rehema yake. Alionyesha huzuni yake ya nyuma na toba yake kwa makosa yake, naye alitoa dua yake kwa kusisitiza ili apate kuokolewa katika mkono wa Esau. Hivyo ndivyo maombi yake ya kusihi sana yalivyoendelea usiku kucha. Alipojikumbusha makosa yake yaliyopita, alikuwa karibu na kukata tamaa kabisa. Lakini alijua kwamba hana budi kupata msaada kutoka kwa Mungu ama sivyo angeangamia. Alimshikilia sana malaika yule, na kusisitiza dua yake kwa kilio cha uchungu, kilichotoka moyoni mpaka akashinda. Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwa wale watakatifu. Watakapojikumbusha matukio ya maisha yao yaliyopita, matumaini yao karibu sana yatazama." 3SG 132,133; SR 97,98.

b. "Shetani anapowashtaki watu wa Mungu kutokana na dhambi zao, Bwana anamruhusu awajaribu upeo. Tumaini lao kwa Mungu, imani yao na uthabiti wao, hujaribiwa sana. Wanapoyapitia maisha yao yaliyopita, matumaini yao huzama, maana katika maisha yao yote wanauona wema kidogo sana." GC 618, 619.

20. Ni ombi gani watakatifu watakalolitoa kwa Mungu kuhusiana na dhambi zao nyingi?

a. "Lakini watakapotambua ya kuwa ni suala la kufa na kupona, watamlilia Mungu kwa dhati, na kumwomba kuhusu huzuni yao iliyopita na toba yao ya unyenyekevu kwa ajili ya dhambi zao nyingi, kisha watamkumbusha ahadi yake, 'Au azishike nguvu zangu, afanye amani nami; Naam, afanye amani nami.' Hivyo ndivyo dua zao za dhati zitakavyotolewa kwa Mungu mchana na usiku...." 3SG 133.

b. "Wanajitesa nafsi zao mbele za Mungu, wakionyesha toba yao ya zamani kwa ajili ya dhambi zao nyingi." GC 619.

21. Ni dhambi ngapi zisizoungamwa zinaletwa katika kumbukumbu zao?

a. "Watajisikia kutokufaa kwao, lakini hawatakuwa na makosa yo yote waliyoyaficha ambayo wanapaswa kuyafunua. Endapo wangekuwa na dhambi zisizoungamwa wala kutubiwa, ambazo zingeonekana mbele yao, wakati wanateseka kwa hofu na uchungu mwingi moyoni mwao, wakiwa wanatambua fika kutostahili kwao, basi, wangeshindwa kabisa." 3SG 134; SR 98.

b. "Kwa hiyo, wakati ule wa taabu, kama watu wa Mungu wangekuwa na dhambi zisizoungamwa ambazo zingeonekana mbele yao wakati wanateseka kwa hofu na uchungu mwingi moyoni, basi, wangeshindwa kabisa; kukata tamaa kungeivunjilia mbali imani yao, nao wasingekuwa na ujasiri wo wote wa kumlilia Mungu ili awaokoe. Lakini wakati wanayo hisia inayoingia ndani sana kuhusu kutokufaa kwao, hawana makosa yo yote waliyoficha wanayopaswa kuyafunua." GC 620.

22. Ni tofauti gani itakayoonekana katika uchungu wa moyo wa watakatifu hao?

"Wale wanaotumia imani kidogo sana hivi sasa, wako katika hatari kubwa sana ya kuanguka chini ya madanganyo ya Shetani na ile amri itakayozilazimisha dhamiri zao. Na hata kama watastahimili jaribio hilo, watatumbukizwa katika dhiki kubwa zaidi na uchungu wa moyo katika wakati ule wa taabu, kwa sababu hawajaifanya kuwa tabia yao kumtegemea Mungu." GC 622.

23. Bwana atayajibuje maombi ya watu wake hata kabla hawajakombolewa kutoka kwa maadui zao?

a. "Ingawa maadui zao wanaweza kuwatupa magerezani, lakini kuta za magereza ya chini ya ardhi haziwezi kukata mawasiliano kati ya roho zao na Kristo. Mmoja ambaye anauona udhaifu wao hasa, yule anayelijua kila onjo, yeye yu juu ya mamlaka zote za dunia; na malaika watakuja kuwatembelea katika seli zao za upweke, wakiwaletea nuru na amani kutoka mbinguni. Gereza litakuwa kama jumba la kifalme; maana walio matajiri wa imani watakuwa wanaishi mle, na kuta zile zenye giza zitaangazwa kwa nuru ya mbinguni, kama vile Paulo na Sila walivyoomba na kuimba sifa usiku ule wa manane katika gereza la chini ya ardhi kule Filipi." GC 627 (Angalia pia PK 512, 513).

b. "Wakati wale wanaopigana mieleka wanapeleka dua zao kwa bidii mbele za Mungu, pazia lile linalowatenga na mambo yale yasiyoonekana litaonekana kana kwamba limeondolewa kabisa. Mbingu zitang'aa kwa macheo ya siku ile ya milele, na kama nyimbo tamu za malaika, maneno haya yataanguka masikioni mwao, 'Simameni imara katika utii wenu. Msaada unakuja kwenu.'... Mwokozi yule wa thamani atatuma msaada wake wakati ule ule tutakapouhitaji." GC 632,633.

c. "Kama wanadamu wangeweza kuona kwa macho ya kimbingu, wangeweza kuyaona makundi kwa makundi ya malaika wenye nguvu zisizo na kifani wakiwa wamewazunguka wale waliolishika neno lile la subira yake Kristo. Kwa upole uliojaa huruma, malaika wameshuhudia dhiki yao [watakatifu], na kuyasikia maombi yao. Wanangojea neno [amri] kutoka kwa Kamanda wao ili wapate kuwanyakua kutoka katika maangamizi yao." GC 630.

24. Bwana atawezaje kuwakomboa watu wake hatimaye?

a. "Kwa kelele za ushindi, kuzomea, na kulaani, makundi ya waovu yatakuwa tayari kuwarukia mateka wao, wakati, tazama utusitusi mzito, mnene kuliko ule wa usiku, unaanguka juu ya uso wa dunia.... Ni usiku wa manane Mungu anapoudhihirisha uweza wake wa kuwaokoa watu wake.... Katikati ya mbingu zilizokasirika ipo nafasi moja iliyo wazi yenye utukufu usioelezeka, ambayo kutoka katika hiyo huja sauti ya Mungu kama sauti ya maji mengi, ikisema, 'Imekwisha.' " GC 635,636.

b. Angalia madondoo chini ya swali la 19, Sura ya 18 nyuma.

25. Idadi ya wale watakaopita kwa ushindi katika Wakati ule wa Taabu ya Yakobo ni wangapi? Ufu. 7:4; 14:1.

26. Uzoefu wao utatofautianaje na ule wa kundi jingine lo lote la Wakristo tangu wakati ulipoanza kuwako?

"Nao wauimba 'wimbo mpya' mbele ya kile kiti cha enzi,... wala hapana mtu aliyeweza kujifunza wimbo ule, ila wale mia na arobaini na nne elfu. Ni wimbo wa Musa na wa Mwana-Kondoo, ----- wimbo wa ukombozi. Wala hapana mtu aliyeweza kujifunza wimbo ule, ila wale mia na arobaini na nne elfu; kwa maana ni wimbo wa uzoefu wao, ----- uzoefu wa namna ile

ambayo hakuna kundi jingine lo lote lililoupata. 'Hawa ndio wamfuatao Mwana-Kondoo kila aendako.' Hawa, wakiwa wamenyakuliwa kutoka duniani, miongoni mwa walio hai, wanahesabiwa kama ndio 'malimbuko ya kwanza kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo.' 'Hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu;' wamepita katika Wakati ule wa Taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa; wamestahimili uchungu mkali wa moyo wa Wakati wa Taabu ya Yakobo; wamesimama bila kuwa na Mwombezi katika kipindi chote cha mwisho cha kumwagwa kwa hukumu za Mungu za mwisho." GC 649.

27. Ni dhambi ngapi watakazotenda katika kipindi chote cha Wakati wa Taabu ile kubwa ----- kuanzia pale mlango wa rehema utakapofungwa mpaka wakati wa kuja kwake Yesu na mawingu?

"Hata kwa wazo moja tu Mwokozi wetu hakuweza kuanguka chini ya nguvu ya majaribu.... Hiyo ndiyo hali ambayo wanatakiwa kuwa nayo wale watakaosimama katika wakati ule wa taabu." GC 623.

28. Kwa faida ya nani maonyesho hayo ya ajabu ya kutokuwa na dhambi yataonyeshwa?

a. "Katika kuyaacha maisha ya mwuaji yule wa kwanza[Kaini], Mungu alionyesha mbele ya malimwengu yote fundisho lililohusiana na lile Pambano Kuu....

"Lilikuwa ni kusudi lake, sio tu kuyakandamiza maasi, bali kuyaonyesha malimwengu yote tabia ya maasi yale.... Wakazi wale watakatifu wa dunia zingine walikuwa wanayachungulia kwa shauku kubwa mno matukio yale yaliyokuwa yanatokea katika dunia yetu hii....

"Mungu anajionyesha kuwa anayo huruma na kupata ukubali wa malimwengu yote wakati mpango wake [wa ukombozi] unapozidi kuendelea mbele hatua kwa hatua mpaka hapo utakapotimilika kabisa." PP 78,79.

b. "Walakini mpango wa ukombozi ulikuwa una kusudi pana na lenye kina kuliko wokovu tu wa mwanadamu. Haikuwa kwa jambo hili peke yake Kristo alikuja hapa duniani; haikuwa tu kwamba wakazi wa dunia hii ndogo wapate kuiheshimu Sheria ya Mungu [Amri Kumi] kama ilivyopaswa kuheshimiwa; bali ilikuwa ni kuitetea tabia ya Mungu mbele ya malimwengu. Mwokozi alitarajia kuyaona matokeo haya ya kafara yake kuu ----- yaani, mvuto wake juu ya wenye hekima wa dunia zile nyingine, pamoja na mwanadamu ----- wakati ule, yaani, kabla ya kusulibiwa kwake aliposema, Sasa hukumu ya ulimwengu huu ipo; sasa mkuu wa ulimwengu huu [Shetani] atatupwa nje. Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu.' Yohana 12:31,32. Tendo hilo la Kristo kufa kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu lisingefanya mbingu tu iweze kupatikana kwa wanadamu; bali mbele ya malimwengu yote lingeithibitisha haki ya Mungu na Mwanawe katika kuyashughulikia maasi yale ya Shetani." PP 68,69.

c. "Malimwengu yale ambayo hayakuanguka [dhambini] na malaika wale wa mbinguni walikuwa wamechungulia kwa shauku kubwa Pambano hilo lilipokuwa linakaribia mwisho wake." DA 693.

d. "Sisi ni kama watu waliokwisha kuhukumiwa kuuawa katika uwanja wa maonyesho, tumekuwa tamasha kwa malimwengu yote ----- kwa malaika na kwa wanadamu." 1 Kor. 4:9 [Tafsiri ya N.E.B.].

e. "Malimwengu yote yanaangalia kwa shauku isiyoelezeka matukio yale ya mwisho ya Pambano lile Kuu kati ya wema na uovu." PK 148.

f. "Dunia yetu hii ndogo ni kitabu cha mafundisho kwa malimwengu yote," DA 19.

# SURA YA 20

## KIPINDI KIKUU CHA WAKATI WA TAABU

(Baada ya Kufungwa kwa Mlango wa Rehema)

1. Ni akina nani leo wanaozizuia nguvu za maangamizi zisipate kuifagilia mbali dunia yetu hii?

Ufu. 7:1-3.

a. "Malaika wanaruka kuizunguka dunia hii, wakiyakataa madai ya Shetani ya ukuu wake [wa dunia hii], anayoyatoa kwa sababu ya umati mkubwa sana wa wafuasi wake. Hatuzisikii sauti zao, lakini mikono yao imeshikana pamoja kuizunguka dunia hii, nao wanakesha bila kulala wakiyazuia majeshi ya Shetani mpaka kazi ya kuwatia muhuri watu wa Mungu itakapomalizika." 7BC 967.

b. "Uwezo ule ule wa maangamizi unaotumiwa na malaika hao watakatifu wa Mungu anapowapa amri kufanya hivyo, utaweza kutumiwa na malaika wale waovu atakapowaruhusu. Kuna majeshi ambayo yako tayari sasa, nayo yanangojea tu ruhusa ya Mungu ili yapate kueneza maangamizi yao kila mahali." GC 614.

2. Ni tendo gani la mwisho katika mfululizo huo wa matukio, ambalo baada ya hilo mlango wa rehema utafungwa, na Shetani ataruhusiwa kufanya apendavyo hapa duniani?

Dunia hii karibu sana imefikia mahali ambapo Mungu atamruhusu yule aangamizaye kufanya apendavyo juu yake. Kule kuziweka sheria za wanadamu mahali pa Sheria ya Mungu [Amri Kumi], kuitukuza Jumapili kwa mamlaka ya kibinadamu tu, mahali pa Sabato ile ya Biblia, hilo ndilo tendo la mwisho katika mfululizo wa matukio. Kuweka [Jumapili] badala yake [Sabato]

kutakapoenea ulimwenguni kote, hapo ndipo Mungu atakapojidhihirisha mwenyewe. Atatoka mahali pake kuja kuwaadhibu wakazi wa ulimwengu huu kwa uovu wao, ardhi nayo itafunua damu yake, wala haitawafunika tena watu wake waliouawa.." 7T 141. [Isa.26:20,21; Ufu.19:17-21; Yer.25:32-37.]

3. Mlango wa rehema utakapofungwa, Shetani atawadhibiti waovu kwa kiwango gani?

a. "[Mungu] atawaambia malaika zake, 'Msiendelee kupigana vita na Shetani katika juhudi zake za kuwaangamiza wanadamu. Mwache afanye uovu wake mkuu juu ya wana hao wa maasi; kwa maana kikombe cha maovu yao kimejaa." RH 9-17-1901.

b. "Atakapoondoka pale patakatifu, giza litawafunika wakazi wa dunia hii. Katika wakati ule wa kutisha wenye haki hawana budi kuishi mbele za macho ya Mungu Mtakatifu pasipokuwa na Mwombezi. Kizuizi kilichowekwa juu ya waovu kimeondolewa, na Shetani amewadhibiti kabisa wale ambao mpaka mwisho watakuwa hawajatubu. Uvumilivu wa Mungu umekwisha. Ulimwengu umeikataa rehema yake, umeudharau upendo wake, na kuikanyaga Sheria yake chini ya miguu yao. Waovu wameuvuka mstari wa muda wao wa majaribio, na kwa kung'ang'ania msimamo wao, hatimaye Roho wa Mungu ameondolewa kwao. Wakiwa hawana ulinzi wa neema ya Mungu, watakuwa hawana kinga yo yote kutoka kwa yule mwovu." GC 614.

4. Biblia inauelezaje wakati kama huo? Dan. 12:1.

5. Mioto ya hasira kali na maasi itakaposhindwa kudhibitiwa ulimwengu utakuwa katika hali gani?

"Roho ya vurugu inayotaka usiwepo utawala wa serikali inaendelea kuenea katika mataifa yote pamoja na milipuko inayotokea mara kwa mara inayoamsha hofu ya walimwengu, hiyo ni ishara ya mioto iliyogandamizwa ya hasira kali na maasi, ambayo, mara itakaposhindwa kudhibitiwa, itaijaza dunia hii na maafa pamoja na maangamizi. Picha iliyotolewa na uvuvio ya kipindi kile cha ulimwengu uliokuwako kabla ya gharika, huwakilisha hali halisi kabisa ya hali ambayo jamii ya leo inaharakisha kuingia ndani yake." PP 102.

6. Je, kuna uwezekano wa hakika wa kutokea vita ya kimataifa itakayoenea katika eneo kubwa?

a. Maandalizi ya vita yanafanyika hivi sasa.

"Kila kitu ulimwenguni humu kimo katika hali ya kutotulia. Mataifa yamekasirika, na maandalizi makubwa ya vita yanafanywa. Taifa linakula njama dhidi ya taifa jingine, na ufalme dhidi ya ufalme mwingine. Siku ile kuu ya Mungu inaharakisha sana. Lakini ijapokuwa mataifa yanakusanya majeshi yao kwa ajili ya vita na umwagaji damu, amri [ya Mungu] kwa malaika wale bado inasimama katika nguvu yake ile ile, kwamba wazizuie pepo zile nne mpaka hapo watumishi wa Mungu watakapokuwa wamekwisha kutiwa muhuri katika vipaji vya nyuso zao." 7BC 968 (1909).

b. Taifa litaondoka kupigana na taifa.

"Kabla tu hatujaingia (katika wakati ule wa taabu), wote tulipokea muhuri wa Mungu aliye hai. Ndipo nikawaona malaika wale wanne wakiacha kuzizuia pepo zile nne. Nami nikaona njaa, tauni na upanga, taifa likaondoka kupigana na taifa, na ulimwengu mzima ulikuwa katika hali ya machafuko." 7BC 968.

c. "Meli zitazikwa chini ya vilindi vya bahari."

"Malaika wanne wenye nguvu wanazizuia mamlaka za ulimwengu huu mpaka hapo watumishi wa Mungu watakapotiwa muhuri juu ya vipaji vya nyuso zao. Mataifa ya ulimwengu huu yana hamu ya kupigana; lakini yamezuiwa na malaika hao. Uwezo huo unaozuia utakapoondolewa, patakuwa na wakati wa taabu na utungu. Silaha za kufisha za vita zitaundwa. Meli pamoja na shehena zao za watu walio hai, zitazikwa chini ya vilindi vya bahari. Wale wote wasiokuwa na roho ya [kuipenda] ile kweli wataungana pamoja chini ya uongozi wa mawakala wa Shetani. Lakini watapaswa kudhibitiwa mpaka wakati ule utakapofika wa vita ile kuu ya Har-Magedoni." 7BC 967.

d. "Mapigano ya wote yanakuja."

"Ni kitambo kifupi tu cha wakati kilichobaki, kama mambo yalivyo. Lakini wakati taifa tayari linaondoka kwenda kupigana na taifa lingine, na ufalme kupigana na ufalme mwingine, bado mpaka sasa hakuna mapigano ya [ulimwengu] wote. Bado hata sasa pepo zile nne zimezuiwa mpaka hapo watumishi wa Mungu watakapotiwa muhuri juu ya vipaji vya nyuso zao. Hapo ndipo mamlaka za dunia zitakapoyakusanya majeshi yao kwa vita kuu ya mwisho." 6T 14 (Angalia pia 7BC 968).

7. Je, kuna uwezekano wa kuwako vita ya nyuklia?

a. "Wakati huo Shetani atawatumbukiza wakazi wa dunia hii katika taabu moja kubwa, ya mwisho. Malaika wa Mungu watakapoacha kuziziuia pepo kali za hasira kali ya wanadamu, kila aina ya migongano itaachiliwa. Ulimwengu wote utaingia katika maangamizi ya kutisha kuliko yale yaliyoupata mji ule wa Yerusalemu zamani." GC 614.

b. "Vyote viwili, mji [wa Yerusalemu] na hekalu vilibomolewa hadi kwenye misingi yake, na ardhi ile iliposimama nyumba takatifu 'ililimwa kama shamba.' Katika kuzingirwa kwake na mauaji yaliyofuata, zaidi ya milioni moja ya watu waliangamia." GC 35.

c. "Unabii wa Mwokozi kuhusu kupatilizwa kwa hukumu juu ya Yerusalemu utakuwa na matokeo mengine, ambayo maangamizi yale ya kutisha yalikuwa kivuli chepesi tu. Katika ajali ya mji ule twaweza kuona maangamizi ya ulimwengu huu ambao umeikataa rehema ya Mungu na kuikanyaga Sheria yake [Amri Kumi] chini ya miguu yao." GC 36.

d. "Safari moja, nilipokuwa katika Mji Mkuu wa New York, niliitwa wakati wa usiku ili nipate kuyaangalia majengo yaliyokuwa yanapanda juu orofa baada ya orofa kuelekea mbinguni. Majengo hayo yalithibitishwa kuwa hayawezi kushika moto, nayo yalijengwa ili kuwatukuza wenye majengo hayo pamoja na wajenzi....

"Mandhari [picha] iliyopita mbele yangu baada ya hapo ilikuwa ni ile ya king'ora cha moto. Watu waliyatazama majengo yale marefu yaliyodhaniwa kuwa hayawezi kushika moto na kusema: 'Hayo yako salama kabisa.' Lakini majengo hayo yaliteketezwa kana kwamba yalikuwa yamejengwa kwa lami. Magari ya kuzima moto hayakuweza kufanya kitu cho chote kuzuia uharibifu ule. Wanaozima moto walishindwa kuziendesha injini za kuzima moto." 9T 12,13.

8. Je, yawezekana kwetu kuwa na picha dhahiri mawazoni mwetu ya maangamizi kamili na vita vile vitakavyotokea baada ya mlango wa rehema kufungwa?

"Malaika hivi sasa wanazizuia pepo zile za vita, ili zisipate kuvuma mpaka hapo ulimwengu utakapokuwa umeonywa juu ya maangamizi yake yanayokuja; walakini tufani inajikusanya, tayari kupasuka juu ya nchi; na Mungu atakapowaamuru malaika zake kuziachilia zile pepo, patakuwa na mandhari za vita ambazo hakuna mwandishi ye yote awezaye kutupatia picha yake." Ed 179,180 (Angalia pia 6T 408).

9. Ni nani atakayelaumiwa kwa shughuli zote za maangamizi hayo ya Shetani?

"Malaika yule wa rehema atakapokunja mabawa yake na kuondoka, Shetani atafanya matendo yake maovu ambayo kwa muda mrefu ametamani sana kuyafanya. Dhoruba na tufani, vita na umwagaji damu ----- mambo hayo ndiyo anayoyafurahia sana, na kwa njia hiyo anavuna mavuno yake [ya waovu]. Na wanadamu watadanganywa naye kabisa kiasi cha kuweza kusema kwamba maafa hayo ni matokeo ya kuinajisi siku ya kwanza ya juma [Jumapili]. Kutoka kwenye mimbara za makanisa yanayopendwa sana na watu wengi utasikika usemi kwamba ulimwengu unaadhibiwa kwa sababu Jumapili haiheshimiwi kama inavyopasa. Wala haitahitaji kuumiza sana kichwa [mawazo] kwa wanadamu kuweza kuamini usemi huo."

RH 9-17-1901.

10. Kuongezea juu ya maangamizi hayo makuu ambayo Mungu atamruhusu Shetani kusababisha, ni mapigo gani kutoka mbinguni yatakayomwagwa juu ya wale wasiotaka kutubu? Ufu. 15:1,8; 16:1.

"Nikaona ya kwamba wale malaika wanne wangeendelea kuzizuia pepo zile nne mpaka kazi ya Yesu itakapomalizika katika patakatifu [pa mbinguni], na baada ya hapo yatakuja yale mapigo saba ya mwisho." EW 36.

11. Mapigo ya kwanza manne yatakuwa ya kuogofya kwa jinsi gani?

"Mapigo hayo sio ya ulimwengu wote, vinginevyo, wakazi wa dunia hii wangekuwa wameangamizwa kabisa. Hata hivyo yatakuwa ni mapigo ya kuogofya mno yaliyopata kujulikana kwa wanadamu wanaokufa." GC 628,629.

12. Mapigo ya kwanza mawili ni mapigo gani? Ufu. 16:2,3.

13. Waovu watafanyaje watakapopigwa na mapigo hayo?

"Mapigo hayo yalikuwa yakianguka juu ya wakazi wa dunia hii. Wengine walikuwa wakimlaumu Mungu na kumlaani. Wengine walikimbia kwenda kwa watu wa Mungu na kuwasihi wawafundishe jinsi ya kuziepuka hukumu zake [Mungu]. Lakini watakatifu hawatakuwa na kitu cha kuwaambia. Chozi lao la mwisho kwa ajili ya wenye dhambi lilikuwa limekwisha dondoka, ombi lao la mwisho lilikuwa limekwisha tolewa kwa uchungu mkubwa, mzigo wao wa mwisho ulikuwa umekwisha kubebwa, onyo la mwisho lilikuwa limekwisha tolewa." EW 281.

14. Kwa nini viongozi wa serikali watadhamiria sasa kuwaangamiza wote wazishikao amri [kumi za Mungu]?

"Mapigo hayo yaliwafanya waovu kuwakasirikia sana wenye haki; walidhani kwamba ni sisi tuliokuwa tumewaletea hukumu hizo za Mungu juu yao, na ya kwamba kama wangeweza kutufutilia mbali na uso wa dunia, basi, mapigo hayo yangeweza kuzuiwa. Amri ikatolewa kuwaua watakatifu, ambayo iliwafanya kulia mchana na usiku ili wapate kuokolewa. Huo ulikuwa ndio Wakati wa Taabu ya Yakobo." EW 36,37.

15. Mungu atafanya nini ili kuijibu amri ile ya kuwaua [watu wake]? Ufu. 16:4-7.

"Na 'mito na chemchemi za maji; zikawa damu.' Ingawa mapigo hayo ni ya kuogofya sana kama yalivyo hasa, haki ya Mungu itathibitishwa kwayo. Malaika wa Bwana anatangaza, akisema: 'Wewe u mwenye haki,... kwa kuwa walimwaga damu ya watakatifu, nawe umewapa damu wainywe; nao wamestahili.' Kule kuwahukumu watu wa Mungu kuuawa, kwa kweli wamejipatia hatia ya damu yao [watakatifu] kana kwamba ilikuwa imemwagwa kwa mikono yao." GC 628.

16. Wenye haki watakapokuwa wanakimbia kuokoa maisha yao ni pigo gani la nne atakalolituma Mungu juu ya nchi? Ufu.16:8,9.

"Katika pigo lile linalofuata, uwezo unatolewa kwa jua 'kuwaunguza wanadamu kwa moto. Wanadamu wakaunguzwa kwa maunguzo makubwa.' Manabii wanaielezea hivi hali hiyo ya nchi kwa wakati huo wa kuogofya: '... nafaka imekauka,' 'Naam, miti yote ya mashamba imekauka; maana furaha imekauka katika wanadamu.' 'Mbegu zinaoza chini ya udongo wake; ghala zimeachwa ukiwa kabisa.... Jinsi wanyama wanavyougua! makundi ya ng'ombe yamefadhaika, kwa sababu hawana malisho.... Kwa maana vijito vya maji mengi vimekauka, Na moto umeyateketeza malisho ya nyikani.'... 'Mizoga itakuwa mingi; kila mahali wataitupa, wakinyamaza kimya.' " GC 628.

17. Kwa jinsi gani Mungu atakomesha ghafula malengo ya waovu wakati wa pigo lile la tano?

"Kwa kelele za ushindi, kuzomea, na kulaani, makundi ya waovu yatakuwa tayari kuwarukia mateka wao, wakati, tazama, utusitusi mzito, mnene kuliko ule wa usiku, unaanguka juu ya uso wa dunia. Kisha upinde wa mvua, unaong'aa kwa utukufu ule utokao kwenye kiti kile cha enzi cha Mungu, utaonekana mbinguni, nao utaonekana kana kwamba unakizunguka kila kikundi kinachoomba [cha watakatifu]. Makundi ya watu wenye hasira kali yatazuiwa ghafula. Makelele yao ya dhihaka yatafifia. Walengwa katika hasira yao watasahaulika. Kwa matarajio yaliyojaa hofu kuu wataiangalia ishara hiyo ya agano la Mungu [upinde wa mvua], na kutamani sana kusitiriwa kutokana na mng'ao wake mkali sana." GC 635,636.

18. Basi, katika wakati ule wa pigo lile la sita, ni pande gani mbili zinazopingana ambazo kila mtu katika ulimwengu mzima atakuwa amekusanywa?

a. "Mamlaka mbili kuu zinazopingana zinafunuliwa katika Pambano Kuu la mwisho. Upande mmoja anasimama Muumbaji wa mbingu na nchi. Wote walio upande wake wana muhuri wake. Ni watiifu kwa amri zake [kumi]. Upande ule mwingine anasimama yule mkuu wa giza, pamoja na wale waliochagua ukafiri na maasi." 7BC 982,983.

b. "Malaika wale waovu wanaziunganisha nguvu zao pamoja na zile za wanadamu waovu, na kwa vile daima wamekuwa katika mapambano, nao wamejipatia uzoefu katika kutumia njia bora za kudanganya na kupigana vita, tena wamekuwa wakijiimarisha kwa karne nyingi, hawatakubali kushindwa katika Pambano hilo Kuu la mwisho bila ya wao kufanya jaribio la mwisho kabisa. Ulimwengu wote utakuwa upande mmoja au mwingine wa hoja hiyo. Vita ile ya Har-Magedoni itapiganwa, na siku ile isimkute mtu ye yote miongoni mwetu aliyelala usingizi.... Uweza wa Roho Makatifu sharti uwe juu yetu, na Kapteni wa Jeshi la Bwana atasimama mbele ya malaika zake wale wa mbinguni na kuliongoza pambano hilo." 7BC 982.

19. Je, jitihada ya Shetani ya kuwakusanya wafalme wote na watu wa ulimwengu mzima chini ya bendera yake ilianza wakati ule wa pigo la sita, au hicho ndicho kilele cha juhudi yake ya miaka mingi kwa upande wake?

a. "Uadui wa Shetani dhidi ya wema utadhihirishwa zaidi na zaidi wakati atakapoyaleta majeshi yake katika mapambano katika kazi yake ya mwisho ya maasi yake; na kila mtu ambaye hajajisalimisha kabisa kwa Mungu, na kulindwa kwa nguvu yake Mungu, ataungana na Shetani kupigana na mbingu, na kujiunga katika vita dhidi ya Mtawala huyo wa malimwengu." TM 465.

b. "Roho za mashetani zitatoka na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote, kuwashikilia katika madanganyo, na kuwashurutisha kuungana na Shetani katika pambano lake la mwisho dhidi ya serikali ile ya mbinguni." GC 624.

c. "Roho wa Mungu anaondolewa taratibu kutoka duniani. Shetani naye anakusanya majeshi yake ya uovu, akiwaendea 'wafalme wa ulimwengu wote,' na kuwakusanya chini ya bendera yake, ili kuwapa mafunzo kwa ajili ya vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi.' "

7BC 983.

d. "Twapaswa... kuelewa maendeleo ya matukio katika kuyakusanya mataifa kwa vita ile ya mwisho ya Pambano hilo Kuu." 8T 307.

e. "Hivi punde wakazi wote wa ulimwengu huu watakuwa wameamua ni upande gani watakaosimama ama kwa ajili ya, ama dhidi ya, serikali ile ya mbinguni." 7T 141.

20. Je, Mungu wa mbinguni amekuwa akiyaandaa majeshi yake pia kwa pambano hilo la mwisho?

"Mamlaka za uovu hazitakubali kuacha kupigana pasipo kufanya jitihada yao. Lakini Mungu ana sehemu yake ya kufanya katika vita ile ya Har-Magedoni. Nchi itakapoangazwa kwa utukufu wa malaika yule wa Ufunuo kumi na nane, ndipo nguvu za kidini, njema na mbaya, zitakapoamka kutoka usingizini, na majeshi ya Mungu aliye hai yatashinda katika uwanja wa mapambano." 7BC 983.

21. Je, vita hiyo ya Har-Magedoni ----- vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi ----- ni vita ya wazi kati ya nguvu za wema na nguvu zile za uovu?

"Pambano la kutisha liko mbele yetu. Tunaikaribia vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi. Kile kilichozuiwa kitaachiliwa. Malaika yule wa rehema [Mikaeli] anayakunja mabawa yake, akijitayarisha kushuka chini ya kiti kile cha enzi, na kuiacha dunia kutawaliwa na Shetani. Wakuu na mamlaka za ulimwengu huu wameasi vibaya sana dhidi ya Mungu wa mbinguni. Wamejazwa na chuki dhidi ya wale wanaomtumikia, na upesi, upesi sana, itapiganwa vita ile kuu ya mwisho kati ya wema na uovu. Ulimwengu mzima utakuwa ndio uwanja wa mapambano ----- yaani, mandhari ya pambano la mwisho na ushindi wa mwisho. Hapa, ambapo kwa muda mrefu sana Shetani amewaongoza wanadamu kupigana na Mungu, maasi hayo yatakomeshwa milele." RH 5-13-1902, uk. 9 (Angalia pia ML 308).

22. Je, vita hiyo ya Har-Magedoni ni vita halisi, yaani, ni vita hasa, au ni vita ya "kiroho", au ni yote mawili?

"Vita zitakazopiganwa kati ya majeshi hayo mawili ni vita halisi kama zile zilizopiganwa na majeshi ya ulimwengu huu, na katika hoja ile ya pambano la kiroho hutegemea mambo yale ya milele." PK 176.

23. Chini ya pigo lile la saba, Bwana ataongoza vita hiyo kwa jinsi gani? Ufu.16:17-21.

"Dunia yote inainuka na kushuka na kutanuka kama vile mawimbi ya bahari. Uso wake unapasuka-pasuka. Misingi yake inaonekana kana kwamba inabonyea. Safu za milima zinazama chini. Visiwa vilivyokaliwa na watu vinatoweka. Bandari ambazo zimegeuka na kuwa kama Sodoma kwa uovu wake, zinamezwa na maji yale yaliyokasirika.... Miji ya ulimwengu iliyojivuna sana inabomolewa na kusawazishwa. Majumba ya kifalme, ambayo wakuu wa ulimwengu huu wametumia utajiri wao mwingi ili kujitukuza wenyewe, yanaporomoka na kuwa magofu mbele ya macho yao. Kuta za magereza zinapasuka vipande vipande, na watu wa Mungu, ambao wamefungwa humo kwa ajili ya imani yao, wanawekwa huru.

"Makaburi yanafunguliwa, na wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi... wataamka, wengine wapate uzima wa milele, wengine wapate aibu na kudharauliwa milele.' " GC 637.

24. Wafuasi wa Shetani watakapoona kuwa wamepoteza kila kitu, majuto yao yatakuwa machungu jinsi gani?

"Matajiri wataomboleza kwa ajili ya kuharibiwa kabisa kwa nyumba zao za kifahari.... Hakuna lugha inayoweza kuelezea shauku kubwa waliyo nayo waasi na wasiokuwa waaminifu kwa kile walichokipoteza milele, ----- uzima wa milele ----- Wote wanaungana pamoja kuwatupia lawama

kali sana wachungaji wao.... Mapanga yale waliyokusudia kuwachinja nayo watu wa Mungu, sasa yatatumika kuwaangamiza adui zao. Kila mahali patakuwa na vita na umwagaji damu." GC 654-656 (Angalia pia EW 290).

b. "Ni vigumu kueleza hofu na kukata tamaa kwa wale walioyakanyaga chini ya miguu yao matakwa [amri kumi] matakatifu ya Mungu." GC 639.

25. Kristo ataifikishaje historia yote kwenye kilele chake kitukufu? Ufu. 19:11-20.

a. "Vita ile ya Har-Magedoni karibu itapiganwa. Yule ambaye juu ya vazi lake limeandikwa jina, Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, atayaongoza majeshi ya mbinguni juu ya farasi weupe, wakiwa wamevikwa kitani nzuri, nyeupe, safi." 7BC 982.

b. "Mara hiyo litaonekana mashariki wingu dogo jeusi.... Mfalme wa wafalme atashuka juu ya wingu, akiwa amezungukwa na moto unaowaka.... Waovu wataomba kuzikwa chini ya miamba ya milima.... Waovu watafutiliwa mbali kutoka katika uso wa ulimwengu mzima." GC 640-652, 657.

# SURA YA 21

# NYUMBANI HATIMAYE

(Katika somo hili hakuna tofauti iliyowekwa katika ya Mbinguni na Nchi Mpya).

1. Je, mbinguni ni mahali halisi au ni mahali pasipojulikana, palipojaa roho zisizoweza kuguswa? Ebr. 11:14,16; 1 Petro 1:4; Yohana 14:3.

a. "Ni chimbuko la furaha ilioje kwa wanafunzi wake kujua kwamba walikuwa na Rafiki kama huyo Mbinguni aliyekuwa akiwaombea! Kwa njia ya kupaa kwake Kristo kulikoonekana wazi maoni yao yote na tafakuri yao juu ya mbinguni yalibadilika. Mawazo yao ya kwanza yalitafakari juu yake [Mbingu] kama eneo la nafasi isiyokuwa na kikomo, linalokaliwa na roho zisizokuwa na mwili. Sasa mbingu iliunganishwa na wazo la Yesu, ambaye walikuwa wamempenda na kumcha kupita wote, ambaye walikuwa wameongea na kusafiri naye, ambaye walimshika-shika, hata katika mwili wake ule wa ufufuo....

"Mbinguni hakukuweza kuonekana kwao tena kama mahali kusipojulikana, yaani, nafasi tupu isiyofahamika, iliyojaa roho zisizoweza kuguswa. Sasa wakaiangalia kama ndiyo makao yao ya baadaye, ambako majumba ya kifalme yalikuwa yanaandaliwa kwa ajili yao na Mkombozi wao aliyewapenda." 6BC 1054.

b. "Hofu ya kuufanya urithi ule wa baadaye kuonekana kana kwamba ni yakinifu [wa kweli] imewafanya wengi kutafsiri kiroho kweli zile zile zinazotufanya sisi tuuangalie kama ndiko nyumbani kwetu." GC 674.

2. Je, Shetani anataka sisi tutumie muda wetu kufikiri habari za mbinguni?

"Majaribu ya Shetani huviweka vitu vya ulimwengu huu na kuvifanya viyachote mawazo yetu yote na kutuvutia, hata mambo yale ya kweli ya mbinguni huwa yamefunikwa, na kule kushikamana na dunia hii huchukua umuhimu wa kwanza." OHC 285.

3. Je, Kristo anataka sisi tutumie muda wetu kutafakari mambo yale ya mbinguni?

"Yesu anakuja kutuonyesha faida na uzuri wa picha ile ya mbinguni, ili vivutio vile vya mbinguni vipate kufahamika katika mawazo yetu, na ukumbi wa kumbukumbu zetu upate kutundikwa na picha zile za uzuri ule ulioko mbinguni, yaani, uzuri ule wa milele." OHC 286.

4. Kwa nini Bwana ametupa habari nyingi sana juu ya maisha yale ya baadaye?

a. "Mwalimu huyo Mkuu anampa mwanadamu picha ya ulimwengu ule ujao. Anauleta, pamoja na vivutio vyake katika upeo wa macho yake.... Kama anaweza kuyakaza mawazo ya mwanadamu huyo juu ya maisha yale ya baadaye na furaha zake, basi, ataweza kuyalinganisha maisha yale na maisha haya ya ulimwengu huu, na tofauti ile inayoonekana wazi itaweza kukazwa sana mawazoni mwake, ikiujaza moyo wake na nafsi na mwili wote." OHC 286 (Angalia pia OHC 250, 319).

b. "Makusudi yenye nguvu zaidi, na njia zenye nguvu zaidi, zisingeweza kutumika kamwe; thawabu kubwa mno kwa kutenda mema, raha ile ya mbinguni, urafiki na malaika, ushirika na upendo wa Mungu na Mwanawe, kuzikuza na kuziendeleza nguvu zetu katika vizazi vile vyote vya milele, ----- Je! hivyo sio vivutio na vitu vya kututia moyo na kutusukuma kutoa huduma yetu ya upendo utokao moyoni kwa Muumbaji na Mkombozi wetu?" SC 21,22.

5. Je, kuna uwezekano kwetu kuweza kuutambua utukufu wa nchi ile bora?

a. "Mambo ya ajabu niliyoyaona kule, siwezi kuyaeleza. Laiti kama ningaliweza kuongea kwa lugha ile ya Kanaani, hapo ndipo ningeweza kusimulia kidogo tu juu ya utukufu wa nchi ile bora. Kule niliziona meza za mawe ambazo ndani yake majina ya wale 144,000 yalikuwa yamenakshiwa kwa herufi za dhahabu. Baada ya kuuona utukufu wa Hekalu, tulitoka na kwenda nje, na Yesu akatuacha na kwenda zake mjini." EW 19.

b. "Lugha ni hafifu kabisa kujaribu kueleza jinsi mbinguni kulivyo. Mandhari [picha] ile inapoonekana mbele yangu, nashikwa na mshangao. Najisahau ninapouangalia uzuri ule usio na kifani na utukufu ule mwingi mno, huwa naiweka chini kalamu yangu, na kumaka, 'Ni upendo ulioje! Ni upendo wa ajabu jinsi gani!' Lugha ya hali ya juu sana inashindwa kuuelezea utukufu ule ulioko mbinguni au kina kile kisicho na kifani cha upendo wake Mwokozi."

EW 289.

c. "Kama kwa mtazamo mmoja tu tungejaliwa kuuona mji ule wa mbinguni, tusingetaka tena kukaa hapa duniani. Pana sura za nchi zinazopendeza hapa duniani, nami nazifurahia mandhari hizo za uzuri katika maumbile. Naziunganisha na yule Muumbaji. Lakini najua kwamba nikimpenda Mungu, na kuzishika amri zake [kumi], basi, kuna utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana niliowekewa mbinguni. Japo mandhari za duniani ni nzuri kama vile zilivyo, haziwezi kulinganishwa kabisa na utukufu ule wa ulimwengu wa milele. ST 4-8-1889, uk.210.

d. "Lugha ya kibinadamu haitoshi kuelezea thawabu waliyowekewa wenye haki. Itajulikana tu kwa wale watakaoitazama. Hakuna akili yo yote ya kibinadamu inayoweza kuufahamu utukufu wa Paradiso ya Mungu." GC 675.

6. Baadhi ya sura za maumbile zinazopatikana kule ni zipi?

a. Milima, Nyanda, na Mito.

"Kuna mito inayotiririka kule daima, maji yake ni maangavu kama kioo, na kando kando yake kuna miti inayopepesuka ambayo vivuli vyake huvitupa juu ya njia zile zilizotengenezwa kwa ajili ya wale waliokombolewa na Bwana. Kule ziko nyanda pana zinazoinuka kwa nyuma kuelekea kwenye vilima vizuri na milima ya Mungu ambayo vilele vyake vinafika juu. Katika nyanda hizo za amani, kando ya mito ile ya uzima, watu wa Mungu, ambao hapa wamekuwa wasafiri na wapitaji, watapata makao yao huko." GC 675.

b. Misitu.

"Kisha tukaingia katika msitu mdogo, sio kama misitu yenye gizagiza tuliyo nayo hapa; la, la; lakini una miti michache, na kila mahali ni utukufu mtupu; matawi ya miti yalipepesuka huku na huku, nasi sote tukapiga kelele, tukisema, 'Tutakaa kwa salama nyikani, na kulala misituni.' Kisha tukapita misituni, kwa kuwa tulikuwa safarini kwenda kwenye Mlima Sayuni." EW 18.

c. Miti ya aina zote.

"Mlima Sayuni ulikuwa mbele yetu tu, na juu ya mlima huo palikuwa na Hekalu, na kulizunguka palikuwa na milima mingine saba ambayo juu yake yaliota maua waridi na yungiyungi. Nami nikawaona watoto wadogo wakipanda, au, kama wenyewe walichagua, basi, walitumia mabawa yao madogo na kuruka kwenda kwenye vilele vya milima ile na kuchuma maua yale yasiyonyauka kamwe. Kulikuwa na miti ya aina zote kulizunguka Hekalu hilo ili kupafanya mahali pale paonekane kuwa panapendeza sana; mti mweupe mgumu, msunobari, mvinje, mzeituni, mti mdogo aina ya 'myrtle', na mkomamanga, mtini uliinama chini kwa uzito wa tini zake zinazokuja kwa wakati wake ----- [matunda] hayo yalipafanya mahali pale pote kujazwa na utukufu." EW 19.

d. Aina zote za maua.

"Nikaliona shamba lingine limejaa aina zote za maua, nami nilipoyachuma, nikapiga kelele, nikisema, 'Hayawezi kufifia kamwe.' Tena nikaona shamba la nyasi ndefu, limejaa utukufu mno kulitazama; zilikuwa na rangi ya chanikiwiti na mwonekano wake ulikuwa kama fedha na dhahabu, zilipokuwa zikipepesuka kwa fahari kwa utukufu wake Mfalme Yesu." EW 18.

e. Aina zote za matunda.

"Nami nikaiona meza ya fedha safi; urefu wake ilikuwa maili nyingi, lakini macho yetu yaliweza kuangalia juu yake mpaka mwisho wake. Nikayaona matunda ya mti ule wa uzima, mana, lozi (almonds), tini, na komamanga, zabibu, na matunda mengi mbalimbali. Nikamwomba Yesu aniruhusu kula matunda yale." EW 19.

f. Mti wa Uzima.

"Hapo tuliuona mti ule wa uzima na kiti kile cha enzi ambako ulitoka mto wa maji safi, na pande zote mbili za mto ule ulikuwako mti ule wa uzima. Upande mmoja wa mto ule palikuwa na shina la mti huo, na shina lingine upande ule mwingine, yote mawili yakiwa yanang'aa kama dhahabu angavu, safi. Mara ya kwanza nilidhani naona miti miwili. Nikatazama tena, na kuona kuwa ilikuwa imeungana juu kufanya mti mmoja. Kwa hiyo mti huo wa uzima ulikuwa kila upande wa mto ule wa uzima. Matawi yake yaliinama chini mpaka mahali pale tulipokuwa tumesimama, na matunda yake yalikuwa yanapendeza sana; yalionekana kama dhahabu iliyochanganywa na fedha." EW 17.

g. Wanyama wote ni wapole na wa kutumainiwa.

"Hakutakuwa na cho chote kinacho'dhuru wala kuharibu katika mlima wangu wote mtakatifu; asema Bwana.' Kule mwanadamu atarejeshewa utawala wake alioupoteza, na viumbe vile vya daraja la chini vitautambua tena utawala wake; wale walio wakali [sasa] watakuwa wapole, waoga, nao watakuwa na imani na sisi." Ed 304.

h. Mchana wa milele.

"Nuru ya jua kule itapitwa kabisa na nuru ile isiyoweza kuleta maumivu kwa macho yetu tutakapoiangalia, lakini ambayo kwa kiwango kisichopimika itazidi nuru ile ya jua letu wakati wa adhuhuri. Utukufu wa Mungu na Mwana-Kondoo utaugharikisha mji ule mtakatifu kwa nuru yake isiyofifia kamwe. Waliokombolewa watatembea katika utukufu ule wa mchana wa milele usiohitaji jua." GC 676.

7. Watu watakuwaje huko? Watakuwa wakubwa kiasi gani? Je, watakuwa na uwezo gani?

a. Urefu wa karibu futi kumi na mbili.

"Wakiwa wamerejeshwa kwenye mti ule wa uzima katika Edeni ile iliyokuwa imepotea zamani sana, wale waliokombolewa wataendelea ku'kua' [Malaki 4:2, KJV, badala ya neno 'kuchezacheza'] na kufikia kimo kamili cha jamii ya wanadamu wa asili [wale wa mwanzo] katika utukufu wake." GC 645.

"Yeye [Adamu] alikuwa na urefu wa zaidi ya mara mbili kuliko ule wa wanadamu wanaoishi duniani sasa, na mwili wake uliumbika ukiwa na uwiano mzuri." 3SG 34.

b. "Nguvu ya uhai mara ishirini kuliko ilivyo sasa.

"Kama Adamu, wakati wa uumbwaji wake, asingalikuwa amepewa nguvu ya uhai mara ishirini zaidi ya ile waliyo nayo wanadamu sasa, basi, jamii ya wanadamu, pamoja na mazoea yao waliyo nayo sasa ambayo yanakiuka sheria ya maumbile yao, ingekuwa imetoweka kabisa." FE 23.

"Hakuna atakayehitaji au kutamani kupumzika. Hakutakuwa na uchovu katika kufanya mapenzi ya Mungu na kulisifu jina lake. Daima tutajisikia tunayo nguvu mpya kama ile ya asubuhi na daima tutakuwa mbali na kuishiwa nguvu mwisho wa siku." GC 676.

"Maumivu hayawezi kuwako katika mazingira yale ya mbinguni. Hapatakuwako na machozi tena, wala misafara ya mazishi, wala tepe za maombolezo. 'Wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio,... kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.' 'Wala hapana mwenyeji atakayesema, Mimi mgonjwa.' " GC 676.

"Mbinguni ni afya tupu." 3T 172.

"Kujipatia maarifa kule hakutauchosha ubongo wala kuzimaliza kabisa nguvu zake."

GC 677.

c. "Sura yetu ya sasa itahifadhiwa.

"Ufufuo wa Yesu ulikuwa mfano wa ufufuo ule wa mwisho wa wale wote wanaolala katika yeye. Uso wa Mwokozi aliyefufuka, desturi yake, usemi wake, vyote hivyo viliweza kutambuliwa na wanafunzi wake. Kama vile Yesu alivyofufuka kutoka kwa wafu, ndivyo wale waliolala katika yeye watakavyofufuka tena. Tutawajua rafiki zetu, kama vile wanafunzi walivyomjua Yesu. Wanaweza kuwa walikuwa na ulemavu, wagonjwa, au wameharibika sura zao katika maisha haya yasiyodumu, nao watafufuka wakiwa na afya kamili na umbo lenye ulinganifu mzuri; lakini watakapokuwa katika mwili huo wa utukufu sura yao itahifadhiwa kwa ukamilifu." DA 804.

d. Kumbukumbu zetu zitakuwa kamili kabisa.

"Watu wale walioishi kabla ya Gharika walikuwa hawana vitabu, hawakuwa na kumbukumbu zo zote zilizokuwa zimeandikwa; lakini pamoja na nguvu zao nyingi za kimwili na kiakili, walikuwa na kumbukumbu zao thabiti, zenye uwezo wa kunasa na kutunza kile walichokuwa wameambiwa, nao kwa zamu yao kuweza kuwapa wazao wao bila kuuathiri ujumbe ule."

PP 83.

e. Akili zenye uwezo wa kukua daima.

"Kadiri watakavyojifunza zaidi na zaidi juu ya hekima, upendo, na uweza wa Mungu, ndivyo kadiri akili zao zitakavyokuwa zikikua daima, na furaha yao ndivyo kadiri itakavyoongezeka daima." 5T 702.

f. Watakuwa na macho kama darubini yaonayo vitu vidogo sana na vile vilivyo mbali sana.

"Kwa macho yao yaonayo wazi kabisa wataangaza na kuuangalia utukufu wa uumbaji ----- yaani, yale majua na nyota na mifumo ya sayari inayoyazunguka majua hayo, vyote hivyo vikizunguka katika mpangilio wake na kukizunguka kiti kile cha enzi cha Mungu." GC 677.

"Kule, pazia hili linaloyatia macho yetu giza litakapoondolewa, ndipo macho yetu yatakapouona ulimwengu ule wa uzuri ambao kwa sasa tunaiona sehemu yake ndogo tu kwa kutumia darubini ya kuona vitu vidogo sana visivyoonekana kwa macho (microscope); na kwa kuuangalia utukufu ule wa mbingu, ambazo kwa sasa tunazichunguza kwa mbali kwa darubini ya kuona mbali (telescope); wakati ule dhambi hii inayoangamiza itakapoondolewa kabisa, na dunia nzima itakapoonekana katika 'uzuri wa Bwana Mungu wetu,' ni eneo kubwa mno lililoje litakalokuwa wazi kwa utafiti wetu!" Ed 303.

"Pazia lile linaloingia kati ya ulimwengu huu unaoonekana na ule usioonekana litawekwa kando na mambo ya kustaajabisha mno yatafunuliwa kwetu." Ed 304.

g. Tutakuwa na uwezo wa kusafiri katika anga.

"Msongamano wa waliokombolewa utazunguka toka dunia moja kwenda dunia nyingine, na wakati wao mwingi utatumika katika kuzichunguza siri za ukombozi." 7BC 990.

"Hazina zote za malimwengu zitakuwa wazi kuchunguzwa na wale waliokombolewa na Mungu. Wakiwa hawafungwi na hali ile ya kufa, wataruka kwa mabawa yao pasipo kuchoka kwenda kwenye dunia zile zilizo mbali...." GC 677.

h. Watapewa taji ile ya uzima.

"Thawabu, yaani, utukufu ule wa mbinguni, watakayopewa washindi wale, italingana na kiwango walichoweza kuiwakilisha tabia ya Kristo katika ulimwengu huu. 'Apandaye haba atavuna haba.' 2 Kor. 9:6.... Taji ya uzima itang'aa sana au itakuwa na mwanga uliofifia, itametameta ikiwa na nyota nyingi, au itaangazwa kwa johari chache sana, kulingana na mwenendo wetu wenyewe [tuliokuwa nao hapa duniani]." OHC 123.

8. Je, kutakuwa na maisha ya kifamilia, ndoa na kuzaa watoto kule? Mathayo 22:23-30.

a. Hakuna ndoa kule wala kuzaa watoto.

"Kuna watu leo wanaoeleza imani yao wakisema kwamba kutakuwa na ndoa na kuzaa watoto katika nchi mpya, lakini basi, wale wanaoyaamini Maandiko hawawezi kulikubali fundisho kama hilo. Fundisho linalosema kwamba watoto watazaliwa katika nchi mpya halina sehemu katika 'lile Neno la Unabii lililo imara zaidi.' " MM 99; 1SM 172.

b. "Tusikisie mahali ambapo hatuna maelezo yo yote.

"Watenda kazi wa Mungu wasiutumie muda wao kukisia-kisia tu hali ya mambo itakayokuwamo katika nchi mpya. Ni kiburi cha makusudi kujiingiza katika kukisia-kisia tu na kuwa na nadharia zinazohusu mambo yale ambayo Bwana hajayafunua kwetu. Amefanya maandalizi yote kwa ajili ya furaha yetu kwa ajili ya maisha yale ya baadaye, na sisi haitupasi kukisia-kisia tu kuhusu mipango aliyo nayo kwa ajili yetu. Wala tusizipime hali za maisha yale ya baadaye kwa kufuata hali za maisha haya tuliyo nayo." GW 314.

"Ni kiburi cha makusudi kujiingiza katika kukisia-kisia tu na kuwa na nadharia zinazohusu mambo yale ambayo Mungu hajatufunulia sisi katika Neno lake. Hatuna haja ya kuingia katika hali ile ya kukisia-kisia tu kuhusu hali yetu ya baadaye." 2SM 260.

d. Watoto wadogo katika nchi mpya.

"Nami nikawaona watoto wadogo wakipanda, au, kama wenyewe walichagua, basi, walitumia mabawa yao madogo na kuruka kwenda kwenye vilele vya milima ile na kuchuma maua yale yasiyonyauka kamwe." EW 19.

e. Tutaungana tena na marafiki zetu.

"Marafiki waliotenganishwa na kifo kwa muda mrefu wataungana, wasiweze tena kutengana kamwe, na kwa nyimbo zao za furaha watapaa pamoja kwenda kwenye mji ule wa Mungu."

GC 645.

f. Tutaishi katika nyumba.

"Kisha tukaanza kuyaangalia mambo yaliyojaa utukufu nje ya mji ule. Kule nje nikaziona nyumba nzuri ajabu zenye utukufu ambazo zilionekana kama vile zina rangi ya fedha, zikiwa zimeimarishwa kwa nguzo nne zilizopambwa kwa lulu zenye utukufu mwingi mno kwa kuziangalia. Hizo zilikuwa zimekusudiwa kukaliwa na watakatifu. Katika kila moja ilikuwamo rafu (shelf) ya dhahabu. Nikawaona wengi wa wale watakatifu wakiingia katika nyumba zao hizo, wakizivua taji zao zinazometameta na kuziweka juu ya rafu hizo." EW 18.

" 'Nao watajenga nyumba, na kukaa ndani yake.' " GC 675; Isa. 65:21.

9. Ni nani tutakayefurahia kupiga gumzo naye uso kwa uso?

a. Malaika wetu mlinzi.

"Kila mmoja aliyekombolewa ataijua huduma ya malaika katika maisha yake mwenyewe. Malaika yule aliyekuwa mlinzi wake tangu dakika ya mwanzo kabisa [ya maisha yake]; malaika yule aliyezilinda hatua zake, na kukifunika kichwa chake wakati wa hatari kubwa; malaika yule aliyekuwa pamoja naye katika bonde lile la uvuli wa mauti, aliyetia alama mahali pake pa kupumzikia [kaburi lake], aliyekuwa wa kwanza kumsalimu asubuhi ile ya ufufuo, ----- litakuwa ni jambo la ajabu jinsi gani kuongea naye, na kujifunza historia ya kuingilia kati kwa Mungu katika maisha yake binafsi, ushirikiano wa mbingu katika kila kazi kwa ajili ya binadamu." Ed l305.

"Kutoka katika hatari ngapi, zinazoonekana na zile zisizoonekana, sisi tumelindwa salama kwa njia ya kuingilia kati kwa malaika hao, sisi hatutaweza kujua kamwe, mpaka kwenye nuru ile ya miele tutakapouona uongozi wa Mungu ulivyokuwa kwetu." DA 240.

b. "Malaika wale wengine pamoja na waaminifu wale wa vizazi vyote.

"Upendo na huruma ambavyo ni Mungu Mwenyewe aliyevipandikiza katika mioyo yetu, kule vitapata nafasi ya kutumika kweli kweli na kuleta maisha matamu sana. Maongezi yetu safi pamoja na viumbe wale watakatifu [malaika], maisha murua ya kijamii pamoja na malaika wale wabarikiwa na waaminifu wale wa vizazi vyote, walioyafua mavazi yao na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo, vifungo vile vitakatifu vitakavyoifunga pamoja 'familia yote ya mbinguni na ya duniani' [Efe.3:15, Tafsiri ya KJV]. ----- hivyo vitasaidia kuleta furaha ya wale waliokombolewa." GC 677 (Angalia Ed 306).

c. Tutaongea na Baba na Mwana.

"Watu wa Mungu wana upendeleo wa pekee kuweza kuongea ana kwa ana na Baba na Mwana.... Tutamwona uso kwa uso, pasipo pazia kuwa katikati kuweza kuihafifisha nuru yake." GC 677.

"Endapo katika kipindi chote cha maisha haya wamekuwa watiifu kwa Mungu, basi, hatimaye 'watamwona uso wake, na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao.' Ufunuo 22:4. Furaha ya mbinguni ni nini kama sio kumwona Mungu? Ni furaha gani kubwa kwa mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema ya Kristo kuliko ile ya kuuona uso wa Mungu na kumjua kama Baba?" 8T 268.

10. Ni kumbukumbu gani moja pekee ya kazi ya kikatili iliyofanywa na dhambi ambayo itakuwa mbele yetu daima?

a. "Kumbukumbu moja pekee itabaki: Mkombozi wetu daima atachukua alama zile za kusulibiwa kwake. Juu ya kichwa chake kilichojeruhiwa, ubavuni pake, katika viganja vyake vya mikono na miguuni, hizo ndizo alama pekee za kazi ya kikatili ambayo dhambi imefanya kwake." GC 674. [Zek.13:6; Hab.3:4.]

b. "Japokuwa huzuni na maumivu na majaribu yao waliyopata hapa duniani vitakuwa vimekwisha, na chanzo chake kitakuwa kimeondolewa, watu wa Mungu watakuwa na uwezo kiakili wa kuelewa kile wokovu wao ulichogharimu." GC 651.

11. Ni shughuli gani na masomo gani tutakayoshughulika nayo kule?

a. Kukusanyika pamoja mara kwa mara kumwabudu Mungu.

" 'Na itakuwa, mwezi mpya hata mwezi mpya, na sabato hata sabato, wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu, asema BWANA.' " PK 733 (Isa. 66:22,23).

b. Kutunga Nyimbo na Kusikiliza Muziki ule ulio mkamilifu sana.

"Kisha nikaona idadi kubwa ya malaika wakizileta taji zile tukufu toka mjini, ----- taji kwa kila mtakatifu, jina lake likiwa limeandikwa juu yake. Yesu alipozitaka taji zile, malaika wale wakazikabidhi kwake, naye kwa mkono wake wa kuume, Yesu yule mpendwa, akaziweka taji zile juu ya vichwa vya watakatifu wale. Vivyo hivyo, malaika wakavileta vinubi, na Yesu akawapa watakatifu pia. Malaika wenye kutoa amri wakapiga kwanza noti moja, kisha kila sauti ikainuliwa juu katika sifa za shukrani na furaha, na kila mkono kwa ufundi ukacharaza nyuzi za kinubi, na kutoa muziki mtamu wa nyimbo zile tamu, zilizo kamilifu." EW 288.

"Kule kutakuwa na muziki, na nyimbo, muziki kama ule na nyimbo kama zile ambazo hazijapata kusikika katika sikio la kibinadamu wala akili kuziwazia isipokuwa labda katika maono ya Mungu peke yake." Ed 307 (Angalia PK 730).

c. Tutajifunza Historia ya Pambano Kuu.

"Hapo ndipo itakapofunuliwa njia ya Pambano Kuu ambalo kuzaliwa kwake kulitokea kabla ya wakati kuanza, na linaloisha tu wakati utakapokoma." Ed 304.

d. Kugundua sababu ya matatizo yote ya maisha haya.

"Matatizo yote yatokanayo na uzoefu wa maisha haya ndipo yatakapoelezwa wazi. Mahali ambapo kwetu sisi yameonekana kuwa ni machafuko tu ya kukatisha tamaa, makusudi yaliyoharibika na mipango iliyozuiwa, litaonekana kusudi lake kuu, lililobatilisha mambo yote, na lenye ushindi, linaloafikiana na mapenzi ya Mungu." Ed 305.

e. Kujifunza ushindi wa kila tendo jema katika maisha haya.

"Kule wale wote waliotenda kwa roho isiyokuwa na uchoyo wataona matunda ya kazi zao. Utendaji bora wa kila kanuni sahihi na matendo bora utaonekana. Kitu kinachofanana na hicho twakiona hapa. Lakini ni kidogo jinsi gani matokeo ya kazi bora katika maisha haya yanaonekana kwa mtendaji! Ni wangapi wanafanya kazi ngumu bila ubinafsi na bila kuchoka kwa ajili ya wale wanaokwenda mbali na kusikojulikana! Wazazi na waalimu wanalala chini katika usingizi wao wa mwisho [mauti], kazi yao ya maisha ikionekana kuwa imefanyika bure; hawajui kwamba uaminifu wao umefungua muhuri wa chemchemi za mibaraka ambazo haziwezi kukoma kutiririka; ni kwa imani tu wanawaona watoto wale waliowapa mafunzo wakiwa mbaraka na mvuto kwa wanadamu wenzao, na mvuto huo unajirudia-rudia wenyewe mara elfu moja. Watenda kazi wengi hupeleka ulimwenguni ujumbe wao unaotia nguvu na tumaini na ujasiri, maneno yao ambayo yanapeleka mbaraka kwa mioyo mingi katika kila nchi; lakini kuhusu matokeo yake hayo wanayajua kidogo sana wale wanaosumbuka kufanya kazi katika hali ya upweke na kutokujulikana. Kwa hiyo, zawadi hutolewa, mizigo hubebwa, kazi hufanyika. Wanadamu hupanda mbegu ambazo wengine huvuna mavuno mengi juu ya makaburi yao. Wanapanda miti, ili wengine wapate kula matunda yake. Hapa wao wanaridhika tu kujua kwamba wameanzisha njia zitakazoleta mema. Katika ulimwengu ule ujao tendo na athari zake kwa mambo yote hayo vitaonekana." Ed 305,306.

f. Kufanya kazi katika bustani na mashambani.

"Katika nchi ile mpya, wale waliokombolewa watajishughulisha kufanya kazi na kuwa na starehe zile zile zilizowaletea furaha Adamu na Hawa hapo mwanzo. Maisha yale ya Edeni ndiyo watakayoishi, maisha ya kufanya kazi katika bustani na mashambani." PK 730 (Angalia pia Ed 304).

"Nikawaona wengi wa watakatifu wale wakiingia katika nyumba zile, wakizivua taji zao zinazometameta na kuziweka juu ya rafu zao, kisha wakaenda mashambani karibu na nyumba zile kufanya kazi fulani na udongo; si kama inavyotupasa kufanya kazi na udongo hapa; la, la. Nuru tutufu iling'aa kuzunguka vichwa vyao, na wakati wote waliendelea kupiga kelele na kutoa sifa kwa Mungu." EW 18.

h. Kujiendeleza daima bila kuona mwisho wake.

"Kule kila nguvu itakuzwa, kila uwezo utaongezeka. Shughuli kubwa mno zinazohitaji ujasiri zitatekelezwa, malengo ya juu kabisa yatafikiwa, tamaa za kufanya mambo makuu zitatimizwa. Hata hivyo, bado vitaonekana vilele vipya vya kuvifikia, maajabu mapya ya kuyastaajabia, kweli mpya za kuzifahamu, malengo mapya yatakayohitaji nguvu zote za mwili, nafsi, na roho kuyatekeleza." Ed 307 (Angalia pia GC 677).

12. Furaha kuu ya waliokombolewa itakuwa ni kitu gani?

"Kila kitu mbinguni ni bora na kinachangamsha. Huko wote wanatafuta mambo na furaha ya wengine. Hakuna anayetumia muda wake kwa kuiangalia na kuitunza nafsi yake. Ni furaha kuu kwa viumbe wale wote watakatifu kushuhudia shangwe na furaha ya wale wanaowazunguka." 2T 239.

13. Nawezaje kuwa na hakika ya kuwa pale?

a. "Lingekuwa ni kusudi la kila mtu, si kutafuta sana kujua yote juu ya hali zile zitakazokuwako katika maisha yale ya baadaye, bali kujua kile ambacho Bwana anataka kwake katika maisha haya." CT 249.

b. "Amani na umoja katika majumba yale ya kifalme kule mbinguni havitaharibiwa kwa kuwapo kwake mmoja ambaye ni mkorofi au ambaye hana huruma. Yule ambaye katika dunia hii anajikweza nafsi yake katika kazi ile aliyopewa kuifanya hataweza kuuona kamwe ufalme wa Mungu mpaka awe amegeuka roho yake, mpaka awe mpole na mnyenyekevu wa moyo, akionyesha hali ya kawaida kama ile ya mtoto mdogo." 8T 140.

c. "Iwapo ninyi mnataka kuwa watakatifu kule mbinguni, basi, yawapasa kwanza kuwa watakatifu hapa duniani." TM 145.

`